# ATHARI ZA KISWAHILI NA KIKUYU KWA UTHABITI WA KISHONA NCHINI KENYA:MTAZAMO WA KIISIMUJAMII

**MERCY MORAA MOTANYA**

**C82/21369/2021**

**CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**IDARA YA KISWAHILI**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA KWA IDARA YA KISWAHILI ILI KUTOSHELEZA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMIFU KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**OKTOBA, 2024**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijawasilishwa popote kwa madhumuni ya shahada yoyote katika chuo chochote.

Sahihi ................................Tarehe 09/10/2024

**Mercy Moraa Motanya**
Idara ya Kiswahili
Chuo Kikuu cha Kenyatta

## WASIMAMIZI

Tasnifu hii imewasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi waliochaguliwa na Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Sahihi ................................Tarehe 9th Oct /2024

**Dkt. Stephen Njihia Kamau**
Idara ya Kiswahili
Chuo Kikuu cha Kenyatta

Sahihi ................................Tarehe 11-10-2024.

**Dkt. Boniface Ngugi**
Idara ya Kiswahili
Chuo Kikuu cha Kenyatta

# TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kuelimika hadi kiwango hiki cha uzamifu. Kwa wazazi wangu mwalimu George Motanya na Bi. Prisca Kemunto, ndugu zangu Stella, Joel na Dinnah. Mume wangu Victor Oginda na mwanangu Samuel Oginda.

## SHUKRANI

Namshukuru Mola kwa kuniwezesha kufika kiwango hiki cha uzamifu. Nawashukuru kwa dhati wasimamizi wangu Dkt. Stephen Njihia Kamau na Dkt. Boniface Ngugi kwa kukubali kuniongoza katika safari hii ya masomo ya uzamifu. Hakika mmenielekeza kwa moyo mweupe na maelekezo yenu yamekuwa taa katika barabara yangu ya utafiti wa uzamifu. Shukrani zimwendee mwenyekiti wa idara ya Kiswahili Prof. Peter Githinji kwa kunielekeza katika upangaji wa kazi hii na kunitia moyo kwamba inawezekana. Aliyekuwa mwenyekiti wa idara ya Kiswahili Dkt. Pamela Ngugi, nakushukuru kwa kunitia moyo katika safari hii ya masomo tangu shahada ya kwanza hadi wakati nilipouanza utafiti wa uzamifu. Dkt. Kenneth Ngure wa idara ya Literature, Linguistics and Foreign Languages, asante kwa kunitafsiria kazi nyingi nilizozipata kwa Kiingereza hadi Kiswahili na pia kuniongoza kuhusu yanayotarajiwa katika utafiti wa uzamifu. Dkt. Elizabeth Mwaniki (Educational Psychology) kwa kuninasihi kuhusu mielekeo mbalimbali ya lugha na Dkt. Samuel Mutweleli (DSVOL) kwa kunielekeza katika uchanganuzi wa data kitakwimu. Cecilia Kamau na Augustine Abuta, asante kwa kukaa nami na kunitia moyo tangu mwanzo wa utafiti huu hadi hatima yake. Mungu wetu awabariki nyote.

## YALIYOMO

**UNGAMO** ..... ii
**TABARUKU** ..... iii
**SHUKRANI** ..... iv
**YALIYOMO** ..... v
**ORODHA YA MAJEDWALI** ..... xi
**ORODHA YA BAA-GRAFU NA PAI-CHATI** ..... xii
**ORODHA YA VIFUPISHO** ..... xiii
**UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU** ..... xiv
**IKISIRI** ..... xvi
**ABSTRACT** ..... xvii
**SURA YA KWANZA**: **MISINGI YA UTAFITI** ..... 1
1.0 Utangulizi ..... 1
1.1 Usuli wa Utafiti ..... 1
1.1 Suala la Utafiti ..... 4
1.3 Malengo ya Utafiti ..... 5
1.4 Maswali ya Utafiti ..... 5
1.5 Sababu za Kuchagua Mada ..... 6
1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti ..... 8
1.7 Nadharia za Utafiti ..... 10
1.7.1 Nadharia ya Uthabiti wa Kiisimujamii wa Lugha ..... 11
1.7.1.1 Umbali wa Jamiilugha Kutoka Mijini au Vijijini ..... 13
1.7.1.2 Maeneo Mbalimbali ya Kijamii Panapotumika Lugha na Wanajamiilugha ..... 14
1.7.1.3 Aina na Viwango vya Uhamishaji wa Msimbo ..... 15
1.7.1.4 Idadi ya Wanajamiilugha Wanaozungumza Lugha Husika ..... 15
1.7.1.5 Mtawanyiko wa Wanajamiilugha Husika Katika Mtandao wa Kijamii ..... 16
1.7.1.6 Mtazamo Ulioko kwenye Jamii kuhusu Wanajamiilugha Husika na Wanajamiilugha Wengine kuhusu Lugha Husika ..... 16
1.7.1.7 Hadhi Iliyopewa Lugha Husika Katika Jamii ..... 17
1.7.1.8 Misingi Imara na Halali ya Kiuchumi ya Jamiilugha Husika ..... 17
1.7.2 Nadharia ya Uzalishaji Kijamii. ..... 18

1.7.2.1 Kila Kizazi Hubuni na Kuweka Mikakati ya Kurithisha Kizazi Kinachofuata Utamaduni Wake ....18
1.7.2.2 Athari Mbalimbali za Mtagusano Lugha Moja na Nyingine ....19
1.8 Mbinu za Utafiti ....20
1.8.1 Utafiti Awali ....20
1.8.2 Jumuiya ya Utafiti ....21
1.8.3 Uteuzi wa Sampuli ....22
1.8.4 Ukusanyaji wa Data ....23
1.8.4.1 Hojaji ....24
1.8.4.2 Mijadala ya Kimakundi ....25
1.8.4.3 Utazamaji au Uchunzaji ....25
1.8.4.4 Kushiriki ....26
1.8.4.5 Mahojiano ....26
1.8.4.6 Vifaa Vingine ....27
1.8.5 Uchanganuzi wa Data ....28
1.8.6 Uwasilishaji wa Matokeo ....29
1.8.7 Maadili ya Utafiti ....29
1.9 Hitimisho ....30
**SURA YA PILI**: **MAPITIO YA MAANDISHI** ....31
2.0 Utangulizi ....31
2.1 Mtagusano Lugha ....31
2.2 Athari za Mtagusano Lugha ....34
2.2.1 Ubadilishaji Msimbo ....35
2.2.2 Ukopaji wa maneno ....38
2.2.3 Wingilugha ....41
2.2.4 Mabadiliko ya lugha ....42
2.2.5 Mielekeo ya Lugha ....45
2.2 Tafiti Kuhusu Mtagusano Lugha Duniani ....52
2.4 Hali ya Kiisimujamii ya Lugha Duniani ....53
2.5 Hali ya Kiisimujamii ya Lugha Barani Afrika ....54
2.5.1 Hadhi ya Lugha za Kiasili Barani Afrika ....56

2.6 Wanajamiilugha wa Kishona ........ 57
2.6.1 Utamaduni wa Washona Nchini Zimbabwe ........ 58
2.6.2 Dini na Imani ya Washona ........ 60
2.6.3 Historia ya Washona Nchini Kenya ........ 63
2.6.4 Hali ya Kiuchumi ya Washona Nchini Kenya ........ 65
2.6.5 Familia za Washona Nchini Kenya ........ 67
2.6.6 Hali ya Elimu kwa Washona Nchini Kenya ........ 67
2.6.7 Yaliyoandikwa kuhusu Washona na Lugha yao ........ 68
2.7 Lugha ya Kiswahili ........ 70
2.7.1 Mielekeo Kuhusu Kiswahili Nchini Kenya ........ 72
2.8 Lugha ya Kikuyu Nchini Kenya ........ 74
2.9 Udumishaji wa Lugha ........ 75
2.10 Uthabiti wa Kiisimujamii wa Lugha ........ 84
2.10.1 Kupokezanwa kwa Lugha Baina ya Vizazi ........ 87
2.10.2 Idadi Kamili ya Wanajamiilugha Wanaozungumza Lugha ........ 88
2.10.3 Asilimia ya Wazungumzaji wa Lugha katika Jumuiya Nzima ya Jamiilugha ........ 89
2.10.4 Ruwaza za Matumizi ya Lugha katika Maeneo Mbalimbali ya Kijamii ........ 90
2.10.5 Ueneaji wa Lugha katika Maeneo Mapya ya Matumizi na Kwenye Vyombo vya Habari ........ 91
2.10.6 Nyenzo Zilizopo za Kufundishia Lugha Husika Hasa Katika Kusoma na Kuandika ........ 93
2.10.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Uthabiti wa Kiisimujamii wa Lugha ........ 94
2.11 Hitimisho ........ 97
**SURA YA TATU: ATHARI ZA MTAGUSANO WA KISWAHILI NA KIKUYU KWA KISHONA** ........ 99
3.0 Utangulizi ........ 99
3.1 Athari Mbalimbali za Mtagusano wa Kiswahili na Kikuyu kwa Kishona ........ 99
3.1.1 Lugha Inayofahamika Zaidi Kati ya Kiswahili, Kikuyu na Kishona kwa Washona ........ 100
3.1.2 Lugha ya Matumizi Kwenye Shughuli Rasmi ........ 102
3.2 Ukopaji wa Maneno ya Kiswahili na Kikuyu kwa Washona ........ 104
3.3 Ubadilishaji Msimbo ........ 108

3.4 Uthabiti wa Kiisimujamii wa Kishona ........................................................ 110
3.4.1 Lugha ya Vijana ya Mazungumzo kwenye Mazingira ya Nyumbani............. 111
3.4.2 Lugha ya Mazungumzo baina ya Vijana na Wazazi Nyumbani .................... 111
3.4.3 Lugha ya Matumizi baina ya Ndugu............................................................. 114
3.4.4 Lugha ya Mazungumzo baina ya Vijana na Viongozi wa Utawala ................ 116
3.4.5 Lugha ya Mazungumzo baina ya Washona na Marafiki wa Nje ya Jamii Yao .... 118
3.4.6 Lugha ya Biashara ......................................................................................... 120
3.4.7 Lugha ya Shughuli za Ibada............................................................................ 122
3.4.8 Lugha ya Matumizi Katika Maeneo ya Shuleni ............................................ 124
3.4.9 Matumizi ya Kiswahili, Kishona na Kikuyu katika Shughuli za Kitamaduni . 126
3.5 Wingilugha ............................................................................................ 130
3.6 Mabadiliko ya Kishona.......................................................................... 133
3.7 Hitimisho ............................................................................................... 134
**SURA YA NNE: SABABU ZA WASHONA ZA KUTUMIA KISWAHILI NA KIKUYU NA MIELEKEO YAO KUHUSU LUGHA HIZI** .................. 137
4.0 Utangulizi ............................................................................................. 137
4.1 Sababu za Washona za Kutumia Kiswahili kwenye Maeneo Mbalimbali ya Kijamii.................................................................................................... 138
4.1.1 Sababu za Kielimu ........................................................................................ 138
4.1.2 Sababu za Utaifa na Urasmi wa Kiswahili Nchini Kenya ............................. 141
4.1.3 Sababu za Mawasiliano na Utangamano ...................................................... 143
4.1.4 Sababu ya Ushirikiano .................................................................................. 145
4.1.5 Sababu za Mahusiano ................................................................................... 146
4.1.6 Sababu za Kiuchumi ..................................................................................... 148
4.1.7 Sababu za Utambulisho ................................................................................ 149
4.1.8 Sababu za Kidini............................................................................................ 151
4.1.9 Sababu za Kiusalama .................................................................................... 152
4.2 Sababu za Washona za Kutumia Kikuyu Nchini Kenya ............................... 153
4.2.1 Sababu ya Ufadhili......................................................................................... 154
4.2.2 Sababu ya Umaarufu wa Kikuyu ................................................................... 156
4.2.3 Sababu ya Mawasiliano ................................................................................. 158
4.2.4 Sababu ya Kushiriki kwenye Sherehe za Kitamaduni ................................... 159

4.2.5 Sababu ya Biashara ........ 160
4.3 Sababu za Washona Kuzungumza Kishona Nchini Kenya ........ 162
4.3.1 Kudumisha Utamaduni Wao ........ 163
4.3.2 Dini 165
4.3.3 Ugwe wa Kuwaunganisha ........ 166
4.3.4 Ukumbusho wa Asili yao ........ 167
4.3.5 Sababu za Udumishaji wa Kishona ........ 169
4.4 Mielekeo ya Washona katika Matumizi ya Kiswahili na Kikuyu ........ 171
4.4.1 Upimaji wa Mielekeo ya Washona kuhusu Kiswahili ........ 171
4.4.2 Mielekeo ya Washona kuhusu Kiswahili Kupitia Shughuli Mbalimbali za Kijamii ........ 172
4.4.2.1 Lugha Inayopendelewa kwenye Shughuli Rasmi ........ 172
4.4.2.2 Lugha ya Mazungumzo kwa Utawala wa Mitaa ........ 175
4.4.2.3 Lugha ya Mazungumzo baina ya Marafiki ........ 177
4.4.2.4 Lugha Inayopendelewa Kutumika kwenye Biashara ........ 179
4.4.2.5 Lugha ya Masomoni ........ 180
4.4.2.6 Mielekeo ya Washona kuhusu Kiswahili kwenye Burudani ........ 182
4.4.2.7 Mielekeo kuhusu Lugha ya Matumizi ya Jumla katika Maisha ........ 183
4.4.2.8 Matumizi ya Kiswahili kwa Hiari ........ 186
4.4.3 Mielekeo ya Washona kuhusu Kikuyu nchini Kenya ........ 186
4.5 Hitimisho ........ 188
**SURA YA TANO: UDUMISHAJI WA KISHONA NCHINI KENYA** ........ 192
5.0 Utangulizi ........ 192
5.1 Mikakati ya Udumishaji wa Kishona ........ 194
5.1.1 Uzungumzaji Kishona katika Maeneo ya Nyumbani ........ 194
5.1.1.1 Namna ya Kujifunza Kishona katika Maeneo ya Nyumbani na Kanisani ........ 197
5.1.2 Udumishaji wa Lugha kupitia kwa Dini ........ 202
5.1.3 Maandishi ya Kishona katika Dini ........ 205
5.1.4 Juhudi za Wazee katika Udumishaji wa Lugha ........ 207
5.1.5 Udumishaji wa Lugha kupitia Ndoa za Ndani na Ndoa za Nje ya Jamii 208
5.1.6 Kutembeleana miongoni mwa Washona ........ 211

5.1.7 Mikutano ya Kijamii....................................................................213
5.1.8 Sherehe Mbalimbali za Washona ..........................................................215
5.2 Hitimisho ....................................................................................217
**SURA YA SITA**: **MUHTASARI**, **MATOKEO**, **MAPENDEKEZO**, **MCHANGO NA HITIMISHO** ..................................................219
6.0 Utangulizi ...................................................................................219
6.1 Muhtasari.....................................................................................219
6.2 Matokeo ya Utafiti...........................................................................224
6.2.1 Athari za Kiswahili na Kikuyu kwa Kishona ................................................224
6.2.2 Sababu za Washona Kutumia Kiswahili na Kikuyu .......................................225
6.2.3 Mielekeo ya Washona kuhusu Matumizi ya Kiswahili na Kikuyu Nchini Kenya 226
6.2.4 Udumishaji wa Kishona Nchini Kenya.........................................................227
6.3 Mapendekezo..................................................................................228
6.3.1 Kuinua Viwango vya Uthabiti wa Kiisimujamii wa Kishona.........................228
6.3.2 Juhudi za Serikali katika Kuinua Uthabiti wa Kiisimujamii wa Kishona........229
6.3.3 Tafiti za Baadaye kuhusu Kishona ...............................................................230
6.4 Mchango wa Utafiti...........................................................................231
6.5 Hitimisho .....................................................................................232
**MAREJELEO**.......................................................................................235
**KIAMBATISHO A**..................................................................................250
**KIAMBATISHO B**..................................................................................253
**KIAMBATISHO C**..................................................................................254
**KIAMBATISHO D**..................................................................................255
**KIAMBATISHO E**..................................................................................257
**KIAMBATISHO F** .................................................................................262
**KIAMBATISHO G** .................................................................................266
**KIAMBATISHO H** .................................................................................269
**KIAMBATISHO I**...................................................................................270
**KIAMBATISHO J**...................................................................................274
**KIAMBATISHO K** .................................................................................275

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 2.1: Idadi ya lugha katika kila Bara Duniani ... 53
Jedwali 2.2: Nchi za Afrika Zenye Lugha nyingi ... 55
Jedwali 2.3: Kupokezanwa kwa Lugha Baina ya Vizazi Tofauti ... 87
Jedwali 2.4: Asilimia ya Wazungumzaji wa Lugha kwenye Jumuiya Nzima ya Jamiilugha .. 89
Jedwali 2.5: Ruwaza ya Matumizi ya Lugha Katika Maeneo Mbalimbali ya Kijamii ... 90
Jedwali 2.6: Maeneo Mapya ya Matumizi ya Lugha Hasa Vyombo vya Habari ... 92
Jedwali 2.7: Uwepo wa Vitabu Vilivyoandikwa kwa Lugha Husika ... 93
Jedwali 3.1: Lugha Muhimu kwenye Shughuli Rasmi ... 103
Jedwali 3.2: Mifano ya Ukopaji wa Maneno na Sentensi fupi za Kikuyu na Tafsiri yake ya Kishona ... 107
Jedwali4.3: Mifano ya Ukopaji wa Maneno na Sentensi Fupi za Kiswahili na Tafsiri yake ya Kishona ... 107
Jedwali 3.4: Ubadilishaji Msimbo kati ya Kiswahili na Kishona ... 109
Jedwali 3.5: Lugha ya Mazungumzo baina ya Vijana na Mama Mzazi ... 112
Jedwali 3.6: Lugha ya Mazungumzo baina ya Vijana na Baba Mzazi ... 112
Jedwali 3.7: Lugha ya Mazungumzo baina ya Vijana na Babu na Nyanya ... 113
Jedwali 3.8: Lugha ya Matumizi katika Shughuli za Biashara ... 121
Jedwali 3.9: Lugha Inayotumika Kanisani ... 122
Jedwali 4.1: Kiswahili Kama Mojawapo ya Somo Shuleni ... 139
Jedwali 4.2: Matumizi ya Kiswahili katika Maeneo ya Shuleni Nje ya Darasa ... 141
Jedwali 4.3: Kauli za Watafitiwa kuhusu lugha ya Taifa na Lugha Rasmi ... 142
Jedwali 4.5: Matumizi ya Kiswahili katika Kutafuta Riziki ... 148
Jedwali 4.6: Matumizi ya Kiswahili kwa Sababu ya Utambulisho ... 150
Jedwali 4.7: Lugha Inayopendelewa kwenye Shughuli Rasmi ... 173
Jedwali 4.8: Sababu za Kupendelea Kutumia Kiswahili kwenye Shughuli Rasmi ... 173
Jedwali 4.9: Lugha Inayopendelewa Kutumika katika Biashara ... 179
Jedwali 4.11: Sababu za Washona za Kupendelea Kutumia Kikuyu ... 187
Jedwali 5.1: Jinsi Watoto na Vijana Hujifunza Kishona ... 198

## ORODHA YA BAA-GRAFU NA PAI-CHATI


Baa-grafu 3.1: Lugha Inayofahamika vyema kwa Washona ........ 101
Baa-grafu 3.2: Ukopaji wa Maneno ya Kiswahili kwa Kishona ........ 104
Baa-grafu 3.3: Maneno ya Kikuyu kwenye Kishona ........ 105
Pai-chati 3.1: Lugha ya Matumizi baina ya Ndugu ........ 115
Baa-grafu 3.4: Lugha ya Mazungumzo na Mzee wa Kijiji ........ 117
Baa-grafu 3.5: Lugha ya Mazungumzo baina ya Marafiki ........ 119
Baa-grafu 3.6: Lugha Nyingine Inayotumika Kanisani mbali na Kishona ........ 123
Baa-grafu 3.7: Lugha inayotumika shuleni ........ 125
Baa-grafu 3.8: Lugha Muhimu kwa Shughuli za Kitamaduni ........ 126
Baa-grafu 3.9: Lugha Wanayotumia Watoto katika Maeneo ya Nyumbani ........ 128
Baa-grafu 3.10: Lugha Wanayotumia Vijana katika Maeneo ya Nyumbani ........ 128
Baa-grafu 3.11: Lugha Wanayotumia Wazee katika Maeneo ya Nyumbani ........ 129
Baa-grafu 3.12: Lugha Nyingine Zinazozungumzwa na Washona ........ 131
Baa-grafu 3.13: Kiwango cha Umilisi wa Kishona ........ 133
Baa-grafu 4.1: Lugha Inayopendelewa katika Kuzungumza na Mzee wa Kijiji ........ 176
Pai-chati 4.1: Lugha Inayochukuliwa kuwa Muhimu katika Mazungumzo na Marafiki .... 178
Baa-grafu 4.2: Lugha Inayochukuliwa kuwa Muhimu Masomoni ........ 181
Baa-grafu 4.3: Lugha Inayopendelewa Kutumika kwenye Burudani ........ 183
Baa-grafu 4.4: Lugha Inayopendelewa Kutumika kwenye Shughuli Muhimu katika Maisha ...... 184
Baa-grafu 5.1: Maeneo ya Vijana na Watoto kujifunza Kishona ........ 196
Baa-grafu 5.2: Kiwango cha Umilisi wa Kishona baina ya Vijana ........ 200
Pai-chati 5.1: Matumizi ya Kishona Kanisani ........ 204

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| **ABS** | **:** | Australian Bureau of Statistics. |
| **BBC** | **:** | British Broadcasting Corporation. |
| **KT** | **:** | Keshatajwa. |
| **KHRC** | **:** | Kenya Human Rights Commission. |
| **KNBS** | **:** | Kenya National Bureau Of Statistics. |
| **$L_1$** | **:** | Lugha ya kwanza. |
| **$L_2$** | **:** | Lugha ya pili. |
| **$MT_1$** | **:** | Mtu wa kwanza. |
| **$MT_2$** | **:** | Mtu wa pili. |
| **NACOSTI** | **:** | National Commission for Science, Technology and Innovation. |
| **SIL** | **:** | Summer Institute of Linguistics. |
| **SPSS** | **:** | Statistical Package for the Social Sciences. |
| **UNESCO** | **:** | United Nations Education Scientific and Cultural Organization. |
| **UNHCR** | **:** | United Nations High Commission for Refugees. |

## UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU

| | |
|---|---|
| **Athari:** | Matokeo yanayotokana na mtagusano lugha mbili tofauti. |
| ***Dare* :** | Kamati inayochaguliwa na Washona ili kuongoza jamii ya Washona. |
| **Demografia:** | Hali ya kitakwimu au idadi ya wanajamiilugha fulani. |
| ***Gospel of God*:** | Kanisa la Washona linalopatikana kando na Chuo Kikuu cha *Daystar* bewa la Nairobi kwenye barabara ya *Valley Road*. |
| ***Hwahwa /doro*:** | Aina ya mvinyo au Pombe inayotumiwa na wazee wa Kishona. |
| **Jamiilugha:** | Watu wanaoongea lugha moja na wanakaa katika eneo moja. |
| **Kishona:** | Lugha inayozungumzwa na Washona. |
| **Mtagusano:** | Mwingiliano wa lugha kati ya jamiilugha tofauti zinazokaa pamoja. |
| ***Musha*:** | Boma ya mtu fulani. |
| ***Mwari*:** | Jina linalotumiwa na Washona la kumwita Mungu. |
| ***Sadza*:** | Ugali unaopikwa na unga wa mahindi. |
| **Uhamaji:** | Hali ya jamiilugha moja kuanza kuacha matumizi ya lugha fulani kuanza kutumia lugha ya pili ambayo si yao asilia. |
| **Udumishaji :** | Juhudi za kuhifadhi lugha za jamiilugha fulani. |

**Uthabiti wa Kiisimujamii**: Uwezo wa jamiilugha fulani wa kudumisha na kulinda uwepo na utambulisho wa utamaduni wao kupitia kwa lugha yao asilia.

**Washona:** Kabila la Kibantu linaloishi nchini Kenya ambalo asili yake ni nchini Zimbabwe.

# IKISIRI

Utafiti huu ulilenga kuchunguza athari za Kiswahili na Kikuyu kwa uthabiti wa Kiisimujamii wa Kishona nchini Kenya. Shona ni kabila mojawapo la Wabantu ambao asili yao ni nchini Zimbabwe na walifika nchini Kenya zaidi ya miaka sitini iliyopita kama wamishenari. Wameishi nchini Kenya kwa miaka hiyo yote bila utambulisho hadi mwaka wa 2020 ambapo walipewa uraia wa kuwa Wakenya. Kufikia sasa, Washona wametagusana na jamiilugha mbalimbali hapa nchini katika Kaunti ya Kiambu inayojulikana kwa wingilugha. Mtagusano lugha unapotokea, lugha husika huathirika kwa viwango mbalimbali: kifonetiki, kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia, kisemantiki na hata kiisimujamii. Hivyo katika kuchunguza athari hizi, malengo yafuatayo yaliongoza utafiti huu: Kuchunguza athari za mtagusano wa Kiswahili na Kikuyu kwa Kishona, kuhakiki sababu zinazopelekea Washona kutumia Kiswahili na Kikuyu katika maeneo yao ya kijamii, kudhihirisha mielekeo yao katika matumizi ya Kiswahili na Kikuyu na kubainisha iwapo Washona wamefaulu kudumisha lugha yao asilia nchini Kenya au la. Nadharia ya Uthabiti wa Kiisimujamii wa lugha iliyoasisiwa na Giles, Bourhis na Taylor (1977) na kuendelezwa na Landweer (2000) na nadharia ya Uzalishaji Kijamii ya Bourdieu (1977), zilitumika katika kuchanganua data ya utafiti. Utafiti huu ulihusisha mawanda mawili ambayo ni utafiti wa maktabani na wa nyanjani. Utafiti wa maktabani ulihusisha kudurusu miswada, vitabu, machapisho na majarida yanayoangazia uthabiti wa kiisimujamii wa lugha, nadharia za uthabiti na udumishaji wa lugha pamoja na mbinu za utafiti. Kabla ya utafiti wa nyanjani, utafiti awali ulifanyika ili kutathmini ubora wa vifaa vya ukusanyaji data. Utafiti wa nyanjani ulifanyika katika makazi ya wanajamiilugha wa Kishona ili kupata data ya moja kwa moja iliyojibu maswali ya utafiti. Jumuiya ya utafiti ilikuwa kabila la Washona wanaoishi katika mitaa mitano ya kaunti ya Kiambu. Sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kimaksudi na kwa njia elekezi ili kumpa mtafiti uhuru wa kutathmini na kuchagua wahojiwa ambao walimpa data inayofaa kutimiza malengo ya utafiti. Mbinu zilizotumiwa katika ukusanyaji data ni pamoja na mahojiano, utazamaji au uchunzaji, mijadala ya vikundi vidogo vidogo na maswali mepesi yaliyoandaliwa awali. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa kutumia mbinu changamano. Matokeo yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo, takwimu na asilimia huku yakiongozwa na nadharia mbili za utafiti. Kufuatia juhudi za UNESCO za kudumisha lugha asilia, utafiti huu utakuwa wa manufaa kwa taifa la Kenya na mataifa mengine kwa kuwa umeongezea data muhimu katika kuhifadhi utamaduni wa Washona na mielekeo ya udumishaji kwa lugha za kabila mbalimbali.

## ABSTRACT

This study aimed at investigating the effect on the Shona language as a result of contact with Kiswahili and Kikuyu languages in Kenya. Shona is a Bantu language whose speakers are predominantly based in Zimbabwe. In the 1950s, a considerable number of Shona speakers immigrated to Kenya, as missionaries and have lived for over 60 years, albeit with no recognition as Kenyan citizens. During this period, the Shona ethnic community have been in contact with speakers of different Kenyan languages. The community has settled in five settlements of Kiambu county which are known for multilingualism. During intense contact between two languages, there is bound to be some linguistic change noticeable in the languages involved as a consequence of the contact. The changes may be lexical, morphological, syntactic, semantic and sociolinguistic levels. In view of this, this research was guided by the following research objectives: Identify the effects of language contact between Kiswahili and Kikuyu language on the Shona language, investigate reasons for using Kiswahili and Kikuyu language among the Shona people in their societal domains, to interrogate their attitudes towards use of Kiswahili and Kikuyu language and finally to assess the maintainance of Shona language among the Shona people living in Kiambu county. The study used Ethnolinguistic Vitality theory which was propounded by Giles, Bourhis and Taylor (1977) and improved by Landweer (2000) and Social Reproductive theory of Bourdieu (1977) to analyse the research data. The research involved both secondary and primary data. The secondary data was obtained from review of library and archival records. A pilot study was done to evaluate the validity of the data collection tools. Primary data was drawn from field as the researcher visited residential areas of Shona people to get first hand information in pursuit of research objectives. Target population was the Shona people who live in five settlements of Kiambu county. Purposive sampling technique was used since it gave the researcher the freedom to choose the sample which gave the required data for purposes of achieving research objectives. The researcher used questionaires, interviews, observation and small group discussions to collect data as guided by research objectives. The collected data was analyzed and presented using the descriptive and numeric method and was guided by the two research theories. Following the guidelines from UNESCO in maintaining endangered indigenous languages, this study is important to the Kenyan nation and the global community interested in maintainance of language diversity because it provides insight in the efforts.

# SURA YA KWANZA: MISINGI YA UTAFITI

## 1.0 Utangulizi

Tasnifu hii inashughulikia athari za Kiswahili na Kikuyu kwa uthabiti wa kiisimujamii wa Kishona nchini Kenya. Sura ya kwanza imeshughulikia usuli wa utafiti ambapo athari mbalimbali za mtagusano lugha zimebainishwa. Uthabiti wa kiisimujamii umefafanuliwa ili kuweka wazi suala la utafiti. Suala la utafiti limewekwa wazi huku malengo yaliyoongoza utafiti huu yakitajwa. Sababu za kuchagua mada zimewekwa bayana pamoja na mipaka ya utafiti. Nadharia mbili zilizoongoza utafiti huu zimebainishwa na mbinu za utafiti pia zimeshughulikiwa katika sehemu hii.

## 1.1 Usuli wa Utafiti

Mtagusano lugha ni mwingiliano wa lugha tofauti katika jamiilugha tofauti zinazokaa pamoja. Thomason (2000) na Weinreich (1953) wanasema kuwa mambo yanayowezesha mtagusano lugha kufaulu ni kama vile ujirani mwema kati ya wanajamiilugha tofauti, kufanya biashara, elimu na hata ndoa baina ya jamiilugha hizo.

Mtagusano lugha huzua athari mbalimbali kwenye lugha husika. Athari ya kwanza ya mtagusano lugha ni wingilugha ambao hutokea panapokuwa na utangamano wa wanajamiilugha tofauti katika jamii. Wingilugha ni hali ya wanajamii ya kujifunza na kuzungumza zaidi ya lugha moja hasa lugha zilizo karibu nao. Kulingana na Mekacha (2011) na Thomason (2000), wingilugha hutokea pale ambapo wanajamiilugha wanaweza kujifunza lugha moja iliyo na hadhi ya juu katika jamii na kuanza kuitumia lugha hiyo kando na lugha yao asilia katika shughuli zao za kila siku.

Athari ya pili ya mtagusano lugha ni kuzuka kwa hadhi mbalimbali za lugha. Hadhi ya lugha ni nafasi ambayo lugha fulani zimepewa katika jamii ama na asasi za kiserikali, jamii, au wazungumaji wake. Appel na Muysken (2005) na Heine (1992) wanasema kwamba lugha iliyo na hadhi ya juu ni ile ambayo inamnufaisha mzungumzaji katika biashara, maingiliano ya kijamii, kazini na hata kwenye siasa. Wanajamiilugha wakipenda lugha tofauti na ile yao asilia na kuanza kujifunza na kuitumia katika shughuli zao mbalimbali za kijamii, basi kuna uwezekano wa kuhamia lugha hiyo mpya au watumie lugha zote mbili. Kupungua kwa matumizi ya lugha asilia katika jamii na kupendelea matumizi ya lugha mpya ni ishara ya uhamaji wa lugha.

Fishman (1991) anasema kuwa uhamaji wa lugha ni hali ambayo wazungumzaji wa lugha fulani huacha kutumia lugha yao asilia na badala yake huanza kutumia lugha nyingine katika mawasiliano na shughuli zao za kila siku. Uhamaji wa lugha huanza kuonekana wakati matumizi yake katika jamii hupunguka. Appel na Muysken (2005) na Mathooko (2007) wanasema kuwa matumizi ya lugha yanapoanza kupunguka katika jamii, lugha hiyo huanza kupoteza uthabiti wake kiisimujamii. Hali hiyo husababisha kubadilishana nafasi ya lugha ya kwanza ($L_1$) na lugha ya pili ($L_2$) kama njia ya kimsingi ya mawasiliano na kutoa mafunzo katika jamii. Jamii inaanza kupendelea kutumia $L_2$ na kuacha kutumia $L_1$ ambapo upendeleo huo huanza na ukopaji wa maneno kutoka $L_2$ kufuatia mielekeo chanya kuihusu.

Mielekeo ya lugha ni jambo la kijamii ambalo hutokana na mazingira ya wanajamii, tajriba zao na matarajio yao. Mielekeo mbalimbali ya lugha huzua mapendeleo kuhusu lugha fulani hasa katika jamii za wingilugha. (Garrett, Coupland na Williams 2003;

Allport 1954; Ryan na Giles 1982 na Garrett 2010). Mazingira ya wanajamiilugha huzua aina mbili za mielekeo kuhusu lugha; mielekeo chanya ya lugha na mielekeo hasi ya lugha. Mielekeo hasi ya lugha hufanya lugha fulani kupoteza uthabiti wake wa kiisimujamii ilhali mielekeo chanya ya lugha hupelekea wanajamii kudumisha lugha yao na kuifanya kuwa na uthabiti wa kiisimujamii.

Uthabiti wa Kiisimujamii wa lugha, kulingana na Giles, Bourhis na Taylor (1977) ni uwezo wa jamiilugha fulani wa kudumisha na kulinda uwepo na utambulisho wa utamaduni wao kupitia kwa lugha yao asilia. Wolck (2004) anasema kwamba jamiilugha nyingi huwa na mikakati ya kudumisha tamaduni zao kupitia kwa lugha zao asilia. Mikakati hii ni kama vile kuitumia lugha yao katika nyanja mbalimbali na mazingira mbalimbali ya kijamii, kuipenda na kuienzi lugha yao, kurithisha vizazi vyao na kuweka sera za lugha kupitia kwa katiba ya nchi husika.

Katiba ya Kenya ya mwaka 2010 sura ya pili, kipengele cha (7a) inafafanua kwamba serikali ya Kenya itakuza na italinda lugha tofauti za wananchi wa Kenya; (7b) na italinda na kustawisha matumizi ya lugha za kiasili. Katika kusherehekea siku kuu ya Jamhuri ya mwaka 2020, Rais wa nne wa jamhuri ya Kenya, Uhuru Kenyatta, aliwapa uraia Washona ambao wanaishi katika kaunti ya Kiambu. Hii ni kufuatia ombi lao la kupewa uraia baada ya kuishi Kenya kwa zaidi ya miaka hamsini bila uraia wala utambulisho. Hii inamaanisha kwamba, Washona wamekuwa raia wa Kenya na wako huru kupata huduma zote za kimsingi kama vile elimu, afya na huduma nyinginezo. Pia, wanafaa kupata usaidizi wa kudumisha lugha yao asilia kupitia asasi mbalimbali nchini Kenya kulingana na katiba ya Kenya ya mwaka 2010 kwa kuwa lugha yao sasa ni

mojawapo ya lugha asilia za Kenya. Utafiti awali unaonyesha kuwa, asasi ya pekee ambayo imekuwa ikiwasaidia kuendeleza lugha yao ni kupitia ibada yao katika kanisa lao la *Gospel of God* na matumizi ya lugha yao katika maeneo ya nyumbani tu.

Ripoti ya KHRC na UNHCR (2019) inaeleza kwamba Washona wa Kenya wamekuwa wakitangamana na kutagusana na wanajamiilugha wengi walio na lugha tofauti ikiwemo Kiswahili na Kikuyu. Kuna uwezekano kwamba mtagusano wa Washona na lugha maarufu nchini Kenya kama vile Kiswahili, umeleta mabadiliko kwa kiasi fulani katika lugha yao. Mabadiliko haya ya lugha yanaweza kuwa kwa viwango tofauti na kwa vizazi tofauti. Blythe na Croft (2012) wanaeleza kuwa mabadiliko ya lugha hufanyika wanajamiilugha wanapoanza kuacha kutumia lugha yao polepole na kuanza kutumia lugha nyingine kwenye maeneo mbalimbali katika jamii. Kauli hii inatupeleka katika suala la utafiti.

### 1.1 Suala la Utafiti

Kama ilivyotajwa awali, Washona wamekuwa wakitangamana na lugha za Kiswahili na Kikuyu hapa nchini Kenya kwa zaidi ya miaka hamsini. Mtagusano lugha ni tukio la kawaida katika jamii na hali hii inapotokea kwa muda mrefu, huwa kuna mabadiliko ambayo hushuhudiwa hasa ikizingatiwa kwamba wanaotangamana si wazungumzaji wa lugha moja. Mapitio ya tafiti mbalimbali yanaonyesha kwamba utafiti kuhusu athari za Kiswahili na Kikuyu kwa uthabiti wa kiisimujamii wa Kishona nchini Kenya haujashughulikiwa. Baadhi ya tafiti hizi ni kama vile: Utafiti wa Machakanja (2006) uliolinganisha sitiari za Kiingereza na za Kishona katika mazingira yaliyo sawa ya kijamii, utafiti wa Akello (2021), Odenyo na Ntinyari (2021) na Wagalla (2019)

uliojikita katika changamoto za kutafuta utambulisho kwa Washona nchini Kenya, Ndubi (2017) na Muchena na Jakaza (2022) waliochunguza changamoto za kuhifadhi lugha ya Kishona nchini Kenya na ripoti ya KHRC na UNHCR (2019) kuhusu uraia wa Washona nchini Kenya na ukabainisha kwamba Washona wanazungumza kwa ufasaha lugha za Kiswahili na Kikuyu katika maeneo yao ya kijamii. Hivyo basi utafiti huu uliziba hili pengo kwa kuchunguza athari za Kiswahili na Kikuyu kwa uthabiti wa Kiisimujamii wa Kishona nchini Kenya na iwapo Washona wameweza kuidumisha lugha yao au la.

## 1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu kimsingi uliongozwa na malengo yafuatayo:

i. Kuchunguza athari za mtagusano wa Kiswahili na Kikuyu kwa Kishona.
ii. Kuhakiki sababu zinazopelekea Washona kutumia Kiswahili na Kikuyu katika maeneo yao ya kijamii.
iii. Kudhihirisha mielekeo ya Washona katika matumizi ya Kiswahili na Kikuyu nchini Kenya.
iv. Kubainisha iwapo Washona wamefaulu kudumisha lugha yao asilia nchini Kenya au la.

## 1.4 Maswali ya Utafiti

i. Athari za mtagusano wa Kiswahili na Kikuyu kwa Kishona ni zipi?
ii. Je, ni sababu zipi zinazopelekea Washona kutumia Kiswahili na Kikuyu katika maeneo mbalimbali ya kijamii?

iii. Mielekeo ya Washona ni ipi katika matumizi ya Kiswahili na Kikuyu nchini Kenya?

iv. Washona wamefaulu vipi kudumisha lugha yao asilia nchini Kenya?

**1.5 Sababu za Kuchagua Mada**

Ripoti ya KHRC na UNHCR (2019) inasema kuwa Washona wa Kenya wamekuwa wakitangamana na lugha rasmi ya Kiswahili na wanajamiilugha wengine kama vile Wakikuyu nchini Kenya tangu miaka ya 1950. Tafiti nyingine kama vile Machakanja (2006), Odenyo na Ntinyari (2021), Wagalla (2019), Muchena na Jakaza (2022), zimefanywa kuhusu Washona nchini Kenya ila hakuna utafiti ambao umefanywa kuhusu kuchunguza athari za mtagusano wa Kiswahili na Kikuyu kwa uthabiti wa kiisimujamii wa Kishona nchini Kenya. Ugunduzi huu ulichochea sababu ya kwanza ya kuchagua mada kwa kuwa Washona walipewa utambulisho na aliyekuwa Rais wa nne wa Kenya, Uhuru Kenyatta, tarehe 12/12/2020 baada ya kuishi nchini Kenya kwa zaidi ya miongo sita.

Ripoti ya KHRC na UNHCR (2019) inasema kwamba Washona wa Kenya wanazungumza Kiswahili vyema katika shughuli zao za kila siku. Ripoti hii ya KHRC na UNHCR (kt.) ilichochea sababu ya pili ya utafiti huu ambayo ilikuwa kuchunguza sababu zinazowapelekea Washona wa Kenya kutumia Kiswahili na Kikuyu katika maeneo yao ya kijamii.

Agoya (2012) anasema kwamba shughuli za uhamaji kutoka vijijini hadi mijini zimepelekea lugha asilia kupuuziliwa mbali na nafasi yao kuchukuliwa na lugha maarufu kama vile Kiswahili. Lugha asilia zimebaki kutumika katika maeneo yasiyo

rasmi kama vile maeneo ya nyumbani na vijijini. Wazo hili la Agoya lilipelekea sababu ya tatu ya kuchagua mada hii ya kutaka kudhihirisha mielekeo ya Washona katika matumizi ya Kiswahili na Kikuyu nchini Kenya.

Rottland na Okombo (1992) wanasema kuwa Kenya ina lugha kadha ambazo zina hatari ya kutoweka kwa sababu ya mtagusano na lugha jirani zilizo na wazungumzaji wengi. Lugha  kama vile Suba, Terik, El molo, Rendile Ogiek, Boni, Burji, Bong'om na Njemps zimo katika hatari ya kuangamia kabisa. Lugha ikiangamia, utamaduni wa jamiilugha hiyo pia hufa na kupotea kabisa. Hali hii ilichangia sababu ya nne ya kufanya utafiti huu ili kubaini iwapo Washona wamefaulu kudumisha lugha yao asilia nchini Kenya au la kwa kuwa wanatangamana na jamiilugha maarufu na kubwa kiidadi nchini Kenya.

Katika Karne hii ya ishirini na moja, mashirika mbalimbali yamechukua jukumu la kuhimiza jamiilugha mbalimbali kuhusu kuhifadhi utamaduni na kudumisha lugha zao ili kuzuia kutoweka kwa lugha asilia. Shirika la UNESCO katika kongamano lililofanyika mjini Paris (Septemba hadi Oktoba 2003) liliamua kuhamasisha jamii mbalimbali ulimwenguni kuhusu umuhimu wa kuhifadhi utamaduni. Katika kongamano hilo la UNESCO, kipengele cha lugha kiliangaziwa kama sehemu kuu ya utamaduni ambapo lazima ihifadhiwe ili kudumisha tamaduni za jamii ulimwenguni.

Kenya ni miongoni mwa nchi ambazo zimejitosa katika juhudi za kuhifadhi utamaduni wake kufuatia sera ya UNESCO kuhusu udumishaji wa lugha. Hili linadhihirika kupitia katiba ya Kenya ya mwaka wa 2010.  Kufuatia juhudi hizi, sababu nyingine ya utafiti huu ilikuwa kuongeza data muhimu katika kuhifadhi utamaduni wa kabila la Washona

na lugha yao kwa kuwa lugha yao inatambulika kama lugha mojawapo ya lugha za Kenya. Sababu hizi ziliashiria upeo na mipaka ya utafiti.

### 1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulishughulikia athari za Kiswahili na Kikuyu kwa uthabiti wa Kiisimujamii wa Kishona nchini Kenya. Lugha tatu zilichaguliwa katika utafiti huu. Lugha ya kwanza ilikuwa Kishona inayozungumzwa na Washona wa Kenya. Ingawa wana asili yao nchini Zimbabwe, lugha ya Washona wa Zimbabwe haikuchunguzwa kwa sababu ya umbali na gharama inayohusiana na usafiri wa mbali. Lugha ya pili iliyochaguliwa ilikuwa Kiswahili kwa sababu ni mojawapo ya lugha asilia nchini Kenya, ni lugha rasmi, ni lugha ya kitaifa na kimataifa kufuatia kutambuliwa na shirika la UNESCO na kupewa Julai 7 kila mwaka kama siku ya kuienzi. Lugha ya tatu ilikuwa Kikuyu kwa sababu mbili: sababu ya kwanza ni kuwa maeneo ambayo Washona wanaishi wamezungukwa na idadi kubwa ya wazungumzaji wa lugha ya Kikuyu. Odenyo na Ntinyari (2021) na Kamau (2015) wanasema kwamba lugha inayotumika kwa wingi katika Kaunti ya Kiambu ni Kikuyu kwa kuwa wakazi wengi ni wa jamii ya Wakikuyu. Sababu ya pili ya kuchagua Kikuyu ni kwamba, kulingana na Mulinya (2020) na ripoti ya KHRC na UNHCR (2019), Washona wa Kwanza kufika nchini Kenya mwaka wa 1959 walikaribishwa na kufadhiliwa na Wakikuyu katika eneo la Ngong na eneo la Juja kabla ya kuhamia maeneo ya Kinoo, Kikuyu, Kiambaa, Gitaru na Githurai.

Utafiti huu ulijihusisha pia katika kudhihirisha mielekeo mbalimbali ya Washona kuhusu matumizi ya Kiswahili na Kikuyu katika maeneo yao ya kijamii. Garrett (2010) na Bartram (2010) wanafafanua mielekeo ya lugha kuwa ni hisia za mtu au watu kuhusu

lugha yao au lugha ya watu wengine katika mazingira ya wingilugha ambayo huchochewa na vigezo mbalimbali ikiwemo mazingira ya wanajamiilugha na mahusiano yaliyomo katika jamiilugha husika. Mielekeo ya Washona kuhusu Kiswahili na Kikuyu ilichunguzwa kwa vizazi vyote kupitia matumizi ya lugha hizi katika maeneo mbalimbali ya Kijamii.

Mikakati ya udumishaji wa Kishona ilishughulikiwa katika utafiti huu. Batibo (2005) na Fishman (1989), wanasema kuwa uwezo wa kudumisha lugha hubainika kupitia matumizi yake miongoni mwa vijana na watoto, matumizi yake katika maeneo mbalimbali ya kijamii pamoja na matumizi kwenye shughuli mbalimbali za jamii. Utafiti huu ulishughulikia mikakati mbalimbali ya kudumisha Kishona nchini Kenya licha ya shinikizo kutoka lugha maarufu zinazowazunguka Washona kwenye mitaa wanamoishi katika Kaunti ya Kiambu.

Kieneo, Utafiti huu ulijikita katika maeneo ya Kiambaa, Kinoo, Kikuyu, Gitaru na Githurai katika kaunti ya Kiambu ambayo ni jirani ya jiji la Nairobi. Maeneo haya ya mpaka wa Kiambu na Nairobi yanajulikana kwa wingilugha lakini kando na Kiswahili, lugha ya Kikuyu inatumika sana kwa vile wakazi katika kaunti hii jirani ni kutoka jamii ya Wakikuyu, anavyosema Kamau (2015). Maeneo haya yalichaguliwa kwa sababu Washona wa kwanza ambao walikuja Kenya kama wamishenari waliishi maeneo ya Kiambaa, na baaadaye walipoendelea kuongezeka wakahamia maeneo ya Kikuyu, Kinoo, Gitaru na Githurai. Miji mingine nchini Kenya haikushughulikiwa kwa kuwa Washona wa kwanza waliowasili Kenya kuanzia mwaka wa 1957 hadi 1959 kama wamishenari waliishi katika sehemu hizi za kaunti ya Kiambu.

Utafiti huu uliwahusisha Washona wa umri wote kuanzia wakongwe hadi watoto kuanzia mwaka mmoja. Hii ni kwa sababu idadi ya Washona haizidi 2500 na pia mtagusano lugha unapofanyika, mabadiliko huanza kuonekana kwa vizazi tofauti vya jamiilugha husika. Pia, Washona wa umri wote walihusishwa ili kupata sampuli tosha katika utafiti huu. Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili zilizojadiliwa kwenye sehemu ya 1.7 kama ifuatavyo.

## 1.7 Nadharia za Utafiti

Uchanganuzi wa yaliyoandikwa kuhusu mada umebainisha kuwa kuna athari mbalimbali za lugha zinazotokana na mtagusano wa jamiilugha tofauti. Athari hizi ni pamoja na ukopaji wa maneno, uhamishaji msimbo, wingilugha, mielekeo tofauti kuhusu lugha, hadhi mbalimbali za lugha, mabadiliko na uhamaji wa lugha, na kufa kwa lugha. (Weinreich 1953, Thomason na Kaufman 1988, Heine 1992, Obiols 2002, Appel na Musyken 2005, Chakrani 2011, Mathooko 2007, Kamau 2015, Ngugi 2014, na Ngure 2012). Vile vile imebainika kuwa uthabiti wa kiisimujamii ni jumla ya juhudi zote za jamiilugha fulani za kudumisha utamaduni wao kupitia kwa lugha yao. (Fishman 1989, Landweer 2000, Batibo 2005 na Sangili 2019).

Kutokana na mawazo haya, nadharia mwafaka zilizotumika kwenye utafiti huu ni nadharia ya uthabiti wa Kiisimujamii wa lugha ya Giles, Bourhis na Taylor (1977) na kuendelezwa na Landweer (2000) na nadharia ya uzalishaji wa kijamii iliyoendelezwa na O’Riagain (1994). Nadharia ya uthabiti wa kiisimujamii itafafanuliwa kwanza.

### 1.7.1 Nadharia ya Uthabiti wa Kiisimujamii wa Lugha

Nadharia hii ilianzishwa na Giles, Bourhis na Taylor mwaka wa 1977. Wanaisimujamii hawa walifafanua uthabiti wa kiisimujamii kuwa ni kile kinachofanya jamiilugha kukaa pamoja katika jamii ya wingilugha. Wao walisema kuwa, uthabiti wa jamiilugha hutegemea viashiria vitatu: hadhi ya lugha husika, demografia ama idadi ya wanajamiilugha na usaidizi au juhudi za taasisi za kiserikali kama vile kwenye elimu, huduma mbalimbali za serikali, dini na vyombo vya habari.

Hadhi ya jamiilugha fulani hutegemea mpangilio wao kijamii, uwezo wa kiuchumi au kiwango cha uchumi na historia ya jamiilugha hiyo. Paulston (1994) anasema kuwa iwapo jamiilugha iliyo na watu wachache iko kwenye kiwango sawa cha kiuchumi na jamiilugha iliyo na idadi kubwa ya wazungumzaji, basi jamiilugha hiyo ina nafasi nzuri ya kudumisha lugha yao. Isitoshe, wakati wanajamiilugha wamekubalika katika jamii na wanajamiilugha iliyo na idadi kubwa ya wazungumzaji, udumishaji wa lugha yao huwa ni jambo rahisi sana.

Demografia ya jamiilugha inaashiria idadi ya wanaozungumza lugha husika, mipangilio yao katika mtandao wao wa kijamii, utaratibu katika ndoa zao na uhamaji au uhamiaji wao. Holmes (2001) anasema kwamba makazi yaliyo na wazungumzaji wengi wa lugha fulani huifanya lugha hiyo kuwa thabiti kwa sababu ya idadi yao na kule kuizungumza kila wakati. Nao Al-khatib na Alzoubi, (2009) wanasema kwamba nguvu zinazotokana na wingi wa wanajamiilugha fulani hutumika kama chombo cha kuhalalisha uwezo wa jamiilugha au makundi ya lugha katika kudhibiti taasisi muhimu za kijamii kuhusu lugha yao kwenye jamii zilizo na wanalugha tofauti.

Kiashiria cha tatu muhimu katika uthabiti kiisimujamii wa lugha ni kutambulika kwake katika jamii na usaidizi wa taasisi za kiserikali na zile za kijamii kuhusu lugha husika. Hii inahusu kujulikana na kutumika kwa lugha fulani kwa mitandao ya kijamii, matumizi yake kwenye elimu na mazingira rasmi kama vile shuleni, matumizi ya lugha hiyo katika huduma muhimu za jamii kama vile idara za afya, idara ya ulinzi, utawala na katika ibada. Mirvahedi, (2014) anasema kwamba lugha isipotumika katika mitandao ya kijamii, elimu na serikalini, lugha hiyo inakosa kudumishwa na kuanza kupotea polepole. Mirvahedi (kt.) anatoa mifano ya lugha ya Kiarabu ambayo inaungwa mkono na taasisi za kielimu Marekani, Uingereza na Australia kupitia kwa shule za Kiislamu ambazo ndizo rasilimali za uthabiti wa lugha ya Kiarabu.

Mwanaisimujamii Landweer (2000), aliendeleza nadharia hii ya uthabiti wa Kiisimujamii wa lugha kwa kupendekeza mihimili minane ifuatayo inayopima uthabiti wa lugha.

i. Umbali wa jamiilugha kutoka mijini au vijijini.
ii. Maeneo mbalimbali ya kijamii panapotumika lugha na wanajamiilugha.
iii. Aina na viwango vya uhamishaji wa msimbo.
iv. Idadi ya wanajamiilugha wanaozungumza lugha husika.
v. Mtawanyiko wa wanajamiilugha husika katika mtandao wa kijamii.
vi. Mtazamo ulioko kwenye jamii kuhusu wanajamiilugha husika na wanajamiilugha wengine kuhusu lugha husika.
vii. Hadhi iliyopewa lugha husika katika jamii.
viii. Misingi imara na halali ya kiuchumi ya jamiilugha husika.

#### 1.7.1.1 Umbali wa Jamiilugha Kutoka Mijini au Vijijini

Jamiilugha inapokuwa mbali na mijini panapozungumzwa lugha nyingi na tofauti, jamiilugha hiyo huweza kukuza lugha yao kwa kuwa hakuna shinikisho la lugha nyingine na pia hakuna maingiliano mengi ya kitamaduni yanayowezesha mabadiliko katika lugha yao asilia. Maeneo yaliyo na watu wengi kama vile asasi za kiserikali, shuleni, hospitalini, migodini, mashamba makubwa na maeneo ya misheni mbalimbali huwa na athari kwa lugha husika kwa sababu ya maingiliano na lugha tofauti. Vivyo hivyo, jamiilugha iliyo karibu na mjini haina budi kuingiliana na lugha mbalimbali na hivyo basi inaathiriwa na wingilugha wa mijini. Hali hii huleta mabadiliko katika lugha husika na kukosa uthabiti wa Kiisimujamii.

Jambo lingine linaloathiri uthabiti wa lugha ni urahisi na mbinu za kusafiri hadi miji mikuu. Hii inamaanisha kuwa, iwapo wanajamiilugha wana mbinu rahisi za kufika mijini kwa shughuli za biashara, elimu na kazi, ni rahisi sana lugha yao kuathiriwa na lugha nyingine zinazozungumzwa kwenye miji husika anavyosema Landweer (2000). Kigezo hiki cha urahisi wa kufika mijini na kurudi kwa shughuli mbalimbali, hugawa wanajamiilugha katika makundi yafuatayo:

i. Jamiilugha zilizo vijijini na hazina uhusiano na jamiilugha zilizo mijini.
ii. Jamiilugha ambazo zinahusiana kwa kiwango kidogo na jamiilugha zinazoishi mijini
iii. Jamiilugha zinazohusiana kwa karibu sana na jamiilugha za mijini.
iv. Jamiilugha ambazo huishi mijini.

Utafiti huu ulijihusisha na jamiilugha ambayo huishi mjini kwa sababu kabila la Washona wa Kenya wanaishi kwenye mitaa mitano ya Kaunti ya Kiambu ambayo ni Kiambaa, Kinoo, Kikuyu, Githurai na Gitaru. Washona hawa, wametengwa na umbali kutoka kwa jamiilugha yao asilia nchini Zimbabwe walikotoka. Kwa sasa wamekaribiana na kutangamana na jamiilugha za Kenya katika kaunti ya Kiambu ambayo ni jirani ya jiji kuu la Nairobi. Mtagusano huu unaweza kuwa umeathiri lugha yao ya Kishona kwa vile Kiswahili na Kikuyu ndizo lugha zilizo karibu sana nao na wanazitumia kwa shughuli zao za kila siku.

#### 1.7.1.2 Maeneo Mbalimbali ya Kijamii Panapotumika Lugha na Wanajamiilugha

Fishman (1972b) na Chambers na Natalie (2013) wanasema kwamba lugha ikitumika sana katika maeneo mbalimbali ya jamii ya watu fulani, inaimarika na kuwa thabiti. Lugha hutumiwa katika maeneo ya nyumbani ambapo watu wa familia moja huishi, sherehe za kitamaduni kama vile sherehe za ndoa, mazishi, kuzaliwa na kupewa jina kwa mtoto, sherehe za jandoni, vita, maabadini, sherehe mbalimbali za ukulima na kadhalika. Lugha pia hutumiwa kwa shughuli za kijamii kama vile elimu, michezo mbalimbali, biashara, na hata maamuzi ya kesi. Landweer (2000) anasema kwamba maeneo ya nyumbani ndio msingi wa matumizi ya lugha ya mama na anaendelea kusema kwamba kuanza kupunguka kwa matumizi ya lugha ya mama katika maeneo ya kijamii huwa ndio chanzo cha kupunguka kwa uthabiti wa Kiisimujamii katika lugha husika.

Utafiti huu ulijikita katika uchunguzi wa sababu zinazopelekea Washona kutumia Kiswahili na Kikuyu katika maeneo yao ya kijamii. Hii ni kwa sababu Washona wanaishi katika mitaa mitano katika kaunti ya Kiambu.

#### 1.7.1.3 Aina na Viwango vya Uhamishaji wa Msimbo

Uhamishaji msimbo ni jambo la kawaida katika jamii iliyo na wingilugha. Uhamishaji msimbo waweza kuwa wa lugha moja ama baina ya lugha mbili na waweza kutokea baina ya sentensi na nyingine, katika neno moja ama katikati ya sentensi moja. Chambers na Jack, (1995) na Myers, (1995) wanasema kwamba ubadilishaji wa msimbo waweza kutumika kama kitambulisho cha muda cha kikundi fulani kwa lengo la kutambua mahusiano katika muktadha wa mazungumzo na mawasiliano. Pia uhamishaji msimbo unaonyesha kwamba wahusika wanajua zaidi ya lugha moja hali inayochangia mabadiliko ya lugha. Landweer (2000) anasema kwamba uhamishaji msimbo unaweza kuwa wa aina tatu kuu ambazo ni:

a) Uhamishaji wa msimbo kwenye  jamii ya diglosia.
b) Hali ya wingilugha imara ambako miktadha ya kijamii ndiyo huamua msimbo utakaotumika.
c) Uhamishaji msimbo ambao haujadhibitiwa. Uhamishaji huo hutokea bila kufuata ruwaza yoyote (Buliba, Njogu na Aswani, 2006)

#### 1.7.1.4 Idadi ya Wanajamiilugha Wanaozungumza Lugha Husika

Landweer (2000) anasema kwamba lugha inaweza kuwa na wazungumzaji wachache, kwa mfano idadi ya chini ya elfu kumi na bado kiisimujamii iwe thabiti kwa kutegemea msaada inayopokea kutoka kwa asasi mbalimbali za kijamii pamoja na juhudi za

wanajamiilugha wenyewe. Kwa hivyo kulingana na maoni ya Landweer, uthabiti wa kiisimujamii wa lugha hutegemea idadi ya wanajamiilugha kwa kiwango fulani lakini sanasana juhudi na msaada kutoka asasi za kijamii kuhusu lugha husika ndizo huchukua nafasi kubwa katika kuhakikisha uthabiti wa kiisimujamii wa lugha.

Halikadhalika, wanajamiilugha wanaozungumza lugha husika sanifu wakiwa wengi, lugha hiyo inaendelea kuimarika. Wanajamiilugha hupungua kwa sababu ya kupata ajira mbali na nyumbani, biashara au ndoa na wanajamiilugha wengine. Utafiti huu ulijikita katika kuangalia idadi ya Washona wanaozungumza Kishona sanifu na pia idadi ya wale walioathiriwa na Kiswahili na Kikuyu.

### 1.7.1.5 Mtawanyiko wa Wanajamiilugha Husika Katika Mtandao wa Kijamii

Mtandao wa kijamii huwa imara wakati ambapo wanajamiilugha huwa na uhusiano wa karibu wanavyotambua Milroy, (1987) na Chambers na Natalie (2013). Katika mazingira ya mashambani, mtandao wa kijamii huwa imara sana kwa sababu ya mipangilio ya makazi yao, kutohamahama na pia mahusiano ya kifamilia na kiukoo. Hali hii huzuia shinikizo la kubadilika kwa lugha kwa sababu ya athari ya lugha nyingine.

### 1.7.1.6 Mtazamo Ulioko kwenye Jamii kuhusu Wanajamiilugha Husika na Wanajamiilugha Wengine kuhusu Lugha Husika

Nash (1987) anasema kuwa juhudi za wanajamiilugha za kutambua upekee wao katika jamii huamua ni lugha ipi watakayoitumia. Utambuzi wa lugha ya matumizi katika jamii huletwa na mielekeo mbalimbali kuhusu lugha husika ambayo inachangiwa na matumizi yake na faida za matumizi yake katika jamii. Garrett (2010) anabainisha

kwamba mielekeo ya lugha yaweza kuwa chanya au hasi kwa kutegemea matumizi yake katika jamii. Lugha iliyo na matumizi mengi katika jamii huwafanya wanajamii kuwa na mielekeo chanya kuihusu na hivyo basi huipatia hadhi ya juu kuliko lugha nyingine katika jamii. Hivyo mtazamo wa wanajamiilugha kuhusu lugha yao huchangia kuimarika na pia kutumika kwa lugha yao. Kamau (2015) anasema kwamba iwapo lugha inatambulika na mashirika kama vile ya kiserikali basi lugha hiyo ni thabiti. Lugha ya Kishona ilitambuliwa rasmi na serikali ya Kenya mwishoni mwa mwaka wa 2020 na hivyo basi utafiti ulilenga kuwatia shime Washona katika juhudi zao za kuhifadhi lugha yao.

#### 1.7.1.7 Hadhi Iliyopewa Lugha Husika Katika Jamii

Lugha ikitambuliwa na ikipewa hadhi ya juu na jamii, huifanya lugha hiyo kuimarika kwa sababu ya kupendwa na kutumika na watu wengi katika jamii. Vivyo hivyo lugha ikiwa na hadhi ya chini uthabiti wake huwa ni wa chini anavyotaja Landweer (2000). Lugha thabiti ni sharti ipate hadhi katika viwango vya vijijini, mikoani, kitaifa na hata kimataifa.

#### 1.7.1.8 Misingi Imara na Halali ya Kiuchumi ya Jamiilugha Husika

Lugha yoyote kuwa thabiti hutegemea misingi imara na halali ya kiuchumi kuhusu hiyo lugha. Lugha ambayo haiwanufaishi wazungumzaji wake kiuchumi hubadilika kwa urahisi na hivyo kukosa uthabiti wake. Lugha ikikosa uthabiti huanza kutoweka na hatimaye kufa na kusahaulika kabisa. Utafiti huu ulitumia mihimili yote minane kushughulia lengo la kwanza hadi la tatu.

Kwa vile nadharia ya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha haijazungumzia mikakati ya udumishaji wa lugha, nadharia ya pili imehitajika kushughulikia lengo la nne la utafiti ambalo lilibaini iwapo Washona wamefaulu katika kudumisha lugha yao au la. Nadharia ya Uzalishaji Kijamii ilitekeleza haya na imefafanuliwa kupitia kwa mihimili yake.

### 1.7.2 Nadharia ya Uzalishaji Kijamii.

Mwitifaki wa nadharia hii ni Bourdieu mwaka wa 1977 kwa minajili ya kufafanua namna ambavyo kizazi fulani hurithisha utamaduni kwa kizazi kinachofuata. Nadharia hii iliendelezwa na O'Riagain (1994) na alipendekeza mihimili miwili ifuatayo.

i. Kila kizazi hubuni na kuweka mikakati ya kurithisha kizazi kinachofuata utamaduni wake.

ii. Athari mbalimbali za mtagusano lugha moja na nyingine.

#### 1.7.2.1 Kila Kizazi Hubuni na Kuweka Mikakati ya Kurithisha Kizazi Kinachofuata Utamaduni Wake

Mikakati ya jamii ya kurithisha kizazi kinachofuata utamaduni wake huwa ni jambo la kimsingi katika jamii. Mikakati mizuri na imara huchangia uthabiti wa kiisimujamii wa lugha husika. Mikakati hii yaweza kuwekwa na mtu binafsi, familia ya mtu binafsi au na jamii nzima kwa makubaliano. O'Riagain (kt.) anadai kwamba wakati mwingine mikakati inayowekwa na mtu binafsi ama na jamii kwa jumla yaweza kuendelezwa na wanajamii bila wao kufahamu kwamba wanadumisha kipengele fulani cha mikakati ile. Lugha ya mama huwa ni kipengele cha kwanza muhimu ambacho wazazi hurithisha wana wao. Hili linawezekana iwapo wazazi hawa hawajaathiriwa na lugha jirani kwa

sababu ikiwa wameathiriwa basi huenda wakawahamisha wana wao zaidi kutoka lugha yao asilia na hivyo lugha yao ikakosa uthabiti. Mambo mengine yanayorithishwa vizazi kupitia kwa lugha ni kama vile dini, elimu, vyakula, sherehe za kuzaliwa na kupewa majina na hata salamu za jamii husika. Mhimili huu wa kwanza wa nadharia hii ulisaidia utafiti huu katika kushughulikia lengo la nne ambapo utafiti uliangalia mikakati ambayo Washona wanatumia ili kudumisha lugha yao licha ya shinikisho kutoka kwa lugha maarufu nchini Kenya.

#### 1.7.2.2 Athari Mbalimbali za Mtagusano Lugha Moja na Nyingine

Ngure (2012) anadai kwamba popote ambapo jamiilugha mbili zinatagusana na kuingiliana, uhamaji wa lugha lazima utatokea. Uhamaji wa lugha kwa mara nyingi hutokea kwa ile jamiilugha hafifu. Hafifu kwa maana ya kutokuwa na uthabiti wa kiisimujamii. Uhafifu huu hutokana ama kwa kupungua kwa wazungumzaji wa lugha husika au kukosa faida za kiuchumi za lugha husika. Kuna pia wakati mwingine jamiilugha thabiti huweza kuhama na kuanza kuzungumza lugha ya jamiilugha hafifu.

Utafiti huu ulitumia mhimili huu kwa kushirikiana na nadharia ya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha katika lengo la kwanza ili kubainisha iwapo lugha ya Kishona imeathiriwa na lugha nyingine wanazotagusana nazo kila siku.

O’Riagain (1994) anafafanua nadharia hii na kusema kwamba ili kufanikisha uchunguzi wa athari za kiisimujamii kwa lugha, ni sharti mtafiti achunguze muundo wa jamii maalum na uhusiano wake na eneo pana yaani kitaifa na kimataifa. Anazungumzia mahusiano ya kila siku ya jamii husika ambayo hudhihirika nyumbani wanamoishi, kazini, shuleni, maabadini, sokoni na sehemu nyinginezo katika jamii.

Nadharia hizi mbili ziliongoza utafiti huu katika kubainisha athari za Kiswahili na Kikuyu kwa Uthabiti wa Kiisimujamii wa Kishona.

### 1.8 Mbinu za Utafiti

Utafiti huu ulikuwa wa nyanjani na wa maktabani. Kombo na Tromp (2006) wanasema kwamba utafiti unaofanyiwa maktabani una dhima kuu kwa mtafiti ambapo humpa mtafiti data chasili inayomwongoza kwa kina katika swala lake la utafiti kupitia kukusanya data kwa njia ya usomaji. Utafiti wa maktabani ulisaidia katika kuchunguza taarifa muhimu kuhusu asili na hali ya Kiisimujamii ya kabila la Washona nchini Kenya. Maktabani, Upekuzi wa vitabu mbalimbali, majarida, tasnifu mbalimbali za wasomi na machapisho mbalimbali yalipekuliwa ili kupata habari muhimu inayolenga utafiti kama vile nadharia za utafiti na maelezo ya wataalamu wengine kuhusu mada ya utafiti. Utafiti wa maktabani uliandamana na utafiti wa nyanjani.

#### 1.8.1 Utafiti Awali

Kabla ya utafiti wa nyanjani, utafiti awali ulifanyika ili kufanya majaribio ya vifaa vya kukusanya data. Janghorban, Latifnejad na Taghipour (2013) wanasema kwamba utafiti awali unasaidia kwa njia nne zifuatazo ambazo zilisaidia utafiti huu; kutambua changamoto zinazohusiana na uteuzi wa sampuli, kumtayarisha mtafiti kwa utafiti halisi hasa katika kuongea na watafitiwa, kuchagua maeneo na makazi halisi ya utafiti na pia kusaili maswala ibuka katika utafiti. Utafiti awali pia ulisaidia katika kukadiria iwapo vifaa vya ukusanyaji data kama vile hojaji na mbinu za utafiti kama vile uchunzaji au usaili zilifaa kwa watafitiwa kabla ya utafiti wa nyanjani (Kothari, 2004; na Kombo na Tromp, 2006).

Utafiti wa nyanjani ulifanyika pale ambapo mtafiti alizuru maeneo ambayo wanajamiilugha wa Kishona wanaishi ili kupata data ya moja kwa moja kutoka kwao. Data za kimsingi zilizopatikana kwa ajili ya kujibu maswali ya utafiti zilikuwa mafungu ya maneno, maswali ya hojaji na majibu yao, mahojiano na mijadala ya kimakundi iliyobainisha jinsi lugha za Kiswahili na Kikuyu zimeathiri lugha ya Kishona, majibu yaliyoonyesha mielekeo na sababu zilizowachochea Washona kutumia Kiswahili na pia mikakati na shughuli zilizoonyesha juhudi za Washona za kudumisha lugha yao. Haya yote yaliwezekana kupitia kwa hatua mbalimbali za utafiti halisi.

Hatua zilizohusika katika utafiti wa nyanjani ni pamoja na kuteua sampuli ya utafiti, kukusanya data, kuchanganua data iliyokusanywa na kuiwasilisha data hiyo kwa njia ya maelezo. Mtafiti alikuwa na wasaidizi na waelekezi. Wasaidizi walisaidia katika kukusanya data na waelekezi wakahusika katika kutambua walengwa wa utafiti ili kupata data faafu ya utafiti kutoka kwa jumuiya ya utafiti.

### 1.8.2 Jumuiya ya Utafiti

Kombo na Tromp (2006) na Mugenda na Mugenda (2003) wanasema kuwa jumuiya ya utafiti ni maeneo yote, matukio yote, vitu vyote au watu wote walio na tabia au sifa zinazolengwa katika utafiti. Jumuiya ya utafiti huu ilikuwa ni watoto, vijana na wazee wa Kabila la Washona ambao wametangamana na makabila mengine nchini Kenya kupitia kwa ndoa, elimu na shughuli nyingine kama biashara ndogondogo. Jumuiya ya kimaeneo ilikuwa mitaa mitano katika kaunti ya Kiambu. Ili kuwafikia walengwa wa utafiti huu ambao tayari walishaanza kuingiliana na kuishi kwenye maeneo tofauti

tofauti nchini Kenya, uteuzi wa sampuli ulifanyika kimaksudi kwa kutegemea malengo ya utafiti ili kupata data faafu kwa haraka na kwa uhakika.

### 1.8.3 Uteuzi wa Sampuli

Utafiti huu uliteua sampuli kimaksudi na kwa njia elekezi kutoka mitaa mitano ya kaunti ya Kiambu ambako Washona wengi wanaishi. Sampuli maksudi ilitumiwa kwa sababu uteuzi huu ulimpa mtafiti uhuru wa kutathmini na kuchagua sampuli ya wahojiwa waliompa data ambayo ilifaa katika kutimiza malengo ya utafiti. Uteuzi wa kimaksudi, kwa maoni ya Lune na wenzake (2010) na Orodho (2004) humwezesha mtafiti kupata majibu kwa haraka kwa sababu haizingatii ukubwa bali muhimu ni ikiwa sampuli iliyoteuliwa itamwezesha mtafiti kushughulikia swala la utafiti kikamilifu kupitia kwa data inayotosha kuafikia malengo ya utafiti. Sampuli ya kimaksudi iliandamana na sampuli elekezi katika utafiti huu.

Sampuli elekezi, kwa mujibu wa Best na Kahn (2010) ni ile inayotumiwa mahali ambapo wahojiwa wamechangamana katika jumuiya. Mhojiwa mmoja anapopatikana, anatumiwa na mtafiti ili kuwafikia wahojiwa wengine wenye sifa sawia huku idadi mwafaka ya sampuli ikizingatiwa.

Milroy (1987) anasema kwamba utafiti wa lugha unahitaji matumizi ya sampuli ndogo kwa sababu sampuli kubwa katika utafiti wa lugha husaidia tu kupata data nyingi iliyojaa urudufu. Ngechu (2004) ana maoni kwamba idadi ya sampuli yafaa kupimwa kimaeneo na kusema kwamba utafiti unaohusu taifa nzima unafaa kuwa na sampuli isiyopungua wahusika elfu moja (1,000) ilhali tafiti zinazolenga maeneo madogo kama vile wilaya zafaa kuwa na sampuli ya wahusika kuanzia hamsini (50) kuelekea juu.

Uteuzi wa sampuli kimaeneo ulizingatia maeneo ambayo ni makazi yaliyo na idadi kubwa ya Washona. Kulingana na utafiti awali, idadi kubwa ya Washona wanaishi kwenye mitaa ya Kiambaa, Kinoo, Kikuyu, Gitaru na Githurai kwa kuwa Washona wa kwanza waliokuja Kenya kama wamishenari na wanaojulikana kama kizazi cha kwanza waliishi hapa.

Utafiti huu ulilenga Washona wa vizazi vyote tangu wafike nchini Kenya. Hii ni kwa sababu lengo kuu la utafiti lilikuwa kubainisha athari za Kiswahili na Kikuyu kwa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha yao ya Kishona. Athari hizi zinaweza kuwa tofauti kwenye vizazi vyao. Asilimia ya kila kizazi ilitegemea idadi ya Washona katika Kizazi husika kwa sababu kulingana na chifu wa eneo la Kinoo, idadi yao ni takriban 2,500. Baada ya kuteua sampuli lengwa iliyohusishwa, shughuli ya kukusanya data faafu ilifuata.

### 1.8.4 Ukusanyaji wa Data

Shughuli ya ukusanyaji data ilianza na mtafiti kwenda nyanjani baada ya kupata vibali kutoka Chuo Kikuu cha Kenyatta, Afisi za kaunti ya Kiambu na Baraza la Kitaifa la Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (NACOSTI). Vibali hivi ndivyo vilivyotumiwa na mtafiti katika kujitambulisha na kupata ruhusa ya kutangamana na Washona katika harakati za kupata data ya utafiti.

Mugenda na Mugenda (2003) wanasema ya kwamba usahihi wa kupata data ya kuaminika hutegemea mbinu zitakazotumika na mtafiti katika ukusanyaji wa data. Mtafiti na wasaidizi wake walitumia hojaji, mahojiano, utazamaji au uchunzaji, kushiriki, mijadala ya vikundi vidogovidogo na maswali mepesi yaliyoandaliwa

kimbele. Vifaa vyote vya kukusanya data viliandaliwa kwa kutegemea malengo maalum ya utafiti.

Data kutoka nyanjani ilikusanywa kutokana na sampuli ya Washona wanaoishi katika mitaa ya Kinoo, Kiambaa, Kikuyu, Githurai na Gitaru katika kaunti ya Kiambu. Maoni ya watafitiwa yalinukuliwa moja kwa moja, Maneno, vishazi na sentensi zilinukuliwa ili kuonyesha hali halisi ya athari za mtagusano wa Kiswahili na Kikuyu kwa Kishona nchini Kenya. Mtafiti alijitambulisha vyema kwa walengwa wake na kuwabainishia lengo na umuhimu wa utafiti huu kwa Washona huku akiwa amejiandaa na vifaa vifuatavyo vya kukusanya data.

#### 1.8.4.1 Hojaji

Hojaji ni zana ya kukusanya na kurekodi data ama taarifa kuhusu jambo fulani. Hojaji huwa na orodha ya maswali yaliyopangwa vyema, yanaweza kuwa huru au funge, na huhitaji kujibiwa na watafitiwa. Kwenye utafiti huu, hojaji zilitumika katika kupata data ya lengo la kwanza na la tatu. Lengo la kwanza lilichunguza athari za mtagusano wa Kiswahili na Kikuyu kwa lugha ya Kishona na lengo la tatu lililoshughulikia mielekeo ya Washona katika matumizi ya Kiswahili na Kikuyu. Mtafiti aliwaeleza wasaidizi na watafitiwa waliopatikana utaratibu wa kujibu maswali yaliyokuwa kwenye hojaji kwa kuwasomea swali moja baada ya lingine ili kuhakikisha kuwa wameelewa kabla ya kusambaza na kabla ya kujibu maswali kwenye hojaji. Watafiti wasaidizi walipewa hojaji na kuzisambaza kwenye maeneo ambayo walikuwa wamechagua na kisha kuzirejesha baada ya wiki moja. Mtafiti alizichukua hojaji zote kutoka kwa watafiti wasaidizi ili kuzipanga na kuzitayarisha kwa uchanganuzi.

### 1.8.4.2 Mijadala ya Kimakundi

Mijadala ya kimakundi ilitumiwa katika kukusanya data inayohusiana na lengo la pili na lengo la nne. Lengo la pili lilishughulikia kubainisha sababu zinazopelekea Washona kutumia Kiswahili na Kikuyu katika maeneo yao ya kijamii. Maswali yaliyotayarishwa mbele yaliongoza data iliyokusanywa kuhusu lengo la nne lililohusu mikakati ambayo Washona walitumia katika kudumisha lugha yao kutoka kwa wazee hadi kwa vijana na watoto.

Mtafiti pia aliwaeleza utaratibu wa kushiriki katika mijadala ya vikundi vidogovidogo. Mjadala wa vikundi vidogovidogo ambavyo vilipangwa kulingana na umri wa walengwa ulihusisha maswali wazi ambayo yalilenga kukusanya data kuhusu sababu za kutumia Kiswahili katika maeneo yao ya Kijamii na mielekeo ya Washona kuhusu matumizi ya Kiswahili na Kikuyu pamoja na mbinu zao za kudumisha lugha yao kwa vizazi vyao. Vikundi hivi vilichaguliwa kwa kutegemea idadi ya walengwa kwenye vizazi mbalimbali katika kabila la Washona na kutoka kwa mitaa mitano ambayo ni makazi ya Washona hapa nchini Kenya. Vikao hivi katika vikundi vidogovidogo viliendeshwa kwa utaratibu unaofanana ule wa hojaji huku majibu yakirekodiwa na mtafiti na wasaidizi wake kwa minajili ya uchanganuzi.

### 1.8.4.3 Utazamaji au Uchunzaji

Uchunzaji ni utazamaji ambao hufanyika wakati mtafiti anazuru maeneo ya watafitiwa huku akichunguza baadhi ya shughuli zao na maeneo yao mbalimbali katika jamii huku akinakili kitabuni kila anapopata habari maalum ya utafiti wake kama anavyosema Patton (1990). Mtafiti alikuwa sehemu ya watafitiwa katika ibada ya kanisa la

walengwa, mikutano ya baraza, biashara zao na hata mikutano yao ya kitamaduni. Mtafiti alidhamiria kupata data kamilifu iliyojibu maswali yaliyohusiana na lengo la kwanza lililochunguza athari za mtagusano wa Kiswahili na Kikuyu kwa Kishona, lengo la pili lililochunguza sababu za kutumia Kiswahili na Kikuyu katika maeneo yao ya kijamii na lengo la nne lililobaini iwapo Washona wamefaulu katika kudumisha lugha yao au la. Maeneo ya uchunzaji yalikuwa Kanisani, nyumbani, kwenye kazi zao za mikono, kwenye sherehe zao mbalimbali na kwenye mikutano yao ya maombi katika maeneo waliokuwa wamechagua.

#### 1.8.4.4 Kushiriki

Kushiriki kulimsaidia mtafiti kuchunguza athari za Kiswahili na Kikuyu hasa pale aliposhiriki katika mazungumzo yao ya kawaida huku akichunguza athari hizo katika stadi ya kuongea, kusoma na kuandika. Mielekeo ya Kiswahili na Kikuyu ilishughulikiwa katika lengo la tatu la utafiti huu ambapo mtafiti alishiriki katika mijadala ya vikundi mbalimbali vya watafitiwa ili kubaini mielekeo yao. Mtafiti aliwapa maswali yaliyochochea mjadala na mazungumzo ya kawaida ambayo yalibainisha mielekeo yao kwa Kiswahili na Kikuyu.

#### 1.8.4.5 Mahojiano

Mahojiano ni maswali mepesi na ya moja kwa moja ambayo yameandaliwa mbele kwa ajili ya kutafuta habari muhimu kuhusu utafiti. Mahojiano yalitumika ili kupata data ya kuthibitisha data iliyokusanywa na hojaji. Mahojiano yalitumika katika kupata data ya lengo la pili lililochunguza sababu za Washona za kutumia Kiswahili na Kikuyu katika maeneo yao ya kijamii, lengo la tatu lililochunguza mielekeo ya Washona kwa

Kiswahili na Kikuyu na hatimaye lengo la nne lililobaini iwapo Washona wamefaulu kudumisha lugha yao ya Kishona au la na mikakati wanayotumia katika udumishaji wa lugha yao. Mahojiano ya kwanza yalifanyika kwa njia ya simu na mzee mmoja wa kanisa la *Gospel of God* ambayo yalithibitisha data iliyokuwa imekusanywa kupitia kwa hojaji. Mahojiano ya pili yalifanyika kwenye mtaa wa Kinoo, kwenye karakana ya mtafitiwa mmoja ambapo watafitiwa wengi walipatikana na kuhojiwa kuhusu sababu za kutumia Kiswahili na Kikuyu na mikakati mbalimbali ya kudumisha Kishona. Mtafiti aliuliza maswali huku akinakili majibu yaliyokuwa yanatolewa na wasailiwa.

Mahojiano mengine yalifanyika kwenye maeneo ya kanisa la *Gospel of God,* ambapo wazee wanne walihusika. Mtafiti na wahojiwa hawa wanne walikaa pembeni mwa kanisa hilo na mahojiano yalichukua dakika hamsini. Vile vile, mtafiti alikuwa akinakili kila jibu lililokuwa linatolewa na wahojiwa baada ya kuulizwa maswali.

#### 1.8.4.6 Vifaa Vingine

Vifaa vingine ambavyo vilitumika katika shughuli ya ukusanyaji data ni kama vile kinasa sauti (simu) iliyotumika katika kunasa matumizi ya lugha wakati wa uchunzaji na kushiriki. Kamera ilitumika kuchukua picha ili kuthibitisha shughuli mbalimbali za ukusanyaji wa data. Shajara ilitumika kunakili tarehe za matukio na shughuli mbalimbali. Kalamu na kitabu vilitumika kuandika au kurekodi shughuli zilizotokana na uchunzaji na majibu yaliyotokana na  mahojiano na pia kutoka mijadala ya vikundi vidogovidogo kwa matayarisho ya shughuli ya uchanganuzi wa data.

### 1.8.5 Uchanganuzi wa Data

Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa kutumia mbinu changamano ambayo kulingana na Denzin na Lincoln (2011), ni mtindo wa kuchanganya mbinu za kitakwimu na maelezo kwa lengo la kuelewa swala la utafiti kwa undani zaidi. Data iliyokusanywa ilipangwa kwa makundi mbalimbali na hatimaye kuchanganuliwa kwa kutegemea malengo ya utafiti. Programu ya kuchanganua data ya SPSS (Kichanganuzi Data za Kitakwimu za Sayansi Jamii) ilitumika hasa kuchanganua data iliyopatikana kutoka hojaji (lengo la kwanza na la tatu ) baada ya kukaguliwa na kupangwa. Data ambayo ilikuwa na upungufu iliwekwa kando ili isipotoshe matokeo ya utafiti.

Data iliyotokana na mijadala ya vikundi vidogovidogo ambayo ilikuwa imerekodiwa ilichanganuliwa kwa njia ya maelezo kuhusu sababu za Washona kutumia Kiswahili na Kikuyu katika maeneo yao ya kijamii na mbinu za udumishaji wa Kishona (lengo la pili na la nne). Data iliyorekodiwa hasa kutoka shughuli za kijamii za Washona kama vile ibada na sherehe ya kuzaliwa na kupewa jina kwa watoto ilichanganuliwa ili kubainisha data asilia.

Data kutoka utazamaji au uchunzaji pia ilichanganuliwa kimaelezo katika malengo yote manne kwa kuwa ilikuwa imenakiliwa na hivyo mtafiti alitoa mifano na maelezo kuhusu athari za Kiswahili na Kikuyu kwa Kishona, sababu za kutumia Kiswahili na Kikuyu katika maeneo yao ya jamii, mielekeo yao ya kutumia Kiswahili na Kikuyu katika jamii na mikakati ya udumishaji wa Kishona licha ya shinikizo kutoka lugha maarufu nchini Kenya. Mtafiti alithibitisha kwa kutumia picha za shughuli ambazo alishiriki na Washona ili kupata habari iliyotakikana kwa minajili ya uwasilishaji.

### 1.8.6 Uwasilishaji wa Matokeo

Matokeo yaliwasilishwa kupitia kwa maelezo, takwimu na asilimia. Kauli mbalimbali za watafitiwa zilinukuliwa kwa nia ya kuthibitisha baadhi ya majibu yaliyotolewa na walengwa. Maelezo yalitangulia kwa kifupi kwa kila kipengele cha malengo kisha yakafuatwa na madondoo au majedwali yaliyoonyesha asilimia ili kuwasilisha data itakayotegemewa. Uchanganuzi na uwasilishaji wa data ulifaulu kwa kuwa maadili ya utafiti yalizingatiwa.

### 1.8.7 Maadili ya Utafiti

Frankael na Wallen (2006) wanadai kuwa maadili ya utafiti hurejelea jambo ambalo limekubalika na lile ambalo halijakubalika katika shughuli za utafiti. Mugenda na Mugenda (2003) wanasema kuwa kuzingatia maadili wakati wa utafiti ni jambo la busara katika kufanikisha utafiti. Maadili ya utafiti yalihusisha kupata idhini kutoka kwa Chuo Kikuu cha Kenyatta pamoja na taasisi zinazohusika, haki ya kuweka siri ya watafitiwa, uwazi wa wanataaluma, na kulinda saikolojia ya watafitiwa.

Mtafiti alipata idhini ya utafiti kutoka Shule ya Umahiri ya Chuo Kikuu cha Kenyatta na baada ya idhini hii, mtafiti alitafuta kibali kutoka Baraza la Kitaifa la Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi (NACOSTI) na kibali kutoka kamishna wa kaunti ya Kiambu ili kukusanya data kutoka mitaa ya Kiambaa, Kikuyu, Kinoo, Gitaru na Githurai.

Baada ya idhini zote kupatikana, mtafiti alienda nyanjani ambapo alihakikishia watafitiwa kuhusu haki ya usiri wa habari walizotoa kupitia kwa kuficha majina yao na kuwahakikishia kwamba habari walizozitoa zilitumika tu kwa minajili ya masomo. Abelson, Frey na Gregg (2004) na Chambers na Natalie (2013) wanasema kwamba

sababu kuu ya kuficha majina ni kuwapa uhuru wa kuelezea mielekeo na hisia zao bila kujulikana. Watafitiwa walihimizwa pia kujaza hojaji bila hofu kwa kuwa hawatatambulikana.

### 1.9 Hitimisho

Sura hii ilishughulikia misingi ya utafiti ambapo usuli wa mada ya utafiti ulishughulikiwa, swala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada na mipaka ya utafiti. Vilevile, sehemu hii ilishughulikia nadharia mbili zilizoongoza utafiti huu ambazo ni nadharia ya Uthabiti wa Kiisimujamii wa lugha na nadharia ya Uzalishaji wa Kijamii. Nadharia hizi ziliongoza utafiti huu katika ukusanyaji wa data na uchanganuzi wake. Vilevile, sehemu hii ilishughulikia mbinu na hatua nne za utafiti zilizotumika.

Sura ya pili inayofuata inashughulikia maandishi mbalimbali yanayohusiana na mada ya utafiti. Maandishi haya yanahusu athari mbalimbali za mtagusano lugha, mielekeo ya lugha na udumishaji wa lugha. Wanajamiilugha wa Kishona wamebainishwa kwa vipengele mbalimbali kama vile utamaduni wao, asili yao, dini na imani yao na historia yao nchini Kenya. Aidha, lugha za Kiswahili na Kikuyu zilishughulikiwa kwa ufupi kisha uthabiti wa kiisimujamii wa lugha na vigezo vya kupima uthabiti wa lugha vimejadiliwa ili kuweka wazi zaidi tatizo la utafiti.

# SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDISHI

## 2.0 Utangulizi

Sura hii inashughulikia athari mbalimbali za mtagusano lugha kama vile ubadilishaji wa msimbo, ukopaji wa maneno, wingilugha, mabadiliko ya lugha, mielekeo ya lugha pamoja na udumishaji wa lugha. Hali ya lugha barani Afrika na nchini Kenya imeangaziwa pamoja na hali ya lugha na historia ya Washona nchini Kenya. Aidha, lugha za Kiswahili na Kikuyu nchini Kenya zimeshughulikiwa katika sura hii. Mwisho, uthabiti wa kiisimujamii wa lugha pamoja na vigezo mbalimbali vya kupima uthabiti wa lugha vimeangaziwa huku maandishi mbalimbali kuhusu uthabiti wa kiisimujamii wa lugha yakipekuliwa ili kuweka wazi zaidi pengo lililopo la utafiti. Mtagusano lugha na athari zake umeshughulikiwa kwanza.

## 2.1 Mtagusano Lugha

Katika mazingira ya wingilugha, mtagusano lugha ni jambo lisiloepukika. Weinreich (1953), Haugen (1953) na Thomason (2000) wanasema kwamba mtagusano lugha ni matumizi ya lugha tofauti na jamiilugha tofauti zinazokaa pamoja. Mambo yanayowezesha mtagusano kufaulu ni kama vile ujirani mwema kati ya wanajamiilugha tofauti, kufanya biashara, elimu na hata ndoa baina ya jamiilugha hizo. Mtagusano lugha ukitokea, lugha moja inaweza kupoteza uthabiti wake huku lugha nyingine ikiendelea kuwa thabiti. Thomason anasema kwamba, katika hali ya mtagusano lugha, ile lugha ambayo itapoteza uthabiti wake kwa mara nyingi ni lugha iliyo na wasemaji wachache na pia lugha ambayo haina kazi nyingi katika jamii.

Utafiti kuhusu mtagusano lugha ulianzishwa na Uriel Weinreich alipofanya utafiti wa uzamifu kuhusu matatizo ya kufanya utafiti katika jamii za uwililugha nchini Uswisi mwaka wa 1951. Katika utafiti wake wa baadaye, Weinreich (1953), alibainisha kwamba mtagusano lugha huzua athari za kimuundo na za kimazingira. Kimazingira kwa maana ya athari zinazotokana na matumizi ya lugha katika jamii hasa katika mazingira ya wingilugha. Weinreich alisema kwamba, athari za mtagusano lugha huwezeshwa na vigezo tofauti katika jamii kama vile uwililugha, muda wa mtagusano, kigezo cha kijiografia, idadi ya wanajamiilugha husika, matumizi katika maeneo ya kijamii, imani na dini, na matumizi katika maeneo rasmi kama vile elimu na ofisi mbalimbali za serikali.

Baada ya utafiti wa Weinreich, baadhi ya watafiti waliofuata kama vile Fishman (1991), alitafitia uhamaji wa lugha baada ya mtagusano lugha, Thomason na Kaufman (1988) walitofautisha viwango mbalimbali vya mtagusano lugha na athari zake. Fishman (kt.) na Thomason na Kaufman (kt.) walichunguza athari mbili za mtagusano lugha ambazo ni ukopaji na uhamaji wa lugha katika mazingira ya wingilugha ambapo lugha iliyo na hadhi ya chini huanza na ukopaji wa maneno kutoka lugha iliyopewa hadhi ya juu katika jamii. Utafiti huu wa Thomason na Kaufman (kt.) ulikuwa wa manufaa kwa utafiti huu hasa katika lengo la kwanza lililoshughulikia athari za mtagusano wa Kiswahili na Kikuyu kwa Kishona nchini Kenya.

Mtagusano lugha ni maingiliano ya lugha baina ya jamiilugha tofauti za watu wanaokaa pamoja. Chambers na Natalie (2013) anasema kwamba mtagusano lugha baina ya jamiilugha mbili au zaidi huchangia pakubwa mabadiliko ya kiisimujamii ya lugha

zinazohusika. Thomason (2000) anasema kwamba, kwenye mtagusano lugha, ile lugha ambayo itapoteza uthabiti wake kwa mara nyingi ni lugha iliyo na wasemaji wachache na pia lugha ambayo haina kazi nyingi katika jamii. Mtagusano lugha hutokea panapokuwa na haja ya mazungumzo kati ya wanajamiilugha tofauti kufuatia shughuli mbalimbali katika jamii na pia hutokea kwa njia mbalimbali.

Thomason (2000) anafafanua njia ya kwanza ya mtagusano lugha ambapo wanajamiilugha moja huhamia sehemu ya wanajamiilugha wengine na kuanza kuishi pamoja au karibu. Hali hii inapotokea, mtagusano katika lugha hizi mbili huwa ni lazima. Jamiilugha iliyo na watu wachache kwa mara nyingi humezwa na jamiilugha iliyo na idadi kubwa ya watu. Hali hii inapotokea, wanajamiilugha walio wachache hawana budi ila kujifunza lugha ya wanajamiilugha waliowengi katika jamii hiyo ili kurahisisha mazungumzo na shughuli zao za kila siku.

Thomason (2001) anadai kwamba mtagusano lugha pia hutokea kupitia uhusiano wa karibu unaotokea kati ya wanajamiilugha tofauti ambao ni majirani wa muda mrefu na unaowezeshwa na biashara, ndoa na shughuli za ibada kanisani kati ya jamiilugha hizi mbili. Shughuli za kuabudu hulazimisha wanajamiilugha kujifunza lugha ya wanajamiilugha wengine ili kufanikisha ibada. Thomason (2000) anasema kuwa wanajamiilugha wanapoendelea kuchangamana katika shughuli za kidini au biashara, uhusiano wa karibu hutokea na kuwezesha ndoa baina ya wanajamiilugha mbili tofauti.

Asasi za elimu pia huchangia mtagusano lugha baina ya wanafunzi. Lee (2002) aligundua kwamba asasi za elimu hasa shuleni huchangia mtagusano lugha ambapo wanafunzi kutoka jamiilugha mbalimbali hujifunza na kuzungumza lugha rasmi kama

vile Kiingereza. Lee aligundua kwamba watoto huchukua muda wao mwingi katika mazingira ya shuleni na hivyo basi hawana budi ila kujifunza lugha rasmi inayotumika katika mazingira ya shuleni. Utafiti wa Lee unabainisha kwamba lugha ya Kiingereza imeenea kwa sababu ya elimu katika nchi nyingi za Afrika na duniani kote.

Maya (2009) anabainisha njia nyingine ya mtagusano lugha ambayo ni kupitia kwa biashara kama vile biashara ya watumwa. Hii ilitokea katika karne ya kumi na tisa ambapo watumwa wengi kutoka Afrika walipelekwa nchi za Marekani kwenda kufanya kazi katika mashamba ya mabepari. Walipofika huko walizua lugha mpya ambayo ilipokuwa thabiti ikawa ni lugha tofauti sana na ile yao na ya wenyeji wao kwa mfano nchini Belize. Belize ni nchi ipatikanayo Amerika ya kati kwenye kisiwa cha St.Vincent ambapo mtagusano kati ya lugha ya Kigarifune inayozungumzwa nchini humo, Kifaranza na Kiingereza ulileta mabadiliko yaliyozua lugha mpya iliyoitwa na wenyeji 'Krioli cha Belize'. Mtagusano lugha mbalimbali huzua athari mbalimbali kwa lugha husika kwa kuwa mabadiliko ya lugha hayawezi kuepukika.

## 2.2 Athari za Mtagusano Lugha

Mtagusano lugha ukitokea, Appel na Muysken (2005) wanasema kwamba lugha zote husika zaweza kuathiriana ila ile iliyo na wazungumzaji wachache au hadhi ya chini katika jamii huweza kuathirika zaidi kupitia mabadiliko mbalimbali. Mabadiliko ya lugha huanza kuonekana kupitia kwa ubadilishaji wa msimbo au uchanganyaji msimbo, ukopaji wa leksimu, kuibuka kwa misimu mbalimbali, uhamaji wa lugha na wingilugha. (Thomason, 2001; Ngure, 2012; na Mathooko, 2007). Ubadilishaji msimbo umeshughulikiwa kwanza.

### 2.2.1 Ubadilishaji Msimbo

Kubadili msimbo ni hali ambayo mzungumzaji huchanganya lugha mbili au zaidi ama lahaja tofauti anapozungumza. Hymes (1975) anasema kwamba ubadilishaji msimbo waweza kutokea ndani ya sentensi moja au baina ya sentensi tofauti kwenye mazungumzo katika mazingira ya wingilugha. Pfaff (1979) anasema kuwa kubadili msimbo ni tukio linaloathiri muundo wa kisemantiki, pragmantiki na isimujamii kwa lugha zinazozungumzwa na wanawingilugha. Cook (2010), Grosjean (1982), Malik (1994) na Milroy na Muysken (1995) wanafafanua ubadilishaji msimbo kwamba ni tukio la kiisimu linalohusu kuingiza neno, kirai, ama sentensi ya lugha moja kwa lugha nyingine katika mazungumzo bila kuathiri sarufi ya lugha pokezi. Hymes (1975) anasema kwamba katika mazingira ya wingilugha, kila lugha huwa na kazi yake: lugha moja inaweza kuwa na kazi ya mazungumzo yasiyo rasmi na kwenye miktadha isiyo rasmi kama vile mazingira ya nyumbani huku lugha nyingine ikipewa jukumu la matumizi rasmi kama vile kwenye elimu na ofisini.

Dhana ya ubadilishaji msimbo ilianzishwa na Blom na Gumperz mwaka wa 1972 katika kazi yake ya kufafanua maana ya muundo wa isimu katika jamii. Kazi nyingi ya Gumperz (1964) ilifanyikia India ambapo alitafitia kuhusu Kihindi kinachozungumzwa India kaskazini. Alitambua viwango vitatu vya ubadilishaji wa msimbo: kiwango cha mashinani au mashambani/vijijini, kiwango cha eneo na kiwango cha wastani. Alisema kwamba, wanaume wengi Wahindi walio na uzoefu wa kusafiri kwa ajili ya biashara wanazungumza lahaja ya vijijini na lahaja za kieneo ambapo lahaja ya vijijini huzungumzwa nyumbani na lahaja za kieneo huzungumzwa na watu kutoka nje ya

vijijini. Aligundua kwamba wanaume hawa walikuwa na mazoea ya kubadilishana msimbo katika lahaja zote kwenye mazungumzo yao.

Katika tafiti za kwanza za Marekani kuhusu anthropolojia ya kiisimu, Baker (1992) alizungumzia kuhusu matumizi ya lugha na kuchanganya msimbo baina ya Wamarekani wenye asili ya Meksiko wanaoishi Tucson, Arizona. Aligundua kwamba uhusiano wa kiuchumi, mtandao wa kijamii na hali ya kijiografia ya wakazi hao ilichangia pakubwa katika kubadili msimbo kwa kuwa walikuwa wanatumia lugha au lahaja mbalimbali katika shughuli mbalimbali. Baker alinuia kujibu swali la "hali ya kuchanganya msimbo hufanyikaje?" kwa mfano utangamano baina ya watu wa familia moja utawawezesha kuzungumza lugha ya Kihispania lakini kwa mazungumzo rasmi watatumia Kiingereza. Hivyo basi, Baker akagundua kwamba uchaguzi wa lugha ya matumizi katika shughuli yoyote hutokea tu kwa wanawingilugha na hivyo basi lugha mbili zinaweza kutumika katika mazungumzo. Baker aligundua pia kwamba vijana wana uwezo wa kutumia lugha nyingi katika mazungumzo kuliko wazee.

Wanaisimujamii wanatazama ubadilishaji msimbo kuwa tukio la kawaida kwa jamiilugha katika hali mbalimbali na kwa madhumuni mbalimbali. Holmes (2001) anasema kuwa ubadilishaji msimbo ni jambo ambalo linawezeshwa na vigezo vya kijumla katika jamii kama vile mtagusano lugha mbalimbali, miktadha mbalimbali ya matumizi ya lugha katika jamii na dhima mbalimbali za lugha katika jamii. Ubadilishaji msimbo hufaulu iwapo wazungumzaji wanaohusika wanajua lugha wanazozitumia na sababu zao za kutumia lugha hizo. Ubadilishaji msimbo hutokea hasa katika jamii za wingilugha ambapo wanajamiilugha wamezungukwa na lugha nyingi.

Lee (2002) na Bhatia na Ritchie (2004), walifanya utafiti nchini Korea kuhusu ubadilishaji wa msimbo kwenye mazungumzo. Walijikita katika mbinu zinazotumika katika uchanganyaji wa msimbo kama vile uchopekaji na ubadilishaji wa leksimu sambamba. Walitambua sababu mbalimbali za kubadili msimbo zikiwemo sababu za kimuktadha, jukumu la washiriki, mada husika, mielekeo ya wanajamiilugha kuhusu lugha chanzi, na ubabe wa kiisimujamii wa lugha chanzi. Tafiti za Bhatia na Ritchie (2004) na Lee (2002) zinahusiana na utafiti huu kwa kuwa mielekeo na sababu mbalimbali za kubadili msimbo katika mazungumzo yaliyohusisha lugha za Kishona, Kiswahili na Kikuyu zililiangaziwa.

Duran (2005) anasema kwamba ubadilishaji msimbo ni mbinu mwafaka kwa wanawingilugha wanapohusiana na watu wanaojua lugha zote husika. Naye Faltis (1989) ana maoni kwamba watoto hujifunza lugha zinanazowazunguka kwa haraka na hivyo katika mazungumzo yao, huchanganya msimbo kwa urahisi wanapoongea na watoto wenzao, watu wa familia zao na walimu wao shuleni. Utafiti wa Duran (kt.) ulisaidia utafiti huu kwa kuwa ulifafanua jinsi watoto wa Kishona wameathiriwa na lugha zinazowazunguka za Kiswahili na Kikuyu kupitia kwa mazingira ya wingilugha na masomo shuleni.

Kalmanlehto (2014) alishughulikia uchanganyaji msimbo na uhamishaji msimbo baina ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha St. Augustine nchini Tanzania. Aligundua kwamba wanafunzi wengi walikuwa wanachanganya Kiswahili na Kiingereza katika mazingira ya wingilugha humo chuoni. Utafiti wake uligundua kuwa sababu moja kuu ya kuchanganya lugha hizi mbili ni kwamba walikuwa na ujuzi finyu wa lugha ya

Kiingereza na hivyo wakawa wanalazimika kuchanganya Kiswahili kila walipoulizwa swali kwa lugha ya Kiingereza. Utafiti wa Kalmanlehto (2014) unahusiana na utafiti huu kwa kuwa, kwanza, Kiswahili ni mojawapo ya lugha zilizoangaziwa. Pili, ubadilishaji msimbo katika mazingira ya wingilugha uliangaziwa kwa kuwa Washona wanaishi katika mazingira ya wingilugha ambapo wamejifunza lugha nyingi na hivyo basi hawana budi ila kuchanganya lugha wanapozungumza katika miktadha mbalimbali.

Barasa (2016) alifanya utafiti kuhusu uhamishaji msimbo baina ya wanafunzi wa vyuo vikuu nchini Kenya na kutambua kuwa wanafunzi hufahamu lugha nyingi kama vile Kiingereza, Kiswahili na lugha zao asilia. Barasa alitambua kwamba wanafunzi hawa walikuwa wakiwasiliana huku wakibadilisha msimbo kupitia majukwaa ya *Facebook*, *Youtube* na jumbe fupi za simu za mkononi. Utafiti wake uligundua kwamba kuwepo kwa lugha nyingi husababisha kubadilisha msimbo miongoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu nchini Kenya. Utafiti wake unasabihiana na huu kwa kuwa utafiti huu unashughulikia ubadilishaji msimbo kama mojawapo ya athari za mtagusano wa Kishona na lugha nyingine. Utafiti wa Barasa unatofautiana na huu kwa sababu yeye alilenga wanafunzi wa vyuo vikuu peke yake huku utafiti huu ukilenga kabila nzima la Washona wa umri wote. Utafiti wa Barasa unapelekea athari ya pili ya mtagusano lugha katika mazingira ya wingilugha ambayo ni ukopaji wa maneno.

### 2.2.2 Ukopaji wa maneno

Athari nyingine ya mtagusano lugha ni ukopaji wa maneno. Ukopaji wa maneno ni hali ya kuchukua neno, au kifungu cha maneno kutoka kwa $L_2$ na kuyaweka katika mazungumzo ya $L_1$ baina ya wazungumzaji walio na ujuzi wa lugha mbili au zaidi.

Chambers na Jack (1995) na Nagy (2010) wanasema kuwa katika mchakato wa ukopaji wa maneno kutoka $L_1$ hadi $L_2$, kuna vigezo vinavyotawala hali hiyo ambavyo ni umri, jinsia, tabaka, mtandao wa kijamii na mielekeo ya wanajamiilugha ya kwanza. Sangili (2019) anasema kwamba, kigezo cha jinsia hudhihirika kupitia kwa ndoa ambapo wanawake kutoka jamiilugha moja wakiolewa na waume kutoka jamiilugha nyingine, basi hujifunza lugha ile ya pili na kukopa maneno kutoka lugha hiyo huku akiyaingiza kwa lugha yake ya kwanza. Kwenye kigezo cha umri, Chambers na Jack (kt.) wanasema kuwa wanajamiilugha wa umri mchanga hujifunza leksimu za lugha pokezi kwa haraka na kuzidadisi kwa lugha yao ya kwanza kuliko wanajamiilugha wazee. Hali hii inafanya maneno yaliyokopwa kutoka $L_2$ kutumika vyema na kufuata mofimu ya lugha pokezi.

Gumperz (1976) na T'sou (2001) wanasema kwamba maneno yaliyokopwa hufuata muundo wa lugha pokezi na huchukuliwa kama sehemu ya leksia, mofolojia na pia sintaksia ya lugha pokezi. Poplack (1980) anasema kwamba tofauti moja iliyoko kwenye ukopaji wa maneno ni kwamba ukopaji hutokea kwenye viwango vya fonolojia, mofolojia na sintaksia ya lugha chanzi ambapo maneno au virai mkopo huingizwa kwenye lugha pokezi. Poplack (1980) na T'sou (kt.) wanasema kuwa ukopaji hauhitaji wingilugha kama vile ubadilishaji msimbo ila ukopaji wa maneno unaweza kutokea hata kama mzungumzaji hana ufahamu mzuri wa lugha ya pili.

Tsangwa (2017) alichunguza ukopaji wa maneno ya Kiswahili katika lugha ya Kigiriama katika kaunti ya Kilifi, pwani ya Kenya ili kubaini nominomkopo na vitenzimkopo vya asili ya Kiswahili katika lugha ya Kigiriama. Utafiti wake

ulichunguza sheria zinazothibiti ukopaji wa maneno na vitenzi vya Kiswahili kwa lugha ya Kigiriama na kubainisha michakato mbalimbali kama vile uchopekaji na kiubadala katika ukopaji wa nomino na vitenzi vya Kiswahili katika lugha ya Kigiriama. Utafiti huu ulifaidika na utafiti wa Tsangwa kwa kuwa ukopaji wa maneno ni mojawapo ya athari za mtagusano lugha ambayo ilishughulikiwa. Utafiti wake ni wa kiisimu huku utafiti huu ukiwa wa kiisimujamii. Tsangwa alitumia nadharia moja tu ya fonolojia zalishi asilia huku utafiti huu ukitumia nadharia mbili ambazo ni nadharia ya Uthabiti wa Kiisimujamii wa Lugha na nadharia ya Uzalishaji Kijamii.

Babusa (2019) alitafitia ukopaji wa lugha huku akijikita katika etimolojia ya maana na utamkaji wa sauti na msamiati wa lugha ya Kiarabu katika Kiswahili katika pwani ya Afrika Mashariki. Aligundua kwamba lugha ya Kiswahili ilikopa maneno ya Kiarabu ambayo hayakuwepo katika Kiswahili asilia na kuyabadili jinsi yanavyotamkwa na hata maana yake. Uingizaji wa maneno na sauti za Kiarabu katika Kiswahili kulisababisha mabadiliko aina mbili: Urahisishaji wa sauti za Kiswahili ili ziweze kutamkwa na wasemaji wa Kiswahili, pili ubadilikaji wa maana asilia ya baadhi ya maneno ya Kiarabu yaliyoingizwa katika Kiswahili. Utafiti wake unahusiana na utafiti huu kwa kuwa utafiti huu ulishughulikia ukopaji wa maneno kama athari mojawapo ya mtagusano lugha ya Kiswahili na Kikuyu kwa Kishona. Utafiti huu unatofautiana na utafiti wa Babusa kwa kuwa utafiti wake ni wa kiisimu huku utafiti huu ukiwa wa kiisimujamii.

### 2.2.3 Wingilugha

Wingilugha, kama athari ya mtagusano lugha, ni uwezo wa mtu, watu, jamiilugha ama wananchi katika kuzungumza zaidi ya lugha moja zilizo karibu nao au katika eneo husika au nchi husika. Wingilugha hutokea kwa sababu mbalimbali zikiwemo sababu za kibinafsi, za kijamii, za kisiasa na sababu za kiuchumi anavyosema Malechova, (2016). Wingilugha huwa na manufaa mengi katika jamii kama vile kuleta uhusiano bora kati ya mataifa na katika jamii, ushirikiano wa biashara, maendeleo katika utamaduni na mahusiano bora baina ya jamiilugha mbalimbali katika nchi fulani. Auer na Wei (2009) wanasema kwamba wingilugha ni sehemu ya suluhisho katika matatizo yanayokumba lugha katika jamii. Hali ya wingilugha huleta uthabiti katika jamii, hufanya maendeleo ya kiuchumi kupiga hatua na kuleta ushirikiano katika jamii.

Mberia (2014) anasema kwamba Waafrika ni baadhi ya wanawingilugha duniani kwa sababu ya lugha nyingi zinazowazunguka. Hii ni kwa sababu bara la Afrika ndilo la pili kwa wingilugha baada ya bara la Asia. Hivyo basi, wingilugha ni jambo lisiloepukika barani Afrika kwa kuwa kando na lugha asilia ambazo zinatumika katika mazingira yaliyo rasmi na yasiyo rasmi, lugha za kigeni kama vile Kiingereza, Kifaranza, Kihispania, Kiitaliano, Kihindi na siku hizi Kichina, zinazungumzwa na kutumika katika miktadha isiyo rasmi na miktadha rasmi. Obiols (2002) anasema kuwa katika jamii za wingilugha, wanajamiilugha huamua kutumia lugha nyingine kwa sababu kuu ya mawasiliano, biashara na elimu. Katika jamii za wingilugha, mabadiliko ya lugha hayana budi kutokea kama athari nyingine ya mtagusano lugha hizo.

### 2.2.4 Mabadiliko ya lugha

Mabadiliko ya lugha ni matokeo yanayotokana na kutagusana au kuingiliana kwa lugha mbili au nyingi katika mazingira ya wingilugha kwa muda mrefu. Florian (1998) anatoa mifano ya hali zinazopelekea lugha kubadilika. Hali ya kwanza ikiwa ni kimakro ambapo athari za mabadiliko ya lugha huhusisha sehemu kubwa na watu wengi wa jamiilugha fulani na hali ya kimaikro ambapo mabadiliko ya lugha huonekana na kuanza na mtu mmoja ama kundi dogo la watu katika jamiilugha na hatimaye kuigwa na wanajamiilugha wote. Mabadiliko ya lugha si jambo ambalo mtu ataona likitendeka moja kwa moja ila huwa bayana kupitia kwa matumizi ya lugha husika katika viwango tofauti na kwenye vizazi tofauti vya jamiilugha husika.

Lugha hubadilika kwa sababu mbalimbali kulingana na Maya (2009) na Nettle na Romaine (2000). Mabadiliko ya kwanza ya lugha hutokea kwa aina mbili. Aina ya kwanza ni mabadiliko yanayolazimishwa ambayo hutokea wakati jamiilugha iliyo na hadhi ya chini hulazimika kuacha lugha yao kwa sababu ya shinikizo la jamiilugha iliyo na hadhi ya juu ama iliyo na watu wengi. Wanajamiilugha waliowengi wanaweza kuifanya lugha yao kuwa ya lazima katika jamii kwa sababu ya matumizi yake mengi katika shughuli mbalimbali na nyingi katika jamii. Hali kama hii yaweza kufaulu japo kwa nadra sana kwa sababu kukandamiza lugha moja kunaweza kuifanya ikawa maarufu na kuenea sana kuliko ilivyotarajiwa. Hata hivyo, jamiilugha yaweza kulazimishwa kuacha lugha yao kwa shughuli kama vile utumwa au kupewa dhima chache na za chini katika jamii.

Maya (2009) na Nettle na Romaine (2000) wanasema pia kwamba mabadiliko ya lugha yanaweza kutokea kwa hiari tu. Mabadiliko ya aina hii hutokea pale ambapo wanajamiilugha huamua na kupendelea kutumia lugha nyingine kuliko ile yao asilia. Mabadiliko ya lugha kwa hiari hutokea taratibu na yanaweza kuchukua muda mrefu kwa kuwa hayalazimishwi. Lugha inayopendelewa hatimaye huchukua nafasi ya lugha asilia. Katika mabadiliko ya hiari, wanajamiilugha huanza kuacha kutumia lugha yao asilia kutoka asasi rasmi za kiserikali kama vile kortini, kwenye biashara na siasani, na kuanza kuitumia kwenye miktadha ambayo si rasmi kama vile shughuli za nyumbani na kanisani. Thomason (2000) anaita mabadiliko ya aina hii mfumo wa kutoka juu kwenda chini. Juu kwa maana ya matumizi ya lugha katika asasi za kiserikali na chini kwa maana ya matumizi lugha nyumbani na kwenye miktadha isiyo rasmi. Bartram (2010) anasema kuwa jambo linalopelekea wanajamii kuacha kutumia lugha yao na kutumia lugha nyingine ni mielekeo mbalimbali watakayokuwa nayo kuhusu lugha mpya na pia kuhusu lugha yao.

Florian (1998) na Fasold na Connor (2014) wanasema kuwa mabadiliko ya lugha hutokea kwa kufuata utaratibu na kwa misingi miwili: Msingi wa kwanza ni kuwa lugha hubadilika kwa kutegemea nyakati mbalimbali na maeneo mbalimbali ya mtagusano. Msingi wa pili ni kwamba lugha yoyote huendelea kubadilika katika viwango vyote kama vile fonolojia, mofolojia, semantiki, sintaksia na diskosi. Thomason na Kaufman (1988) wanakubaliana na Florian (1998) kwamba mabadiliko ya lugha hasa katika mazingira ya wingilugha ni jambo lisiloweza kuzuilika. Lugha ikianza kubadilika, hubadilika kwa viwango vyote kwa mfano kiwango cha fonolojia, kiwango cha leksimu, kiwango cha mofolojia na kadhalika. Thomason na Kaufman (kt.) na Florian

(kt.) wanasema kwamba sehemu tu inayoweza kuzuiliwa kubadilika ni lugha ya maandishi pekee wala si lugha ya mazungumzo.

### 2.2.4.1 Kiwango cha Leksimu/Msamiati

Nagy (2010) anasema kwamba panapokuwa na mtagusano kati ya lugha mbili au zaidi, kiwango cha leksia ndicho huathirika pakubwa hasa kwa lugha iliyo na wanajamiilugha wachache. Athari inayotokea kwenye kiwango hiki ni ukopaji wa leksimu kutoka lugha lengwa hadi lugha pokezi. Ukopaji wa leksimu ukiendelea kwa muda mrefu, wingilugha au uhamaji wa lugha hutokea. T'sou (2001) anasema kwamba lugha pokezi inapokopa maneno kutoka lugha chanzi, huhakikisha kwamba maneno yaliyokopwa yamefuata muundo wa lugha ili kukubalika katika matumizi ya maneno hayo.

Utafiti wa Poplack na Meechan (1998) na utafiti wa Van Hout na Muysken (1994) unaonyesha kwamba aina za maneno ambayo hukopwa na lugha ya jamiilugha ya wachache ni nomino, vitenzi na vivumishi. Poplack na Meechan (1998) wanatoa sababu ya ukopaji wa aina hizi za maneno kuwa ndizo za kimsingi katika lugha zinazotumika kwenye shughuli za mawasiliano baina ya wanajamiilugha zinazohusika. T'sou (2001) anasema kuwa baadhi ya nomino ambazo hukopwa kutoka lugha ya wengi ni majina ya vyakula, maneno yanayoashiria shughuli mbalimbali za nyumbani na hata shughuli za kibiashara iwapo wanajamiilugha husika ni wafanyabiashara. Utafiti huu ulitumia maoni ya T'sou (kt.), Poplack na Meechan (kt.) na Van Hout na Muysken (kt.) kubainisha athari za Kiswahili na Kikuyu kwa Kishona nchini Kenya.

#### 2.2.4.2 Kiwango cha Mofolojia

Mtagusano lugha hupelekea ukopaji wa vipengele vya kimofolojia. Habwe na Karanja (2004) wanasema kuwa mofolojia hushughulikia uundaji wa maneno na mnyambuliko wa maneno hasa vitenzi katika lugha husika. Mtagusano lugha huathiri kiwango cha mofolojia kwa njia zifuatazo: lugha pokezi yaweza kuchukua neno zima kutoka lugha chanzi na kulifanyia mabadiliko ili lilingane na muundo wa maneno ya lugha pokezi. Pili, lugha pokezi yaweza kuchukua neno maalum na kulichopeka jinsi lilivyo kwenye lugha hiyo. Maneno haya yanapoingizwa kwenye lugha pokezi, mabadiliko ya lugha hubainika moja kwa moja kupitia mofolojia ya maneno ya lugha pokezi. Mufwene (2014) alitoa mfano wa lugha ya Kiswahili ilipoingia nchini Kongo, maneno ya Kiswahili yalifanyiwa marekebisho kupitia viambishi awali na tamati vya lugha za Kongo kuchopekwa kwenye mizizi ya maneno ya Kiswahili hasa kwenye vitenzi. Kwa mfano neno la Kiswahili –enda, liliongezewa viambishi awali –ba- na viambishi tamati –nga- na likakuwa “baliendanga”. Mufwene (kt.) anasema kwamba ukopaji na utohozi wa vipengele vya kimofolojia ni suala linalowezekana katika mtagusano lugha kwa kutegemea mielekeo mbalimbali ya lugha kwenye mazingira ya wingilugha. Mielekeo ya lugha imejadiliwa kwenye sehemu ya 2.2.5 inayofuata.

### 2.2.5 Mielekeo ya Lugha

Allport (1954) na Hidalgo (1986), wanafafanua mielekeo kuwa ni hali ya kumfikiria mtu au kuwa na hisia kuhusu mtu, jambo, hali fulani kwa njia fulani. Mtu hazaliwi na mielekeo bali hujifunza mielekeo kwa kutegemea mazingira anamojikuta kuhusu mtu, jambo au hali fulani kwa kutegemea hulka zilizopo kuhusu hali hiyo. Baker (1992) na Bartram (2010) wanafafanua mielekeo ya lugha kuwa ni hisia za mtu au watu kuhusu

lugha yao au lugha ya watu wengine katika mazingira ya wingilugha. Mielekeo ya lugha huzua matokeo mbalimbali katika jamii, ambayo yanaweza kuwa ya kuridhisha au ya kutoridhisha anavyosema Sarnoff, (1970)

Triandis (1971) anadai kwamba mielekeo ya lugha ni hali ya kuthamini au kutothamini lugha moja katika mazingira ya wingilugha. Mielekeo ya lugha yaweza kuwa ni dhana iliyo ndani ya mawazo ya mtu kuhusu lugha fulani au mtazamo kupitia vitendo ambavyo huonyesha mielekeo yake kuhusu lugha fulani. Fasold (1984) anakubaliana na Triandis (kt.) kwa kusema kwamba mielekeo ya lugha huanza akilini mwa mtu binafsi kupitia kwa hatua tatu. Hatua ya kwanza ni utambuzi ambao hufanyika mtu anapokuwa na imani kuhusu lugha fulani katika mazingira ya wingilugha. Hatua ya pili ni ya athari ambapo ile mielekeo ya mtu kuhusu lugha fulani huanza kumwathiri kihisia kwa njia chanya au hasi. Hatua ya mwisho ni ya utendaji ambapo mtu huwa tayari kutenda kwa njia ambayo inaonyesha mielekeo yake halisi kuhusu lugha fulani. Hatua ya utendaji inahusu kuitumia lugha katika maeneo mbalimbali katika jamii iwapo mielekeo yake ni chanya au kutoitumia katika maeneo mbalimbali kama vile nyumbani iwapo mielekeo yake ni hasi. Hatua hizi tatu zilisaidia kupima mielekeo ya Washona kuhusu Kiswahili na Kikuyu katika lengo la tatu la utafiti huu.

Mielekeo ya lugha huwa ni tukio la kijamii. Garrett (2010) anafafanua kwamba mielekeo hii ya lugha huwa na jukumu la kujenga maoni kuhusu wazungumzaji wa lugha fulani kupitia kwa matumizi ya lugha yao. Garrett (kt.) anasema mielekeo ya lugha huchochewa na vigezo mbalimbali kama vile tajriba ya mtu kuhusu lugha, mazingira yake na mahusiano yaliyomo katika jamiilugha husika. Garrett, Coupland na

Williams (2003) wanasema kwamba mielekeo ya lugha huja kwa sababu ya uwepo wa lugha mbalimbali na pia mielekeo yaweza kuzua maoni chanya au hasi kuhusu jamiilugha fulani. Garrett, Coupland na Williams (kt.) wanasema kwamba kuna mielekeo aina mbili ya lugha: Mielekeo chanya na mielekeo hasi ya lugha.

#### 2.2.5.1 Mielekeo Chanya ya Lugha

Wolck (2004) alibainisha kwamba iwapo wanajamiilugha wana mielekeo chanya kuhusu lugha husika, basi wao huitumia katika miktadha mbalimbali ya jamii. Baker (1992) anasema kuwa mielekeo ya jamii kuhusu lugha husika ikiwa chanya, basi jamiilugha hiyo huamua kujitambulisha na lugha hiyo kupitia matumizi ya lugha hiyo kwa wingi katika maeneo mbalimbali ya kijamii. Mielekeo chanya kuhusu lugha husika hufanya lugha hiyo iwe thabiti kwa kuwa matumizi yake ni mengi katika jamii.

Al-Nahar (2009) alichunguza mchango wa mielekeo katika udumishaji wa lugha baina ya Waarmeni wa Yordan na kugundua kwamba Waarmeni walikuwa na mielekeo chanya kuhusu lugha yao ya Kiarmeni kwa kuwa waliiona kuwa lugha ya kifahari, rahisi na lugha yenye faida kwao hasa katika kueleza dhana na hisia zao. Lugha ya Kiarmeni ilibainisha utambulisho, utamaduni na historia yao huko Yordani. Al-Nahar aligundua kwamba Waarmeni hawakuruhusu wanawe kutumia lugha tofauti katika maeneo ya nyumbani isipokuwa Kiarmeni pekee. Utafiti wa Al-Nahar ulichangia utafiti huu kwa kuwa mielekeo ya Washona kuhusu Kiswahili ilichunguzwa na kubainika kwamba Washona wanakitumia Kiswahili kwa shughuli mbalimbali katika jamii na maeneo mengi kwa kuwa wana mielekeo chanya.

Dweik na wenzake (2014) walifanya utafiti kuhusu lugha ya Kiarabu mjini Vancouver, Magharibi mwa Kanada na kubainisha kwamba jamii zilizokuwa zinatumia lugha ya Kiarabu nchini humo zilikuwa na mielekeo chanya kuhusu kujifunza na kutumia Kiarabu. Matokeo ya utafiti wao yalionyesha kwamba Waislamu wa asili ya Kiarabu waliamini kwamba lugha ya Kiarabu ndiyo lugha iliyokuwa ya kifahari kwa kuwa ndiyo iliyokuwa imetumiwa katika Korani Takatifu. Wahusika katika utafiti wao walisema kwamba lugha ya Kiarabu ndiyo lugha ya kitaifa iliyo ya kifahari na pia kitambulisho cha Waislamu. Wazazi Waarabu waliwafunza wanao Kiarabu nyumbani na pia waliwapeleka wanao katika shule zilizofunza Kiarabu ili wakajifunze lugha hii waliyojivunia sana. Sawia na utafiti wa Dweik na wenzake, utafiti huu ulishughulikia mielekeo ya Washona kuhusu Kiswahili na pia kuhusu lugha yao wenyewe na kudhihirika kwamba Washona walikuwa na mielekeo chanya kuhusu lugha hizi mbili kwa kuwa zinawasaidia katika mawasiliano.

Dweik na Al-Obaidi (2014) walifanya utafiti baina ya Wakaldayo-Waashuru (Chaldo-Assyrians) nchini Baghdad, Iraqi. Waligundua kwamba Wakaldayo –Waashuru walikuwa wakitumia lugha ya Kiashuru katika maeneo kadhaa hasa nyumbani na katika sehemu za ibada. Walitumia pia lugha ya Kiarabu katika maeneo mbalimbali kama vile uanahabari, kazini na mikutano rasmi. Jamiilugha ya Wakaldayo –Waashuru walionyesha mielekeo chanya kwa lugha za Kiashuru na Kiarabu na kuzitumia lugha zote kwa njia sawa. Licha ya tofauti za kimaeneo kati ya utafiti wa Dweik na Al-Obaidi na utafiti huu, tafiti zote zilifanyika katika mazingira ya wingilugha na matumizi mbalimbali ya lugha baina ya wanajamiilugha husika.

Veettil na wenzake (2020) walibainisha kwamba mielekeo kuhusu lugha ya Kimalayam inayozungumzwa na Wakerala (Keralites) wanaoishi nchini Oman, ilifanya lugha hiyo kuendelea kudumishwa licha ya Wakerala kuwa wachache. Waomani ni watu wakarimu sana kwa Wakerala na wamekuwa na mweleko chanya kwa lugha yao ya Kimalayam. Jambo hili limewafanya Waomani kujifunza lugha ya Wakerala kama vile Washona walivyojifunza lugha za Kiswahili na Kikuyu nchini Kenya ilivyobainika katika utafiti huu.

Khadidja (2013) alichunguza mielekeo mbalimbali ya wanajamiilugha wa Kabyle wanaoishi katika eneo la Oran nchini Algeria. Matokeo ya utafiti wake yalionyesha kwamba wanajamiilugha ya Wakabyle walikuwa na mielekeo chanya kuhusu udumishaji wa lugha yao licha ya shinikisho kutoka kwa lugha maarufu ya kitaifa ya Kiarabu nchini Algeria. Hii ni kwa sababu waliiona lugha yao kuwa ya kifahari na kitambulisho cha utamaduni wao. Wakabyle walikuwa wakitumia lugha yao katika maeneo ya nyumbani na maeneo mbalimbali ya kijamii kama vile katika ibada zao na hivyo ikawa rahisi sana kwa vizazi vyao kujifunza ligha yao. Sawia na utafiti wa Khadidja, utafiti huu ulibainisha mielekeo ya Washona kuhusu lugha yao hasa baada ya Kupewa uraia wa Kenya. Ilibainika kwamba Washona wanatumia lugha yao katika maeneo ya nyumbani na kwenye ibada ili wanao wapate kujifunza lugha yao licha ya shinikizo kutoka lugha maarufu kama vile Kiswahili na Kikuyu.

Simandan (2016) anasema kwamba umuhimu wa mielekeo mbalimbali katika kujifunza lugha ya pili ni kwamba ikiwa watu wana mielekeo chanya kuhusu lugha hiyo, ni hamasisho tosha la kujifunza lugha hiyo. Vivyo hiyo, iwapo mtu ana mielekeo hasi

kuhusu lugha fulani, hataweza kujifunza lugha hiyo. Mielekeo chanya au hasi ya lugha huchochewa na itikadi na imani zilizo katika jamii ambazo pia huamua lugha ya matumizi katika jamii.

**2.2.5.2 Mielekeo Hasi ya lugha**

Mielekeo hasi ya lugha ni hali inayobainika wakati jamiilugha fulani haina juhudi za kutumia lugha yao katika maeneo mbalimbali katika jamii. Mathiot na Garvin (1968) wanasema kwamba mielekeo hasi ya lugha ni hali ya wanajamiilugha ya kutotaka kutumia lugha yao katika maeneo ya kijamii. Kutotumika kwa lugha fulani katika jamii huifanya lugha hiyo kupoteza uthabiti wake wa kiisimujamii. Baker (2011) anasema kwamba iwapo wanajamiilugha wana mielekeo hasi kuhusu lugha fulani, watadhihirisha tabia ya kuona lugha hiyo kama kitu kisichokuwa na umuhimu, kuona umuhimu wa kutumia lugha ya pili kuliko lugha yao kwanza, kutoona haja na umuhimu wa kutumia na kudumisha lugha yao asilia na pia kuwa na fikra kwamba ujuzi wa lugha ya pili ni ishara ya kufaulu maishani. Tabia hizi zote za kubainisha mielekeo hasi ya lugha fulani, huifanya lugha kupoteza uthabiti wa kiisimujamii na kufanya lugha hiyo kuhama au kupotea.

Mielekeo hasi ya lugha yaweza kuwa hadharani au isiwe hadharani. Ginting (2018) alitoa mfano wa wanafunzi wenye asili ya Kikaro waliokuwa wakisomea kwenye Chuo Kikuu cha Medan nchini Indonesia. Wanafunzi hawa walikuwa na mielekeo hasi hasa katika matumizi ya lugha ya Kikaro kwa kuwa walikuwa na mtazamo kwamba matumizi ya lugha ya Kikaro ni kukosa ustaarabu na ni jambo lililopitwa na wakati. Wanafunzi hawa wa Kikaro walikuwa na mazoea ya matumizi ya lugha ya Kiindonesia

kwa kuwa waliionea fahari kuliko lugha yao asilia. Matokeo ni kwamba lugha ya Kikaro ilikosa uthabiti wa kiisimujamii miongoni mwa vijana wanafunzi.

Kulingana na Ginting (2018), mielekeo hasi ya lugha imegawika katika hali tatu. Hali ya kwanza ni uasi wa lugha. Hii ni hali ambapo wanajamiilugha hawaoni haja ya kutumia lugha yao na kukosa kuidumisha katika jamii. Wanajamiilugha hukosa kuienzi lugha yao na hukosa bidii ya kuzuia lugha ya pili isichukue nafasi ya lugha yao asilia. Wanajamiilugha wenye mielekeo hasi kuhusu lugha yao asilia, huathirika kwa urahisi kupitia kwa hali zinazowafanya kuacha kutumia lugha yao na kutumia lugha ya pili kwenye mazungumzo yao ya kila siku katika jamii.

Ginting (2018) anasema kwamba hali ya pili kwenye mielekeo hasi ya lugha ni wanajamiilugha kukosa kuionea lugha yao fahari. Wanajamiilugha wakikosa kuonea lugha yao fahari katika jamii ya wingilugha huwa wanakosa kuitumia na kukosa kuitambua kama chombo cha utambulisho na umoja wao katika jamii ya wingilugha. Kukosa kuonea lugha fahari inamaanisha kwamba wanajamiilugha wana uwezo wa kutumia lugha nyingine kwa mazungumzo na shughuli mbalimbali kwa kuwa hawaoni sababu kuu ya kutumia lugha yao asilia.

Hali ya mwisho kwenye mielekeo hasi ya lugha ni kutotambua kaida za lugha husika. Kutotambua kaida za lugha ni wakati ambapo wanajamiilugha wanakosa kutumia lugha yao vilivyo, kukosa kuzingatia usanifu wa lugha hiyo na pia kukosa kuitumia lugha yao kwa wingi katika mitandao yao ya kijamii. Florian (1998) anasema kwamba kukosa kuhifadhi lugha kwenye maandishi ni kubainisha mielekeo hasi ambapo

wanajamiilugha wanaojua lugha yao hawajali kizazi cha kesho kitajuaje lugha yao ambapo matokeo yake ni kutoweka au kuhama kwa lugha husika.

## 2.2 Tafiti Kuhusu Mtagusano Lugha Duniani

Thomason (2001) anasema kwamba mtagusano lugha upo kila mahali na kwamba hakuna jamiilugha ambayo itaishi bila kutagusana na jamiilugha nyingine duniani. Mtagusano lugha hutokea kwa sababu mbalimbali zinazowezesha watu wa jamiilugha mbalimbali kukutana au kushirikiana. Hata hivyo kuna sehemu nyingine duniani ambapo mtagusano lugha ni wa hali ya juu na sehemu nyingine ambapo mtagusano ni wa hali ya chini. Thomason (2000) anatupatia mfano wa lugha ya Kisali cha Montana ambayo ina mtagusano lugha wa hali ya juu, hali ambayo inaipatia shinikizo la kiuchumi na kijamii la kuhamia hadi lugha ya Kiingereza. Mfano mwingine ni wa wanajamii wanaozungumza lugha ya Kiingereza hasa katika nchi za Marekani. Hawa huwa hawaoni haja ya kujifunza lugha nyingine kwa kuwa lugha ya Kiingereza inajulikana na kutumika karibu duniani kote.

Nove (2021) alichunguza kuhusu uhamaji wa lugha ya wachache hadi lugha ya waliowengi miongoni mwa wakimbizi waliotoka mashariki mwa Uropa na kuhamia sehemu ya Newyork, Marekani. Alishughulikia mtagusano lugha ya Kihasidiki Kiyidi na lugha ya Kiingereza. Utafiti wake ulibainisha kuwa lugha ya Kihasidiki Kiyidi ina wanajamiilugha wachache huko Newyork lakini imedumu kwa vizazi vingi kufuatia upekee katika ushirikiano wa kidemografia na kiitikadi za wanajamiilugha wa Kihasidiki Kiyidi. Wanajamiilugha hawa wana itikadi kwamba familia zao lazima ziwe na watoto wengi, na wafunzwe lugha yao ya kwanza kwa kila jambo kabla ya kufunzwa

lugha ya Kiingereza. Lugha yao pia imefungamanishwa na dini na imani yao. Nove (kt.) aligundua kwamba licha ya mtagusano wa Kihasidiki Kiyidi na lugha maarufu ya Kiingereza, Wayidi wamefaulu kudumisha lugha yao kufuatia itikadi zao na mielekeo yao kuhusu lugha yao. Utafiti wa Nove(kt.) ni muhimu kwa utafiti huu kwa kuwa watafitiwa ni wanajamiilugha wachache na wamefaulu katika kudumisha lugha yao kwenye mazingira ya wingilugha na shinikizo kutoka lugha maarufu za Kiswahili na Kikuyu katika mazingira wanamoishi.

## 2.4 Hali ya Kiisimujamii ya Lugha Duniani

Lugha ni nyingi duniani na hazijasambazika kwa usawa wowote. Sehemu nyingine zina lugha nyingi na sehemu nyingine zina lugha chache. Gordon (2005) anasema kwamba duniani kuna jumla ya lugha 6,912. Makundi makubwa ya lugha maarufu kama vile Kiingereza, Kichina cha Mandarini na Kihispani zinajulikana duniani kote na zina wazungumzaji wengi kuliko lugha nyingine duniani hasa lugha za kiasili. Crystal (1997) anatoa mfano wa lugha ya Kiingereza ambayo huzungumzwa sana duniani kote. Lugha nyingi pia zinaendelea kutoweka hasa zile za kiasili. Kila bara lina idadi tofauti ya lugha kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali la 2.1

**Jedwali 2.1: Idadi ya lugha katika kila Bara Duniani**

| **Bara** | **Idadi ya lugha** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Asia | 2269 | 32.8 |
| Afrika | 2062 | 30.3 |
| Pacific | 1310 | 19.0 |
| Amerika | 1002 | 14.5 |

| | | |
|---|---|---|
| Uropa | 239 | 3.5 |
| **Jumla** | **6912** | **100.0** |

Chanzo: Gordon (2005)

Jedwali 2.1 linaonyesha kwamba Mabara Afrika na Asia ndiyo yanaongoza kwa wingi wa lugha asilia kuliko Mabara mengine duniani huku Bara la Uropa likiwa ndilo lililo na idadi ya chini ya lugha. Hali hii inamaanisha kwamba mtagusano lugha ni jambo ambalo haliwezi kuepukwa kwa kuwa kila uchao, jamiilugha mbalimbali hutangamana kwa sababu mbalimbali kama vile masomo, biashara na utalii anavyosema Weinreich (1953).

## 2.5 Hali ya Kiisimujamii ya Lugha Barani Afrika

Kwa mujibu wa Gordon (Toleo la tano la Ethnologue) (2005), bara Afrika lina lugha 2,092. Mberia (2014) na Kame (2012) wanasema kwamba bara Afrika ni la pili kwa uwingi wa lugha baada ya bara Asia. Bara linalotangulia kwa uwingi lugha ni bara la Asia ambalo lina lugha 2,269 zinazozungumzwa na watu takribani billioni tatu unusu. Kulingana na Greenberg (1963), lugha za kiasilia barani Afrika zimegawika katika makundi manne ambayo ni Niger-congo, Nilo-saharan, Afro-asiatic na Khoisan. Grimes (2009) anasema kwamba Niger-congo ndilo kundi lililo na lugha nyingi (1,436) barani Afrika na hata duniani kote ikilinganishwa na makundi mengine matatu.

Kuna lugha mbalimbali za kiasili zinazozungumzwa katika nchi mbalimbali barani Afrika. Kulingana na Gordon (2005), nchi ya Nigeria inaongoza kwa idadi ya lugha zinazozungumzwa nchini humo, ikifuatwa na Cameroon ambayo ina lugha 247, Kongo ikifuata na lugha mia mbili na sita (206). Nchi ya Sudan ina lugha 120 huku Tanzania

ikiwa na lugha 112. Kenya ina lugha zaidi ya 43 huku Rwanda, Burundi na Djibouti zikiwa na lugha tatu tatu kila moja. Nchi za Swaziland, Mauritania, visiwa vya Comoro na Sao Tome e Principe zina lugha nne zinazozungumzwa nchini humo huku nchi zilizo na idadi ya chini ya lugha barani Afrika zikiwa ni Lesotho na visiwa vya Cape Verde ambapo panazungumzwa lugha mbili tu kwa kila mojawapo. Kwa jumla, nchi nyingi za Afrika zina kati ya lugha kumi na lugha mia moja za kiasili ambazo zina hadhi mbalimbali na majukumu au matumizi mbalimbali. Jedwali 2.2 lifuatalo linaonyesha nchi za Afrika ambazo zina lugha nyingi.

**Jedwali 2.2: Nchi za Afrika Zenye Lugha nyingi**

| | **Nchi za Sub-Saharan** | **Idadi ya lugha zinazozungumzwa humo** |
|---|---|---|
| 1. | Nigeria | 514 |
| 2. | Cameroon | 278 |
| 3. | Congo DRC | 215 |
| 4. | Chad | 131 |
| 5. | Tanzania | 128 |
| 6. | Ghana | 79 |
| 7. | Cote d’Ivoire | 78 |
| 8. | Central African Republic | 71 |
| 9. | Kenya | 69 |
| 10. | Burkina Faso | 68 |
| 11. | Congo Brazzaville | 62 |
| 12. | Mali | 57 |

| | | |
|---|---|---|
| 13. | Benin | 54 |

Chanzo: Gordon (2005)

Jedwali 2.2 linaonyesha nchi kumi na tatu zinazoongoza kwa wingi wa lugha barani Afrika. Nigeria inaongoza kwa lugha 514 huku visiwa vya Cape Verde na nchi ya Lesotho zikiwa na lugha mbili mbili kila moja zinazozungumzwa nchini humo. Hali hii inawezesha mtagusano lugha ambao unazua athari mbalimbali kwa lugha zote zinazohusika.

### 2.5.1 Hadhi ya Lugha za Kiasili Barani Afrika

Lugha mbalimbali za kiasili barani Afrika zina matumizi mbalimbali na hadhi mbalimbali katika jamii. Lugha za kiasili kama vile Luganda nchini Uganda imepewa hadhi ya juu kwa kuwa ina matumizi kadha wa kadha kwa mfano kutumiwa shuleni hasa madarasa ya chini nchini humo. Lugha ya Kilingala katika Demokrasia ya Kongo (DRC), Lugha ya Sango katika taifa la Afrika ya Kati na lugha ya Kisomali nchini Somalia zina hadhi ya juu kwa kuwa zina nguvu za kidemografia na matumizi mengi katika jamii. Lugha ya Hausa ina hadhi ya juu na nguvu za kidemografia Magharibi mwa Afrika. Lugha ya Kiswahili ina hadhi ya juu barani Afrika ikilinganishwa na lugha nyingine kwa sababu ni lugha inayozungumzwa na eneo kubwa linalojumuisha Afrika Mashariki na Afrika ya Kati. Lugha zilizopewa hadhi ya juu zaidi katika nchi nyingi barani Afrika ni lugha za Kigeni kwa mfano Kiingereza na Kifaransa ambazo hutumika kwenye miktadha na shughuli rasmi.

Lugha ya Kishona ina hadhi ya juu nchini Zimbabwe kwa kuwa ina majukumu mengi sana kuliko lugha nyingine ishirini nchini humo. Kishona pia huzungumzwa nchini

Msumbiji, Botswana, Zambia, Afrika Kusini na Kenya. Inabainika kwamba Waafrika ni miongoni mwa wanawingilugha duniani kwa sababu ya kutagusana na lugha mbalimbali na nyingi zinazowazunguka. Nchini Kenya, kuna lugha zaidi ya 43 zinazozungumzwa na Wakenya ikiwemo lugha ya Kishona.

**2.6 Wanajamiilugha wa Kishona**

Hachipola (1998), Mhlanga (2018) na Maho (2009) wanasema kwamba Washona ni kundi la Wabantu ambao asili yao ni Mashariki mwa Zimbabwe, Kaskasini mwa mto Lundi. Wengine huishi Kusini mwa Zambia na sehemu ya kati mwa Msumbiji. Kishona ni mojawapo ya lugha za taifa nchini Zimbabwe kando na lugha ya Kindebele na Kingereza. Kishona hufunzwa katika shule za msingi na huzungumzwa na watu zaidi ya milioni 9.8 nchini Zimbabwe. Gordon (2005) anaorodhesha lahaja tano za Kishona ambazo ni Karanga, Zezuru, Manyika, Ndau na Korekore na kubainisha makundi yao.

Kulingana na Gordon (2005), lahaja tano za Kishona zimepangwa kwa makundi mbalimbali: S14-Karanga (Chikaranga) ni lahaja inayozungumzwa Kusini mwa Zimbabwe karibu na eneo la Masvingo. Karanga huzungumzwa kwenye mkoa wa Midlands katika wilaya za Mberengwa na Zvishavane. Lahaja ya pili ni Kundi la S12-Zezuru (Chizezuru/Wazezuru). Lahaja hii inazungumzwa kwenye sehemu za Mashonaland iliyo kati na Mashariki mwa Zimbabwe, karibu na jiji kuu la Harare. Zezuru ndiyo lahaja inayozungumzwa na Washona wengi nchini Zimbabwe. Lahaja ya tatu ni Kundi la S11-Korekore. Hii ni lahaja inayozungumzwa Kaskazini mwa Zimbabwe. Lahaja mbili za Kishona ni tofauti kidogo na lahaja zingine tatu kimatamshi ambazo wazungumzaji wake wanaelewana kwa kiasi fulani. Lahaja hizi ni S15-Ndau

izungumzwayo Mzumbiji na sehemu ndogo ya Zimbabwe na S13- Manyika ambayo huzungumzwa Mashariki mwa Zimbabwe sehemu iitwayo Chipinge.

Maho (2009) anasema kwamba lahaja za Kishona zinasaidia kutambua Mshona fulani ametoka sehemu gani, ukoo upi, kijiji au mji gani nchini Zimbabwe. Hachipola (1998) anaeleza kuwa nchini Zimbabwe, lugha zote za Kibantu zinaaminika kuwa zilitoka kwa Kishona, hali ambayo imeipatia lugha ya Kishona umaarufu mkubwa ndani na nje ya Zimbabwe. Lugha nyingine zinazozungumzwa nchini Zimbabwe ni pamoja na Chibarwe, Kiingereza, Koisan, Nambya, Shangani, Tonga, Kalanga, Sotho, Tswana, Chewa, Venda, Xhosa na Ndebele.

### 2.6.1 Utamaduni wa Washona Nchini Zimbabwe

Utamaduni wa Washona una vipengele mbalimbali kama vile ukuzaji wa mimea na mifugo, familia na jamii zao, utaratibu wa uongozi na mahusiano ya kisiasa, mbinu za utabibu, dini na imani yao na uchumi wao. Mhalanga (2018) anasema kwamba Washona ni wakuzaji wa mtama, mahindi na mimea mingine kama vile mpunga, maharawe, njugu na viazi ili kupata chakula chao. Wao pia hufuga wanyama kama vile ng’ombe, mbuzi na kondoo kwa matumizi ya chakula kama maziwa na nyama. Mifugo ndiyo ilikuwa ishara ya utajiri wao. Walitumia mtama na mahindi ili kutengeneza mvinyo wao unaojulikana kama *hwahwa* na *sadza*.

Jamii zao huundwa na koo tofautitofauti ambapo makazi yao huitwa *musha* ambayo huwa na nyumba zilizojengwa kwa umbo la mviringo zilizo na paa za nyasi. Kila familia huwa na mzee na familia ambayo ina mke na watoto kadhaa. Kila familia ya

Kishona hujenga nyumba zao ndani ya boma moja ambayo huongozwa na mzee wa boma hilo, yaani baba wa familia hiyo.

Kuhusu mahusiano ya kisiasa, Washona hutawaliwa na utawala wa kurithi kutoka kwa viongozi wao hasa ukoo wa mwanamume. Vijiji vyao hutawaliwa na wasimamizi ambao hurithi uongozi kutoka kwa jamaa wao viongozi. Viongozi wa Washona huheshimiwa kuanzia vijijini hadi mikoani ambapo viongozi hawa hutarajiwa kuongoza watu wao kwa hekima hasa katika kusuluhisha matatizo ya kijamii yanayowakumba mara kwa mara.

Kwenye uwanja wa utabibu, Washona walitumia madawa asilia ili kutibu magonjwa mbalimbali yaliyoibuka katika jamii zao na pia kujikinga kutokana na nguvu za uchawi. Magonjwa sugu ambayo yangepatikana miongoni mwao, yalitibiwa kupitia kwa nguvu za roho kupitia kwa dini yao. Baada ya wamishenari kufika nchini Zimbabwe, utabibu wa kisasa ulikaribishwa na Washona ila kuna wale ambao waliendelea na utabibu wa asilia.

Kuhusu uchumi wa Washona, Danver (2015) anasema kwamba Washona wanajulikana kwa kujitegemea kupitia kazi zao za mikono ili kujikimu kimaisha. Walijulikana kwa kazi za uchongaji na ufuaji wa vyuma mbalimbali. Walikuwa pia ni wafinyanzi waliojulikana ndani na nje ya Zimbabwe. Akina mama walijulikana kwa ujuzi wa kutengeneza vikapu hata sasa kwa biashara. Kuhusu umiliki wa mashamba, walimiliki mashamba kwa pamoja na hivyo haikuwa rahisi kuuza au kununua shamba lililokuwa linamilikiwa na jamii. Iwapo kulikuwa na shamba ambalo halitumiki, lilikuwa linarudishwa kwa jamii ili liweze kupewa kazi nyingine.

### 2.6.2 Dini na Imani ya Washona

Bourdillon (1976) anasema kwamba Washona waliamini kwamba kuna maisha baada ya kifo cha binadamu na kwamba kulikuwa na mbingu au mahali kwema kwa wale waliokuwa wema katika siku zao za kuishi duniani. Waliamini Mungu kwa jina *Mwari* alikuwa anawaona kila walichokuwa wakifanya. Waliamini pia kwamba iwapo mtu aliaga dunia na alikuwa mzuri, basi huyo moja kwa moja alienda kuishi na *Mwari*, na iwapo mtu hakuwa mzuri basi huyo alipotea bure tu hivyo. Ujio wa wamishenari ulileta maoni mapya kuhusu imani yao kuhusu dini ila wamishenari waliwakandamiza Washona kwa kuchukua mashamba yao. Kwa sababu hiyo, Washona walirudia njia zao za kumwabudu mungu wao *Mwari*. Hali hii ilifanya Washona kuwa na makanisa yao yaliyokuwa yanafunza imani yao asilia pamoja na mafunzo ya dini yao kwa njia za Kiafrika.

Danver (2015) anasema kwamba manabii wa Kishona kama vile Johane Marange (1912-1963) na mwenzake Johane Masowe (1914-1973) waliibuka wakati ambapo uchumi wa Zimbabwe ulikuwa umedorora na watu walikuwa wamepoteza matumaini. Manabii hawa hasa Johane Masowe alifanya kazi ya injili nchini Zimbabwe kupitia kanisa aliloanzisha la *Gospel of God* na kuwapatia watu imani kwamba Mungu wao angemaliza shida za kiuchumi walizokuwa wakipitia zilizoletwa na Wazungu.

Nabii Johane Masowe, aliwapa motisha Wazimbabwe kwamba Mungu alikuwa tayari kuwaokoa kutoka kwa mateso ya Wazungu. Mahubiri yake yalileta mwamko mpya kwa watu na hivyo wakamfuata kila alipokwenda. Nabii huyu, alitabiri mwaka wa 1956 kwamba nchi ya Kenya ndiyo iliyokuwa nchi ya ahadi na makao makuu ya uinjilisti

wao. Utabiri huu uliwapa msukumo mpya washiriki wa Kanisa la *Gospel of God* kuanza safari ya kwenda nchini Kenya, hasa jiji kuu la Nairobi ili kutimiza unabii wa mwanzilishi wa kanisa lao. Mwaka wa 1959, Washona wa kwanza walifika nchini Kenya na kuanza kanisa lao la *Gospel of God* mahali ambapo walipewa shamba baadaye na aliyekuwa Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Kenya, hayati Mzee Jomo Kenyatta, eneo la *Valley Road*, jijini Nairobi.

#### 2.6.2.1 Kanisa la *Gospel of God* Nchini Kenya

Wagalla (2019) anasema kwamba kanisa la *Gospel of God* ni kanisa la kiroho la Kiafrika lililoanzishwa Oktoba tarehe 1, 1932 kwenye mlima wa Marimba karibu na Salisbury (Harare siku hizi) na nabii Johanne Masowe. Hii ndiyo tarehe nabii anaaminika kuzaliwa upya na kupewa jukumu la kuhubiri injili na *Mwari*. Waumini wa kanisa hili huabudu siku ya Jumamosi ambayo ni sabato yao kupitia kwa mafundisho ya Biblia. Nchini Kenya, kanisa hili linapatikana jijini Nairobi kwenye barabara ya *Valley Road*, karibu na Chuo Kikuu cha *Daystar*, bewa la Nairobi. Waumini wa kiume hukutana kanisani kuanzia ijumaa jioni kwa matayarisho ya ibada ya siku ya Jumamosi ambayo ni siku ya sabato. Katika ibada yao, waumini wa kiume hukaa sehemu ya mbele huku waumini wa kike wakikaa sehemu ya nyuma ya kanisa wakati wa ibada. Waumini wote huvalia au kujifunika mavazi meupe. Wao huimba na kusoma Biblia kisha inafasiriwa na kiongozi wa ibada kwa waumini wote kwa Kishona huku ikitafsiriwa kwa Kiswahili.

Mafunzo ya kanisa la Washona yanahimiza watoto wa kike kuishi kwa heshima ili waweze kuhudumu kanisani kama masista. Utafiti wa KHRC na UNHCR (2019)

uligundua kwamba familia za Kishona zinaruhusiwa kuwatuma wana wao wa kike kwa hiari kwenda kanisani ili wajifunze kuhudumu kama masista kuanzia miaka minne. Hii ni ishara ya malezi mema katika familia husika ambayo inawaletea fahari kuu katika jamii ya Washona. Masista hufunzwa mafunzo ya ndani ya kidini ili baadaye wawe waombezi wa kanisa lao na jamii yao kwa jumla.

Wanaume, kwa upande mwingine, wana kamati (*Dare*) zao tatu ambazo zinafanya kazi katika jamii na pia kanisani. Kamati ya kwanza inayohusisha wazee kumi na wawili ambao ndio viongozi wa kanisa na jamii ya Washona. Kamati hii ina jukumu la kusuluhisha migogoro yoyote inayoibuka katika jamii na kanisani. Kamati hii pia ndio husimamia sherehe muhimu kama vile ndoa na mazishi. Wana*dare* hii ya kwanza wanastahili kuwa wasiri wa hali ya juu katika shughuli zote za jamii na za kanisani. Kamati ya pili, *dare* ya pili, ni ile inayosimamia eneo fulani ambayo inahusisha wahubiri na wanaume wa eneo hilo. *Dare* ya eneo ina jukumu la kuwapa mafunzo watoto na vijana wa kiume jinsi ya kuishi na maadili mema katika jamii kabla na baada ya ndoa. *Dare* ya vijana ndiyo kamati ya tatu kwenye jamii ya Washona. *Dare* ya vijana huhusisha vijana ambao wamejitolea kuhudumu kanisani kama wahubiri, kuwafunza vijana wenzao maadili mema, kuwahudumia wazee wakongwe, kuwapasha habari *Dare* ya eneo na kuhusika katika mipangilio ya sherehe muhimu za jamiilugha ya Washona.

Shughuli hizi zote za kidini huchangia uthabiti wa kiisimujamii wa Kishona kupitia kwa matumizi yake katika kanisa la *Gospel of God* kwa sababu hapa ndipo lugha hii hutumika sana. Biblia iliyoandikwa kwa Kishona pia imechangia katika udumishaji wa

lugha yao kwa kuwa waumini huhimizwa kuisoma kwa lugha yao ya kwanza ya Kishona.

### 2.6.3 Historia ya Washona Nchini Kenya

Shirika la KHRC kwa ushirikiano na shirika la UNHCR (2019) walitafiti kuhusu asili ya Washona nchini Kenya. Utafiti wao uligundua kwamba Washona walianza safari za umishenari kutoka Zimbabwe kuelekea nchi mbalimbali za Afrika kwa nia ya kuhubiri injili kupitia kwa kanisa la *Gospel of God*. Katika safari zao za umishenari, walipitia Zambia, Malawi na Tanzania ambapo baadhi yao walibaki nyuma katika nchi hizo na kutangamana na wanajamiilugha wengine katika harakati za kueneza injili. Baadhi yao waliendelea na safari kuelekea Afrika mashariki hadi wakaingia nchini Kenya. Lengo lao la kuingia Kenya, anavyosema Wagalla (2019), liliegemea kwenye imani yao ya kidini kuhusu nchi ya Kenya kupitia kwa utabiri wa mwanzilishi wa kanisa lao Nabii Johanne Masowe.

Mwanzilishi wa kanisa lao, kwa jina la Shoniwa Masedza, aliyebadilisha jina na kuitwa Johanne Masowe baada ya kupokea wito wa kuwa nabii, alikuwa ametabiri kwamba Kenya ndiyo iliyokuwa nchi yao ya ahadi katika imani yao na hivyo basi kuwasili kwao nchini Kenya kulikuwa ni kutimiza unabii huo. Johanne Masowe alizaliwa katika Mkoa wa Manicaland, Wilaya ya Makoni Mashariki mwa Zimbabwe. Alikuwa mwana wa pili katika familia ya watoto saba wa  mzee Jack na mama Efie Masedza. Johanne Masowe alianzisha kanisa la *Gospel of God* mwaka wa 1932 na akaendelea kuhubiri hadi alipoaga dunia mwaka wa 1973. Kabla ya kifo chake, Nabii Johanne Masowe alizuru nchi mbalimbali za Afrika kwa ajili ya kueneza injili. Ingawa nabii hakufika Kenya,

aliwaagiza wafuasi wake kuhubiri injili jinsi alivyofanya kwa nchi nyingine za Afrika. Inasemekana kwamba nabii Johanne Masowe aliwatabiria waumini waliokuja Kenya kwamba hatimaye watakubalika kuwa raia wa Kenya.

Kulingana na Mulinya (2020) na ripoti za KHRC na UNHCR (2019), Washona wa kwanza waliofika Kenya kuanzia mwaka wa 1959 hadi 1961 walikuwa wamishenari kumi na sita wakiongozwa na mzee Arthur Dirorimwe akiandamana na Robinson Sichaya, Phillip Muregera, Samuel Chinyanga, Enoc Gavaza, Steven Motsi, Cripen Boka, Edward Manogara, Sensly Gavara, Manjoe, James Mgugu, Martin Zambe, Nxumalo, Mkuta, Kephas Nyandoro na Richard Mpofu. Walipofika Kenya, walijigawa katika makundi mawili ambapo kundi moja lilienda sehemu za Ngong, Kaunti ya Kajiado ambapo walikaribishwa na Wakikuyu watatu Joshua Kiarie, Timothy Muiruri na Gerald Njuguna.  Kundi la pili lilienda maeneo ya Juja ambalo lilikaribishwa na Peter Muigai Kenyatta, mwana wa aliyekuwa Rais wa Kwanza wa Kenya, Mzee Jomo Kenyatta kupitia kwa urafiki wake na mzee wa Kishona Arthur Dirorimwe.

Wakati huo, Kenya ilikuwa imeanza harakati za kupigania uhuru kutoka kwa Wazungu. Baada ya miaka michache, Kenya ilipata uhuru na kufutilia mbali pasipoti na nyaraka za usafiri zilizokuwa zinapeanwa na watawala kutoka Uingereza. Washona wa Kenya walijipata katika njia panda kwa kuwa hawangesajiliwa kama raia wa Kenya kwa vile hawakuwa na stakabadhi za uraia wala za kusafiri kurudi kwao kwa sababu Zimbabwe pia ilipata uhuru na sheria za uraia zikabadilishwa nchini humo. Wakati huo, Washona walikuwa wanaishi katika mitaa ya Kikuyu, Kinoo, Kiambaa na Gitaru. na walikuwa na kanisa lao la *Gospel of God* liliko kwenye barabara ya *Valley Road* jijini Nairobi hadi

sasa. Washona wakawa wakosa uraia kwani hawakuweza kuthibitisha uhalali wao kutoka nchi yao walikotoka kama walivyohitajika kufuatia sheria mpya za uraia za Kenya. Baada ya Kenya kupata uhuru mwaka wa 1963, Washona waliendelea kuhangaika nchini Kenya kutafuta utambulisho wao kama mojawapo ya kabila za Kenya kwa zaidi ya miongo sita bila mafanikio. Lakini juhudi zao zilitambuliwa na aliyekuwa Rais wa nne wa Kenya Uhuru Kenyatta kwa kuwapatia uraia na kuwatambua kama kabila mojawapo la Kenya tarehe 12/12/2020. Kwa miaka hiyo yote, Washona walikuwa wakitangamana na jamiilugha mbalimbali nchini Kenya na hivyo basi utangamano huu umezua mtagusano wa Kishona na lugha mbalimbali za Kenya kama vile Kiswahili na Kikuyu. Watafiti mbalimbali wamechunguza kuhusu Washona kama inavyobainika hapa chini.

### 2.6.4 Hali ya Kiuchumi ya Washona Nchini Kenya

Tafiti za UNHCR (2019) na KNBS (2020) zinabainisha kiwango cha umaskini miongoni mwa Washona ni asilimia 24 zaidi ya Wakenya wengine. Asilimia 52 ya Washona katika kaunti ya Kiambu wanaishi chini ya kiwango cha umaskini ikilinganishwa na asilimia 25 ya wanajamii wanaoishi mijini (UNHCR, 2021). Sababu kuu ni kwamba Washona wengi hawajafanikiwa kupata elimu nchini Kenya kwa sababu ya changamoto za uraia walizozipitia kabla ya kupewa uraia mwishoni mwa mwaka wa 2020. Umaskini huu pia umechangiwa na kutokuwa na stakabadhi na vibali vya uraia kwa muda mrefu nchini Kenya. Jambo hili linafanya Washona wasipate ajira rasmi na badala yake inabidi wajihusishe na kazi za mikono ambazo pia hazileti kipato kikubwa kwao.

Washona wa Kenya hasa wanaume wana karakana za useremala kwenye makazi yao ambapo wana vibali vya kufanya biashara. Wanawake hufanya kazi ya kusuka vikapu kama njia moja ya kujipatia riziki. Kwa kuwa wengine hawakuwa na vitambulisho vya kuwaruhusu kufungua biashara, wengi wa Washona walisaidiwa na majirani zao Wakikuyu ili kufungua biashara wakitumia vitambulisho vyao. Hali hii huwaweka kwenye hatari ya kupoteza biashara zao iwapo aliyewafungulia biashara kwa jina lake si mwaminifu. Ripoti ya KHRC na UNHCR (2019) inasema kuwa baadhi ya Washona walio na vitambulisho walivipata kwa njia isiyo ya halali kwa sababu ya shida walizozipitia. Wengi wao walisaidiwa na majirani zao ili kupata vitambulisho wakitumia majina ya wanajamiilugha wa Kenya kwa mfano Wakikuyu. Washona hutembea masafa marefu wakitafuta wanunuzi wa bidhaa wanazotengeneza kwa mikono hali ambayo iliwaweka kwenye hatari ya kushikwa na polisi kwa kukosa stakabadhi muhimu za kuwa humu nchini.

Kulingana na Landweer (2000) hadhi ya jamiilugha hutegemea uwezo wa kiuchumi au kiwango cha uchumi na historia ya jamiilugha hiyo. Paulston (1994f) anasema kuwa iwapo jamiilugha iliyo na watu wachache iko kwenye kiwango sawa cha kiuchumi na jamiilugha iliyo na idadi kubwa ya wazungumzaji, basi jamiilugha hiyo ina nafasi nzuri ya kudumisha lugha yao. Landweer anaendelea kusema kuwa uthabiti wa lugha yoyote hutegemea misingi imara na halali ya kiuchumi wa hiyo lugha. Lugha ambayo haiwanufaishi wazungumzaji wake kiuchumi hubadilika kwa urahisi na hivyo kukosa uthabiti wake. Lugha ikikosa uthabiti huanza kutoweka na hatimaye kufa na kusahaulika kabisa. Wanajamiilugha wa Kishona wamepitia changamoto nyingi hasa kwa kukosa stakabadhi muhimu za utambulisho. Hali hii inaweka uthabiti wa

kiisimujamii wa lugha yao ya Kishona kwenye matata kwa kuwa lugha yao haiwanufaishi kwa biashara.

### 2.6.5 Familia za Washona Nchini Kenya

Utafiti wa KHRC (2019) unabainisha kwamba mwanaume anaruhusiwa kuoa wake wengi ila maamuzi huwa ni ya mtu binafsi kuhusu jambo hili. Msichana wa Kishona huwa tayari kuanza familia kuanzia miaka 18. Kupanga uzazi hakuruhusiwi kwa kuwa Washona wanaamini watoto ni baraka kutoka kwa *Mwari* na hivyo kupanga uzazi ni kuasi maagizo ya *Mwari* hasa kwa kizazi cha wazee wa Kishona. Hivyo basi familia za Washona huwa na watoto wengi. Nchini Kenya, kwenye familia za Washona, idadi ya wanaokaa kwenye nyumba ni kubwa ikilinganishwa na familia zingine zinazoishi mijini. Kwenye familia za Washona, idadi ya watu wazima wanaokaa kwa nyumba moja ni sawa na familia nyingine za Wakenya mijini ila idadi ya watoto wa Kishona kwenye familia moja ni wengi kuliko familia za Wakenya wengine katika kaunti ya Kiambu. Hali hii inabainisha mzigo mkubwa wa kiuchumi kwa Washona walio na umri wa kufanya kazi.

### 2.6.6 Hali ya Elimu kwa Washona Nchini Kenya

Kwa jumla idadi ya watoto walio na umri wa kusoma katika jamiilugha ya Washona ni ya chini nchini Kenya kwa viwango vya shule za msingi na pia shule za sekondari. Utafiti wa KHRC (2019) uligundua kwamba kuna tofauti ya kijinsia katika maswala ya elimu kwa kuwa jinsia ya kike wengi hawajapata elimu ikilinganishwa na wanajamiilugha wa jinsia ya kiume. Hii ni kwa sababu ya utamaduni wao ambapo wanaamini kwamba mwanamke anafaa kukaa nyumbani ili atunze familia. Wasichana

huanza kupewa mafunzo mapema kuhusu maadili mema ya kutunza familia. Jambo lingine linalosababisha tofauti hizi za kielimu kati ya watoto wa Kishona na watoto wa jamiilugha nyingine za Kenya ni ile hali ya kukosa vibali na vyeti vya kimsingi kama vile vyeti vya kuzaliwa ambavyo vingewawezesha Washona kusajiliwa shuleni (KHRC na UNHCR,2019).

### 2.6.7 Yaliyoandikwa kuhusu Washona na Lugha yao

Muchena na Jakaza (2022) walichunguza kuhusu mambo yanayochangia kutoweka kwa lugha ya Kishona inayozungumzwa nchini Kenya. Kupitia utafiti wa maktabani, Muchena na Jakaza waligundua kwamba lugha ya Kishona nchini Kenya imo katika hatari ya kuangamia kwa sababu tatu: Kwanza ni hali ambayo imewafanya Washona kukubali utamaduni wa kabila za Wakenya kama njia mojawapo ya kukubalika na kutambulika katika jamii, kwa mfano kuchukua majina ya kabila tofauti za Kenya ili kupata vitambulisho. Sababu ya pili ni ya kidini ambapo Washona walikuja kama wamishenari na lazima wangejifunza lugha maarufu za Kenya ili waweze kufanya kazi yao barababara. Sababu ya tatu ni ya kiuchumi ambapo kazi wanazozifanya kwa ajili ya kujikimu kimaisha zinahitaji kwamba wazungumze Kiswahili na lugha nyingine asilia za Kenya ili waweze kufanya biashara kwa urahisi. Sababu hizi tatu zina athari ya moja kwa moja kwa lugha yao kwa kuwa inabidi watagusane na kujifunza lugha za jamiilugha mbalimbali za Kenya. Utafiti wa Muchena na Jakaza unatofautiana na utafiti huu kwa sababu wao walitumia utafiti wa maktabani kushughulikia uwezekano wa utowekaji wa lugha ya Kishona huku utafiti huu ukiwa wa nyanjani ambao unashughulikia athari za Kiswahili na Kikuyu kwa uthabiti wa kiisimujamii wa Kishona nchini Kenya.

Wagalla (2019) alitafiti kuhusu utambulisho na utaifa wa Washona nchini Kenya. Aliangalia changamoto ambazo zimewafanya Washona kukosa uraia nchini Kenya kwa zaidi ya miaka hamsini tangu Kenya kupata uhuru. Katika utafiti wake, alijikita katika muungano wa kihistoria wa Washona baina ya Zimbabwe na Kenya, mbinu zao za kukabiliana na changamoto za kuishi bila uraia nchini Kenya na kiwango cha utangamano na mwingiliano wao nchini Kenya. Utafiti huu ulihusisha Kabila la Washona nchini Kenya katika kuchunguza athari za Kiswahili na Kikuyu kwa Uthabiti wa Kiisimujamii wa Kishona nchini Kenya.

Shirika la KHRC kwa ushirikiano na Shirika la UNHCR (2019) walifanya ripoti za hali ya uraia wa jamii ya Washona nchini Kenya. Kwenye ripoti yao, waligundua kwamba Washona wameishi nchini Kenya kwa miaka mingi bila utambulisho hali ambayo imewalazimu kujifunza baadhi ya lugha za Kenya zinazowazunguka kama njia mojawapo ya kukubalika katika jamii. Ripoti ya mashirika haya ilibainisha kuwa Washona wanazungumza Kiswahili na Kikuyu kwa ufasaha. Japo utafiti huu ulitaja lugha hizi, haukubainisha ni vipi lugha ya Kishona imeathiriwa kiisimujamii na lugha hizi maarufu katika makazi wanamoishi. Ripoti hiyo pia haikubainisha ni kizazi kipi ambacho kimeathiriwa sana na mtagusano wa Kiswahili na Kikuyu kwa lugha yao ya Kishona na hivyo basi utafiti huu utajaza pengo hilo.

Machakanja (2006) alilinganua na kulinganisha sitiari za Kishona na Kiingereza katika mazingira yanayofanana ili kubainisha tofauti za kiisimu na za kitamaduni. Aligundua kwamba kuna sitiari zinazofanana baina ya lugha hizi mbili hasa zile za kitamaduni. Hii ni kwa sababu sitiari za kitamaduni hujengwa kutokana na mazingira anamoishi

binadamu. Utafiti wa Machakanja (kt.) ulifanana na huu kwa kipengele kimoja tu ambacho ni lugha ya Kishona ambayo imeshughulikiwa katika utafiti huu. Utafiti wa Machakanja ulitofautiana na utafiti huu kwa sababu utafiti wake ni wa kiisimu ilhali utafiti huu ni wa kiisimujamii ulioshughulikia athari za Kiswahili na Kikuyu kwa uthabiti wa Kishona nchini Kenya.

Maandishi haya kuhusu Washona na lugha yao yanatupeleka kwenye sehemu ya yaliyoandikwa kuhusu Kiswahili na Kikuyu nchini Kenya. Kwenye sura ya kwanza sehemu ya 1.6, utafiti ulishughulikia upeo na mipaka ya utafiti ambapo ilibainika kwamba lugha zinazoshughulikiwa kwenye utafiti huu ni Kishona, Kiswahili na Kikuyu. Kwa misingi hii, sehemu zifuatazo za 2.7 na 2.8 zitaangazia lugha za Kiswahili na Kikuyu kwa kifupi.

## 2.7 Lugha ya Kiswahili

Agoya (2012) anasema kwamba Kiswahili ni mojawapo ya lugha asilia nchini Kenya ambayo imepewa hadhi ya juu kuliko lugha nyingine zote za kiasilia. Tangu mwaka wa 1963, lugha ya Kiswahili ilitambulika kama lugha ya taifa na pia lugha rasmi kulingana na katiba ya Kenya ya mwaka 2010. Kiswahili ni lugha iliyo katika kundi la Kibantu inayozungumzwa na Wabantu wa pwani mwa Kenya na Tanzania na ina lahaja nyingi kama vile Kimvita, Kibajuni, Kisiu, Kiamu, Kipate, Kivumba, Kiunguja na nyinginezo.

Lugha ya Kiswahili imeenea katika nchi za Afrika Mashariki na Kati. Githaiga (2022) anasema kwamba Lugha hii ilikubalika na jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka wa 2017 kama lugha rasmi katika nchi zote za jumuiya ya Afrika Mashariki kama vile Kenya, Tanzania, Uganda, Rwanda, Burundi, Sudan Kusini na Demokrasia ya Kongo.

Mwaka wa 2022, Taifa la Uganda lilipitisha sheria kupitia kwa bunge lao kwamba Kiswahili iwe lugha rasmi ya pili nchini humo baada ya Kiingereza. Isitoshe, Shirika la UNESCO lilitambua Julai 7 kila mwaka kuwa siku ya kuienzi lugha ya Kiswahili duniani.

Kimemia (2002) anasema kuwa Kiswahili ni lugha ya kuwaunganisha Wakenya na kujenga utaifa wao na kukuza uzalendo wao. Naye Githiora (2002) anasema kwamba lugha ya Kiswahili inatumika kama Lingua franka baina ya makabila mbalimbali nchini hasa mijini ambapo kuna hali ya wingilugha. Hutumika katika miktadha rasmi kama vile kortini, masomoni kuanzia chekechea hadi vyuo vikuu, kwenye biashara, katika sekta ya uchukuzi, na matumizi mengine mengi. Ontieri (2017) anasema kwamba Kiswahili hutumika kama nyenzo ya kufundishia shuleni na vyuoni nchini Tanzania lakini nchini Kenya inafundishwa kama mojawapo ya somo kuanzia shule za msingi hadi vyuoni.

Kufikia sasa, lugha ya Kiswahili imeendelea kupata umaarufu na kuzambaa hadi mataifa ya kigeni kupitia juhudi za Wamishenari hasa Wajerumani ambao walitafiti na kuchapisha vitabu na kuanzisha masomo ya lugha za Kiafrika katika vyuo vikuu Marekani, Uingereza, Ujerumani na siku hizi Uchina. Lugha ya Kiswahili imevutia watafiti wengi wa Kiafrika na Wageni kwa sababu ya upekee wake. Tafiti hizi zinaendelea kueneza lugha hii kila uchao anavyosema Amatubi (2002), na kuiafanya kuwa thabiti.

Utangazaji kupitia kwa vyombo vya habari Afrika Mashariki na nje ya Afrika umefanya pia Kiswahili kupata umaarufu na kuendelea anavyosema Githiora (2002). Yeye

anasema kwamba nchini Kenya, lugha ya Kiswahili inatumika katika vyombo vya habari kama vile redio, televisheni na magazetini. Vitabu na majarida mengi ambayo yamechapishwa kwa Kiswahili. Were-Mwaro (2002) anasema kuwa idhaa za utangazaji duniani kama vile *Radio China*, *Dutche Welle* (DW,Ujerumani), *Radio Moscow*, *Voice of America*, na BBC zimechangia katika kueneza Kiswahili ulimwenguni kote na kuifanya kuwa lugha ya kimataifa. Lugha ya Kiswahili imeendelea kuwa na uthabiti wa kiisimujamii kwa sababu ya mielekeo chanya waliyonayo wazungumzaji wake kama ilivyojadiliwa kwenye sehemu ya 2.7.1 ifuatayo. Kiswahili ni mojawapo ya lugha ambazo ziliangaziwa kwenye utafiti huu kuhusu athari zake kwa uthabiti wa kiisimujamii kwa Kishona nchini Kenya.

### 2.7.1 Mielekeo Kuhusu Kiswahili Nchini Kenya

Muaka (2011) na Orcutt-Gachiri (2009) wanadai kwamba hata ingawa Kiswahili ni lugha ya taifa na rasmi nchini Kenya, Wakenya hawajaipatia hadhi ya juu kuliko Kiingereza, hasa katika maeneo rasmi kama vile elimu, afisi za serikali na bungeni. Orcutt-Gachiri anasema kwamba Wakenya hawajaitambua lugha ya Kiswahili kama lugha ya kimataifa bali wanaiona kama lugha mojawapo maarufu Afrika Mashariki. Naye Nabea (2009) anasema kwamba watu wengi huchukulia Kiswahili kama lugha ya kuwaunganisha Wakenya na lugha ya kuondoa ukabila. Mielekeo ya Washona kuhusu Kiswahili ilichunguzwa katika utafiti huu ili kubainisha iwapo lugha ya Kishona imeathiriwa na Kiswahili. Watafiti mbalimbali wafuatao wamechunguza kuhusu mieleko ya Kiswahili chini Kenya.

Mohochi (2005) alitafitia mielekeo ya Kiswahili katika mitihani ya kitaifa nchini Kenya baina ya wanafunzi wa mkoa wa Nyanza na mkoa wa Pwani. Utafiti wake uligundua kwamba mielekeo huathiri matokeo ya wanafunzi katika mitihani ya kitaifa. Mohochi alitambua kwamba mielekeo ya wanafunzi waliotafitiwa ilikuwa sawa kinyume na imani ya wengi kwamba Mkoani Nyanza, mielekeo kuhusu Kiswahili ni hasi. Aidha, utafiti wake ulihitimisha kwamba mielekeo haiathiri matokeo ya wanafunzi kwa sababu kuna wanafunzi walioanguka mtihani wa Kiswahili licha ya kuwa na mielekeo chanya. Utafiti wa Mohochi unatofautiana na utafiti huu kwa kuwa yeye alishughulikia mielekeo ya wanafunzi pekee ilhali utafiti huu uliangazia mielekeo ya Washona wa umri wote kuanzia watoto hadi wazee. Usawa wa utafiti huu na wa Mohochi ni kwamba tafiti zote zinashughulikia mielekeo ya Kiswahili japo kwa watafitiwa tofauti.

Utafiti wa Babusa (2019) ulichanganua na kulinganua mielekeo ya wanafunzi wa shule za upili kati ya Mkoa wa Pwani na Mkoa wa Nairobi nchini Kenya kuhusu Kiswahili, viwango vya umilisi wa Kiswahili na sababu ambazo ziliwafanya kuwa na mielekeo iliyojitokeza, kimkoa na kijinsia. Matokeo ya utafiti wake yalibainisha kwamba wanafunzi wa mkoa wa Pwani walikuwa na mielekeo chanya zaidi kuhusu Kiswahili kuliko wanafunzi wa mkoa wa Nairobi. Utafiti wake pia ulibainisha kwamba wasichana walikuwa na mielekeo chanya kuhusu Kiswahili kuliko wanafunzi wavulana kupitia kwa matumizi mbalimbali ya Kiswahili.

Ontieri (2017) anasema kwamba mielekeo ya Wakenya kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili itakwaza kukubalika kwake kama lugha rasmi. Fasold (1984) anafafanua kuwa mielekeo kuhusu lugha yaweza kuilenga lugha husika, wasemaji wake, maswala

ya uimarishwaji wa lugha pamoja na juhudi za uendelezaji wake. Wasomi wengi katika nyanja mbalimbali isipokuwa wale wa Kiswahili wana mazoea ya kutumia Kiingereza katika shughuli zao nyingi za kikazi. Lugha ya Kiswahili imepewa hadhi ya juu kuliko lugha za kiasili nchini Kenya kama vile Kikuyu na lugha nyingine.

## 2.8 Lugha ya Kikuyu Nchini Kenya

Ripoti ya takwimu ya kitaifa ya idadi ya watu nchini Kenya mwaka wa 2019 (KNBS) inabainisha kuwa jamii ya Kikuyu ndiyo iliyo na idadi kubwa ya watu nchini Kenya ambao ni zaidi ya milioni 8.1. (Kenya National Bureau of Statistics 2019). Kibui (2014) na Kamau (2015) wanasema kwamba lugha ya Kikuyu ina wazungumzaji wengi nchini Kenya na huzungumzwa kwa wingi katika eneo la kati nchini Kenya linalojumuisha Kaunti nne ambazo ni Nyandarua, Nyeri, Murang’a na Kiambu. Muriuki (1976) anasema kwamba miji mikuu ya Kenya kama vile jiji la Nairobi, Nakuru na Eldoret ina idadi kubwa ya wazungumzaji wa Kikuyu. Hali hii imeipa lugha ya Kikuyu uthabiti wa kiisimujamii kwa kuwa ina matumizi mapana nchini Kenya kama vile katika biashara. Kikuyu ni mojawapo ya lugha zinazoshughulikiwa katika utafiti huu kwa kuwa wanajamiilugha wa Kishona walikaribishwa nchini Kenya na Wakikuyu mwishoni mwa miaka ya 1950 na pia maeneo wanamoishi ni makazi ya idadi kubwa ya wanajamiilugha Wakikuyu kama anavyosema Kamau (2015).

Kibui (2014) alifanya uchunguzi kuhusu sera ya lugha nchini Kenya na kugundua kwamba lugha zilizo na wazungumzaji wengi nchini Kenya ni Kikuyu, dholuo na Kiluhya. Alisema kwamba Kikuyu ndiyo lugha inayoongoza kwa wingi wa wazungumzaji nchini Kenya. Lugha ya Kikuyu inahusiana na lugha nyingine kama vile

Kimbeere, Kimeru na Kiembu ambao ni majirani wa Wakikuyu. Katika Miji mikuu nchini Kenya, idadi ya Wakikuyu ni kubwa kwa kuwa wengi wao ni wafanyabiashara. Hali hii imechangia Kikuyu kuwa thabiti kwa kuwa wanajamiilugha wengine wamejifunza Kikuyu ili kurahisisha utangamano katika biashara.

Muchemi (2011) alitafiti kuhusu athari za mtagusano Kikuyu na Kiingereza baina ya vijana wa mashambani. Aligundua kwamba lugha ya Kiingereza ina athari kwa umilisi wa Kikuyu kwa vijana wa mashambani hasa kwa sababu ya matumizi ya Kiingereza katika shule za upili. Mucheni aligundua kwamba lugha ya Kikuyu ilikuwa imeanza kupoteza vipengele fulani vya kiisimu kama vile mpangilio wa maneno katika sentensi. Utafiti wa Muchemi (kt.) ni muhimu kwa utafiti huu kwa kuwa ulibainisha kwamba mtagusano baina ya lugha mbili au zaidi huleta athari mbalimbali kama vile kukopa maneno kutoka kwa lugha moja hadi lugha nyingine, kupendelea kutumia lugha moja kuliko lugha nyingine na pia Kikuyu ni mojawapo ya lugha zinazoshughulikiwa katika utafiti huu. Kama tulivyokwisha kutaja hapo awali, mtagusano lugha ukifanyika, lugha moja yaweza kudumumishwa huku nyingine ikipoteza uthabiti wake wa kiisimujamii. Sehemu ifuatayo inafafanua udumishaji wa lugha kwenye jamii za wingilugha.

## 2.9 Udumishaji wa Lugha

Udumishaji wa lugha ni hali ya kukuza uwepo, uhai na matumizi ya lugha asilia licha ya kukumbwa na shinikizo kutoka lugha nyingine maarufu zilizo na idadi kubwa ya wazungumzaji. Hii ina maana kwamba lugha inayodumishwa ina uwezo mkubwa wa kujikinga kutoka athari zitokanazo na lugha maarufu (Batibo 2005 na Fishman 1989). Uwezo wa kudumisha lugha hubainika kupitia matumizi yake miongoni mwa vijana na

watoto, matumizi katika maeneo na shughuli mbalimbali za jamii na matumizi yake kwenye maeneo rasmi. Matumizi haya mbalimbali ya lugha katika jamii huifanya lugha hiyo kuwa imara na kupata uthabiti wa kiisimujamii anavyosema Fishman (1989).

Umuhimu wa kudumisha lugha umefafanuliwa na Wolck (2004). Anasema kwamba kudumisha lugha ni kuitumia kwa uaminifu wote, kurithisha vizazi vyote na kuonyesha mielekeo chanya kuhusu lugha hiyo. Wolck anabainisha sababu tisa za kijumla zinazohusishwa na udumishaji na uhamaji wa lugha. Kulingana naye, sababu kuu ya udumishaji wa lugha ni kuirithisha kutoka kwa wazazi hadi kwa watoto wao. Pale ambapo kuna mwachano wa vizazi katika matumizi ya lugha, wakati mababu hutumia lugha zao asilia kuongea na wajukuu wao, wazazi kutumia lugha hiyo asilia kuongea na wazazi wao lakini wanatumia lugha nyingine wanapoongea na watoto wao, pana uwezekano wa kufa kwa lugha. Iwapo ni sharti lugha idumishwe, basi lazima kuwe na mwendelezo wa vizazi na kuwe na urithisho wa lugha kutoka kwa wazazi hadi kwa watoto wao.

Pauwels (2005), Baker (2011) na Richards na Schmidt (2002) wanafafanua udumishaji lugha kama hali ya jamiilugha kuendelea kutumia lugha yao katika baadhi au miktadha yote ya jamii licha ya kuwepo kwa shinikizo kutoka kwa lugha iliyo na wazungumzaji wengi. Kulingana nao, udumishaji wa lugha huchochewa na uchumi hasa matumizi yake katika biashara, wanajamiilugha kuifahamu lugha yao vizuri, matumizi katika elimu, matumizi yake katika vyombo vya habari kama vile runinga, redio, magazeti na kadhalika.

Paulston (1994f) anadai kwamba udumishaji wa lugha waweza kutazamwa kama zao la kijamii la makabila ambayo yanashindania huduma muhimu za kiserikali na kwamba uamuzi na uaminifu wa kutumia lugha fulani ni mbinu inayoteuliwa na jamiilugha hiyo kwa minajili ya kuendelea kukaa kwa mazingira ya wingilugha. Hali hii hutokea pale ambapo jamiilugha huona kwamba kujifunza lugha nyingine kutakuwa na manufaa kwa watoto wao. Hapo jamiilugha husika huwa wanauwililugha wanapohamia matumizi ya lugha ya pili ambayo ni lugha iliyo na hadhi ya juu katika jamii. Hata hivyo, wanajamiilugha hawa wanaponyanyaswa ama kukosa ajira, wao hurudia lugha yao ya kwanza kama mkakati wa uhamazishaji wa jamiilugha yao na matokeo huwa ni udumishaji lugha usiotarajiwa. Hali kama hii imeshuhudiwa katika utafiti huu ambapo watafitiwa (Washona) wamehangaika sana kupata huduma muhimu za kiserikali nchini Kenya kama vile huduma za afya na elimu. Jambo hili liliwapelekea kudumisha lugha yao ili kuwaliwaza na pia kuficha siri ya mazungumzo yao. Hatimaye walipopewa uraia mwishoni mwa mwaka wa 2020, walipata nguvu mpya za kudumisha lugha yao.

Veettil, Binu na Karthikeyan (2020) walifanya utafiti kuhusu udumishaji wa lugha baina ya jamiilugha ya Wakerala wanaoishi nchini Oman. Oman ni nchi ya wingilugha ambapo lugha ya Kiarabu ndiyo inazungumzwa na idadi kubwa ya watu huku lugha za Kiingereza, Balushi, Kiswahili na lugha nyingine zikiwa na idadi ya chini ya wazungumzaji. Lugha ya Wakerala (Kimalayalam) ina asili yake katika jimbo la Kerala, India. Wakerala hufanya kazi katika sekta mbalimbali kama vile elimu, afya, biashara, teknolojia na vyombo vya habari ambapo wanalazimika kutumia lugha za Kiingereza, Kiarabu au Kihindi katika utangamano wao na wanajamiilugha zingine za Oman**.**

Matokeo ya utafiti wa Veettil, Binu na Karthikeyan (2020) yalibainisha kuwa udumishaji wa Kimalayalam uliwezeshwa na muundo wa mtandao wao kijamii, mielekeo yao na ya wenyeji wao kuhusu lugha ya Kimalayalam na juhudi za asasi za kiserikali nchini Oman kuhusu lugha hiyo kama vile kufundisha lugha ya Kimalayalam kama lugha ya ziada shuleni, kupitia vyombo vya habari kama vile magazeti yaliyoandikwa kwa Kimalayalam, kutazama chaneli za runinga za Kimalayam na kujihusisha na mijadala ya siasa mitandaoni wakitumia lugha yao. Utafiti wa Veettil, Binu na Karthikeyan (2020) ni sawia na utafiti huu kwa kuwa watafitiwa ambao ni Washona wana idadi ya chini nchini Kenya na pia mbinu mbalimbali za kudumisha lugha yao ziliangaziwa na ikabainika kwamba mtandao wao wa kijamii ni imara na ni nguzo kuu ya udumishaji wa lugha yao.

Utafiti wa Fang (2017) kuhusu udumishaji wa lugha ya wanajamiilugha wachache katika eneo la Shanghai, Uchina ulibainisha kwamba lugha za wachache katika eneo la Shanghai, Han na Dong zilikumbwa na changamoto nyingi sana ikiwemo shinikisho kutoka jamiilugha zilizo na idadi kubwa ya wazungumzaji. Fang (kt.) aliorodhesha mbinu za udumishaji wa lugha ya wachache katika jamii kama vile matumizi ya lugha husika, usaidizi kutoka asasi za kiserikali, mielekeo chanya kuhusu lugha za wachache, matumizi katika elimu kwa mfano kufunza lugha ya pili nyumbani na katika shule za msingi katika jimbo la Liping na sera za nchi kuhusu lugha husika. Matokeo yaliashiria kwamba lugha ya Han ilianza kushabikiwa na wengi hasa ilipoanza kufunzwa katika shule za msingi katika eneo la Shanghai.

Utafiti wa Hamde (2005) kuhusu udumishaji wa lugha ya Kibilini (Blin) miongoni mwa Waeritrea wanaoishi Eritrea na Waeritrea waliohamia nchini Uswidi, ulibainisha kuwa juhudi kubwa za kidini zilionekana katika harakati za kufufua na kudumisha lugha ya Kibilini. Utafiti wa Hamde (kt) ulionyesha kwamba matumizi ya lugha ya Kibilini katika shughuli mbalimbali za kidini yalileta faida kubwa kwa kufufua na kuendeleza lugha ya Kibilini kwa kuwa katika miaka ya awali, lugha ya Kibilini ilikuwa imepigwa marufuku katika shughuli za ukateksti kwenye dini ya kikatoliki na hivyo ikaanza kudidimia. Wakati huo, lugha ya Kitigirinya ilipewa kipaumbele huku wanafunzi wa upadre na utawa waliojaribu kutumia Kibilini wakipewa adhabu kali. Jambo hili lilipelekea wanafunzi hawa kukoma kutumia lugha hii katika maeneo ya kanisani. Baadaye, kuanzia mwaka wa 1990, Vatican iliingilia kati na kutatua shida hiyo na kupatia lugha ya Kibilini hadhi ya kutumika. Maamuzi haya ya Vatican yalichochea shughuli za kufufua na kuendeleza lugha ya Kibilini ambayo ilikuwa imehama na kudidimia. Utafiti wa Hamde unakaribiana na utafiti huu kwa kuwa juhudi za kidini za kudumisha Kishona nchini Kenya zilichunguzwa.

Utafiti wa Iseke (2013) ulichunguza juhudi za wazee nchini Kanada katika udumishaji wa lugha ya Kimichifu. Iseke alitambua kuwa wazee walisisitiza kutumia lugha ya Kimichifu katika kusimulia hadithi kwa watoto. Hadithi hizi kwa watoto kwa lugha ya Kimichifu zilisaidia kuendeleza utamaduni wa Wamichifu kupitia kwa lugha. Utafiti wa Iseke (kt.) unasabihiana na utafiti uliofanywa na *Department of Culture, Language, Elders and Youth* (2014) huko Canada uliotambua kwamba wazee ni hazina kuu katika udumishaji wa utamaduni wa jamii hasa lugha. Utafiti wa Iseke ni muhimu kwa utafiti

huu kwa kuwa juhudi za wazee zimeangaziwa katika udumishaji wa Kishona nchini Kenya.

Kedrebéogo (1998) alitafiti kuhusu juhudi za udumishaji wa lugha ya Kikoromba nchini Bukinafaso. Wakoromba ni mojawapo ya jamiilugha 42 nchini Bukinafaso ambao wamepakana na wanajamiilugha ya Kimoore na lugha nyingine zilizo karibu nao. Kedrebéogo aligundua kwamba uhamaji wa lugha ya Kikoromba umepiga hatua kubwa kwa sababu nyingi kama vile matumizi ya lugha ya Kimoose katika maeneo ya nyumbani, ndoa baina yao na Wamoose, biashara na kupewa hadhi ya juu kwa lugha ya Kimoose. Utafiti wake ulibainisha pia kwamba watoto wa Kikoromba wanazungumza lugha ya Kimoose kama lugha yao ya kwanza. Hali hii inaashiria kwamba uhamaji wa lugha uko katika kiwango cha juu kwa vile imebainika kwamba wazazi hawawafundishi watoto wao lugha yao ya kwanza. Utafiti wa Kedrebéogo ulibainisha juhudi za udumishaji wa lugha ya Kikoromba zinazoonekana tu kwa wazee ambao ndio huthamini lugha yao asilia. Utafiti wa Kedrebéogo unahusiana na utafiti huu kwa kuwa lengo mojawapo la utafiti huu ni kubainisha iwapo Washona wamefaulu kudumisha lugha yao nchini Kenya.

McDuling na Barnes (2012) alitafitia kuhusu udumishaji wa lugha ya Kigiriki nchini Afrika Kusini baina ya wanafunzi wa vyuo vikuu nchini humo na kugundua kwamba Wagiriki walikuwa na mikutano ya sherehe tofauti za kijamii kama vile harusi na densi za vilabuni kwa minajili ya kukutana na kuzungumza lugha yao. McDuling na Barnes waligundua kwamba wanafunzi wengi walijihusisha na hafla tofauti za chuoni kupitia michezo ya kuigiza ya Kigiriki, mavazi na vyakula, ibada na mikutano ya jinsia ya

wanafunzi wa Kigiriki nchini Afrika Kusini. Mikutano hii yote ililenga kuendeleza na kudumisha lugha ya Kigiriki. Utafiti wa McDuling na Barnes ulikuwa na manufaa kwa utafiti huu kwa kuwa utafiti huu ulichunguza mbinu mbalimbali za kudumisha Kishona nchini Kenya. Utafiti wa McDuling na Barnes ulijikita kwenye wanafunzi wa vyuo vikuu pekee ilhali utafiti huu ulijikita kwenye watafitiwa wa umri wote wa jamiilugha ya Kishona.

Van Aswegen (2008) alitafitia udumishaji na uhamaji wa lugha ya Kimaale ambayo ina wazungumzaji wachache nchini Ethiopia. Yeye alishughulikia michakato ya kijamii inayosaidia Wamaale katika udumishaji wa lugha yao. Aligundua kuwa Lugha ya Kimaale imedumishwa kwa sababu ya elimu ya lugha za kwanza nchini Ethiopia na pia juhudi za wazazi za kufunza wana wao lugha asilia. Utafiti wa Van Aswegen ni muhimu kwa utafiti huu kwa kuwa ulibainisha michakato ya kudumisha lugha ya wanajamiilugha wachache sawia na watafitiwa katika utafiti huu ambao ni wachache nchini Kenya na juhudi zao za kudumisha lugha yao ya Kishona licha ya shinikizo ya lugha maarufu nchini Kenya.

Bichang’a (2019) alitafitia lugha ya Ilwana katika kaunti ya Tana River, Eneobunge la Bura ili kuona iwapo lugha hiyo imehama au imedumishwa. Lugha ya Ilwana ina idadi ndogo ya wazungumzaji katika kaunti ya Tana River na hivyo changamoto ya kwanza kwa udumishaji wa lugha hii ni idadi ndogo ya wazungumzaji. Bichang’a aligundua kuwa, matumizi ya Ilwana yamepungua hasa katika maeneo ya nyumbani na katika jamii kwa sababu zifuatazo: Kwanza, wazazi hawajatia juhudi katika kuwafunza wanao lugha yao asilia. Pili, wasomi katika jamiilugha ya Ilwana wana mielekeo hasi kuhusu

matumizi ya lugha yao asilia na mwisho ni shinikizo kutoka kwa lugha maarufu ya Kiswahili na Kiingereza. Wanajamiilugha walio na kiwango cha juu wanatumia Kiswahili na Kiingereza katika mazungumzo yao katika jamii na maeneo rasmi. Utafiti wa Bichang'a unafanana na utafiti huu kwa kuwa jamiilugha inayotafitiwa hapa ina idadi ndogo ya wazungumzaji kama vile jamii ya Ilwana na pia utafiti huu ulibaini iwapo Washona wamedumisha lugha yao licha ya shinikizo kutoka lugha maarufu nchini Kenya kama vile Kiswahili na Kikuyu.

Batibo (2005) anasema kuwa kudumishwa kwa lugha kunaweza kutokea kwenye mazingira ya umoja lugha na wingilugha. Batibo anaendelea kusema kuwa kwenye mchakato wa udumishaji wa lugha, wanajamii huweka na kupanga mikakati inayokubalika na wakati mwingine mikakati hii hutokea bila kupangwa. Utafiti wa Sangili (2019) unabainisha kuwa mikakati inayopangwa na jamiilugha huwa inakubaliwa na wazee katika jamii kwa kuwa wazee ndio wamiliki na waendeshaji wa mila na desturi zote za jamii ikiwemo lugha. Kuna mikakati mingine ambayo hutokea kwa kushtukia tu na ambayo hawakuipangia ila jamiilugha itajikuta imeikubali. Mfano mzuri ni misamiati inayohusiana na UVIKO au Korona. Misamiati hii ilitokea tu mwaka wa 2020 wakati ambapo homa ya Korona iliathiri dunia nzima na hivyo basi jamiilugha hazikuwa na budi ila kubuni na kukubali misamiati mipya. Tafiti za Batibo (2005) na Sangili (2019) zinahusiana na utafiti huu kwa kuwa utafiti huu ulibainisha mbinu mbalimbali zinazotumiwa na Washona katika kudumisha lugha yao licha ya shinikizo kutoka lugha maarufu nchini Kenya.

Charo na Ong'onda (2022) walichunguza kuhusu mbinu za udumishaji wa lugha ya Kigiriama katika kaunti ya Kilifi nchini Kenya. Waligundua kwamba maeneo ya nyumbani ndiyo yanaongoza katika juhudi za udumishaji wa lugha kwa kuwa wazee (wazazi) hawatumii lugha yoyote kwa mazungumzo ya nyumbani isipokuwa lugha ya Kigiriama. Watafitiwa wa umri mkubwa walikiri kwamba matumizi ya lugha ya Kigiriama ni njia mojawapo ya kuwafunza wana wao lugha ya kwanza na hivyo basi ni njia mojawapo ya kudumisha lugha yao. Utafiti wa Charo na Ong'onda ni muhimu kwa kuwa utafiti huu ulichunguza mbinu mbalimbali za kudumisha Kishona nchini Kenya.

Obiero na Matu (2013) walitafitia udumishaji na ufufuaji wa lugha ya Kisuba ambayo ilikuwa imeanza kudidimia. Waligundua kwamba wazee walijisatiti sana katika harakati za kufufua na kudumisha lugha yao kwa kuwa walipewa nafasi katika redio ya Kisuba iliyoanzishwa kwa minajili ya kuwafundisha Wasuba lugha yao. Wazee pia walikuwa kwenye mstari wa mbele ili kuhakikisha serikali imefanikisha juhudi za udumishaji wa lugha yao kando na kuwafunza wanawe kwenye maeneo ya nyumbani. Utafiti wa Obiero na mwenzake unasabihiana na utafiti huu kwa kuwa lengo la nne lilishughulikia mikakati ya udumishaji wa Kishona ambapo juhudi za wazee wa Kishona zilibainika kuwa mojawapo ya mikakati hiyo.

Mathooko (2007) anafananisha udumishaji wa lugha na uhifadhi wa lugha. Anasema kwamba uhifadhi wa lugha ni kule kuendelea kutumia lugha fulani hasa katika miktadha ambapo pana mashindano makali kutoka kwa lugha ambayo ina nguvu za kidemografia, usaidizi wa asasi za kiserikali na pia lugha inayochukua eneo kubwa kijiografia. Maoni ya Mathooko yanafaa utafiti huu kwa kuwa mbinu za kudumisha

Kishona zilishughulikiwa kwenye mazingira ya mashindano makali ya lugha maarufu nchini Kenya kama vile Kiswahili na Kikuyu. Utafiti wa Mathooko unatupeleka kwa tafiti mbalimbali kuhusu uthabiti wa kiisimujamii wa lugha.

## 2.10 Uthabiti wa Kiisimujamii wa Lugha

Utafiti huu kupitia kwa lengo la kwanza, unashughulikia athari za Kiswahili na Kikuyu kwa uthabiti wa kiisimujamii wa Kishona nchini Kenya. Giles, Bourhis na Taylor (1977) wanafafanua uthabiti wa kiisimujamii wa lugha kuwa ni juhudi za jamiilugha za kudumisha utamaduni wao hasa lugha yao licha ya shinikizo kutoka jamiilugha zilizo na watu wengi katika jamii. Uthabiti wa kiisimujamii wa lugha hudhihirika kupitia kwa matumizi mbalimbali ya lugha katika miktadha mbalimbali. Kiashiria kikuu cha uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ni matumizi yake katika maeneo ya nyumbani, katika jamii, kwenye asasi mbalimbali za kiserikali, miktadha rasmi na miktadha isiyo rasmi na kwenye vizazi vyote vya jamiilugha husika. Shirika la SIL (Summer Institute of Linguistics) linabainisha uthabiti wa kiisimujamii wa lugha kupitia kwa matumizi yake mbalimbali, urithisho wake kwa vizazi tofauti, sababu za kutumia lugha hiyo katika jamii, sera za serikali kuhusu lugha na miktadha mbalimbali ambapo lugha hutumika.

Giles, Bourhis na Taylor (1977) wanasema kwamba hadhi, demografia na usaidizi wa asasi za kijamii ndiyo mambo matatu yanayohakikisha uthabiti wa kiisimujamii wa jamiilugha fulani. Jamiilugha inaweza kuwa na uthabiti wa viwango mbalimbali kwa kutegemea juhudi zao katika mazingira ya wingilugha. Inabainika kwamba jamiilugha zilizo na uthabiti wa chini huwa rahisi kwa lugha zao kumezwa na jamiilugha zilizo na

uthabiti wa hali ya juu. Kwa upande mwingine, jamiilugha zilizo na uthabiti wa hali ya juu, hudumisha lugha zao na tamaduni zao.

Bourhis, Giles na Rosenthal (1981) walifanya utafiti kuhusu uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kituruki kwa kujikita kwenye Waturuki waliohamia sehemu mbalimbali kama vile Australia, Ufaranza, Ujerumani na Uholanzi. Utafiti wao ulibainisha kwamba Waturuki walikuwa na mtandao mzuri wa kijamii kwa kuwa sheria za uhamiaji na kufanya kazi ugenini zilikuwa na changamoto si haba. Kwa hivyo Waturuki wakawa wanasaidiana wao kwa wao wakiwa ugenini. Utafiti huu ulibainisha kwamba Waturuki walikuwa pia na changamoto ya kuwasajili wanao katika shule za nchi hizi walikohamia. Changamoto hizi ziliwapa motisha ya kudumisha lugha yao kwa kuwa ndicho kitu cha thamana walichobaki nacho cha kuwaleta pamoja. Extra na Yagmur (2004) wanasema kwamba Kituruki ndiyo lugha inayopendelewa na inayotumiwa sana na vijana na watoto wahamiaji. Hii inamaana kwamba lugha hii itadumu kwa kuwa vizazi vimeirithi na kuipendelea.

Clement na Norton (2021) walifanya utafiti kuhusu uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kiingereza na lugha za kiasili nchini Uganda ambapo zaidi ya lugha 40 zinazungumzwa. Walichunguza matumizi ya lugha za kiasili na lugha ya Kiingereza shuleni Mashariki mwa Uganda baina ya wazazi waliokuwa na watoto wanaosoma. Clement na Norton waligundua kwamba wazazi waliona faida kubwa kwa wanao kujifunza na kutumia lugha za asilia kwa sababu kuu ya utambulisho. Wazazi walisema kwamba wanao wakijifunza lugha zao za kwanza, huwa wanajua mizizi yao katika jamii vyema kwa kuwa lugha ni kitambulisho chao. Kwa upande mwingine, wazazi

walikuwa na maoni kwamba lugha ya Kiingereza ndiyo itakayokuwa na manufaa katika maisha ya baadaye ya wanao kwa kuwa itawapatia nafasi nyingi za ajira. Kwa hivyo walitaka wanao kujifunza kuzungumza na kuandika lugha ya Kiingereza vyema. Utafiti wa Clement na Norton(kt.) ulibainisha kwamba Waganda wengi hasa watoto walijifunza Kiingereza kwa kuwa walijua kwamba Kiingereza ni lugha ya kimataifa na hivyo itawasaidia kupata nafasi nyingi za ajira duniani. Lugha ya Kiingereza ilipata kuenea sana kwa sababu ilipewa matumizi mengi katika jamii.

Fishman (1991), Yamamoto (1998) na Crystal (2002) wanakubaliana kwamba ili lugha fulani iwe thabiti kiisimujamii, ni lazima itambulike na asasi za kiserikali kuwa lugha mojawapo katika jamii husika na pia ipewe usaidizi kutoka asasi hizo za kiserikali. Jamiilugha ya watu wachache isipopewa usaidizi wa kiserikali kupitia kutambuliwa, shinikizo kutoka lugha maarufu zitaifanya kupoteza uthabiti wake na hivyo basi lugha hiyo itahama. Washona walitambuliwa mwishoni mwa mwaka wa 2020 na aliyekuwa Rais wa nne wa Kenya, Uhuru Kenyatta. Utambulisho huu wa Washona umewafanya kuwa na mwamko mpya wa kudumisha lugha yao kwa kuwa inatambulika kuwa lugha mojawapo za Kenya. Licha ya mwamko huu mpya, lugha ya Kishona inapigania nafasi na Kiswahili ambayo ina nguvu za kidemografia na usaidizi wa asasi za serikali ya Kenya kuliko Kishona.

Shirika la UNESCO (2003, 2011) liliorodhesha vigezo vya kupima uthabiti wa kiisimujamii wa lugha. Kulingana na utafiti huo, lugha nyingi za Kiasili barani Afrika zipo katika hatari ya kuangamia iwapo juhudi za kuzidumisha hazitazingatiwa na mataifa husika.  Vigezo sita vya kupima uthabiti wa kiisimujamii wa lugha

vimejadiliwa kwa ufupi kwenye sehemu ya 2.10.1 inayofuata. Vigezo hivi vilisaidia utafiti huu wakati wa uchanganuzi wa data ya lengo la kwanza lililobainisha athari za Kiswahili na Kikuyu kwa uthabiti wa kiisimujamii wa Kishona na lengo la nne lililobainisha iwapo Washona wamefaulu katika udumishaji wa lugha yao au la.

### 2.10.1 Kupokezanwa kwa Lugha Baina ya Vizazi

Kigezo kinachotumika sana kupima uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ni iwapo lugha husika inapokezanwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine au la kama anavyosema Fishman (1991). Lugha iliyo hatarini inaweza kupimwa kupitia viwango mbalimbali kuanzia lugha thabiti hadi lugha iliyotoweka au iliyokufa. Hii ni kwa sababu wanajamiilugha wanaweza kuacha kupokeza vizazi vyao lugha wakati wowote kwa kutegemea hali wanamojikuta ambayo inaweza kufanya lugha yao isipokezanwe. Jedwali 2.3 lifuatalo linaonyesha upimaji wa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha kupitia kwa kigezo cha kupokezanwa kwa lugha baina ya vizazi vya jamiilugha.

**Jedwali 2.3: Kupokezanwa kwa Lugha Baina ya Vizazi Tofauti**

| **Hadhi** | **Kiwango cha lugha kuhatarishwa** | **Kupokezanwa kwa lugha baina ya vizazi tofauti** |
|---|---|---|
| 5 | Lugha salama | Lugha inazungumzwa na vizazi vyote bila pingamizi yoyote. (kuanzia watoto hadi wazee) |
| 4 | Lugha imeanza kuathirika kidogo | Watoto wengi huzungumza lugha husika katika maeneo yote lakini kwa mara nyingi huizungumza kwenye maeneo ya nyumbani. |
| 3 | Lugha iliyo hatarini | Watoto hawajifunzi wala kuzungumza lugha hiyo kama lugha yao ya kwanza kwenye maeneo ya nyumbani. Lugha hiyo hutumika sana kuanzia kwa wazazi kuelekea juu. |
| 2 | Lugha inayoelekea kuangamia | Lugha husika inazungumzwa na babu na nyanya na vizazi vya wazee tu lakini wazazi hawaizungumzi licha ya kuielewa. Wazazi hawa pia hawawazungumzii wanawe kwa |

| | | |
|---|---|---|
| | | lugha asilia bali huwazungumzia kwa lugha ya pili. |
| 1 | Lugha iliyoangamia lakini ina wazungumzaji wachache sana | Wazungumzaji wa umri wa chini ni babu na nyanya tu. Na hawaizungumzi kwa ufasaha. |
| 0 | Lugha iliyokufa | Hakuna wazungumzaji wa lugha husika waliobaki/waliohai. |

Chanzo: UNESCO, Machi 2003

Jedwali 2.3 linaonyesha viwango mbalimbali vya uthabiti wa lugha kupitia kwa kigezo cha kupokezanwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwenye jamiilugha husika. Lugha iliyo na uthabiti wa hali ya juu, imewakilishwa na nambari (5) ambapo lugha hiyo iko imara na salama. Lugha hiyo inazungumzwa na vizazi vyote vya jamiilugha husika na inapokezanwa kwa vizazi vyote. Lugha iliyo na uthabiti wa chini na ambayo imeathiriwa na changamoto mbalimbali imewakilishwa na nambari (1) ambapo wazungumaji wake ni wenye umri mkongwe tu. Vizazi vingine havizungumzi lugha hiyo. Lugha hiyo iko kwenye hatua ya mwisho ya kuangamia. Lugha inayowakilishwa na sufuri (0) ni lugha ambayo haina wazungumzaji wanaojulikana au waliohai.

### 2.10.2 Idadi Kamili ya Wanajamiilugha Wanaozungumza Lugha

Utafiti wa UNESCO (2003) unabainisha kwamba kwa mara nyingi, ni vigumu kukadiria idadi kamili ya wazungumzaji wa lugha husika. Lugha iliyo na wazungumzaji wachache huwa katika hatari kubwa ya kuangamia kupitia kwa majanga kama vile vita au magonjwa ambayo yanaweza kuangamiza wanajamiilugha wote kwa mara moja. Wanajamiilugha wachache wanaweza pia kumezwa na wanajamiilugha walio na idadi kubwa. Hali hii ikifanyika hivyo, lugha na utamaduni wa jamiilugha ya waliowachache hutoweka na hivyo basi lugha hiyo hufa. Utafiti huu unashughulikia lugha ya Kishona

ambayo ina idadi ndogo ya wazungumzaji ikilinganishwa na lugha maarufu zinazoizunguka ambazo ni Kiswahili na Kikuyu.

### 2.10.3 Asilimia ya Wazungumzaji wa Lugha katika Jumuiya Nzima ya Jamiilugha

Asilimia ya wazungumzaji wa lugha inayohusiana na kundi zima la wanajamiilugha ni kiashiria tosha cha lugha husika kuwa na uthabiti wa kiisimujamii au kukosa uthabiti wa kiisimujamii. Jedwali 2.4 lifuatalo linaweza kutumika kupima viwango vya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha husika.

**Jedwali 2.4: Asilimia ya Wazungumzaji wa Lugha kwenye Jumuiya Nzima ya Jamiilugha**

| **Kiwango cha hatari ya kuangamia** | **Hadhi** | **Asilimia ya wazungumzaji kwenye kundi zima la jamiilugha** |
|---|---|---|
| Lugha iliyo Salama. | 5 | Wanajamiilugha wote wanazungumza lugha hiyo. |
| Lugha iliyo salama kidogo. | 4 | Karibu wanajamiilugha wote wanazungumza lugha hiyo. |
| Lugha iliyoanza kuwa hatarini. | 3 | Wanajamiilugha wengi wanazungumza lugha hiyo. |
| Lugha iliyo hatarini. | 2 | Wanajamiilugha wachache huzungumza lugha hiyo. |
| Lugha iliyohatarishwa sana. | 1 | Wanajamiilugha wachache sana wanazungumza lugha hiyo |
| Lugha iliyotoweka. | 0 | Hakuna mwanajamiilugha anayezungumza lugha hiyo. |

Chanzo: UNESCO, Machi 2003

Kwenye jedwali 2.4, lugha iliyo salama ambayo imewakilishwa na (5), ni ile ambayo wanajamiilugha wote wanaizungumza kwa ufasaha. Lugha iliyo kwenye hatari ya kuangamia, inayowakilishwa na (1) ni ile ambayo wanajamiilugha wake wachache sana hasa wazee ndiyo huzungumza lugha hiyo. Lugha iliyotoweka huwa haina mwanajamiilugha hata mmoja anayejulikana ambaye anazungumza lugha husika.

### 2.10.4 Ruwaza za Matumizi ya Lugha katika Maeneo Mbalimbali ya Kijamii

Uthabiti wa kiisimujamii wa lugha hubainika kwenye matumizi yake kwenye maeneo mbalimbali katika jamii kama vile kwenye biashara, elimu, katika ibada, mahakamani, nyumbani na kadhalika. Ruwaza ya matumizi ya lugha katika maeneo mbalimbali hujihusisha na maswali yafuatayo: Je, ni maeneo gani ambapo lugha husika hutumika? Ni akina nani huzungumza lugha husika katika jamii? Ni mada gani huwa wanazungumzia wakitumia lugha hiyo? Kwa kuwa utafiti huu unashughulikia Kishona nchini Kenya, maswali haya yanalenga kubainisha iwapo lugha husika imerithishwa kizazi kitakachofuata au la. Jedwali 2.5 lifuatalo linaashiria viwango mbalimbali vya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha kwa kutegemea ruwaza za matumizi kwenye maeneo mbalimbali panapotumika lugha husika:

**Jedwali 2.5: Ruwaza ya Matumizi ya Lugha Katika Maeneo Mbalimbali ya Kijamii**

| **Kiwango cha hatari ya kutoweka** | **ukadiriaji** | **Maeneo na kazi mbalimbali za lugha husika** |
|---|---|---|
| Matumizi ya lugha na wanajamiilugha wote katika maeneo yote. | 5 | Lugha husika inazungumzwa na wanajamiilugha wote kwenye maeneo yote. |
| Uwingilugha ulio sawa. | 4 | Lugha mbili au zaidi zaweza kutumika kwenye maeneo mengi ya jamii na kwenye shughuli nyingi. |
| Kupunguka kwa Maeneo ya matumizi ya lugha. | 3 | Lugha imesalia kutumika katika maeneo na shughuli za nyumbani. Lugha maarufu huanza pia kutumika katika maeneo ya nyumbani. |
| Maeneo machache ya matumizi ya lugha. | 2 | Matumizi ya lugha yanaanza kupungua kwenye maeneo ya kijamii na kwenye shughuli nyingi za kijamii. |
| Maeneo machache sana ya matumizi lugha. | 1 | Lugha hii inatumika kwenye maeneo machache sana na kwa shughuli chache sana hasa nyumbani. |
| Lugha iliyokufa. | 0 | Lugha haitumiki tena kwenye maeneo yoyote katika jamii. |

Chanzo: UNESCO, Machi 2003

Lugha thabiti inayowakilishwa na (5), ni ile ambayo huzungumzwa katika maeneo yote ya kijamii na wanajamiilugha wote kuanzia nyumbani hadi ofisini. Uthabiti wa lugha huanza kupunguka iwapo lugha husika pamoja na lugha maarufu huanza kupigania nafasi katika maeneo mengi ya kijamii kama vile nyumbani. Lugha hii imewakilishwa na nambari (4) kwenye jedwali 2.5. Lugha ambayo imesalia kutumika katika maeneo ya nyumbani tu na tena kwa shughuli chache sana, iliyowakilishwa na (1), ipo kwenye hatari ya kuangamia kwa kuwa nafasi yake tayari imechukuliwa na lugha nyingine. Iwapo lugha haitumiki kabisa kwenye maeneo yoyote hata kama ni nyumbani, basi lugha hiyo imekufa.

### 2.10.5 Ueneaji wa Lugha katika Maeneo Mapya ya Matumizi na Kwenye Vyombo vya Habari

Maeneo mapya ya matumizi ya lugha yanaweza kutokea iwapo hali za maisha zitabadilika kwa jamiilugha husika. Maeneo kama vile taasisi za elimu, mahali pa kazi, vyombo vya habari kama vile utangazaji kwenye runinga na redio na kwenye mitandao ya kijamii hutumika kupanua viwango na maeneo ya lugha iliyo na wazungumzaji wengi kuliko lugha ya waliowachache. Jedwali 2.6 lifuatalo linaonyesha jinsi maeneo mapya ya matumizi yanaweza kuathiri uthabiti wa kiisimujamii wa lugha kulingana na UNESCO (2003).

**Jedwali 2.6: Maeneo Mapya ya Matumizi ya Lugha Hasa Vyombo vya Habari**

| **Kiwango cha hatari ya kutoweka kwa lugha.** | **Hadhi** | **Maeneo mapya ya matumizi yaliyokubalika na vyombo vya habari vinavyokubaliwa na lugha iliyo hatarini kuangamia.** |
|---|---|---|
| Lugha iliyo imara. | 5 | Lugha husika inatumika kwenye maeneo yote mapya. |
| Lugha iliyo hai. | 4 | Lugha husika inatumika kwenye maeneo mengi mapya ya kijamii, |
| Lugha iliyo imara kidogo. | 3 | Lugha husika inatumika kwenye maeneo mengi ya kijamii. |
| Lugha iliyoanza kupoteza uthabiti wake. | 2 | Lugha husika inatumika kwenye maeneo machache ya kijamii. |
| Uthabiti uliopungua. | 1 | Lugha husika inatumika kwenye maeneo mapya machache sana ya kijamii. |
| Lugha isiyo hai. | 0 | Lugha husika haitumiki kwenye maeneo mapya yoyote katika jamii. |

Chanzo: UNESCO, Machi 2003

Iwapo lugha ni thabiti, itatumika kwenye maeneo yote mapya hasa vyombo vya habari na inawakilishwa na (5) kwenye jedwali 2.6. Lugha ambayo imeanza kupoteza uthabiti wake, inayowakilishwa na (2) matumizi yake ni machache kwenye maeneo mapya katika jamii. Vivyo hivyo, lugha iliyokufa inayowakilishwa na (0) haitumiki kwenye maeneo mapya yoyote katika jamii. Maeneo mapya ya matumizi ya lugha kama vile mahali pa kazi, kwenye elimu au katika vyombo vya habari yatazingatiwa wakati wa kutathmini viwango vya lugha iliyo thabiti ama iliyo kwenye hatari ya kuangamia. Maeneo mapya yanamaanisha lugha husika itapata kuenezwa kwenye maeneo ambayo haikuwa inatumiwa na kudumishwa kupitia vyombo vya habari.

### 2.10.6 Nyenzo Zilizopo za Kufundishia Lugha Husika Hasa Katika Kusoma na Kuandika

Lengo la nne la utafiti huu linahusu kubainisha mikakati mbalimbali ambayo Washona wanatumia katika udumishaji wa lugha yao. Mojawapo ya mikakati ni iwapo lugha ya Kishona imeandikwa vitabuni au la ili iwe rahisi kwa vizazi vijavyo kuisoma na kuiandika. Elimu ya lugha ni muhimu kwenye uthabiti wa kiisimujamii wa lugha yoyote. Ujifunzaji wa lugha hasa kwenye maandishi ni jambo la kujivunia kwa kuwa vizazi vyote vitapata kusoma lugha yao na kuiandika ipasavyo. Vitabu vinahitajika kwa mada zote katika jamii na kwa marika yote katika jamiilugha husika. Hali hii huifanya lugha kuwa thabiti kwa kuwa lugha ya maandishi haiwezi kufa kama vile lugha ya mazungumzo wanavyosema Thomason na Kaufman (1988) na Florian (1998). Jedwali 2.7 lifuatalo linadhihirisha uthabiti wa lugha kupitia ufundishaji.

**Jedwali 2.7: Uwepo wa Vitabu Vilivyoandikwa kwa Lugha Husika**

| **Kiwango** | **Uwepo wa vitabu vililvyoandikwa lugha husika** |
|---|---|
| 5 | Vitabu vipo kwa wingi vilivyoandikwa kuhusu lugha husika. Lugha hii hutumika kwenye maeneo yote. |
| 4 | Vitabu vilivyoandikwa vipo hata shuleni na hata watoto wanavisoma ilhali vitabu vipya haviendelei kuandikwa kwa lugha husika. |
| 3 | Maandishi mbalimbali ya lugha husika yapo ilhali lugha hiyo haiendelezwi kupitia kwa vyombo vya habari na mitandaoni. |
| 2 | Maandishi ya lugha husika yapo lakini yanafaidi wanajamiilugha wachache na kuwa na umuhimu kwa wanajamiilugha wachache. Lugha hiyo haifunzwi tena shuleni. |
| 1 | Hakuna maandishi yoyote kuhusu lugha husika. |
| 0 | Lugha hiyo imesahaulika kabisa. |

Chanzo: UNESCO, Machi 2003

Kutokana na jedwali 2.7, lugha iliyo thabiti kupitia kwa vitabu vilivyoandikwa inayowakilishwa na (5) ni ile ambayo ina vitabu mbalimbali na vingi vilivyoandikwa na

vinapatikana kwa urahisi shuleni na hata madukani. Lugha ambayo imeanza kupoteza uthabiti wake kupitia maandishi na mafunzo yake shuleni, imewakilishwa na (3) na (2) ambapo maandishi yake yapo lakini vitabu vipya haviendelei kuandikwa na hata wanajamiilugha hawasomi vile vinavyopatikana. Kwenye kiwango cha lugha kinachowakilishwa na (1), lugha husika haina maandishi yoyote vitabuni. Lugha ikifika kwenye kiwango hiki, lugha hiyo ipo kwenye hatari kubwa ya kuangamia iwapo wanajamiilugha hawatakuwa na juhudi zozote za kuihifadhi.

Vigezo hivi vyote sita vilivyotafitiwa na shirika la UNESCO (2011, 2003) vilisaidia katika kupima iwapo lugha maarufu zimeathiri Kishona na kwa viwango vipi kwenye lengo la kwanza la utafiti huu. Aidha vigezo hivi vinatumika kupima iwapo Washona wamefaulu katika kudumisha lugha yao au imo hatarini kwenye lengo la nne la utafiti huu. Watafiti mbalimbali wametafiti kuhusu uthabiti wa kiisimujamii wa lugha duniani kote kupitia  sehemu 2.10.7 ifuatayo.

### 2.10.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Uthabiti wa Kiisimujamii wa Lugha

Roche (2017) alichunguza hali ya kiisimujamii ya lugha ya Saami inayozungumzwa katika nchi nne za Ulaya: Norway, Sweden, Finland na Urusi. Maeneo haya yanajulikana kwa wingilugha ambao umeleta changamoto katika kuhifadhi na kuendeleza lugha hii ya Kisaami. Roche (kt.) aligundua kwamba lugha ya Kisaami ilikuwa katika hatari ya kuangamia kwa kuwa idadi ya wazungumzaji wake ilididimia na nafasi yake kuchukuliwa na lugha ya Kilatini. Hali hii ilifanyika kwa sababu ya uhamaji uliotokea kuanzia karne ya kumi na migawanyiko ya Wasaami iliyotokea baada ya mipaka ya nchi zile nne kuwekwa. Baadaye lugha hii ilipewa hadhi ya chini

katika jamii hasa katika miktadha ya kidini na biashara ambapo lugha ya Kiswidi ilipewa hadhi ya juu. Matumizi ya lugha ya Kisaami yakapungua kutoka kwa jamii na kubakia tu kutumika katika mazingira ya familia nyumbani. Hali hii ilifanya lugha ya Kisaami kupunguza uthabiti wake kiisimujamii. Ingawa kuna sera za udumishaji wa lugha ambazo ziliwekwa kuanzia miaka ya tisini, bado kuna changamoto kubwa za udumishaji wa Kisaami kwa kuwa idadi ya wazungumzaji wake ni ya chini mno.

Maya (2009) alitafitia hali ya kiisimujamii ya lugha ya Garifuna nchini Belize, Amerika ya kati kwenye kisiwa cha St. Vincent na kugundua kwamba lugha ya Kigarifune ilianza kupoteza uthabiti wake wa kiisimujamii na ilikuwa katika hatari ya kuangamia kufuatia shinikizo na lugha zingine kama vile Kiingereza na Kifaransa. Mabadiliko haya yaliwezeshwa na mtagusano uliotokea miaka ya 1700 kati ya Wazungu, Wamarekani na Waafrika watumwa na baadaye Wafaransa. Mtagusano huu ulizua athari ya uhamaji wa lugha ya Kigarifune ambayo kwa sasa inazungumzwa na watu wachache sana. Utafiti wa Maya (kt.) ulibainisha kuwa wanajamiilugha wengi wa Kigarifune walishahamia lugha maarufu nchini humo kama vile Kiingereza na Krioli cha Belize (lugha mpya iliyozuka baada ya mtagusano wa Kigarifune, Kiingereza na Kifaranza).

Chakrani (2011) alichunguza matumizi ya lugha baina vijana wa Morocco na hali ya kiisimujamii ya lugha nchini humo. Yeye aligundua kwamba mielekeo mbalimbali ya lugha imechangia hadhi tofauti za lugha miongoni mwa vijana wa Morocco. Utafiti wake ulibainisha kwamba vijana wanajihusisha sana na lugha ya Kifaranza na Kiingereza kwa kuwa zimepewa taadhima ya juu katika jamii ikilinganishwa na

Kiarabu cha Morocco na lugha ya asilia ya Kiamazigh (Kiberber). Utafiti wa Chakrani ulibainisha kwamba mielekeo ya vijana ni kuwa, Kiarabu cha Morocco na Kiamazigh hutumika na watu wa tabaka la chini na maeneo ya nyumbani tu huku wasomi na wanafunzi, wanabiashara na watu wa tabaka la juu wakitumia Kifaranza na Kiingereza. Utafiti wa Chakrani (kt.) ni tofauti kieneo na hata kijumuiya kwa kuwa yeye alishughulikia vijana tu nchini Morocco ilhali utafiti huu ulishughulikia watafitiwa wa vizazi vyote vya Washona tangu kuwasili Kenya. Utafiti wake ulikuwa wa manufaa kwa utafiti huu hasa katika lengo la tatu lililoshughulikia mielekeo ya Washona katika matumizi ya Kiswahili na Kikuyu nchini Kenya.

Kamau (2015) alitafitia athari za lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng' kwa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Wakikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Alichunguza iwapo lugha hizo zinaathiri uthabiti wa kiisimujamii wa Kikuyu miongoni mwa vijana. Utafiti wake ulibaini kuwa viwango vya uthabiti wa kiisimujamii kwa Kikuyu vinaendelea kushuka kwa sababu ya mtagusano na lugha maarufu za humu nchini ambazo zimeiathiri lugha hiyo kwa sababu mbalimbali. Utafiti wa Kamau (kt.) ulikuwa na mchango mkubwa kwa utafiti huu kwa kuwa athari za Kiswahili na Kikuyu kwa Kishona zilibainishwa. Utafiti wa Kamau (kt.) ulitofautiana na wetu katika lugha inayoathiriwa na lugha nyingine ambayo ni Kishona cha Kenya.

Ngure (2012) alichunguza uhamaji wa lugha unaohusisha lugha ya Kirendile na lugha ya Kisamburu. Alichunguza hatua na sababu za uhamaji wa lugha ya Rendile hadi ya Samburu na athari za uhamaji wa lugha kwa muundo wa Kirendile. Ngure (kt.) aligundua sababu kadhaa zilizochochea uhamaji wa lugha hiyo kama vile hali ya

kiuchumi ya kabila la Samburu na ndoa baina ya makabila haya mawili. Alitumia nadharia ya Giles, Bourhis na Taylor (1977) katika kushughulikia swala lake la utafiti. Utafiti wake ulitofautiana na huu kwa kuwa yeye alilenga uhamaji wa lugha ilhali utafiti huu ulilenga athari za Kiswahili na Kikuyu kwa uthabiti wa Kishona nchini Kenya.

Sangili (2019) alitafiti kuhusu udumishaji wa lugha ya Kimaragoli kwenye eneobunge la Uriri, nchini Kenya. Utafiti wake ulichunguza athari za lugha ya Dholuo kwa lugha ya Kimaragoli inayozungumzwa katika eneobunge la Uriri na mielekeo ya wasemaji wa Dholuo na Kimaragoli kuhusu lugha hiyo. Aligundua kuwa licha ya jamiilugha ya Kimaragoli kuwa mbali kimasafa na eneo lao asilia, wametumia mbinu mbalimbali kama vile sherehe za kitamaduni, watoto kufundishwa lugha yao miongoni mwa mbinu zingine katika kudumisha lugha yao. Utafiti wake ulitofautiana na huu kwa sababu ulitafitia kuhusu athari za Kiswahili na Kikuyu kwa uthabiti wa Kishona. Utafiti wa Sangili (kt.) ulikuwa wa mchango mkubwa kwa utafiti huu kwa kuwa ulionyesha mbinu mbalimbali za kudumisha lugha ya Kimaragoli katika sehemu ya Uriri nchini Kenya na pia utafiti wake ulikuwa wa Kiisimujamii sawia na utafiti huu.

## 2.11 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia mapitio mbalimbali ya maandishi kwa kuanza na mtagusano lugha na athari mbalimbali za mtagusano lugha. Ilibainika kwamba mtagusano lugha ni jambo lisiloepukika kwa sababu wanajamiilugha mbalimbali wanapoishi katika mazingira sawa, lugha zao lazima zitaingiliana. Hali ya kiisimujamii ya lugha duniani ilishughulikiwa pamoja na hadhi ya lugha za kiasili barani Afrika. Lugha za Kiswahili

na Kikuyu zilishughulikiwa kwa ufupi kwenye sura hii kwa kuwa ndizo zinazotafitiwa jinsi zinavyoathiri Kishona nchini Kenya. Udumishaji wa lugha ulishughulikiwa kwenye sura hii na ikabainika kuwa, ili lugha yoyote idumu, wanajamiilugha hiyo lazima waweke juhudi na mikakati mbalimbali ili waweze kufaulu katika udumishaji wa lugha yao.

Asili ya wanajamiilugha wa Kishona ilijadiliwa katika sura hii na ikabainika kwamba Washona wengi (80%) huishi nchini Zimbabwe na mataifa jirani kama vile Zambia na Msumbiji. Ilidhihirika pia kwamba Kishona ni moja kati ya lugha za kitaifa nchini Zimbabwe iliyo na wazungumzaji milioni 8.9 ambayo ni idadi kubwa kuliko lugha nyingine zinazozungumzwa nchini humo. Pia, ilibainika kwamba Washona wana lahaja tano zinazowatambulisha nchini Zimbabwe. Ilidhihirika kuwa Washona walifika Kenya mara ya kwanza kati ya mwaka wa 1957 hadi 1959 kama wamishenari na kuendelea kuishi nchini hadi sasa ambapo wametagusana na lugha mbalimbali za Kenya zikiwemo lugha ya taifa na rasmi ya Kiswahili pamoja na lugha nyingine kama vile Kikuyu.

Aidha, uthabiti wa kiisimujamii wa lugha uliangaziwa na ikabainika kwamba, kulingana na UNESCO (2003), kuna vigezo sita vinavyopima uthabiti wa kiisimujamii wa lugha na kuonyesha iwapo lugha ni thabiti ama imepoteza uthabiti wake katika jamii. Kutokana na vigezo hivyo, ilikuwa wazi kwamba lugha iliyo na majukumu mengi katika jamii huwa na uthabiti wa kiisimujamii kwa kuwa inaendelea kukua inapotumiwa. Sura ya tatu inayofuata inashughulikia matokeo ya utafiti kwa njia ya kitakwimu na kimaelezo kuhusu lengo la kwanza la utafiti huu ambalo ni athari za Kiswahili na Kikuyu kwa Kishona.

# SURA YA TATU: ATHARI ZA MTAGUSANO WA KISWAHILI NA KIKUYU KWA KISHONA

## 3.0 Utangulizi

Sura ya pili ilihusika na mapitio ya maandishi mbalimbali kuhusu mtagusano lugha na athari zake, hali ya kiisimujamii ya lugha duniani na barani Afrika, historia na utamaduni wa wanajamiilugha wa Kishona. Lugha za Kiswahili na Kikuyu ziliangaziwa kwa kuwa ndizo ambazo Washona hutagusana nazo kila siku katika maeneo yao ya kijamii. Aidha, udumishaji wa lugha uliangaziwa huku upekuzi ukifanywa kuhusu uthabiti wa kiisimujamii wa lugha na vigezo mbalimbali vya kupima uthabiti wa kiisimujamii wa lugha, (UNESCO, 2003).

Sura hii inashughulikia uwasilishaji na uchanganuzi wa data kutokana na lengo la kwanza la utafiti ambalo linahusu athari mbalimbali zinazotokana na mtagusano wa Kiswahili na Kikuyu kwa Kishona nchini Kenya. Washona wa Kenya wanaishi kwenye mitaa mitano ya Kaunti ya Kiambu ambayo ni jirani ya jiji kuu la Nairobi linalojulikana kwa wingilugha anavyosema Kamau (2015).

## 3.1 Athari Mbalimbali za Mtagusano wa Kiswahili na Kikuyu kwa Kishona

Appel na Muysken (2005) wanasema kwamba mtagusano lugha unapotokea, lugha husika zinaweza kuathiriana ila ile lugha isiyo na nguvu za kidemografia huathirika zaidi. Athari hizo huonekana kupitia ubadilishaji msimbo, ukopaji wa maneno, wingilugha, mabadiliko ya lugha, uhamaji wa lugha na mielekeo mbalimbali kuhusu lugha. Utafiti ulilenga kubainisha athari mbalimbali za mtagusano wa Kiswahili na

Kikuyu kwa Kishona kupitia matumizi mbalimbali ya lugha hizi katika jamii. Landweer (2000) na UNESCO (2003) wanapendekeza mojawapo ya mihimili inayopima uthabiti wa lugha kuwa ni maeneo mbalimbali ambapo lugha husika hutumika. Landweer (kt.) anaendelea kusema kwamba lugha yoyote ikitumiwa katika maeneo mbalimbali ya kijamii huwa na uthabiti wa hali ya juu. Naye Mirvahedi (2014) anasema kwamba lugha isipotumika katika mitandao ya kijamii, elimu na shughuli za kiserikali, inakosa kuwa na uthabiti wa kiisimujamii na kuanza kupotea polepole.


Katika lengo la kwanza, matumizi mbalimbali ya Kiswahili, Kikuyu na Kishona katika jamii na baina ya watafitiwa yalichunguzwa. Miktadha mbalimbali ya matumizi ya lugha pamoja na sababu mbalimbali za matumizi ya lugha zilichunguzwa pia ili kuthibitisha hali halisi ya Kishona kwenye mazingira ya mtagusano na lugha za Kiswahili na Kikuyu. Utafiti ulianza na usaili kuhusu lugha ambayo watafitiwa wanafahamu vyema baina ya Kiswahili, Kikuyu na Kishona.

### 3.1.1 Lugha Inayofahamika Zaidi Kati ya Kiswahili, Kikuyu na Kishona kwa Washona

Giles, Bourhis na Taylor (1977) na Holmes (2001) walibainisha kwamba kutambulika kwa lugha fulani katika jamii ni mojawapo ya uthibitisho kwamba lugha hiyo ina uthabiti wa kiisimujamii. Hii inamaanisha kwamba, lugha hiyo inafahamika na kutumika kwenye shughuli mbalimbali za kijamii, kwenye mitandao ya kijamii, kutumika kwake katika taasisi za kielimu na katika huduma muhimu za jamii kama vile idara ya afya, idara ya ulinzi, utawala na katika ibada, (UNESCO, 2003). Utafiti

ulilenga kubainisha lugha ambayo watafitiwa wengi walikuwa wanafahamu kati ya Kishona, Kiswahili na Kikuyu. Majibu yao yanabainika kwenye baa-grafu 3.1 ifuatayo.

**Baa-grafu 3.1: Lugha Inayofahamika vyema kwa Washona**




*Chanzo: Data ya nyanjani*

Kutokana na baa-grafu 3.1, ni dhahiri kwamba asilimia 49.18 ya Washona wanafahamu Kiswahili vyema sana. Asilimia 47.54 wanafahamu Kishona huku asilimia 3.28 wakifahamu Kikuyu. Hii ni ishara kwamba lugha ya Kishona imeanza kuathiriwa na Kiswahili kwa kuwa ndiyo lugha maarufu wanayotagusana nayo katika maeneo wanamoishi. Landweer (2000) anasema kwamba wanajamiilugha wanaozungumza lugha husika sanifu wakiwa wengi, huifanya lugha hiyo kuendelea kuimarika. Hii inamaanisha kwamba idadi ya wazungumzaji wa lugha fulani huchangia uthabiti wa

kiisimujamii wa lugha. Pia, kutokana na maoni ya Giles, Bourhis na Taylor (1977) kuhusu uthabiti wa lugha kwa kutegemea matumizi yake katika jamii, matokeo ya baa-grafu 3.1 yanathibitisha kwamba lugha ya Kiswahili inaendelea kuwa thabiti kwa kuwa inafahamika na kutumika na asilimia kubwa ya watafitiwa.

Utafiti wa UNESCO (2003) kuhusu upimaji wa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha kupitia kwa ruwaza katika matumizi ya lugha kwenye maeneo mbalimbali ya kijamii, unabainisha kwamba lugha ambayo imeanza kuathirika ni ile ambayo inang'ang'ania nafasi na lugha maarufu katika jamii. Utafiti huo wa UNESCO unaonyesha kwamba iwapo lugha mbili zinatumika kwenye maeneo mengi ya jamii, basi lugha husika ipo kwenye kiwango cha nne (4) cha kuathirika (Taz. jedwali 2.5). Lugha ya Kishona inapigania nafasi na Kiswahili kwa kuwa wanajamiilugha wa Kishona hasa wenye umri mkubwa bado wanaithamini lugha yao huku wanajamiilugha wa umri mchanga wakitumia Kiswahili kwenye maeneo mengi ya kijamii. Lugha ya Kikuyu haina shinikizo kubwa kwa Kishona kwa sababu asilimia ndogo (3.28%) ya watafitiwa ndio wanaifahamu na kuitumia. Kulingana na lengo la kwanza la utafiti huu, ni dhahiri kwamba matumizi haya mengi ya Kiswahili yanaathiri Kishona kimatumizi.

### 3.1.2 Lugha ya Matumizi Kwenye Shughuli Rasmi

Landweer (2000), UNESCO (2003) na Mirvahedi (2014) wanasema kwamba mojawapo ya kiashiria cha uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ni kutambulika na kutumika kwake katika jamii na usaidizi wa kiserikali kuhusu lugha husika. Lugha inayokubalika kutumiwa kwenye miktadha rasmi kama vile kwenye elimu na mazingira rasmi kama vile shuleni, hospitalini na idara nyingine za serikali ni lugha ambayo imepewa hadhi ya

juu katika jamii hasa zile za wingilugha. Utafiti ulisaili kuhusu lugha ya matumizi ya Washona katika shughuli rasmi kama vile masomoni, mikutano ya kijamii na huduma za serikali miongoni mwa Washona. Jedwali 3.1 lifuatalo linabainisha matokeo ya usaili huo:

**Jedwali 3.1: Lugha Muhimu kwenye Shughuli Rasmi**

| Lugha | Mirudio | Asilimia |
|---|---|---|
| Kishona | 8 | 17.8 |
| Kiswahili | 37 | 82.2 |
| Kikuyu | 00 | 00 |
| **Jumla** | **45** | **100.0** |

Chanzo: Data ya nyanjani

Kutokana na jedwali la 3.1, asilimia 17.8 walikiri kwamba wanatumia Kishona katika shughuli rasmi. Asilimia 82.2 ya watafitiwa walisema kwamba wanatumia Kiswahili kwenye shughuli zote rasmi na kutoa sababu mbalimbali kama vile Kiswahili ni lugha ya taifa la Kenya, ni lugha rasmi kwa hivyo shughuli zote rasmi zinastahili kutumia lugha ya Kiswahili, (Katiba ya Kenya 2010), Kiswahili ni lugha ya masomo, ni lugha ya mawasiliano nchini na ni lugha ya biashara. Watafitiwa walikiri kutotumia Kikuyu kwenye shughuli rasmi.


Maoni ya Krauss (1992), Landweer (2000) na Mirvahedi (2014) ni kweli wanaposema kwamba lugha isipotumika kwenye maeneo rasmi serikalini, inakosa uthabiti na kuanza kupotea polepole. Kufuatia matokeo ya jedwali 3.1 kwamba asilimia 82.2 wanapendelea kutumia Kiswahili katika shughuli zote rasmi kuliko Kishona ni ishara kwamba Kishona ina nafasi ndogo sana ya matumizi kwenye shughuli na miktadha rasmi. Hii inamaanisha kwamba uthabiti wake wa kiisimujamii unaendelea kupungua

ikilinganishwa na Kiswahili. Hii inamaanisha kwamba lugha ya Kishona imeanza kuathirika kimatumizi na Kiswahili kwa kuwa haitumiki kwenye maeneo rasmi. Athari za lugha huanza kuonekana wakati ambapo matumizi yake yanaanza kudidimia katika jamii.

## 3.2 Ukopaji wa Maneno ya Kiswahili na Kikuyu kwa Washona


Chambers na Jack (1995) na Nagy (2010) wanasema kuwa ukopaji wa maneno hutokea katika mazingira ya wingilugha. Chambers na Jack wanaendelea kusema kwamba katika mchakato wa ukopaji wa maneno kutoka $L_1$ hadi $L_2$, kuna vigezo vinavyotawala hali hiyo ambavyo ni umri, jinsia, tabaka, mtandao wa kijamii na mielekeo ya wanajamiilugha husika. Wanajamiilugha wa umri mchanga hujifunza leksimu za lugha chanzi kwa haraka na hivyo basi hukopa maneno ya $L_2$ wanapozungumza lugha yao asilia. Utafiti huu ulidhamiria kubainisha iwapo Washona wameathirika na mtagusano wa Kiswahili na Kikuyu kupitia kwa ukopaji wa maneno wanapozungumza lugha yao. Matokeo yanadhihirika katika baa-grafu 3.2 na 3.3 zifuatazo:

**Baa-grafu 3.2: Ukopaji wa Maneno ya Kiswahili kwa Kishona**



Chanzo: Data ya nyanjani

**Baa-grafu 3.3: Maneno ya Kikuyu kwenye Kishona**




Chanzo: Data ya nyanjani

Utafiti ulibainisha kwenye baa-grafu ya 3.2 kwamba asilimia 68.18 wanapozungumza Kishona, kuna maneno ya Kiswahili ambayo wanakopa ili kuendeleza mazungumzo yao. Asilimia 31.82 walikiri kwamba wao hawakopi maneno ya Kiswahili wanapotumia Kishona kwenye mazungumzo yao. Katika baa-grafu 3.3, utafiti ulibainisha pia kwamba asilimia 71.76 ya Washona hawakopi maneno ya Kikuyu wanapozungumza Kishona na walitoa sababu kwamba, lugha ya Kikuyu kwao haina matumizi mengi katika jamii. Asilimia 28.24 waliokiri kukopa maneno kutoka kwa Kikuyu walisema kwamba wamezungukwa na wanajamiilugha wengi wa Kikuyu na hivyo walikuwa na ufahamu mdogo wa lugha hiyo. Ilifahamika kwamba maneno wanayokopa kutoka kwa Kikuyu ni yale yanayohusiana na salamu tu ili kuanzisha mazungumzo kwa urahisi ili wayaendeleze kwa Kiswahili.

Kulingana na T’sou (2001), Nagy (1996) na Poplack na Meechan (1998), mtagusano lugha mbili kwa kipindi kirefu hufanya lugha mojawapo kuingiza leksimu za lugha hiyo kwa lugha nyingine. Mtagusano kati ya Kishona, Kiswahili na Kikuyu kwa zaidi ya miongo sita kulibainisha baadhi ya maneno yaliyokopwa kutoka kwa Kiswahili hadi kwa Kishona na maneno machache kutoka kwa Kikuyu. Utafiti huu ulidondoa mifano mbalimbali ya leksimu hizo kama vile maneno na sentensi zinazohusika katika salamu na shughuli za maeneo ya nyumbani na vyombo vya matumizi ya nyumbani kama vile kikombe (*komichi au kapu*), sufuria (*hari*), kupika chakula (*kubika chekudya*) (Taz. Jedwali 3.3). Utafiti huu ulibainisha kwamba Washona wanakopa maneno ya Kiswahili wanapozungumza lugha yao ya Kishona.

Hii inamaanisha kwamba lugha ya Kishona imo kwenye hatari ya kupunguka kwa uthabiti wake kwa sababu kulingana na Landweer (2000) na UNESCO (2003), lugha maarufu ikianza kutumika kwenye maeneo ya nyumbani, ni ishara tosha kwamba matumizi ya lugha asilia kwenye maeneo ya nyumbani yameanza kupungua. Kupunguka kwa matumizi ya lugha asilia katika maeneo ya kijamii huwa ndio mwanzo wa kupunguka kwa uthabiti wa Kiisimujamii wa lugha husika.

Matokeo kwenye baa-grafu 3.2 na baa-grafu 3.3 yanaonyesha kwamba lugha ya Kishona imeanza kupunguza uthabiti wake katika jamii kupitia kwa ukopaji wa maneno kutoka lugha maarufu za Kiswahili na Kikuyu zinazoizunguka. Jedwali lifuatalo la 3.2, linabainisha mifano ya maneno yaliyokopwa kutoka kwa Kikuyu na tafsiri yake kwa Kishona.

**Jedwali 3.2: Mifano ya Ukopaji wa Maneno na Sentensi fupi za Kikuyu na Tafsiri yake ya Kishona**

| | Neno la Kikuyu/sentensi fupi kwa Kikuyu | Matumizi yake kwa Kishona |
|---|---|---|
| 1. | Kuhana atĩa/ Marauga atĩa. | (M)urirayiti? / (M)uribho here? |
| 2. | Wĩ mwega. | Mhoro/Mhoroi. |
| 3. | Uhoro waku. | Tikukwazisei. |
| 4. | Uhoro wa rucinĩ. | Mangwanani. |
| 5. | Watinda atĩa. | Makadinizvako? |
| 6. | Watinda atĩa. | Makadinizvenyu? |
| 7. | Nĩ kwega. | Ndirirayiti / ndiripo. |

Chanzo: Data ya nyanjani.

**Jedwali4.3: Mifano ya Ukopaji wa Maneno na Sentensi Fupi za Kiswahili na Tafsiri yake ya Kishona**

| | Sentensi fupi za Kiswahili | Tafsiri ya Kishona |
|---|---|---|
| 1. | Unasemaje? | (M)urirayiti? / (M)uribho here? |
| 2. | Uko salama? | Mhoro(i) |
| 3. | Habari yako? | Tikukwazisei. |
| 4. | Habari ya asubuhi? | Mangwanani. |
| 5. | Habari za mchana? | Maskati |
| 6. | Umeshindaje? | Makadinizvako? |
| 7. | Mmeshindaje? | Makadinizvenyu? |
| 8. | Niko salama. | Ndirirayiti / ndiripo. |
| 9. | Kikombe. | komichi au kapu. |
| 10. | Sufuria. | Hari. |
| 11. | Kupika chakula. | kubika chekudya. |
| 12. | Mgeni anakuja kulala kwetu | mueni alikuja kuzorara kwedu |
| 13. | Kuja tushone vikapu kwa sababu mvua nyingi inanyesha | Uya usone mabaskiti kwa sababu mvura zhinji ilikunaya |

Chanzo: Data ya nyanjani.

Kikuyu ni yale ambayo yanahusiana na salamu na kujuliana hali, jambo ambalo ni kawaida kwa wanajamii wanapoishi katika mazingira ya wingilugha. Vile vile, kwenye jedwali la 3.3, baadhi ya maneno na sentensi za Kiswahili zilizokopwa ni zile zinahusiana na salamu na maneno ya shughuli za nyumbani. Poplack (1980) anasema

kwamba ukopaji wa maneno hutokea kwenye viwango mbalimbali ambapo maneno au virai mkopo huingizwa kwenye lugha pokezi. Poplack (1980) na T'sou (2001) wanasema kuwa ukopaji wa maneno unaweza kutokea hata kama mzungumzaji hana ufahamu mzuri wa lugha ya pili au lugha nyingi. Hii huwa ndio hatua ya kwanza ya kujifunza lugha ya pili.

### 3.3 Ubadilishaji Msimbo

Utafiti huu ulinuia kutambulisha nafasi ya ubadilishaji msimbo kama athari mojawapo ya mtagusano lugha za Kiswahili na Kikuyu kwa Kishona nchini Kenya. Cook (2010), Grosjean (1982), Malik (1994) na Milroy na Muysken (1995) wanafafanua ubadilishaji msimbo kwamba ni tukio la kiisimu linalohusu kuingiza neno, kirai, ama sentensi ya lugha moja kwa lugha nyingine katika mazungumzo bila kuathiri sarufi ya lugha pokezi. Pfaff (1979) anasema kuwa kubadili msimbo ni tukio linaloathiri muundo wa kisemantiki, pragmantiki na isimujamii kwa lugha zinazozungumzwa na wanawingilugha.

Holmes (2001) anasema kwamba ubadilishaji msimbo waweza kutokea ndani ya sentensi moja au baina ya sentensi tofauti kwenye mazungumzo katika mazingira ya wingilugha. Hymes (1975) anasema kwamba katika mazingira ya wingilugha, kila lugha huwa na kazi yake: Lugha moja inaweza kuwa na kazi ya mazungumzo yasiyo rasmi na kwenye miktadha isiyo rasmi kama vile mazingira ya nyumbani huku lugha nyingine ikipewa jukumu la matumizi rasmi kama vile kwenye elimu na ofisini.

Holmes (2001) anasema kuwa ubadilishaji msimbo ni jambo ambalo linawezeshwa na vigezo vya kijumla katika jamii kama vile mtagusano lugha mbalimbali, miktadha

mbalimbali ya matumizi ya lugha katika jamii na dhima mbalimbali za lugha katika jamii. Ubadilishaji msimbo hufaulu iwapo wazungumzaji wanaohusika wanajua lugha wanazozitumia na sababu zao za kutumia lugha hizo. Ubadilishaji msimbo huwezekana hasa katika jamii za wingilugha ambapo wanajamiilugha wamezungukwa na lugha nyingi. Jedwali 3.4 lifuatalo linabainisha mifano ya ubadilishaji msimbo katika mazungumzo ya Washona.

**Jedwali 3.4: Ubadilishaji Msimbo kati ya Kiswahili na Kishona**

| | **Kuchanganya Kiswahili na Kishona** | **Sentensi Sahihi za Kiswahili** |
|---|---|---|
| 1. | Kuja *ndikutume.* | Kuja nikutume. |
| 2. | Nipe *chekudya.* | Nipe chakula. |
| 3. | *Ndiunzire* maji. | Niletee maji. |
| 4. | Mama *wari kupi.* | Mama yuko wapi. |
| 5. | Enda *kuchikoro.* | Enda shuleni. |
| 6. | Handeyi *chechi.* | Twende kanisani. |
| 7. | Handeyi *hospitari*. | Twende hospitali. |
| 8. | *Ingua ye kuzorora* kidogo. | Ni wakati wa kupumzika kidogo. |
| 9. | Mwana *vhangu akarara*. | Mwana/mtoto wangu amelala. |
| 10. | *Ndipe mari* yangu. | Nipe mali yangu. |
| 11. | Mgeni alikuja *kuzorara kwedu.* | Mgeni alikuja kulala kwetu. |
| 12. | *Uya usone mabaskiti* kwa sababu *mvura zhinji ilikunaya.* | Kuja ushone vikapu kwa sababu mvua nyingi inanyesha |

Chanzo: Data ya Nyanjani

Kwenye jedwali 3.4, mifano ya ubadilishaji msimbo kati ya Kiswahili na Kishona inadhihirika hasa baina ya watafitiwa vijana. Utafiti huu uligundua kwamba Washona wanabadili msimbo wanapozungumza kwenye maeneo yao ya nyumbani na maeneo ya kanisani kwa sababu hapa ndipo wanatumia lugha yao ya Kishona kwa wingi kuliko maeneo mengine. Hii inamaanisha kwamba lugha ya Kishona imo kwenye hatari ya

kutoweka kwa sababu lugha maarufu ya Kiswahili inapigania nafasi na Kishona kwenye maeneo ya nyumbani ambapo ndipo panafaa kwa matumizi ya lugha asilia.

Utafiti ulibainisha kwamba Washona pia wanafahamu Kiswahili vyema sana. (Taz.Baa-grafu 3.1). Hali hii inawafanya kubadilisha msimbo kwa lugha hizi mbili hasa katika sentensi wanapozungumza. Landweer (2000) anasema kwamba uhamishaji msimbo unaweza kuwa wa aina tatu kuu: uhamishaji msimbo kwenye jamii ya diglosia, hali ya wingilugha imara ambako miktadha ya kijamii ndiyo huamua msimbo utakaotumika kwa wakati fulani na uhamishaji msimbo ambao haujadhibitiwa unaotokea bila kufuata ruwaza yoyote (Buliba, Njogu na Mwihaki, 2006). Utafiti ulibainisha kwamba aina zote tatu za ubadilishaji msimbo zilizotajwa na Landweer zinafanyika baina ya Washona wa umri wote kwa kuwa wanaishi kwenye mazingira ya wingilugha. Hii inamaanisha kwamba lugha ya Kishona imeanza kuathiriwa na Kiswahili kwa kuwa ndiyo lugha maarufu inayozungumzwa kwenye maeneo wanamoishi Washona na hivyo basi uthabiti wa kiisimujamii wa Kishona umeanza kushuka.

### 3.4 Uthabiti wa Kiisimujamii wa Kishona

Giles, Bourhis na Taylor (1977) wanasema kwamba hadhi, demografia na usaidizi wa asasi za kijamii ndiyo mambo matatu yanayofanya viwango vya uthabiti wa kiisimujamii wa jamiilugha fulani kuinuka. Jamiilugha inaweza kuwa na uthabiti wa viwango mbalimbali kwa matumizi mbalimbali ya lugha yao katika mazingira ya wingilugha. Jamiilugha zilizo na uthabiti wa kiisimujamii usio imara huwa rahisi kwa lugha zao kumezwa na jamiilugha zilizo na uthabiti ulio imara kwa kuwa matumizi ya

lugha hiyo huwa mengi katika jamii. Sehemu zifuatazo zinaonyesha lugha inayotumiwa na Washona wa umri tofauti kwenye mazingira tofauti.

### 3.4.1 Lugha ya Vijana ya Mazungumzo kwenye Mazingira ya Nyumbani.

Landweer (2000) anasema kwamba maeneo ya nyumbani ndio msingi wa matumizi ya lugha ya mama. Kupunguka kwa matumizi ya lugha ya mama katika maeneo ya kijamii hasa nyumbani huwa ndio mwanzo wa kupunguka kwa uthabiti wa kiisimujamii katika lugha husika. Kuhusu uthabiti wa kiisimujamii wa lugha, shirika la UNESCO (2003) liliorodhesha vigezo ambavyo vinatumika kukadiria uthabiti wa lugha. Mojawapo ya vigezo hivyo ni kupokezanwa kwa lugha baina ya vizazi tofauti vya jamiilugha husika. Utafiti wa UNESCO (2003, 2011) uligundua kwamba lugha imo kwenye hatari ya kuangamia iwapo haitapokezanwa kwa kizazi cha vijana na watoto. Vijana na watoto wakianza kupunguza matumizi ya lugha husika kutoka maeneo mengine na kusalia kutumia lugha husika kwenye mazingira ya nyumbani pekee, basi lugha hiyo ipo kwenye hatari ya kuangamia. Utafiti huu ulilenga kubainisha lugha ambayo vijana wanatumia wanapoongea na wahusika mbalimbali katika maeneo ya nyumbani kama ifuatavyo:

### 3.4.2 Lugha ya Mazungumzo baina ya Vijana na Wazazi Nyumbani

Utafiti wa Fishman (1991) na UNESCO (2003) unasema kwamba kigezo cha kwanza kinachotumika kupima uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ni iwapo lugha husika inatumika katika maeneo ya nyumbani na iwapo inapokezanwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine au la. Utafiti huu ulilenga kubainisha lugha ambayo vijana hutumia katika

kuzungumza na wazazi nyumbani. Matokeo yanabainika kwenye jedwali 3.5 na jedwali 3.6 :

**Jedwali 3.5: Lugha ya Mazungumzo baina ya Vijana na Mama Mzazi**

| | Mirudio | Asilimia |
|---|---|---|
| Kishona | 102 | 100.0 |

Chanzo: Data ya Nyanjani

**Jedwali 3.6: Lugha ya Mazungumzo baina ya Vijana na Baba Mzazi**

| Lugha | Mirudio | Asilimia |
|---|---|---|
| Kishona | 60 | 58.8 |
| Kishona na Kiswahili | 30 | 29.4 |
| Kikuyu | 12 | 11.7 |
| **Jumla** | **102** | **100.0** |

Chanzo: Data ya nyanjani

Kutokana na matokeo katika jedwali la 3.5, watafitiwa vijana walikiri kwamba wanatumia Kishona pekee japo si sanifu wanapozungumza na mama mzazi. Vijana walitoa sababu kwamba kabla ya wanajamiilugha wa Kishona kupewa uraia nchini Kenya, wanajamiilugha wa kike hawangeweza kutoka nyumbani kwenda kujitafutia riziki au kuweza kusoma kwa sababu ya vikwazo vya kutokuwa raia wa Kenya. Hivyo basi, hawakupata fursa nzuri ya kujifunza Kiswahili ama lugha nyingine kupitia kwa utangamano na wanajamiilugha wengine au kupitia kusoma shuleni. Kwa upande mwingine, hilo lilikuwa jambo zuri katika juhudi za kudumisha Kishona katika maeneo ya nyumbani na hata katika kurithisha wanawe lugha yao ya Kishona. Vilevile, vijana

walikiri kwamba wanapozungumza na baba mzazi, kwenye jedwali la 3.6, asilimia 58.8 wanatumia Kishona huku asilimia 29.4 ya vijana wakichanganya lugha za Kishona na Kiswahili wanapozungumza na baba mzazi. Asilimia 11.7 wanatumia Kikuyu wanapozungumza na baba mzazi. Asilimia ya vijana waliokiri kutumia lugha nyingine isipokuwa Kishona wanapozungumza na baba mzazi walitoa sababu kwamba wanaume Washona wamejifunza lugha nyingine zinazowazunguka kwa kuwa ilikuwa imewalazimu kujitafutia riziki hata kama bado walikuwa hawana uraia. Hali ya kutafuta riziki iliwafanya kutangamana na wanajamiilugha wengine na hivyo basi wakajifunza lugha maarufu ya Kiswahili na baadhi yao wakajifunza Kikuyu. Hii inamaana kwamba lugha ya Kishona imeanza kuathirika kwa sababu kuna matumizi ya Kiswahili na Kikuyu na pia kuna kubadili msimbo kwenye maeneo ya nyumbani hasa vijana wanapoongea na baba mzazi.

Landweer (2000) anasema kwamba maeneo ya nyumbani ndio msingi wa matumizi ya lugha ya mama na anaendelea kusema kwamba kuanza kupunguka kwa matumizi ya lugha ya mama katika maeneo ya kijamii huwa ndio chanzo cha kupunguka kwa uthabiti wa kiisimujamii katika lugha husika. Jedwali 3.7 lifuatalo linaonyesha lugha ya mazungumzo baina ya vijana na babu na nyanya zao kwenye maeneo ya nyumbani.

**Jedwali 3.7: Lugha ya Mazungumzo baina ya Vijana na Babu na Nyanya**

| | Mirudio | Asilimia |
|---|---|---|
| Kishona | 94 | 92.2 |
| Kishona na Kiswahili | 8 | 7.8 |
| **Jumla** | **102** | **100.0** |


Chanzo: Data ya nyanjani

Kutokana na jedwali 3.7, lugha ya Kishona ilichaguliwa na asilimia 92.2 ya watafitiwa kama lugha ambayo vijana wanatumia kila wanapozungumza na babu na nyanya zao. Asilimia 7.8 ya vijana walikiri kwamba wanachanganya Kiswahili na Kishona au wanabadilisha msimbo wanapozungumza na wazee wao huku wakitoa sababu kwamba wazee hawa wanafahamu vyema lugha zote mbili. Utafiti wa UNESCO (2003) unasema kwamba idadi nzima ya wanajamiilugha wanaouzungumza lugha yao ni kiashiria tosha cha lugha husika kuwa na uthabiti au kukosa uthabiti wa kiisimujamii. Kwa kutumia kigezo cha idadi kamili ya wanaozungumza lugha husika, UNESCO wanasema kwamba lugha iliyo hatarini ni ile ambayo wanajamiilugha wengi wanaizungumza. Hii inamaanisha kwamba ingawa ni wanajamiilugha wengi wanaizungumza, kuna asilimia fulani ya wanajamiilugha hiyo ambao hawaizungumzi. Katika jedwali la 3.7, asilimia 7.8 ambayo hawatumii Kishona wanapozungumza na babu na nyanya ni ishara kwamba lugha ya Kishona imeanza kuathirika kwa mujibu wa lengo la kwanza la utafiti huu na pia lugha ya Kishona imeanza kupunguza uthabiti wake wa kiisimujamii.

### 3.4.3 Lugha ya Matumizi baina ya Ndugu.

Kerswill na Williams (2000) wanasema kwamba vijana ndio huonyesha sifa za kutalii matumizi ya lugha mbalimbali katika jamii kwa kufanyia lugha zilizo karibu nao majaribio kuliko kundi lolote katika jamii. Wanajamiilugha vijana hujifunza lugha zinazowazunguka kwa sababu mbalimbali ambazo zinawafaa kama vile sababu za kielimu, za kibiashara au za mazungumzo ya faraghani. Utafiti ulinuia kujua lugha ya matumizi baina ya ndugu katika familia. Matokeo yalionyeshwa katika Pai-chati 3.1 kama ifuatavyo:

**Pai-chati 3.1: Lugha ya Matumizi baina ya Ndugu**




Chanzo: Data ya nyanjani

Matokeo katika pai-chati 3.1 yanabainisha kwamba wahojiwa vijana asilimia 42.57 walipendelea kutumia Kishona baina yao wenyewe huku asilimia 41.58 wakizungumza Kiswahili baina yao. Asilimia 11.88 walikiri kuchanganya lugha za Kishona na Kiswahili katika mazungumzo yao huku asilimia 3.96 wakitumia lugha nyingine wakati wa mazungumzo baina yao katika maeneo ya nyumbani. Matokeo kwenye pai-chati 3.1 yanadhihirisha wazi kwamba kuna kipengele cha ubadilishaji msimbo miongoni mwa watafitiwa vijana.

Ilidhihirika kwamba lugha ya Kishona inapigania nafasi ya matumizi katika maeneo ya nyumbani na Kiswahili hasa baina ya vijana ambao wanavyosema Williams na Kerswill

(2000), ndio hufanyia lugha zote zinazowazunguka majaribio na hivyo wanajifunza na kutumia lugha hizo zote wanazokumbana nazo. Landweer (2000) anasema kwamba maeneo ya nyumbani ndio msingi wa matumizi ya lugha ya mama na anaendelea kusema kwamba kuanza kupunguka kwa matumizi ya lugha ya mama katika maeneo ya kijamii hasa baina ya vijana huwa ndio mwanzo wa kupunguka kwa uthabiti wa Kiisimujamii katika lugha husika. Landweer (kt.) na williams na Kerswill (2000) wanasema kwamba vijana na watoto ndio huendeleza lugha asilia. Kwa hivyo kulingana na maoni ya Landweer, uthabiti wa kiisimujamii wa Kishona unaendelea kupunguka kwa sababu vijana wameathiriwa na matumizi ya Kiswahili.


Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kwamba lugha za Kishona na Kiswahili zinatumiwa na asilimia iliyo sawa ya vijana katika jamii. UNESCO (2003)(taz. Jedwali 2.5) wanasema kwamba iwapo ruwaza ya matumizi ya lugha katika maeneo mbalimbali imeanza kubadilika basi lugha mojawapo imeanza kuathirika. Utafiti wa UNESCO unasema kwamba matumizi ya uwingilugha uliosawa katika jamii upo katika kiwango cha nne katika lugha iliyo kwenye hatari ya kutoweka. Lugha ya Kishona imeanza kuathirika kwa sababu nafasi yake katika jamii inaanza kuchukuliwa na Kiswahili katika maeneo mbalimbali katika jamii. Ilibainika pia kwamba mojawapo ya athari za mtagusano lugha mbalimbali katika jamii ya wingilugha ni ubadilishaji msimbo ambapo baadhi ya vijana (11.88%) wanatumia lugha zote wanapozungumza baina yao.

### 3.4.4 Lugha ya Mazungumzo baina ya Vijana na Viongozi wa Utawala

Hymes (1975) anasema kwamba katika mazingira ya wingilugha, kila lugha huwa na kazi yake. Lugha moja inaweza kuwa na kazi ya mazungumzo yasiyo rasmi na kwenye

miktadha isiyo rasmi kama vile mazingira ya nyumbani huku lugha nyingine ikipewa jukumu la matumizi rasmi kama vile kwenye elimu na ofisini. Washona wameishi nchini Kenya kwa zaidi ya miongo sita na wakati huo wote, wamekuwa wakitangamana na wanajamiilugha wengine. Utafiti ulidhamiria kubainisha lugha ambayo wasailiwa walipendelea kutumia wakati wa kuzungumza na viongozi wao hasa mzee wa kijiji ambaye si Mshona. Maoni yao yanadhihirika katika baa-grafu 3.4 ifuatayo.

**Baa-grafu 3.4: Lugha ya Mazungumzo na Mzee wa Kijiji**




Chanzo: Data ya Nyanjani

Matokeo katika baa-grafu 3.4 yanabainisha kwamba lugha ya Kiswahili ndiyo ilikuwa inatumika katika mazungumzo na mzee wa kijiji kwa sababu asilimia 59.80 walikiri kutumia Kiswahili. Asilimia 25.49 walikiri kutumia Kishona huku asilimia 14.71 wakitumia Kikuyu katika kuzungumza na mzee wa kijiji. Matokeo haya yanabainisha kwamba Washona hawakuwa na budi ila kujifunza Kiswahili na baadhi yao wakajifunza Kikuyu ili kurahisisha mawasiliano na utawala wa kijiji kwenye mitaa


walimoishi kupitia kwa mzee wa kijiji. Hii inamaanisha kwamba lugha ya Kishona imeanza kuathirika kwa kuwa haitumiki sana na haipati usaidizi wa asasi za kiserikali.

Kutokana na baa-grafu 3.4, inafahamika kwamba, kwa kuwa Washona hawakuwa na vibali vya uraia nchini Kenya anavyosema Wagalla (2019), haikuwa rahisi kwao kuwa na mzee wa kijiji kutoka jamiilugha yao ya Kishona. Ilibidi waishi chini ya uongozi wa mzee wa kijiji ambaye si Mshona. Hali hii iliwalazimu kujifunza lugha maarufu ya Kiswahili katika mitaa wanamoishi ili kufanikisha mawasiliano.

### 3.4.5 Lugha ya Mazungumzo baina ya Washona na Marafiki wa Nje ya Jamii Yao

Weinreich (1953) anasema kwamba katika hali ya ubadilishaji msimbo, wahusika huwa na ujuzi wa lugha nyingi ambazo wanazitumia katika hali au mazingira tofauti tofauti. Naye Hymes (1975) anasema kuwa lugha moja inaweza kuwa na kazi ya mazungumzo yasiyo rasmi na kwenye miktadha isiyo rasmi kama vile mazingira ya nyumbani na mazungumzo baina ya marafiki huku lugha nyingine ikipewa jukumu la matumizi rasmi kama vile kwenye elimu na ofisini. Utafiti ulitaka kubainisha lugha ambayo Washona hutumia wanapozungumza na marafiki ambapo baa-grafu 3.5 hapa chini inadhihirisha matokeo ya uchunguzi huo.

**Baa-grafu 3.5: Lugha ya Mazungumzo baina ya Marafiki**




Chanzo: Data ya nyanjani

Matokeo katika baa-grafu 3.5 kuhusu lugha ya mazungumzo baina ya marafiki wa jamiilugha ya Kishona yalibainisha kwamba asilimia kubwa (67.65%) ya watafitiwa hutumia Kiswahili huku asilimia 6.86 wakitumia Kishona katika mazungumzo yao na marafiki wa nje ya jamiilugha ya Kishona kwenye maeneo yao ya kijamii kama vile kazini au sokoni. Asilimia 7.84 walikiri kutumia Kikuyu kuzungumza na marafiki, asilimia 2.94 wakakiri kutumia lugha za Kiswahili na Kikuyu. Asilimia 6.86 walikiri kutumia lugha za Kishona na Kiswahili katika mazungumzo na marafiki wao na mwisho asilimia 7.84 wakakiri kutumia Kiswahili na lugha nyingine zinazowazunguka kama vile Kiingereza, Kimeru na Kikamba. Mufwene (2003) anasema kwamba wanajamiilugha huanza kupoteza uthabiti wa kiisimujamii wa lugha yao wakati

wanakosa kuitumia kwenye mazingira mbalimbali katika jamii. Mufwene anaendelea kusema kwamba wakati wanajamiilugha fulani huhamia mahali kwingine, huwa wanatangamana na lugha ambayo wamepata ikizungumzwa walikohamia na matokeo ni kwamba lugha hii mpya huwa na manufaa kwao kwa kuwa mazingira yao ni mapya.

Mugaddam (2006) anasema kwamba wanajamiilugha waliowachache kwenye mazingira mapya ya wingilugha huogopa kutumia lugha yao kwa kuhofia unyanyapaa. Wao hupendelea kuongea lugha maarufu ili wasitengwe na wenzao katika mazingira hayo. Bichang'a (2019) aligundua kwamba wanajamiilugha wa Ilwana walipendelea kutumia Kiswahili katika mazungumzo na marafiki ili waonekane kuwa Wabantu na pia wasitengwe na Wabantu wengine huko Tana River. Vivyo hiyo, Washona wanapoongea na marafiki zao ambao pia ni wa kutoka jamiilugha mbalimbali, utafiti huu ulibainisha kwamba wanatumia Kiswahili kwa sababu ya kuogopa kutengwa hasa kabla ya kupewa uraia, kwa sababu ya maelewano, kujenga mahusiano yao na pia kuwa sehemu ya jamii kwenye mitaa wanamoishi. Hii ni dhahiri kwamba lugha ya Kiswahili inapendelewa sana na inatoa ushindani mkubwa kwa Kishona katika mazungumzo baina ya marafiki. Kwa mujibu wa lengo la kwanza la utafiti huu, lugha ya Kishona imeanza kuathirika kwa kuwa haitumiki sana katika jamii. Landweer (2000) anasema kwamba lugha inayotumiwa sana katika jamii huwa na uthabiti wa kiisimujamii kuliko ile lugha ambayo haitumiki katika jamii.

### 3.4.6 Lugha ya Biashara

Obiols (2002) anasema kuwa katika jamii za wingilugha, wanajamiilugha huamua kutumia lugha moja au nyingine kwa sababu mbalimbali. Kwa mfano, wananaweza

kutumia lugha moja kwa biashara huku wakitumia lugha nyingine kwa shughuli nyingine katika jamii. Utafiti huu ulilenga kubainisha lugha ambayo Washona hutumia wakati wa biashara wakiwa katika maeneo wanamoishi kama inavyoonyeshwa katika jedwali 3.8 lifuatalo:

**Jedwali 3.8: Lugha ya Matumizi katika Shughuli za Biashara**

| | Mirudio | Asilimia |
|---|---|---|
| Kishona | 5 | 4.9 |
| Kiswahili | 92 | 90.2 |
| Kikuyu | 5 | 4.9 |
| **Jumla** | **102** | **100.0** |

Chanzo: Data ya nyanjani

Katika jedwali 3.8 ilibainika kwamba asilimia 4.9 ya wahojiwa wote walitumia Kishona katika kufanya shughuli za kibiashara. Asilimia 90.2 walikiri kwamba wanatumia Kiswahili katika shughuli zao za biashara. Asilimia 4.9 wanatumia Kikuyu katika shughuli za biashara kwenye maeneo yao. Appel na Muysken (2005) na Heine (1992) wanasema kwamba lugha iliyo na hadhi ya juu ni ile ambayo inamnufaisha mzungumzaji katika biashara na maingiliano ya kijamii. Naye Maya (2009) anadai kwamba katika biashara hasa katika karne ya kumi na tisa, njia moja iliyowezesha mtagusano ilikuwa kupitia kwa biashara ambapo ilibidi wafanyabiashara hasa wa watumwa wajifunze lugha maarufu ili waweze kuendesha shughuli zao sawasawa. Matokeo yalikuwa kwamba watumwa waliacha kutumia lugha zao asilia na kuanza kutumia lugha iliyokuwa maarufu.

Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kwamba matumizi ya Kishona yamepungua katika jamii ikilinganishwa na Kiswahili. Hii inamaanisha kwamba lugha ya Kishona imeanza

kuathiriwa na Kiswahili kimatumizi. Maoni ya Landweer (2000) ni sawa kwa hali hii anaposema kwamba kuanza kupunguka kwa matumizi ya lugha ya mama katika maeneo ya kijamii huwa ndio chanzo cha kupunguka kwa uthabiti wa Kiisimujamii katika lugha husika. Matokeo yanaonyesha kwamba lugha ya Kiswahili inaendelea kupata umaarufu katika jamiilugha ya Washona huku lugha ya Kishona ikiendelea kupunguka kwa uthabiti wake wa kiisimujamii.

### 3.4.7 Lugha ya Shughuli za Ibada

Thomason (2001) na Hamde (2005) wanakubaliana kwamba matumizi ya lugha kwenye dini huwa na mchango mkubwa katika kuendeleza na kudumisha lugha fulani. Waumini wanapokutana kwa shughuli za ibada na kutumia lugha wanayochagua kwenye kanisa lao, ni njia moja ya kudumisha lugha hiyo na pia ni njia moja ya kurithisha vizazi vichanga lugha hiyo. Utafiti huu ulilenga kudhihirisha lugha ambayo watafitiwa wanatumia katika shughuli za ibada hasa kwenye kanisa lao la *Gospel of God* lililoko katika maeneo ya *Valley Road* jijini Nairobi kama inavyowakilishwa katika jedwali 3.9 hapa chini:

**Jedwali 3.9: Lugha Inayotumika Kanisani**


| | Mirudio | Asilimia |
|---|---|---|
| Kishona | 48 | 47 |
| Kiswahili | 52 | 51 |
| Kikuyu | 2 | 2 |
| **Jumla** | **102** | **100.0** |

Chanzo: Data ya Nyanjani

Kutokana na jedwali 3.9, ilibainika kwamba asilimia 47 ya watafitiwa wanatumia Kishona katika shughuli za ibada, asilimia 51 wanatumia Kiswahili katika ibada huku

asilimia 2 wakitumia Kikuyu wakiwa katika maeneo ya ibada. Matokeo kwenye jedwali 3.9 ni wazi kwamba lugha za Kishona na Kiswahili zinatumika sana katika ibada ya Washona. Hali hii ni sawia na maoni ya O'Riagain (1994) anaposema kwamba mojawapo ya mambo yanayorithishwa vizazi vichanga kupitia kwa dini ni lugha. Kufikia sasa, Washona nchini Kenya wamefikia kizazi cha nne na wanatia juhudi za kuendeleza lugha yao kupitia kwa ibada yao ambayo wanaiendesha kutumia Kishona na kutafsiri kwa Kiswahili kwa washiriki ambao si Washona. Kwenye baa-grafu 3.6 ifuatayo, utafiti ulitaka kubainisha lugha nyingine zinazotumika kwenye ibada kando na Kishona.

**Baa-grafu 3.6: Lugha Nyingine Inayotumika Kanisani mbali na Kishona**





Chanzo: Data ya nyanjani

Katika baa-grafu la 3.6 ilibainika kwamba lugha nyingine inayotumika katika shughuli za ibada ya Washona ni Kiswahili ambayo iliwakilishwa na asilimia 84.62. Asilimia 15.38 walikiri kwamba lugha ya Kiingereza inatumika pia kanisani kwa shughuli za ibada. Hii inamaanisha kwamba, kando na Kishona kutumika katika maeneo ya kanisani, lugha ya Kiswahili pia inatumika. Lugha ya Kiingereza inatumika japo si asilimia kubwa. Watafitiwa walikiri kwamba lugha ya Kiingereza inatumika hasa na vijana wanapochanganya lugha zote wanaweka maneno ya Kiingereza kwenye mazungumzo yao wakiwa katika maeneo ya Kanisani. Kwa mujibu wa lengo la kwanza linalobainisha athari mbalimbali za mtagusano wa Kiswahili na Kikuyu kwa Kishona, matokeo yanamaanisha kwamba lugha ya Kishona imeathirika kwa kuwa haijapewa nafasi kubwa katika shughuli za ibada.

### 3.4.8 Lugha ya Matumizi Katika Maeneo ya Shuleni

Kwa mujibu wa Pauwels (2005) watoto wa umri wa kwenda shule ndiyo huwa kwenye hatari kubwa ya kutotumia lugha asilia kwa sababu iwapo shule yao haitilii maanani lugha asilia kwenye maeneo hayo au maeneo ya umma, basi lugha hiyo itatoweka tu. Watoto hukosa muda mwingi wa kuongea lugha yao asilia wakiwa kwenye maeneo ya shuleni na hivyo basi wanaanza kuisahau na badala yake wanatumia lugha maarufu au lugha rasmi.  Utafiti huu ulilenga kubainisha lugha iliyopewa umuhimu na katika maeneo ya shuleni kama inavyobainika katika baa-grafu 3.7 ifuatayo:

**Baa-grafu 3.7: Lugha inayotumika shuleni**





Chanzo: Data ya nyanjani

Kutoka baa-grafu 3.7, ilibainika kwamba lugha ya Kiswahili imepewa umuhimu mkubwa. Asilimia moja tu walikiri kutumia Kishona na Kiswahili kwenye maeneo ya shuleni na asilimia 6.86 wakakiri kutumia Kiswahili na Kikuyu huku asilimia 5.88 wakikiri kutumia Kiswahili na lugha nyingine katika maeneo ya shuleni. Githiora (2002) na Ontieri (2017) wanasema kwamba Kiswahili hutumika kama mojawapo ya somo nchini Kenya kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu. Fishman (1972b) na Landweer (2000) wanasema kwamba lugha inapotumika kwenye maeneo mbalimbali hasa maeneo rasmi kama vile shuleni, lugha hiyo huimarika kuliko ile lugha ambayo haitumiki. Utafiti huu ulibainisha kwamba lugha ya Kiswahili imepewa kipaumbele kuliko Kishona kwenye maeneo ya shuleni. Hii inamaana kwamba lugha ya Kishona inaendelea kupoteza uthabiti wake kwa kuwa haitumiki katika maeneo ya shuleni.

### 3.4.9 Matumizi ya Kiswahili, Kishona na Kikuyu katika Shughuli za Kitamaduni

King'ei (2010) anaeleza kwamba lugha ni zao la jamii na ni kipengele muhimu cha utamaduni wa jamii yoyote na haiwezi kutenganishwa na utamaduni wa jamii. Utafiti huu ulinuia kubainisha lugha ambayo imepewa kipaumbele katika shughuli za kitamaduni kama inavyodhihirika katika baa-grafu 3.8 ifuatayo:

**Baa-grafu 3.8: Lugha Muhimu kwa Shughuli za Kitamaduni**




Chanzo: Data ya nyanjani


Utafiti ulibainisha lugha inayopendelewa katika shughuli za kitamaduni kama vile harusi, kumpa mtoto jina, ndoa ama harusi na hata mazishi kwenye jamiilugha ya Washona. Asilimia 66.67 ya watafitiwa walikiri kwamba wanatumia Kishona katika shughuli zao za kitamaduni. Asilimia 29.41 walikiri kutumia Kiswahili kwenye shughuli za utamaduni. Asilimia 3.92 walikubali kutumia Kikuyu wanapofanya

shughuli mbalimbali za kitamaduni. Matokeo kwenye baa-grafu 3.8 yanawiana na maoni ya Giles, Bourhis na Taylor (1977), Wolck (2004) na Landweer (2000) wanaposema kwamba jamiilugha nyingi huwa na mikakati ya kudumisha tamaduni zao kupitia kwa lugha yao asilia.

Jamii ya Washona hasa wazee wanatumia lugha yao ya Kishona kwenye shughuli zao mbalimbali za kitamaduni licha ya kuwepo kwa lugha maarufu zinazowazunguka. Pia anavyosema O'Riagain (1994), kila kizazi hubuni na kuweka mikakati ya kurithisha kizazi kinachofuata utamaduni wake ambapo lugha ya mama huwa ni kipengele cha kwanza muhimu cha utamaduni ambacho wazazi hurithisha wana wao. Matumizi ya Kishona na urithisho wake kwa vizazi vichanga ni juhudi nzuri za kufanya lugha hii kuwa na uthabiti wa kiisimujamii licha ya shinikizo kutoka lugha maarufu.


Kwa kutumia vipimo vya UNESCO (2003, 2011), utafiti ulichunguza iwapo lugha ya Kishona ni thabiti kupitia kipimo cha kupokezanwa kwa lugha kwa vizazi vyote vya Washona. Baa-grafu 3.9, 3.10 na 3.11 zifuatazo zinabainisha matumizi ya lugha kwa watoto, vijana na wazee wa jamiilugha ya Kishona katika maeneo ya nyumbani ambapo ndipo kupokezanwa kwa lugha hufanyika.

**Baa-grafu 3.9: Lugha Wanayotumia Watoto katika Maeneo ya Nyumbani**





Chanzo: Data ya Nyanjani

**Baa-grafu 3.10: Lugha Wanayotumia Vijana katika Maeneo ya Nyumbani**




Chanzo: Data ya Nyanjani

**Baa-grafu 3.11: Lugha Wanayotumia Wazee katika Maeneo ya Nyumbani**




Chanzo: Data ya Nyanjani

Kutokana na baa-grafu 3.9, inabainika kwamba watafitiwa watoto wanatumia Kiswahili katika maeneo ya nyumbani kuliko Kishona. Asilimia 68.63 ya watoto wanatumia Kiswahili huku asilimia 31.37 wakitumia Kishona katika maeneo ya nyumbani. Kwenye baa-grafu 3.10, asilimia 31.37 ya vijana wanatumia Kishona wakiwa katika maeneo ya nyumbani, asilimia 62.75 walikiri kutumia Kiswahili katika maeneo ya nyumbani na asilimia 5.88 walikiri kutumia Kikuyu katika maeneo ya nyumbani. Katika baa-grafu la 3.11, asilimia 59.80 walikiri kutumia Kishona kwenye maeneo ya nyumbani, asilimia 35.29 wakakiri kutumia Kiswahili na asilimia 4.90 wakakiri kutumia Kikuyu kwenye maeneo ya nyumbani.

Utafiti wa UNESCO (2003) unabainisha kwamba lugha iliyo kwenye hatari ya kuangamia ni ile ambayo wazazi wameacha kuwapokeza wanao. Kwenye mizani ya UNESCO (2003) (taz jedwali 2.3) iliyo na vipimo sita, lugha ya Kishona ipo kwenye kipimo cha tatu (3) katika kiwango cha kupokezanwa lugha kwa vizazi mbalimbali vya jamiilugha ya Washona. Kipimo hicho cha tatu kinasema kwamba lugha iliyo hatarini ni lugha ambayo watoto hawajifunzi wala kuizungumza kama lugha yao ya kwanza kwenye maeneo ya nyumbani. Lugha hiyo hutumika sana kuanzia wazazi kuelekea juu.


Ang'iela (2002) anasema kwamba watoto wasiporithishwa lugha yao asilia huishia kujifunza lugha ya watoto wenzao katika mazingira yale yale ya wingilugha. Utafiti huu ulibainisha kwamba asilimia kubwa ya watoto wanatumia Kiswahili kwenye maeneo ya nyumbani kuliko Kishona. Asilimia kubwa ya vijana pia hutumia Kiswahili kwenye maeneo ya nyumbani. Matokeo kwenye baa-grafu 3.9, 3.10 na 3.11 yanabainisha kwamba lugha ya Kishona imeanza kubadilika na kuhama na ipo kwenye hatari ya kuangamia kwa kuwa vijana na watoto wengi hawaizungumzi katika maeneo ya nyumbani na badala yake wanatumia Kiswahili.

### 3.5 Wingilugha

Wingilugha ni athari nyingine ya mtagusano lugha katika jamii ambapo mtu au watu huwa na uwezo wa kuzungumza zaidi ya lugha moja. Malechova (2016) anasema kwamba wingilugha hutokea kwa sababu nyingi zikiwemo sababu za kibinafsi, za kijamii, za kisisasa, na za kiuchumi. Wingilugha huwa na manufaa mengi katika jamii kwa kuwa huleta uhusiano bora kati ya jamii na mataifa mbalimbali. Utafiti ulitaka

kujua iwapo Washona wanazungumza lugha nyingine za Kenya. Baa-grafu 3.12 ifuatayo inadhihirisha matokeo:

**Baa-grafu 3.12: Lugha Nyingine Zinazozungumzwa na Washona**




Chanzo: Data ya Nyanjani

Utafiti ulibainisha kwamba Washona ni wanawingilugha kwa kuwa baadhi yao wanazungumza na kufahamu lugha nyingine kama vile Kiingereza, Kimeru, Kikamba na lugha nyingine za kutoka nje ya Kenya. Asilimia 62.36 walikiri kujua lugha ya Kiingereza, asilimia 20.79 walikiri kujua lugha ya Kimeru na asilimia 10.89 walikiri kufahamu na kuzungumza lugha za Kikamba. Asilimia 8.9 walikiri kufahamu lugha za nje ya Kenya ambazo ni Kindebele na Kizulu zinazozungumzwa maeneo ya kusini mwa Afrika. Madai ya Auer na Wei (2009) kwamba wingilugha ni sehemu ya suluhisho katika matatizo yanayokumba wanajamiilugha katika jamii ni kweli kwa

wanajamiilugha wa Kishona kwa sababu kulingana na nao, Washona walipitia shida chungu nzima nchini Kenya kabla ya kupewa uraia mwaka wa 2020. Kujua lugha za Kenya ilikuwa mbinu mojawapo ya kukwepa kufungwa. Watafitiwa walisema:

> *"Ilikuwa ni poa kwetu Washona kuzungumza Kiswahili na Kikuyu kwa sababu askari hawangegundua haraka kama sisi si Wakenya. Lugha hizi za Kenya zilituficha sana. Lakini kuna wakati mwingine wanajamii walitusema na tukajipata tumefungwa.".*
>
> *Chanzo: Data ya Nyanjani.*


Washona pia ni wanawingilugha kwa kuwa mazingira walimojipata ni mazingira ya wingilugha. Mberia (2014) anasema kwamba Waafrika ni baadhi ya wanawingilugha duniani kwa sababu ya mtagusano na lugha nyingi zinazowazunguka. Naye Kamau (2015) alithibitisha haya kwa kusema kwamba Kaunti ya Kiambu na jiji la Nairobi ni maeneo ya wingilugha kwa kuwa wanajamiilugha wengi huishi katika maeneo haya. Washona wengi huishi katika mitaa mitano ya Kaunti ya Kiambu ambayo ni Kikuyu, Kinoo, Kiambaa, Gitaru na Githurai.

Obiols (2002) anasema kuwa katika jamii za wingilugha, wanajamiilugha huamua kutumia lugha nyingine kwa sababu kuu ya mawasiliano, biashara na elimu. Hili ni kweli kwa wanajamiilugha wa Kishona kwa kuwa kama ilivyodhihirika katika majedwali 3.8 na 3.9, pai-chati 3.1, na baa-grafu 3.4, 3.5, 3.6 na 3.7, Washona hutumia Kiswahili kwa sababu mbalimbali kama vile biashara, elimu, ibada, mawasiliano na kujitafutia riziki. Hali hii ya wingilugha ambayo inawezesha lugha moja kupewa majukumu mengi katika jamii kuliko lugha nyingine, imefanya lugha ya Kishona kuathirika kwa sababu haitumiki sana kwenye maeneo mengi na katika shughuli nyingi za kijamii. Uthabiti wa kiisimujamii wake umeshuka ikilinganishwa na Kiswahili.

### 3.6 Mabadiliko ya Kishona

Thomason na Kaufman (1988) na Florian (1998) na Ngure (2012) wanasema kwamba mabadiliko ya lugha hasa katika mazingira ya wingilugha ni jambo lisiloweza kuzuilika. Lugha hubadilika kwa hali mbili: Hali ya kimakro inayohusisha sehemu kubwa iliyo na watu wengi wa jamiilugha husika. Hali ya pili ya kimaikro ambayo huhusisha watu wachache kisha huigwa na kundi kubwa la watu katika jamiilugha husika anavyosema Florian (1998). Utafiti ulilenga kubainisha iwapo watafitiwa wanazungumza Kishona kwa usanifu au la. Baa-grafu 3.13 ifuatayo inadhihirisha majibu yao.

**Baa-grafu 3.13: Kiwango cha Umilisi wa Kishona**




Chanzo: Data ya Nyanjani

Watafitiwa asilimia 70.30 walikiri kwamba hawazungumzi Kishona sanifu huku asilimia 29.70 wakikubali kwamba wanazungumza Kishona kwa undani. Hii ni dhahiri

kwamba asilimia kubwa ya Washona wameanza kuhama kutoka lugha ya Kishona huku asilimia ndogo (30%) wakitumia lugha yao kwa usanifu.

Lugha yaweza kubadilika kupitia kulazimishwa au kwa hiari tu anavyosema Thomason (2000). Utafiti huu ulibainisha kupitia matokeo ya baa-grafu 3.13 kwamba lugha ya Kishona imeanza kubadilika kwa hiari tu na wala si kulazimishwa. Kama tulivyokwisha kutaja awali, mabadiliko ya lugha yanayotokea kwa hiari huchukua muda mrefu. Lugha ya Kishona imechukua muda mrefu kubadilika ambapo sasa mabadiliko yanaweza kuonekana kwenye viwango vya mofolojia na sintaksia ambapo maneno ya Kiswahili na machache ya Kikuyu yanaingizwa kwenye Kishona wanapozungumza. (Taz. Jedwali 3.2 na jedwali 3.3)

**3.7 Hitimisho**

Sura hii imeshughulikia uwasilishaji na uchanganuzi wa data kutoka lengo la kwanza lililolenga kubainisha athari za mtagusano wa Kiswahili na Kikuyu kwa Kishona. Athari mbalimbali zilizojadiliwa ni kama vile ukopaji wa maneno, ubadilishaji msimbo, hali ya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha, wingilugha na mabadiliko ya lugha. Ilibainika kwamba kwenye maeneo ya wingilugha, lugha iliyo na idadi ya chini ya wazungumzaji huathiriwa na lugha maarufu inayowazunguka. Ilifahamika kwamba lugha maarufu kwa wanajamiilugha wa Kishona ni Kiswahili kwa kuwa imepewa majukumu mengi katika maeneo wanamoishi na hivyo basi hawana budi ila kujifunza na kutumia lugha hiyo. Ilifahamika pia kwamba lugha ya Kiswahili inatumika kwenye maeneo ya nyumbani ambapo lugha asilia inafaa kudumishwa.

Ukopaji wa maneno kutoka Kiswahili na Kikuyu na ubadilishaji wa msimbo katika Kishona ulidhihirika wakati wasailiwa walikiri kwamba wameathirika na mtagusano wa Kiswahili na Kikuyu. Hii ni kwa sababu lugha ya Kiswahili ina majukumu mbalimbali katika shughuli nyingi za kijamii kama vile masomoni, biashara na matumizi muhimu ya maisha. Kutokana na matumizi haya mengi ya Kiswahili kwenye maeneo mengi ya jamii ya Washona, ukopaji wa maneno na ubadilishaji msimbo katika mazungumzo ni jambo lisiloweza kuepukika. Ukopaji wa maneno na ubadilishaji msimbo ni ishara ya kwanza inayoonyesha kwamba lugha ya Kishona imeanza kuathirika.

Utafiti ulibainisha kwamba, lugha ya Kishona imepewa majukumu machache katika jamii kama vile kwenye maeneo ya nyumbani na katika sherehe za kitamaduni. Hii ni kwa sababu kuna lugha nyingi maarufu zinazowazunguka wanajamiilugha Washona. Hali hii ya wingilugha imefanya wanajamiilugha kuchagua lugha maarufu na lugha iliyo na manufaa kwa Washona kama vile kwenye biashara na kwa shughuli rasmi kama vile masomoni. Ilidhihirika kwamba kwenye maeneo ya nyumbani, wahusika wazee ndio hutumia Kishona wanapoongea na wanawe ilhali wahusika vijana hutumia Kiswahili wanapozungumza na watoto wao pamoja na marafiki wao na pia wanapozungumza baina yao. Hali hii inaashiria mabadiliko na uhamaji wa lugha ya Kishona na pia inaonyesha kwamba viwango vya uthabiti wa kiisimujamii wa Kishona vimeshuka.

Mabadiliko na uhamaji wa Kishona ulianza kuonekana wakati ambapo wasailiwa walikiri kwamba hawazungumzi kwa usanifu lugha yao ya Kishona. Hali hii hutokea wakati ambapo wanajamiilugha hukoma kutumia lugha yao asilia na kuanza kutumia

lugha ya pili kwa shughuli nyingi za kijamii hasa kwenye maeneo ya nyumbani ambapo ni kitovu cha matumizi ya lugha asilia. Utafiti huu ulithibitisha kwamba Washona wengi hasa vijana na watoto hutumia Kiswahili kwa shughuli nyingi na kwenye maeneo mengi katika jamii kuliko Kishona na Kikuyu. Hali hii ni bayana kwamba uthabiti wa kiisimujamii wa Kishona umepungua kutokana na athari zinazotokana na mtagusano wa Kiswahili na Kikuyu. Ni dhahiri kwamba lengo la kwanza la utafiti huu la kubainisha athari mbalimbali za mtagusano wa Kiswahili na Kikuyu kwa Kishona lilitimia kwa kuwa athari mbalimbali zilibainishwa.

Sura ifuatayo ya nne inashughulikia sababu zinazopelekea Washona kutumia Kiswahili na Kikuyu kwenye maeneo mbalimbali ya kijamii na mieleko yao kuhusu matumizi ya lugha za Kiswahili na Kikuyu.

# SURA YA NNE: SABABU ZA WASHONA ZA KUTUMIA KISWAHILI NA KIKUYU NA MIELEKEO YAO KUHUSU LUGHA HIZI

## 4.0 Utangulizi

Sura ya tatu ilishughulikia athari mbalimbali zinazosababishwa na mtagusano wa Kiswahili na Kikuyu kwa Kishona nchini Kenya. Ilibainika kuwa lugha ya Kishona nchini Kenya imeathirika kwa njia kadhaa kutokana na mtagusano wake na lugha za Kiswahili na Kikuyu kwa kuwa ndizo zinazowazunguka kwenye maeneo wanamoishi na zimepewa majukumu mengi katika jamii kuliko Kishona.

Sura hii ya nne imetokana na malengo mawili ya utafiti ambayo ni sababu zinazowafanya Washona kutumia Kiswahili, Kikuyu na Kishona katika maeneo mbalimbali ya kijamii na mielekeo yao kuhusu matumizi ya Kiswahili na Kikuyu katika maeneo mbalimbali ya kijamii. Sababu mbalimbali zinazowafanya Washona kutumia Kiswahili katika maeneo mbalimbali zilizobainishwa kwenye sura hii ni kama vile: sababu za kielimu, utaifa wa lugha, sababu za mawasiliano, sababu za kiutangamano, kujenga mahusiano, utambulisho, sababu za kidini na sababu za kiusalama.

Baker (1992) na Bartram (2010) wanafafanua mielekeo ya lugha kuwa ni hisia za mtu au watu kuhusu lugha yao au lugha ya watu wengine katika mazingira ya wingilugha. Mielekeo hasa ya lugha huzua matokeo mbalimbali katika jamii, ambayo yanaweza kuwa ya kuridhisha au kutoridhisha. Simandan (2016) anasema kwamba ikiwa watu wana mielekeo chanya kuhusu lugha husika, basi ni hamasisho tosha la kujifunza lugha hiyo ya pili. Vivyo hiyo, iwapo mtu ana mielekeo hasi kuhusu lugha fulani, hataweza kujifunza au kutumia lugha hiyo. Landweer (2000) anasema kwamba lugha ikitumika

katika maeneo mbalimbali ya kijamii, huwa na uthabiti wa kiisimujamii wa hali ya juu ikilinganishwa na ile lugha ambayo haitumiki. Lugha ikipewa kipaumbele katika jamii ya wingilugha, itaathiri ile lugha ambayo ina wazungumzaji wachache au ile lugha iliyo na matumizi machache katika jamii. Katika sura hii, sababu za Washona za kutumia lugha za Kiswahili, Kikuyu na Kishona zilishughulikiwa kwanza kwa mujibu wa lengo la pili la utafiti huu kisha kwenye sehemu ya pili ya sura hii, mielekeo ya Washona katika matumizi ya Kiswahili na Kikuyu ikashughulikiwa kwa mujibu wa lengo la tatu la utafiti huu.

## 4.1 Sababu za Washona za Kutumia Kiswahili kwenye Maeneo Mbalimbali ya Kijamii

Landweer (2000) anasema kwamba lugha hutumiwa kwa sababu mbalimbali na kwenye maeneo mbalimbali ya kijamii ambapo watu wa familia moja huishi. Uchanganuzi wa data ulibainisha kwamba Washona wana sababu nyingi za kutumia lugha ya Kiswahili kwenye maeneo mbalimbali ya kijamii. Sababu hizi ni kama vile sababu za kielimu, urasmi wa lugha, sababu za mawasiliano, mahusiano ya kijamii, kiuchumi, utambulisho, kueneza injili na sababu za kiusalama. Sababu ya kiusalama imejadiliwa kwanza.

### 4.1.1 Sababu za Kielimu

Lugha ya Kiswahili ina matumizi chungu nzima nchini Kenya ikiwemo matumizi yake katika elimu. Katika mtalaa wa elimu nchini Kenya, Kiswahili hufunzwa kama mojawapo ya somo kuanzia shule za chekechea hadi vyuo vikuu nchini Kenya. Kloss (1966), Fishman (1966), Campbell na Schnell (1987) wanasema kwamba elimu ni

kigezo muhimu katika ujifunzaji wa lugha. Kalantizis (1985) anatoa mfano wa lugha ya Kigiriki ambapo Wagiriki wengi nchini Amerika walianzisha madarasa hasa vipindi vya mchana kanisani na kwenye shule za kibinafsi ambapo lugha yao ya Kigiriki ilikuwa ikifunzwa kwa watoto wa Kigiriki. Hii ilisaidia watoto kujifunza Kigiriki hasa ikizingatiwa kwamba Marekani kuna lugha nyingi tena maarufu ambazo zinaleta shinikisho kwa lugha za waliowachache. Kalantizis (kt.) anaendelea kusema kwamba lugha ikifunzwa kama mojawapo ya somo shuleni, huwa inawapatia wanafunzi motisha ya kuizungumza na hivyo kuinua hadhi yake.

Tsounis (1974) anakubaliana na maoni ya Kalantizis (1985) kwa kusema kwamba mielekeo chanya na juhudi za serikali ya Australia katika kuhimiza shule zao kufunza watoto Wagiriki lugha yao ya kwanza zilihimiza ujifunzaji wa lugha asilia nchini humo. Utafiti huu ulilenga kubainisha lugha iliyokuwa inatumika katika masomo. Jedwali 4.1 lifuatalo linaonyesha majibu ya watafitiwa ambao ni watoto kupitia swali la lugha ambayo wanaongea shuleni.

**Jedwali 4.1: Kiswahili Kama Mojawapo ya Somo Shuleni**

| Watafitiwa | Swali: Mnaongea lugha ipi shuleni? |
|---|---|
| 1. | Tulipoingia shuleni, mwalimu anatuzungumzia kwa lugha ya Kiswahili. Kisha tunasoma mambo mbalimbali yaliyoandikwa kwa Kiswahili. |
| 2. | Mimi niko darasa la saba, moja ya masomo tunayosoma ni Kiswahili. Ninapenda sana tunaposoma sehemu ya ufahamu kwa sababu ya hadithi hizo zilizoandikwa kwa Kiswahili. |
| 3. | Niko kidato cha pili. Huwa tunasoma somo la Kiswahili mara moja kwa kila siku. Ninapenda upande wa fasihi simulizi. |
| 4. | Niko katika kidato cha nne. Kiswahili ni somo rahisi sana. Kuna hata fasihi ambapo tunasoma riwaya na tamthilia ili kuelewa mambo katika jamii. |
| 5. | Kwanza, shuleni tunatumia Kiswahili... |

Chanzo: Data ya Nyanjani

Katika jedwali 4.1 watafitiwa walikiri kwamba wanafunzwa Kiswahili kama mojawapo ya somo katika shule zao huku wakisema kwamba somo la Kiswahili ndilo lililokuwa rahisi ikilinganishwa na masomo mengine. Hii inamaanisha kwamba kwa mujibu wa lengo la pili la utafiti huu, sababu ya kwanza ya Washona ya kutumia Kiswahili ni ya kielimu kwa kuwa kutokana na jedwali 4.1, lugha ya Kiswahili inatumika shuleni. Watafitiwa watoto kuanzia umri wa miaka sita hadi vijana wa umri wa miaka 35 walikiri kwamba katika safari ya masomo yao, somo la Kiswahili ndilo lililokuwa rahisi sana shuleni kwa kuwa hata baada ya vipindi vya darasani, bado walikuwa wanatumia Kiswahili katika mazungumzo yao.

Lee (2002) anasema kwamba kujifunza lugha ya waliowengi inawezekana bila kulazimishwa hasa inapokuwa kwamba ndiyo lugha inayotumika katika maeneo ya shuleni. Lee anatoa mfano wa Kiingereza ambapo ilibidi watoto wa nchi ya *Ireland* kujifunza lugha ya Kiingereza ili waweze kupata elimu shuleni walipokuwa wahamiaji. Holmes (2001) anasema kwamba ni rahisi sana kwa watoto wadogo kuhama kutoka kwa lugha yao ya kwanza hadi lugha maarufu kwa kuwa muda mwingi wanapokuwa shuleni, wanaposoma au wanapocheza katika mazingira ya shuleni, wanatangamana na watoto wengine wanaozungumza lugha maarufu. Hali hii huwezekana hasa kwa sababu katiba ya Kenya 2010, kipengele cha 53(1)b, inasema kwamba kila mtoto ana haki ya elimu ya msingi bila malipo ya lazima. Watoto wakiwa shuleni, hutumia lugha rasmi katika masomo ambapo Kiswahili ni mojawapo ya somo na pia lugha ya matumizi katika mazingira ya shuleni. Katika jedwali 4.2, watafitiwa wanathibitisha matumizi ya Kiswahili nje ya mazingira ya darasani kutokana na swali la iwapo wanazungumza Kiswahili nje ya darasa.

**Jedwali 4.2: Matumizi ya Kiswahili katika Maeneo ya Shuleni Nje ya Darasa**

| Watafitiwa | Je, mnazungumza Lugha ya Kiswahili nje ya darasa? |
|---|---|
| 1. | Tukitoka darasani wakati wa mapumziko mafupi bado tunazungumza Kiswahili. |
| 2. | Tunazungumza Kiswahili njiani tunapoenda shuleni na marafiki na hata tunapocheza. |
| 3. | Hata tukiwa  na marafiki zetu Washona na wale si Washona kule nyumbani tunazungumza Kiswahili. |
| 4. | Naam, tunapenda kutumia Kiswahili tukiwa kwenye mapumziko mafupi shuleni. Lakini bado pia siku hizi, lugha ya Sheng' imeanza kubobea japo hairuhusiwi kutumika kwenye mazingira ya shule yetu. |

Chanzo: Data ya Nyanjani

Kwenye jedwali la 4.2, majibu ya vijana na watoto yanabainisha wazi kwamba wanatumia Kiswahili nje ya darasa na nje ya mazingira ya shuleni kwa kuwa ni lugha maarufu nchini Kenya na ni mojawapo ya somo linalofunzwa shuleni na wanafunzi wanajipata wakitumia lugha hii hata baada ya masaa ya shuleni. Kwa mujibu wa lengo la pili la utafiti huu, watoto wanaosoma bado wanatumia lugha hii kwa sababu ya elimu hata wakiwa nje ya mazingira ya shuleni. Landweer (2000) anasema kwamba lugha iliyopewa hadhi ya juu katika jamii, huwa inapewa majukumu mengi katika jamii na hivyo basi huendelea kuimarika na kuwa thabiti.

### 4.1.2 Sababu za Utaifa na Urasmi wa Kiswahili Nchini Kenya

Sababu ya pili ya kujifunza na kuzungumza Kiswahili kwa Washona ni kwamba Kiswahili ni lugha ya taifa la Kenya, Afrika Mashariki na pia lugha ya kimataifa. Kimemia (2002) anasema kwamba kwa kuwa Kiswahili ni lugha ya taifa nchini Kenya, ina matumizi mapana sana kuliko lugha za kiasili za Kenya na ina idadi kubwa ya wazungumzaji ikilinganishwa na lugha nyingine za kiasilia. Utafiti wa Landweer (2000) na UNESCO (2003) unaonyesha kuwa wanajamiilugha wanaozungumza lugha husika

sanifu wakiwa wengi, lugha hiyo inaendelea kuimarika. Lugha ya Kiswahili inaendelea kupata idadi kubwa ya wazungumzaji na kuendelea kuwa imara kila uchao ikilinganishwa na Kishona na lugha nyingine za kiasilia nchini Kenya. Maoni ya wasailiwa kwenye mjadala wa kikundi cha vijana na watoto kwenye jedwali 4.3 yanathibitisha sababu ya pili ya Washona kutumia Kiswahili kama lugha ya taifa na lugha rasmi nchini Kenya.

**Jedwali 4.3: Kauli za Watafitiwa kuhusu lugha ya Taifa na Lugha Rasmi**

| Watafitiwa | Mnaongea lugha ipi sana kwa sasa na kwa nini? |
|---|---|
| 1. | Tunazungumza Kiswahili sana... |
| 2. | Kwanza, shuleni tunatumia Kiswahili, pili, Kiswahili ni lugha rasmi hapa Kenya... Tatu, tumezungukwa na makabila mengi na lugha mwafaka ni Kiswahili kwa kuwa ni lugha rasmi na lugha ya taifa. Lakini tukikutana na marafiki Wakikuyu, huwa tunajaribu kuongea lugha yao. |
| 3. | Tunatumia Kiswahili kwa sababu ni lugha ya taifa, na pia kwa sababu ni lugha ya mawasiliano. Kiswahili pia kinatumiwa kutuunganisha na wakenya wengine. |

Chanzo: Data ya Nyanjani

Kutokana na jedwali 4.3, ni wazi kwamba Washona wanatumia Kiswahili kwa sababu ni lugha rasmi nchini Kenya na ni lugha ya taifa la Kenya kwa mujibu wa lengo la pili la utafiti huu. Tangu mwaka wa 1963, Kiswahili kilitambulika kama lugha ya taifa na pia lugha rasmi kulingana na katiba ya Kenya ya mwaka 2010. Githaiga (2022) anasema kwamba lugha ya Kiswahili ilikubalika na Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka wa 2017 kama lugha rasmi katika nchi zote za jumuiya ya Afrika Mashariki kama vile Kenya, Tanzania, Uganda, Rwanda, Burundi, Sudan Kusini na Demokrasia ya Kongo. Hivyo basi, Washona walipofika Kenya kuanzia mwaka wa 1957, hawakuwa na budi ila kujifunza lugha ya taifa na lugha rasmi ili kuelewana na Wakenya katika

nyanja mbalimbali kama vile masomoni, shughuli za mahakamani na kwenye sekta ya uchukuzi. Washona walikiri kwamba sababu kuu ya kujifunza Kiswahili ni kwamba ni lugha ya taifa na lugha rasmi.

#### 4.1.3 Sababu za Mawasiliano na Utangamano

King (2022) anaeleza kuwa watu hujifunza lugha ya pili ili mawasiliano yawe rahisi hasa wageni wanapoishi katika taifa geni ama jamii mpya. Landweer (2000) anasema kwamba kujifunza lugha ya pili hutokea wakati ambapo utamaduni na lugha ya watu wa jamiilugha fulani huwa na hadhi ya juu katika jamii za wingilugha kuliko jamii nyingine. Vilevile nguvu za kidemografia za watu wa jamii katika eneo fulani huchangia kujifunza lugha mpya. Hapa ni kusema kwamba, katika jamii ya wingilugha, ile jamiilugha iliyo na idadi ya chini hulazimika kujifunza lugha ya jamiilugha iliyo na idadi kubwa ya watu kwa kuwa wana nguvu za kidemografia na hivyo matumizi ya lugha yao huwa mengi katika jamii anavyosema Holmes (2001). Utafiti ulitaka kubainisha iwapo Washona walijifunza na kuzungumza Kiswahili ili kuondoa kikwazo kinachozuia mawasiliano ambacho huwafanya watu wasizungumze kwa kuwa hawajui lugha zinazohusika. Maoni ya watafitiwa yanathibitisha kwamba Kiswahili ni lugha ya mawasiliano kupitia kwa jedwali 4.4

**Jedwali 4.4: Kauli za Watafitiwa kuhusu Lugha ya Mawasiliano na Utangamano**

| **Watafitiwa** | Maoni Kuhusu Kiswahili Kama Lugha ya Mawasiliano. |
|---|---|
| **Mtafitiwa II** | ...tunazungumza Kiswahili kwa sababu ya kurahisisha mazungumzo kati yetu na makabila mengine hapa nchini Kenya. Lugha ya Kiswahili ni lugha ya Kuwasiliana. |
| **Mtafitiwa IV** | Katika safari yetu tulikuwa tumepitia Kongo na Tanzania ambapo lugha ya Kiswahili inazungumzwa. Tulikuwa |

| | |
|---|---|
| | tumejifunza kidogo lugha hii na sasa tulipofika Kenya, ilikuwa rahisi kidogo kuzungumza na kuwasiliana na Wakenya. |
| **Mtafitiwa X** | Ndiyo, mawasiliano ni mojawapo ya sababu kuu ya kuzungumza Kiswahili. |
| **Kijana IV** | Lugha ya Kiswahili ina manufaa mengi kama vile masomoni, mawasiliano na makabila mengine, biashara na mambo mengi... |

Chanzo: Data ya Nyanjani

Kutokana na kauli za watafitiwa kwenye jedwali 4.4, Washona wanatumia Kiswahili kwa sababu ya mawasiliano na utangamano kwa kuwa mawasiliano hayawezi kukamilika iwapo wahusika hawaelewi lugha inayotumika kwa mujibu wa lengo la pili la utafiti. Hii inamaanisha kuwa lugha ya Kiswahili imepewa majukumu mengi katika jamii wanamoishi Washona ikilinganishwa na Kikuyu na Kishona. Landweer (2000) anasema kwamba lugha ikitambuliwa na kupewa hadhi na jamii huwa inapewa majukumu mengi na kuifanya lugha hiyo kuimarika kwa sababu ya kupendwa na kutumika na watu wengi katika jamii.

Austin (1962) anasema kwamba lugha ni chombo cha kuwaunganisha wanajamii wanapotangamana. Wanajamiilugha wanapokutana katika maeneo mbalimbali ya kijamii kama vile sokoni, au sehemu yoyote huwa rahisi kwao kutangamana kwa vile wanatumia lugha wanayoielewa wote. Utangamano ni jambo la kawaida kwa wanajamiilugha mbalimbali wanapoishi katika jumuiya moja. Kwenye mahojiano yaliyofanyika tarehe 11/03/2023 katika kanisa la *Gospel of God*, watafitiwa walikiri kwamba walijifunza Kiswahili ili waweze kutangamana na wanajamiilugha wengine nchini Kenya bila kubaguliwa katika maeneo tofauti ya kijamii kama vile sokoni, kanisani, burudani na kadhalika. Pia, Washona wanazungumza Kiswahili ili wapate

kuelewana na wanajamiilugha wengine katika maeneo wanamoishi wanapofanya shughuli zao mbalimbali. Haya yanathibitika kwenye dondoo 1 lifuatalo:

**Dondoo 1**

> *"Tulijifunza lugha ya Kiswahili ili kurahisisha maingiliano yetu na makabila mengine ya Kenya. Kwa vile katika maisha ya kila siku lazima tuongee na watu, na lugha ya Kiswahili ilikuwa lugha nzuri kwetu."*
>
> *Chanzo: Data ya nyanjani.*

Katika mitaa wanamoishi Washona, Kiswahili hutumika kwa wingi na hivyo basi kulingana na usemi wa dondoo 1, ilikuwa lazima kwa Washona kujifunza na kuzungumza Kiswahili ili kurahisisha shughuli zao katika jamii kwa mujibu wa lengo la pili la utafiti huu. Kutokana na dondoo 1, wanajamiilugha wa Kishona walijifunza Kiswahili kwa sababu ya kuingiliana na makabila mengine kwenye maeneo wanamoishi. Watu kutoka jamii moja ambao wamejifunza lugha ya pili, hutambua na kuenzi sanaa, mila, dini, na historia ya watu wa jamiilugha ya pili. Lugha huwaleta watu pamoja hasa wakigundua kwamba wageni wamejifunza lugha yao na utamaduni wao. Wanajamiilugha wakigundua kwamba wageni wanazungumza lugha yao, wao huamua kuwaleta karibu nao na kuwakubali ili kurahisisha utangamano kati ya jamiilugha nyingine.

### 4.1.4 Sababu ya Ushirikiano

Utafiti uligundua kwamba jambo lingine linaloleta watu pamoja ambalo lilipelekea Washona kujifunza na kuzungumza Kiswahili ni kutaka kushirikiana na wanajamiilugha wengine kwa mambo mengi kama vile biashara, elimu na tamaduni mbalimbali zinazohusishwa na lugha ya pili. Utafiti wa KHRC na UNHCR (2019) unabainisha kwamba Washona walipofika Kenya kuanzia mwaka wa 1959, ilibidi

wajifunze Kiswahili ili waweze kushirikiana na Wakenya kama inavyobainika kupitia kwa maneno ya watafitiwa kwenye dondoo 2 lifuatalo:

**Dondoo 2**

> *"Tulipofika Kenya wakati huo hatukuwa tunajua lugha ya Kiswahili vizuri lakini tulijifunza haraka kushirikiana raisi. Kiswahili kilikuwa rahisi kujifunza kwa sababu safari yetu kutoka Zimbabwe tulipitia Tanzania kwenye tulijifunzia Kiswahili kidogo. Tulipata Wakenya wanazungumza Kiswahili pia na sisi tukaendelea. Lugha hii ilirahisisha ushirikiano hapa Kenya. Lugha ya Kiswahili ilituunganisha na Wakenya."*
>
> *Chanzo: Data ya Nyanjani.*

Maelezo ya watafitiwa yanabainisha kwamba Washona hawakuwa wanafahamu vyema Kiswahili walipofika Kenya. Ilibidi waendelee kujifunza kwa kuwa hakuna mwanadamu ataishi bila kushirikiana na wengine. Kulingana nao, Kiswahili ilifanya kazi ya kuleta ushirikiano na Wakenya kama inavyodhihirika kwenye dondoo la 2. Ushirikiano kupitia kwa lugha huleta umoja na mahusiano mema kati ya wanajamiilugha tofauti wanaoishi pamoja. Kulingana na lengo la pili la utafiti huu, Washona walikuwa na sababu mbalimbali za kujifunza na kutumia Kiswahili katika maeneo yao ya kijamii na mojawapo ya sababu hizi ni ushirikiano.

### 4.1.5 Sababu za Mahusiano

Washona walijifunza Kiswahili ili kuimarisha mahusiano baina yao na wanajamiilugha wengine nchini Kenya wanaozungumza lugha tofauti hasa katika nyanja za elimu, familia na hata biashara. Kimemia (2002) anasema kwamba lugha ni chombo cha kuunganisha watu kupitia kwa mahusiano. Hivyo basi, ikiwa watu wa jamii mbili tofauti au zaidi wanaishi katika eneo moja, mahusiano kati ya jamii hizo huwa ni muhimu. Kunaweza kutokea uhasama baina yao ikiwa wana mahusiano mabaya.

Kukiwa na mahusiano mema jamii hizo hupata kushirikiana katika kutekeleza shughuli nyingi za kuendeleza maisha yao kupitia kwa lugha.

Mahojiano kati ya watafitiwa wazee tarehe 11/03/2023 kwenye Kanisa la *Gospel of God* linalopatikana katika barabara ya *Valley Road*, jijini Nairobi yalithibitisha kwamba Washona walitaka sana kujifunza na kutumia Kiswahili ili waweze kuhusiana vyema na wenyeji wao. Haya yanathibitika kupitia maneno kwenye dondoo 3 lifuatalo.

**Dondoo 3**

> *"Ilibidi tuongee na Wakenya sababu lengo letu lilikuwa ni kueneza injili. Hivyo basi lugha ya Kiswahili ilikuwa nzuri kwa mahusiano yetu na Wakenya sababu ndiyo ilikuwa lugha ya taifa la Kenya. Tulijifunza kwa haraka sana ili tuweze kuhubiria Wakenya kwa maana katika dini, ushirikiano ni lazima"*

*Chanzo: Data ya nyanjani.*

Kupitia kwa maelezo kwenye dondoo 3, Kiswahili iliwawezesha Washona kuhusiana vyema na Wakenya kwa kuwa walikuwa wageni. Uhusiano huu uliwawezesha kuishi vyema na Wakenya kwa zaidi ya miaka hamsini huku wakifanya kazi za mikono na biashara ndogondogo. Mahusiano pia yalipelekea baadhi ya Washona kuoana na wanajamiilugha wengine wa Kenya ili kuimarisha uhusiano wao zaidi. Mahusiano yakiendelea kuimarika zaidi, uchumi nao unaendelea kuwa bora zaidi kupitia kwa biashara. Kwa mujibu wa mada ya utafiti na lengo la pili la utafiti huu, ndoa baina ya wanajamiilugha wa Kishona na wanajamiilugha wengine husaidia kuinua uthabiti wa Kishona na Kiswahili. Ndoa zinapofanyika baina ya jamiilugha mbili tofauti, huwa wana kila sababu ya kutumia lugha ambayo wote wanaelewa kwa pamoja na hivyo basi ilibidi wajifunze Kiswahili ili waweze kuhusiana vyema.

### 4.1.6 Sababu za Kiuchumi

Sababu nyingine ya Washona ya kutumia Kiswahili ni kufungua na kuimarisha nafasi za kujipatia riziki. Kulingana na King (2022), watu ambao ni wageni katika nchi nyingine hulazimika kujifunza na kutumia lugha ya wenyeji ili kurahisisha utafutaji wa riziki. Jambo hili hutokea wakati idadi ya wageni katika taifa husika ni ndogo mno kiasi kwamba wahamiaji hawa hawatambuliwi kisheria katika taifa kama jamii inayojisimamia. Hapa inabidi wageni wajifunze lugha za wenyeji ili kurahisisha shughuli zao kwa kuwa lugha ndiyo hufanikisha biashara na utafutaji wa riziki. Jedwali 4.5 lifuatalo linabainisha jinsi Washona wanavyotumia Kiswahili katika shughuli za kujitafutia riziki na kufanya biashara na wenyeji wao.

**Jedwali 4.5: Matumizi ya Kiswahili katika Kutafuta Riziki**

| Watafitiwa | Je, nyinyi mnafanya biashara katika maeneo mnayoishi? Lugha mnayotumia sana ni ipi? |
|---|---|
| 1. | Tunatumia lugha ya Kiswahili katika kazi zetu za mikono tunazozifanya. |
| 2. | Tukitumwa dukani tunaongea Kiswahili na mwenye duka tukienda kununua kitu. |
| 3. | Tunafanya kazi ya kusuka vikapu ambavyo tunauza kwa ajili ya hela. Huwa tunatumia Kiswahili tukiongea na wateja wetu. |
| 4. | Tumekuwa tukitumia Kiswahili katika kazi yetu ya useremala tunapotafuta wanunuzi kwa kuwa wateja wetu wengi ni Wakenya. |
| 5. | Tunatumia lugha ya Kiswahili kutafuta na kufanya kazi zetu za mikono ili tupate wateja ... |

Chanzo: Data ya nyanjani

Majibu yaliyotolewa na watafitiwa wa umri mbalimbali kama yalivyonakiliwa kwenye jedwali la 4.5 yanabainisha kwamba Kiswahili ni muhimu katika shughuli za biashara kwa kuwa bila kuelewana kupitia kwa lugha ni vigumu wahusika kusikilizana wanapofanya biashara zao na kujenga uchumi wa nchi yao. Hii inamaanisha kwamba

lugha ya Kiswahili ina jukumu kubwa kwa maisha ya Washona hasa wanapojitafutia riziki kulingana na lengo la pili la utafiti huu. Landweer (2000) anasema kwamba lugha yoyote kuwa thabiti hutegemea misingi imara na halali ya kiuchumi ya jamiilugha hiyo. Lugha ambayo haiwanufaishi wazungumzaji wake kiuchumi haithaminiwi na haitumiki sana katika jamii na matokeo yake ni kubadilika kwa urahisi na kukosa uthabiti wake wa kiisimujamii. Kwa kuwa lugha ya Kiswahili inahusishwa na biashara tangu zamani, inaendelea kupata umaarufu na kuwa thabiti kuliko lugha nyingine za kiasilia nchini Kenya.

### 4.1.7 Sababu za Utambulisho

Utafiti uligundua pia kwamba Washona wanatumia Kiswahili kwa sababu ya kujitambulisha na wenyeji wa jamiilugha za Kenya. Hili hutokea wakati ambapo kujihusisha na lugha ya jamii fulani huwa na faida nyingi ikilinganishwa na hasara zinazotokana na kujifunza lugha hiyo ya pili. King (2022) anasema kuwa kujifunza lugha ya pili na kutambuliwa kama mwenyeji wa lugha hiyo huwa na msisimko mkubwa kwa anayejifunza na kwa wenyeji wake.

Kwenye mahojiano yaliyofanyika tarehe 11/03/2023 katika Kaunti ya Kiambu kwenye mtaa wa Kinoo, wahojiwa walieleza kuwa wao hutumia Kiswahili ili kujitambulisha na Wakenya wengine ambao pia huzungumza Kiswahili. Kulingana na wahojiwa hao, kuzungumza Kiswahili kunawahusisha Washona na Wakenya badala ya kuonekana kama wahamiaji. Washona wameishi katika taifa la Kenya kwa takribani miongo sita bila stakabadhi muhimu za utambulisho. Jambo hili liliwafanya kuonekana kama

wasotaifa anavyosema Mulinya (2020). Jedwali 4.6 linaonyesha maoni ya watafitiwa ambao pia ni wachungaji wa kanisa la Washona la *Gospel of God* :

**Jedwali 4.6: Matumizi ya Kiswahili kwa Sababu ya Utambulisho**

| Watafitiwa | Je, Kuna sababu zinawafanya kuzungumza Kiswahili? |
|---|---|
| **1.** | Ili kuepuka changamoto hasa zile zinazohusiana na utambulisho hapa Kenya, ilibidi tujifunze Kiswahili ili turahisishe utambulisho na Wakenya... |
| **2.** | Tulikuwa tunatumia Kiswahili ili kutambulikana kama Wakenya. Kwanza siku hizi ndiyo imekuwa vizuri vile tulitambuliwa kama Wakenya mwaka wa 2020. Tunaongea Kiswahili sasa tukiwa Wakenya... |
| **3.** | zamani tulikuwa tunatumia Kiswahili kwa sababu ya usalama wetu. Hii ilikuwa inafanyika kwa sababu hatukuwa tumepewa vitambulisho, tulikuwa tunaongea Kiswahili ili polisi wasijue ati sisi si wakenya. Lakini siku hizi tunafurahia sababu tulitambuliwa kama Wakenya. |

*Chanzo: Data ya nyanjani.*

Inadhihirika kutoka jedwali 4.6 kupitia maneno ya watafitiwa kwamba walitumia Kiswahili ili kujitambulisha kama Wakenya. Kwa mujibu wa King (2022), wakati mwingine wahamiaji hukosa kupatiwa stakabadhi muhimu zinazowatambulisha kama wananchi halali wa taifa fulani. King anasema pia kuwa watu wanaweza kuishi katika taifa fulani kihalali bila wao kutambuliwa kama wananchi wa taifa hilo. Watu kama hao hulazimika kujifunza na kutumia lugha za wenyeji wa taifa hilo katika mazungumzo yao ili wasitengwe na wenyeji wao na warahisishe mawasiliano. Vivyo hivyo, kwa mujibu wa lengo la pili la kubainisha sababu za kujifunza na kutumia Kiswahili nchini Kenya, ilibidi Washona wajifunze Kiswahili ili waweze kutambuliwa na majirani wao na kuepuka changamoto za kushikwa na kufungiwa na polisi kwa kutokuwa raia wa Kenya.

Washona walianza kuishi nchini Kenya kama wamishenari wakiwa wachache lakini walivyozidi kuishi nchini ndivyo idadi yao ilivyozidi kuongezeka na hadi sasa kufikia takribani watu zaidi ya 2500 anavyofafanua Wasike, (2021). Kwa sasa Washona wanatambuliwa kama mojawapo ya makabila ya Kenya baada ya kuidhinishwa rasmi na aliyekuwa Rais wa nne wa Kenya, Uhuru Kenyatta, tarehe 12.12.2020.

### 4.1.8 Sababu za Kidini

Dini na shughuli za kueneza injili ni jambo lingine lililowahimiza Washona kujifunza Kiswahili. Muchena na Jakaza (2022), Wagalla (2019), Odenyo na Ntinyari (2021), na UNHCR (2019) wanasema kwamba lengo kuu lililowaleta Washona hadi nchini Kenya ni kuhubiri injili kupitia kanisa la *Gospel of God*. Ilibidi Washona wajifunze Kiswahili na lugha nyingine za Kenya ili waweze kufanikisha lengo lao la kueneza injili. Hivyo basi lugha ya Kiswahili ikapata nafasi ya kwanza katika jamiilugha ya Washona kwa kuwa ilikuwa inazungumzwa na watu wengi nchini Kenya. Kupitia mbinu ya uchunzaji, mtafiti aligundua kwamba katika kanisa la *Gospel of God* lililoko kwenye barabara ya *Valley Road* jijini Nairobi, Kiswahili hutumika wakati wa ibada na shughuli nyinginezo za kanisani kama vile maombi na sherehe mbalimbali. Wakati mwingine, lugha ya Kishona inatumika huku ikitafsiriwa kwa Kiswahili kwa kuwa waumini wamechanganyika kutoka jamiilugha mbalimbali. Mahojiano kati ya mtafiti na watafitiwa ambao ni wazee wa kanisa la *Gospel of God*, yalibainisha kwamba lugha zinazotumika sana kanisani mwao ni Kiswahili na Kishona. Watafitiwa walipoulizwa iwapo wanatumia Kiswahili kanisani, walijibu kupitia dondoo 4 kwa kusema:

**Dondoo 4**

> *"Mwanzoni tulikuwa tunatumia lugha ya Kishona pekee kanisani, tulikuja tukagundua kwamba kuna waumini walijiunga na kanisa letu ambao si Washona,ndio tukaanza kutumia lugha ya Kiswahili pia katika ibada kupitia kwa ukalimani."*
>
> *Chanzo: Data ya Nyanjani*

Maneno ya wasailiwa kwenye dondoo 4 yanadhihirisha wazi kwamba lugha ya Kiswahili imeendelea kupanuka na kutumika katika maeneo mengi yakiwemo maeneo ya kanisani kwa ajili ya kueneza injili nchini Kenya. Katika kanisa la *Gospel of God,* si jambo geni kuwapata vijana na watoto na hata wazee wakizungumza Kiswahili kwa wingi kuliko lugha yao Kishona. Kupitia kwa lengo la pili la utafiti huu la kubainisha sababu mbalimbali za Washona za kutumia Kiswahili, ni dhahiri kwamba sababu nyingine ya kutumia Kiswahili ni kuhubiri injili kwenye dhehebu lao la *Gospel of God* lililoko *Valley Road* jijini Nairobi.

### 4.1.9 Sababu za Kiusalama

Washona pia walijifunza na kutumia Kiswahili kwa sababu ya usalama wao. Miaka ya sitini hadi miaka ya elfu mbili, ilikuwa ni kipindi kigumu kwa jamiilugha ya Washona kwa kuwa baada ya taifa la Kenya kupata uhuru, anavyoelezea Odenyo na Ntinyari (2021), Washona walijipata katika njia panda; hawakuwa Wakenya na pia hawakuwa na stakabadhi za kuwawezesha kusafiri kurudi kwao nchini Zimbabwe. Watafitiwa wanaeleza wazi kwamba huu ulikuwa wakati mgumu sana kiusalama kwa Washona nchini Kenya. Ripoti za KHRC na UNHCR (2019) zinadhihirisha machungu waliyokuwa wakipitia kwa mfano kushikwa na polisi na kufunguliwa mashtaka ya kuwa nchini bila vibali, kukosa huduma muhimu kama vile za matibabu na pia kukosa nafasi za elimu katika shule za Kenya. Jambo lililowaletea afueni kubwa ni kujua

kuzungumza lugha maarufu ya Kiswahili na Kikuyu wanavyoelezea watafitiwa kupitia dondoo 5 baada ya kuulizwa iwapo wana sababu nyingine ya kuzungumza Kiswahili:

**Dondoo 5**

> *"Ilikuwa ni poa kwetu Washona kuzungumza Kiswahili na Kikuyu kwa sababu askari hawangegundua haraka kama sisi si Wakenya. Lugha hizi za Kenya zilitufícha sana. Lakini kuna wakati mwingine wanajamii walitusema na tukajipata tumefungwa..."*
>
> *Chanzo: Data ya nyanjani*

Kutokana na maelezo ya watafitiwa, ni dhahiri kwamba lugha za Kiswahili na Kikuyu ziliwakinga Washona na kuwaepusha kufungwa gerezani kwa kukosa stakabadhi muhimu za kuwatambulisha kabla ya kupewa uraia nchini Kenya. Kwa mujibu wa lengo la pili la kubainisha sababu mbalimbali za kutumia lugha ya Kiswahili katika maeneo mbalimbali ya kijamii, hii ilikuwa sababu ya kuendelea kuzungumza Kiswahili katika maeneo mengi ya kijamii na wakabaki kutumia lugha yao ya Kishona kwenye maeneo tu ya nyumbani kwa usalama wao. Baadhi ya Washona pia wanazungumza Kikuyu katika maeneo mbalimbali ya kijamii kwa sababu ambazo zimejadiliwa kwenye sehemu ya 4.2 hapa chini.

## 4.2 Sababu za Washona za Kutumia Kikuyu Nchini Kenya

Kikuyu ni mojawapo ya lugha asilia za Kenya iliyo na wazungumzaji wengi ambao ni zaidi ya watu milioni 8.14 kulingana na ripoti ya Shirika la Kitaifa la Takwimu nchini Kenya (Kenya National Bureau of Statistics, KNBS 2019). Kibui (2014) na Kamau (2015) wanasema kwamba Kikuyu huzungumzwa na idadi kubwa ya Wakenya katika eneo la kati nchini Kenya kwenye kaunti nne ambazo ni Nyandarua, Nyeri, Murang'a na Kiambu. Takwimu hii haijajumuisha wazungumzaji wengine ambao huzungumza Kikuyu kama lugha yao ya pili. Miji mikuu kama vile Nairobi na miji jirani kama vile

Kiambu, ina idadi kubwa ya wazungumzaji wa Kikuyu kama lugha yao ya pili na ya tatu, hali ambayo imeipatia lugha ya Kikuyu matumizi mapana nchini Kenya. Kuna pia wageni ambao hawakuwa Wakenya kwa mfano Washona lakini wamejifunza Kikuyu kwa sababu mbalimbali kama vile ufadhili, umaarufu wa lugha hii, kushiriki kwenye sherehe mbalimbali za kijamii na sababu ya biashara. Sababu ya ufadhili inashughulikiwa kwanza.

### 4.2.1 Sababu ya Ufadhili

Kulingana na ripoti ya KHRC na UNHCR (2019), Washona wa kwanza waliofika Kenya kuanzia mwaka wa 1959 hadi 1961 walikuwa wamishenari kumi na sita wakiongozwa na mzee Arthur Dirorimwe. Walipofika Kenya, walijigawa kwa makundi mawili ambapo kundi moja lilienda sehemu za Ngong, Kaunti ya Kajiado ambapo walikaribishwa na Wakikuyu watatu Joshua Kiarie, Timothy Muiruri na Gerald Njuguna. Kundi la pili lilienda maeneo ya Juja ambapo lilikaribishwa na Peter Muigai Kenyatta, ambaye alikuwa mwana wa aliyekuwa Rais wa Kwanza wa Kenya, Mzee Jomo Kenyatta kupitia kwa urafiki wake na mzee wa Kishona Arthur Dirorimwe.

Ilidhihirika kwamba, watu wa kwanza waliotangamana na Washona nchini Kenya walikuwa Wakikuyu na hivyo basi ilikuwa rahisi kwa Washona kuwa na mielekeo chanya kwa Kikuyu. Kupitia kwa ukarimu wa jamiilugha ya Wakikuyu kwa Washona, ilikuwa rahisi kwao kujifunza Kikuyu ili kufanikisha mawasiliano baina yao katika mazingira ya ugenini. Mahojiano ya mtafiti na watafitiwa ambao ni waumini katika Kanisa ya *Gospel of God* yalithibitisha kwamba utangamano wa kwanza ulikuwa baina

yao na Wakikuyu. Waliulizwa ni vipi walijifunza Kikuyu na majibu yao yanaonyeshwa kwenye dondoo la 6 lifuatalo.

**Dondoo 6**

> *"Baba zetu walipofika nchini Kenya, walikaribishwa na Wakikuyu katika sehemu za Ngong na Juja kabla ya kuhamia kwenye mitaa ya Kinoo na Kiambaa. Kando na kuzungumza lugha ya Kiswahili, baba zetu pia walijifunza lugha ya Kikuyu."*
>
> *Chanzo: Data ya nyanjani*

Dondoo 6 linathibitisha kwamba Washona wa kwanza nchini Kenya walikaribishwa na kufadhiliwa na Wakikuyu. Hii ikakuwa sababu kuu yao kujifuza  Kikuyu ili waweze kuwasiliana kwa urahisi. Wanajamiilugha wa Kikuyu waliwasaidia Washona kupata makazi ambapo baadhi yao wanaishi hadi sasa. Kulingana na mahojiano yaliyofanyika tarehe 11/03/2023 katika mtaa wa Kinoo katika Kaunti ya Kiambu, wahojiwa wazee walieleza kuwa Washona hutumia Kikuyu kwa sababu jamiilugha ya Wakikuyu iliwasaidia kupata makazi katika Kaunti ya Kiambu. Washona wameishi katika Kaunti za Kiambu na Nairobi tangu walipofika Kenya. Licha ya kuwa wanasafiri na kufanya umishenari, biashara na shughuli nyingine katika maeneo mengine nchini, makazi yao ya kwanza ni katika Kaunti ya Kiambu kwenye mitaa ya Kinoo, Kikuyu, Kiambaa, Gitaru na Githurai. Washona walichukulia Wakikuyu kama ndugu na rafiki zao kwa sababu ya msaada mkubwa wa ufadhili waliopata kutoka kwao na kustawisha hali zao za maisha na hivyo basi wakajifunza Kikuyu. Dondoo la 7 lifuatalo linabainisha maneno ya Watafitiwa baada ya kusailiwa walivyojifunza Kikuyu:

**Dondoo 7**

> *"Mimi na wenzangu tumeishi sehemu hii ya Kinoo kwa zaidi ya miaka ishirini. Lugha inayozungumzwa hapa sana ni lugha ya Kikuyu kwa*

> *sababu hapa kuna Wakikuyu wengi sana na hivyo ilikuwa rahisi kwetu kujifunza lugha hii ili kufanya shughuli zetu kwa urahisi. Pia, ndugu zetu Wakikuyu ndio waliwakaribisha Washona wa kwanza waliofika hapa nchini kwa shughuli za kueneza injili."*
>
> *Chanzo: Data ya Nyanjani*

Kwenye kaunti ya Kiambu katika maeneo ambapo Washona huishi, wanajamiilugha wengi ni Wakikuyu kulingana na Kamau (2015). Kutokana na dondoo la 7, lugha ya Kikuyu ina idadi kubwa ya Wazungumzaji, hali ambayo inarahisisha ujifunzaji wa lugha hiyo. Hii inamaanisha kwamba lugha ya Kishona ina nafasi ndogo ya kukua kwenye mazingira haya yaliyo na idadi kubwa ya wanajamiilugha wa Wakikuyu na pia wazungumzaji wa Kiswahili. Ilibainika kwamba Wakikuyu ndio waliowapatia Washona makazi kwenye mitaa mitano wanamoishi nchini Kenya ndio maana baadhi yao walijifunza na kuzungumza Kikuyu. Landweer (2000) anasema kwamba iwapo idadi ya wanajamiilugha wanaozungumza lugha fulani ni wengi kwenye maeneo fulani, kuna uwezekano wa wanajamiilugha wachache kujifunza lugha ya wanajamiilugha walio na idadi kubwa. Kwa mujibu wa lengo la pili la utafiti huu linalolenga kubainisha sababu za Washona za kutumia Kiswahili na Kikuyu kwenye maeneo yao ya kijamii, baadhi ya Washona hawakuwa na budi ila kujifunza Kikuyu kwa sababu Wakikuyu ndio waliowahifadhi na pia kiidadi, Wakikuyu walikuwa wengi kwenye maeneo ambayo Washona wanaishi.

### 4.2.2 Sababu ya Umaarufu wa Kikuyu

Baadhi ya Washona huzungumza Kikuyu kwa kuwa wazungumzaji wengi katika Kaunti ya Kiambu hutumia Kikuyu licha ya kuwa Kaunti hiyo ina wanajamiilugha mbalimbali kulingana na Kamau (2015). Kwa mujibu wa mahojiano yaliyofanyika tarehe 11/03/2023 katika Kaunti ya Kiambu kwenye mtaa wa Kinoo, wasailiwa vijana

walieleza kuwa Washona huzungumza Kikuyu kwa sababu ni lugha maarufu katika Kaunti ya Kiambu. King (2022) anadokeza kuwa sababu kuu watu kujifunza lugha ya wenyeji ni kwamba waweze kuimarisha mahusiano baina yao na wenyeji hasa ikiwa lugha hiyo ni lingua franka katika eneo hilo. Kulingana na Shirika KNBS (2019), na Kamau (2015), Kaunti ya Kiambu ni moja kati ya maeneo ambayo ni nyumbani mwa jamiilugha ya Wakikuyu. Hata hivyo, wanajamiilugha wengine kama vile Wakamba, Wameru, Wakisii na Wajaluo ni miongoni mwa jamiilugha zinaoishi katika kaunti hiyo lakini asilimia ya watu kutoka jamiilugha hizo kwa pamoja ni ndogo mno ikilinganishwa na jamiilugha ya Wakikuyu. Hivyo basi, kwa sababu ya idadi kubwa ya jamiilugha ya Kikuyu kwenye eneo hili, ni kawaida kwa lugha yao kuwa maarufu katika eneo hili. Wahojiwa walieleza kuwa ili kuhusiana vyema na wanajamii wengine, Washona walikuwa na kila sababu ya kujifunza na kutumia Kikuyu kupitia kwa maneno yao kwenye dondoo la 8 kuhusu jinsi walivyojifuza Kikuyu.

**Dondoo 8:**

> *"Hata saii ukitoka hapa kwa barabara na umpate mtu yeyote, jaribu kumzungumzia Kikuyu, atakujibu tu kwa Kikuyu kwa sababu watu wengi hapa ni Wakikuyu na wale ambao si Wakikuyu kama sisi Washona, wamejifunza lugha hii."*
>
> *Chanzo: Data ya Nyanjani*

Maneno kwenye dondoo la 8 yanathibitisha kwamba kwenye maeneo ambapo Washona huishi, idadi kubwa ya wazungumzaji Wakikuyu inawazunguka. Hali hii imewafanya baadhi yao kujifunza na kuzungumza Kikuyu, jambo ambalo linapunguza uthabiti wa kiisimujamii wa Kishona. Landweer (2000) anasema kwamba lugha iliyo na idadi kubwa ya wazungumzaji na pia iliyo na hadhi ya juu katika jamii, huenea kwa haraka

kwa kuwa imepewa majukumu mengi katika jamii husika. Maoni ya Ngure (2012) ni kwamba popote ambapo jamiilugha mbili zinatagusana, matokeo huwa ni uhamaji wa lugha iliyo na idadi ya chini ya wazungumzaji. Uhamaji huu huanza polepole kupitia kwa kupunguka kwa uthabiti wa kiisimujamii kwa lugha husika na hatimaye lugha humezwa na ile lugha iliyo na idadi kubwa ya wazungumzaji.

### 4.2.3 Sababu ya Mawasiliano

Sababu nyingine ya Washona kutumia Kikuyu ni kufanikisha mawasiliano. Kulingana na mahojiano yaliyofanyika kwenye kanisa la *Gospel of God, Valley Road* jijini Nairobi tarehe 11/03/2023, wazee walikuwa na maoni kuwa walikuwa wanatumia Kikuyu kwa sababu wanajamiilugha ya Kikuyu ni majirani wao na mawasiliano ni lazima kati yao. Majibu ya jinsi walivyojifunza Kikuyu yanabainishwa kwenye dondoo la 9 lifuatalo:

**Dondoo 9**

> *"...Wale Washona wanasungumsa Kukuyu, husungumsa kwa sababu kuwasiliana. Wakikuyu ni majirani zetu na mawasiliano ni lazima kati yetu. Tunaposungumsa lugha hii ya Kikuyu, watu wengine hufikiria kwamba sisi pia ni Wakukuyu*."
>
> *Chanzo: Data ya Nyanjani*

Katika mahojiano na watafitiwa, ilibainika kuwa baadhi ya Washona hawana budi ila kujifunza Kikuyu ili kurahisisha mawasiliano kati yao na jamiilugha ya Wakikuyu. Mitaa ya Kiambaa na Kinoo ambayo ni makazi ya asilimia kubwa ya Washona, ipo katika Kaunti ya Kiambu ambapo ni nyumbani kwa wanajamiilugha Wakikuyu. Watafitiwa pia walidokeza kuwa wakati mwingine wanajamiilugha wengine huwafikiria na kuwachukulia Washona kuwa Wakikuyu kwa sababu baadhi yao wanazungumza Kikuyu kwa ufasaha. Kulingana na Landweer (2000), kuanza

kupunguka kwa matumizi ya lugha ya mama katika maeneo ya kijamii huwa ndio chanzo cha kupunguka kwa uthabiti wa Kiisimujamii katika lugha husika. Hii inamaanisha kwamba Washona wanatumia Kikuyu kwa sababu kuu ya mawasiliano kulingana na lengo la pili la utafiti huu kuliko lugha yao asilia katika maeneo ya nyumbani. Mawasiliano kupitia kwa Kikuyu katika maeneo yao ya nyumbani yanawasidia pia kushiriki kwenye sherehe mbalimbali za kitamaduni za Wakikuyu.

### 4.2.4 Sababu ya Kushiriki kwenye Sherehe za Kitamaduni

Jambo lingine linalowafanya Washona kutumia Kikuyu ni kwamba waweze kushiriki katika sherehe mbalimbali za kijamii zinazojumuisha jamiilugha hizi mbili. Sherehe kama vile ndoa au harusi, mazishi miongoni mwa zingine, huwalazimisha wanajamii kuungana pamoja ili waweze kuzifanya kwa urahisi. wasailiwa walieleza kuwa shughuli kama vile harusi au mazishi, huwafanya wanajamiilugha hizi kutumia lugha ya waliowengi katika jamii. Utafiti ulisaili iwapo kuna sherehe za Wakikuyu ambazo wanahudhuria. Maneno yao yanathibitisha jambo hilo kupitia dondoo la 10.

**Dondoo 10**

> *"... Sherehe kama vile za harusi au mazishi tunahudhuria. Wakikuyu hutumia lugha yao wakati wa sherehe kama hizi. Inabidi tujue lugha yao ili ikuwe rahisi kwetu kushiriki. Lakini si Washona wote wanajua lugha ya Kikuyu."*
>
> *Chanzo: Data ya Nyanjani.*

Kwenye dondoo la 10, inadhihirika kwamba wanajamiilugha huwa na sherehe mbalimbali ambazo ni sehemu ya utamaduni wao. Landweer (2000) anasema kwamba lugha hutumika kwenye maeneo mbalimbali ya kijamii ili kupata uthabiti wa kiisimujamii. Landweer anaendelea kusema kwamba lugha hutumiwa katika maeneo ya

nyumbani ambapo watu wa familia moja hufanya sherehe za kitamaduni kama vile sherehe za ndoa, mazishi, kuzaliwa na kupewa jina kwa mtoto, sherehe za jandoni, vita, maabadini, sherehe mbalimbali za ukulima na kadhalika. Kamau 2015, KHRC na UNHCR 2019 wanasema kuwa Kikuyu hutumika sana katika mitaa ya Kikuyu, Kinoo, Kiambaa, Gitaru na Githurai, ambayo ni makazi ya idadi kubwa ya wanajamiilugha ya Wakikuyu. Washona wamejifunza na kutumia Kikuyu ili waweze kushiriki katika sherehe hizi za kitamaduni ambazo hufanyika katika jamii. Hii inamaanisha kwamba ni muhimu kwa wanajamiilugha Washona kujifunza Kikuyu kwa kuwa wao sasa ni sehemu ya jamii wanamoishi. Kulingana na lengo la pili, ni dhahiri kwamba baadhi ya Washona wanajua lugha ya Kikuyu na wanaitumia katika shughuli zao mbalimbali.

### 4.2.5 Sababu ya Biashara

Kwa mujibu wa mahojiano yaliyofanyika tarehe 19/03/2023 katika mtaa wa Gitaru katika Kaunti ya Kiambu, wahojiwa vijana walidokeza kuwa baadhi ya Washona hutumia Kikuyu katika shughuli za biashara. Hii ni kwa sababu kama tulivyotaja hapo awali, lugha ya Kikuyu ndio iliyo na idadi kubwa ya wazungumzaji katika Kaunti ya Kiambu, (Kamau, 2015). Wasailiwa vijana waliulizwa wanavyochukulia Kiswahili na Kikuyu na wakatoa majibu yao kupitia kwa dondoo 11:

**Dondoo 11**

> *“Katika maeneo haya tunaishi, biashara nyingi ni za Wakikuyu ambao hutuzungumzia kwa lugha yao ya Kikuyu tunapoenda kununua. Hivyo hata sisi imebidi tujifunze lugha ya kikuyu ili kufanikisha shughuli za biashara.”*

*Chanzo: Data ya nyanjani*

Kulingana na maneno ya wahojiwa, wakati mwingine, wafanyabiashara wa aina zote katika Kaunti ya Kiambu huchukuliwa kuwa wanajamiilugha wa Kikuyu na hivyo basi mazungumzo mengi huanzishwa kwa lugha ya Kikuyu. Isitoshe, Washona wana makazi yao katika mitaa ya Kinoo, Kiambaa, Kikuyu, Gitaru na Githurai kwenye kaunti ya Kiambu ambapo panajulikana kuwa na idadi kubwa ya wanajamiilugha wa Kikuyu na hivyo basi Washona huchukuliwa kuwa wenyeji wa Kaunti hiyo. Ripoti ya KHRC na UNHCR (2019) inathibitisha kwamba kwa kuwa Washona hawakupata fursa nzuri ya kusoma kwa sababu ya kukosa vibali muhimu nchini Kenya, wao hujihusisha na biashara ndogondogo na kazi za mikono pia. Wanapofanya biashara zao, baadhi yao wamejifunza Kikuyu kwa kuwa mitaa wanamoishi ina idadi kubwa ya wanajamiilugha ya Kikuyu.

Watafitiwa walidokeza kuwa Washona wamefungua maduka ya rejareja ambayo wanatumia kuendesha biashara mbalimbali katika mtaa wa Kinoo na maeneo mengine katika Kaunti ya Kiambu. Dondoo la 12, linadhihirisha maneno ya watafitiwa kuhusu shughuli za biashara.

**Dondoo la 12**

> *"...tulijishughulisha na biashara ndogondogo kama vile vioski na biashara za kuuza mboga na matunda. Wateja wetu wengi ni wakikuyu sababu sehemu hii wako wengi. Kupitia shughuli za biashara, tumejifunza lugha ya Kikuyu ili kuzirahisisha."*
>
> *Chanzo: Data ya nyanjani*

Kutokana na maneno ya watafitiwa, baadhi ya Washona hufanya biashara ndogondogo mitaani wanapoishi. Wateja wao wengi huwa ni Wanajamiilugha ya Wakikuyu. Ripoti za KHRC (2019) na UNHCR (2019) zinasema kuwa Washona hujishughulisha na

uuzaji wa bidhaa kama vile matunda, mboga na kazi nyingine za mikono kama vile useremala kwa kuwa hawakuwa na stakabadhi muhimu za kuwasaidia kufanya biashara kubwa au kutafuta ajira. Vilevile, mbali na kuwa wauzaji wao pia ni wanunuzi wa bidhaa katika maduka ya wanajamii wengine hasa jamii ya Wakikuyu iliyo na asilimia kubwa ya wafanyabiashara katika Kaunti ya Kiambu. Licha ya kuwa lugha nyingine kama Kiswahili hutumika katika maeneo ya kibiashara, lugha ya Kikuyu ina wazungumzaji wengi pia ikilinganishwa na lugha nyingine za kiasili katika kaunti ya Kiambu. Hivyo basi, Washona hawana budi ila kujifunza na kuzungumza Kikuyu ili kuimarisha shughuli za kibiashara baina yao na Wakikuyu. Uchunzaji ulibainisha kwamba katika karakana moja mtaani Kinoo inayomilikiwa na Mshona, vijana na wazee wanaofanya kazi humo mara nyingine huchanganya Kikuyu na Kiswahili wanapoongea na wateja wao ambao pia wengi wao ni Wakikuyu.

### 4.3 Sababu za Washona Kuzungumza Kishona Nchini Kenya

Utafiti ulibainisha kwamba bado Washona wanazungumza lugha yao ya Kishona licha ya shinikizo kutoka kwa lugha maarufu za Kiswahili na Kikuyu. O'Riagain (1994) anasema kwamba kila jamii huwa na mikakati ya kurithisha vizazi vyao utamaduni wao ikiwemo lugha yao asilia. Lugha asilia huwa ni kipengele cha kwanza muhimu ambacho wazazi hurithisha wana wao. Washona hasa wenye umri mkubwa (miaka 36+) wanazungumza lugha yao ya kishona kwa sababu mbalimbali kama vile: kudumisha lugha yao, kueneza injili kupitia kwa kanisa la Gospel of God, ukumbusho wa asili yao na pia wanatumia Kishona kama ugwe wa kuwaunganisha. Sababu ya kudumisha utamaduni wao imeshughulikiwa kwanza

### 4.3.1 Kudumisha Utamaduni Wao

Kulingana na Mhlanga (2018), Kishona ni lugha ambayo asili yake ni nchi ya Zimbabwe na inazungumzwa na jamii ya Washona katika taifa hilo lililo katika sehemu za Afrika Kusini. King'ei (2010) anaelezea kuwa lugha ni zao la jamii na kuwa ni kipengele muhimu sana cha utamaduni wa jamii inayohusika. Iwapo jamii inanuia kudumisha utamaduni wake basi haina budi kuendeleza matumizi ya lugha yake kwa kuwa lugha na utamaduni haviwezi kuachana. Kulingana na mahojiano yaliyofanyika tarehe 11/03/2023 katika mtaa wa Kinoo Kaunti ya Kiambu, ilibainika kuwa mojawapo ya sababu ambazo huwafanya Washona kuzungumza lugha yao ya Kishona ni kudumisha utamaduni wao. Wasailiwa waliulizwa sababu ambazo zinawafanya bado wazungumze lugha yao. Majibu yao yanadhihirika kwenye dondoo 13 lifuatalo:

**Dondoo 13**

> *"...Sisi wazee tunasungumsa Kishona sababu ni lugha yetu. Na ni utamaduni wetu. Utamaduni wetu unaenda pamoja na lugha yetu kwa hivyo tunajaribu kila njia ili kuendeleza utamaduni huu. Watoto wetu wanaweza kujua utamaduni wetu kupitia kwa lugha yetu. Kwa mfano jinsi tunavyowapatia watoto wetu majina ya ukoo."*
>
> *Chanzo: Data ya Nyanjani*

Maneno ya wahojiwa wazee kwenye dondoo la 13 yanathibitisha kwamba lugha yao haiwezi kutenganishwa na utamaduni wao. Kwa hivyo, wanazungumza lugha yao ya kwanza kwa kuwa ni lugha ya mama na pia ni kudumisha utamaduni wao. Data ya nyanjani inabainisha kwamba Washona huwapa watoto wao majina ambayo yanaashiria utamaduni wa Kishona. Kwa mfano, watafitiwa walikiri kwamba mtoto wa kiume hupewa jina la jamaa wa kiume kama vile jina la babu yake aliyeaga dunia ili kuhifadhi

jina hilo la ukoo katika jamii. Mtoto wa kike pia hupewa jina la jamaa ya babake wa kike kama vile nyanya yake aliyefariki dunia ili kulihifadhi jina hilo. Idadi ya Washona ni ndogo mno ikilinganishwa na idadi ya wanajamiilugha wengine wanaowazunguka nchini Kenya. Hii inamaanisha kwamba Washona wametia juhudi za kuendeleza lugha yao licha ya shinikizo na changamoto kutoka kwa lugha maarufu nchini Kenya. Landweer (2000) anasema kwamba jamiilugha iliyo na idadi ya chini ya wazungumzaji inaweza kuendeleza lugha yao iwapo wameweka mikakati bora ya kutunza lugha yao. Hii ina maana kwamba Washona wameweka mikakati iliyo bora ya kudumisha lugha yao kwa muda mrefu nchini Kenya. Licha ya kuwa na idadi ndogo nchini Kenya, Washona walinuia kuendeleza utamaduni wao na kufanya lugha yao kuwa thabiti kwa kuwa inavyodhihirika kwenye dondoo la 14, lugha ya Kishona ndiyo kitu cha thamana walichobaki nacho baada ya kupitia mateso ya kutokuwa na uraia nchini Kenya. Watafitiwa waliulizwa swali la kwa nini wameendelea kuongea Kishona licha ya shinikizo kutoka kwa lugha maarufu, walijibu kama ifuatavyo kwenye dondoo la 14.

**Dondoo 14**

> ***"**Tumejaribu kudumisha lugha yetu kwa miaka isitini sasa hata kama kulikuwako na changamoto tulipata kama vile za utambulisho ambazo zingetufanya kusahau lugha yetu. Lakini lugha ya Kishona ndio kitu tu tulibaki nayo ya muhimu tulipoishi bila stakabadhi za uraia nchini Kenya."*
>
> *Chanzo: Data ya Nyanjani*

Maneno ya watafiti kwenye dondoo la 14 kwamba hata baada ya Washona kupitia changamoto chungu nzima, hawakusahau lugha ya mama kwa kuwa waliithamini sana. Wamejaribu kuwafunza wanawe lugha hii licha ya shinikizo kutoka lugha zilizo na nguvu za kidemografia na umaarufu kwenye mitaa wanamoishi. Washona walikiri

kwamba hii ilikuwa na bado ni sababu kuu ya kuendelea kuzungumza lugha yao licha ya changamoto kutoka kwa lugha maarufu zinazowazunguka. Jambo lingine ambalo linawafanya Washona kuzungumza lugha yao ni shughuli za ibada kwenye kanisa lao la *Gospel of God*.

### 4.3.2 Dini

Kulingana na mahojiano yaliyofanyika tarehe 21/01/2023 katika kanisa la *Gospel of God* lililoko *Valley Road* jijini Nairobi, watafitiwa walisema kuwa sababu nyingine ya Washona kuzungumza Kishona ni dini. Wasike (2021) anaeleza kuwa Washona wa kwanza kufika Kenya walifika kuanzia mwaka wa 1959 kama Wamishenari na waanzilishi wa kanisa la *Gospel of God* nchini Kenya. Utafiti huu ulibainisha kwamba, kanisa la *Gospel of God*, ni kitovu cha matumizi ya lugha yao ya Kishona kwa kuwa wanapokuja kwa ibada, hutumia Kishona, huimba nyimbo za Kishona na pia husoma Biblia iliyoandikwa kwa Kishona. Hivyo basi, ili kusoma na kuelewa maandishi ya Biblia, watoto Washona wanalazimika kujifunza na kuhifadhi lugha yao kupitia kwa dini yao. Watafitiwa vijana walithibitisha kupitia kwa dondoo la 15 lifuatalo walipoulizwa jinsi walivyojifunza lugha yao ya Kishona:

**Dondoo 15**

> *"Ingawa sanasana tunaongea lugha za Kiswahili na Kiingereza, tumejifunza lugha yetu ya Kishona kwa sababu kanisani ndiyo lugha inayotumika sana na pia Biblia tunayosoma kanisani imeandikwa kwa Kishona"*
>
> *Chanzo: Data ya nyanjani.*

Maneno ya watafitiwa kwenye dondoo 15 yanathibitisha kwamba watoto na vijana hupata fursa ya kujifunza na kutumia Kishona wakiwa kanisani. Katika maeneo ya

kanisani, mtafiti alithibitisha maneno ya wahojiwa kwa kuwa ilibainika kwamba lugha ya Kishona ilikuwa inatumika kwenye ibada huku ikitafsiriwa kwa Kiswahili kwa sababu ya waumini ambao si Washona.

### 4.3.3 Ugwe wa Kuwaunganisha

Washona pia wanatumia Kishona kama ugwe wa kuwaleta pamoja na kuimarisha mahusiano baina yao. Kulingana na mahojiano yaliyofanyika tarehe 21/01/2023 katika mtaa wa Kiambaa katika Kaunti ya Kiambu, wahojiwa wazee walieleza kuwa wanatumia Kishona kuwasiliana na wanajamiilugha wenzao, jambo ambalo huchangia kuwaleta pamoja. Maneno yao yanathibitishwa na usemi katika dondoo 16 lifuatalo lililotokana na swali la kwa nini bado watafitiwa wanazungumza lugha yao ya Kishona:

**Dondoo 16**

> *"Tunazungumza Kishona ili tuwasiliane vyema na Washona wengine na pia mawasiliano haya kwa lugha yetu hutuweka pamoja."*
>
> *Chanzo: Data ya Nyanjani*

Wanajamiilugha wanapokutana katika maeneo tofauti ya kijamii kama vile sokoni, au sehemu yoyote huwa rahisi kwao kuanzisha mahusiano kwa vile wanatumia lugha moja. Pia, lugha ni chombo muhimu ambacho huwawezesha wanajamii kujadili masuala tofauti yanayohusu maendeleo yao kijamii. Kwenye mahojiano yaliyofanyika tarehe 21/01/2023, watafitiwa walikuwa na kauli ifuatayo kuhusu iwapo bado wanazungumza Kishona na kwa nini. Majibu yao ni kama inavyodhihirika katika dondoo la 17:

**Dondoo 17**

> *Kitu ambacho kimetuweka pamoja kwa muda huu wote ni lugha yetu na utamaduni wetu kama Washona. Huwa tunatembeleana hata kupigiana simu ili tuweze kuongea lugha yetu ndio tusisahau.*
>
> *Chanzo: Data ya nyanjani*

Watafitiwa walikiri kwamba lugha yao imewaweka pamoja kwa kuwa nchini Kenya, kuna lugha nyingi zinazozungumzwa ambazo ni maarufu kuliko Kishona. Hivyo basi, kama inavyodhihirika kwenye dondoo la 17, lugha yao ndio iliyowaweka pamoja kwa kuwa hawakuwa na uraia au jamaa yeyote kwa miongo sita isipokuwa wao wenyewe. Kwa hivyo, hii ilikuwa sababu mojawapo ya kuzungumza lugha yao kwa muda mrefu bila kuisahau. O'Riagain (1994) anasema kwamba lugha ya mama huwa ni kipengele cha kwanza muhimu ambacho wazazi hurithisha wana wao. Hii inamaanisha kwamba kando na kurithisha utamaduni kwa vizazi vya Washona, wanaitumia lugha yao ili waweze kuendelea kuwa pamoja. Lugha yao iliwadumisha pamoja na kuwakumbusha asili yao kila siku kama inavyofafanuliwa katika sehemu ifuatayo ya 4.3.4.

### 4.3.4 Ukumbusho wa Asili yao

Washona hutumia Kishona kama ukumbusho wa asili yao. Kulingana na Wasike (2021), asili ya Washona ni nchi ya Zimbabwe ambapo asilimia 80 ya wakazi huzungumza Kishona. Kulingana na mazungumzo yaliyofanyika tarehe 21/01/2023 katika mtaa wa Kinoo katika Kaunti ya Kiambu, watafitiwa walieleza kuwa Washona wanaoishi Kenya wanaitumia Kishona kwa sababu wanataka kuendelea kuhifadhi kumbukumbu za asili yao. Wazee wa Kishona wana kumbukumbu nzuri kuhusu nchi ya Zimbabwe walikotoka na hivyo wanaamini kwamba lugha yao ya Kishona inawaunganisha na taifa la Zimbabwe. Dondoo 18 linabainisha maneno ya watafitiwa:

**Dondoo 18**

> *"Lugha ya Kishona inatuunganisha pamoja kwa sababu siku hizi Washona wengi wameenda mitaa mbalimbali hapa Nairobi. Lugha ya Kishona pia inatukumbusha kwenye tulitoka Zimbabwe kwenye Washona original wengi wanaishi."*
>
> ***Chanzo: Data ya Nyanjani***

Kutokana dondoo 18, inadhihirika kwamba Washona wanachukulia lugha yao kama ukumbusho wa asili yao. Washona wanaoishi Kenya ni sehemu ya kabila la Washona wa Zimbabwe waliofika nchini Kenya kama Wamishenari kuanzia mwaka wa 1959. Kulingana na Mulinya (2020), Washona walipewa uraia na kuwatambulisha kama mojawapo ya jamii za Kenya katika mwaka wa 2020. Hivyo basi, lugha ya Kishona inawakumbusha wanajamiilugha hawa asili yao nchini Zimbabwe.

Kishona ni mojawapo ya lugha ambazo zinazungumzwa nchini Kenya. Kwenye mahojiano yaliyofanyika tarehe 21/01/2023 katika mtaa wa Kiambaa katika Kaunti ya Kiambu, ilibainika kuwa Washona huzungumza Kishona kwa sababu ni lugha ya kwanza ambayo wao hujifunza baada ya kuzaliwa na ni mojawapo ya lugha zinazotambuliwa kisheria na kuzungumzwa nchini Kenya kuanzia mwaka wa 2020. Watafitiwa waliulizwa sababu nyingine ya kuzungumza Kishona nchini Kenya na kutoa sababu kupitia kwa dondoo la 19 lifuatalo.

**Dondoo 19**

> *"Tunasema Kishona sababu ni lugha yetu ya mama na pia sisi sasa ni Wakenya kwa sababu tulipewa uraia wa kuwa Wakenya tarehe 12/12/2020 na rais Kenyatta. Kwa hivyo lugha yetu imetambuliwa hapa Kenya."*
>
> *Chanzo: Data ya nyanjani.*

Baada ya kutambuliwa kuwa Wakenya, Washona walipata nguvu mpya za kuzungumza Kishona bila kuogopa mitazamo ya wanajamiilugha wengine kuwahusu. Awali, Washona walikuwa hawana uraia hali ambayo iliwapa hofu kuitumia lugha yao kwa kuogopa kutiwa mbaroni kwa kuishi nchini Kenya bila stakabadhi muhimu. Kutambuliwa kuwa Wakenya kuliwapa motisha ya kutumia na kudumisha lugha yao na hivyo wakawa na sababu ya kuendelea kutumia lugha yao ya Kishona.

### 4.3.5 Sababu za Udumishaji wa Kishona

Washona pia wanaitumia lugha yao ya Kishona kwa minajili ya kuidumisha. Clyne (2005) anasema kwamba maeneo ya nyumbani huwa ni chemichemi ya kujifunza na kufunza watoto lugha yao asilia. Naye Letsholo (2009) anakubaliana na Clyne (kt.) kwamba maeneo ya nyumbani ndiyo mazingira bora ya kufunza vizazi vyote lugha yao ya kwanza. Kwa mujibu wa mahojiano yaliyofanyika tarehe 21/01/2023 katika mtaa wa Kiambaa katika Kaunti ya Kiambu, watafitiwa vijana walipoulizwa sababu za kuzungumza Kishona, walisema kuwa Washona wanazungumza Kishona ili kuhahakisha udumishaji na maendelezo ya lugha yao kama inavyodhihirika kwenye dondoo la 20.

**Dondoo 20**

> *"Siku hizi ninaelewa kwamba tukizungumza Kishona, tunaendeleza lugha yetu."*
>
> *Chanzo: Data ya nyanjani.*

Washona wanazungukwa na wanajamiilugha wengine wanaozungumza lugha anuwai nchini Kenya. Jambo hili limewafanya kujifunza lugha nyinginezo zinazowazunguka

kama vile Kikuyu iliyo na wanajamiilugha wengi kwenye mitaa wanamoishi. Hata hivyo, kujifunza lugha mpya hakujawafanya kupoteza lugha yao. Hii inamaana kwamba bado Washona wana sababu ya kuongea lugha yao na kuwafunza wanawe lugha yao ya Kishona kwa mujibu wa lengo la pili la utafiti huu. Katika juhudi za kudumisha lugha yao, Washona huwafunza wanawe na kuwahimiza vijana kuzungumza Kishona wakiwa nyumbani na wanapotangamana na wanajamiilugha wenzao katika maeneo mengine. Wasailiwa walipoulizwa njia ambazo wanatumia kuendeleza lugha yao ya Kishona, walidokeza kwamba:

**Dondoo 21**

> *"Mimi najaribu kuwafunza wanangu lugha yetu. Huko nyumbani , hatuzungumzi lugha yoyote isipokuwa Kishona. Hata kama watoto wanazungumza lugha hii ya Kiswahili, mimi husisitiza matumizi ya Kishona nyumbani."*
>
> *Chanzo: Data ya nyanjani.*

Utafiti uligundua kwamba wazee wamejitahidi katika kudumisha lugha yao kupitia kuizungumza na pia kuwazungumzia wanawe. O'Riagain (1994) anasema kwamba kuzungumza lugha asilia ni kuidumisha na kuiendeleza. Wazee wa Kishona wamefaulu kwa hili kupitia kuwazungumzia wanao lugha yao ya Kishona japo kuna hatari ya kuathiriwa na lugha maarufu zinazowazunguka kama vile Kiswahili na Kikuyu. O'Riagain (kt.) anasema kwamba kila kizazi hubuni na kuweka mikakati ya kurithisha kizazi kinachofuata utamaduni wao ikiwemo lugha yao. Naye Mufwene (2003) anasema kwamba iwapo wazazi hawatawafunza wanao lugha yao asilia, wao ndio chanzo cha kufa kwa lugha. Wazee wa Kishona wanakiri kwamba lugha yao hutumika sana katika mazingira ya nyumbani ambapo ndicho kitovu cha kuifanya iwe thabiti.

Sababu hizi za Washona kutumia lugha yao ya Kishona hadi sasa, zinapeleka utafiti huu kwa mielekeo mbalimbali ya Washona kwenye matumizi ya lugha za Kiswahili na Kikuyu katika sehemu ya 4.4 ifuatayo.

## 4.4 Mielekeo ya Washona katika Matumizi ya Kiswahili na Kikuyu

Sehemu hii ya sura ya nne ilidhihirisha mielekeo ya Washona katika matumizi ya Kiswahili na Kikuyu kwenye maeneo yao ya kijamii. Baker (1992) na Bartram (2010) wanafafanua mielekeo ya lugha kuwa ni hisia za mtu au watu kuhusu lugha yao au lugha ya watu wengine katika mazingira ya wingilugha. Mielekeo ya lugha huzua matokeo mbalimbali katika jamii, ambayo yanaweza kuwa ya kuridhisha au ya kutoridhisha. Simandan (2016) anasema kwamba ikiwa watu wana mielekeo chanya kuhusu lugha husika, basi ni hamasisho tosha la kujifunza lugha hiyo ya pili. Vivyo hiyo, iwapo mtu ana mielekeo hasi kuhusu lugha fulani, hataweza kujifunza lugha hiyo.

### 4.4.1 Upimaji wa Mielekeo ya Washona kuhusu Kiswahili

Upimaji wa mielekeo ya lugha waweza kuwa wa moja kwa moja au usiwe wa moja kwa moja kwa watafitiwa. Baker (1992) anasema kwamba upimaji wa moja kwa moja huhitaji watafitiwa kuyajibu maswali ya hojaji au mahojiano ya mielekeo na matumizi mbalimbali ya lugha. Majibu yao hutumiwa na mtafiti kubainisha mielekeo yao kuhusu lugha husika. Mizani ya likati hutumika ili kutoa majibu kwa mpangilio maalum ili watafitiwa wachague jibu moja kati ya yale majibu waliyopewa kwenye mizani hiyo ya likati.

Baker (1992) na Walker (1982) wanasema kwamba upimaji usio wa moja kwa moja wa mielekeo hutumia mbinu ambazo hazitabainika hadharani na watafitiwa kama vile

uchunzaji na mijadala isiyo rasmi. Mbinu zisizo za moja kwa moja za kupima mielekeo huja mwanzoni kabla ya kutumia mbinu za moja kwa moja kwa kuwa iwapo wasailiwa hawajui kwamba wanatafitiwa huwa wanatoa data ya kuaminika kuhusu mielekeo ya lugha kuliko wakati ule wanajua kwamba wanatafitiwa.

Utafiti huu ulitumia mawazo haya ya Baker (1992), Triandis (1971) na Fasold (1984) ili kupima mielekeo ya Washona kuhusu matumizi ya Kiswahili kwa njia isiyokuwa ya moja kwa moja. Utafiti ulitumia kushiriki, mahojiano na hojaji zilizochunguza matumizi mbalimbali ya Kiswahili na Kikuyu kwenye maeneo mbalimbali katika jamii ili kubainisha mielekeo inayowachochea Washona kutumia lugha wanayopendelea katika shughuli mbalimbali.

### 4.4.2 Mielekeo ya Washona kuhusu Kiswahili Kupitia Shughuli Mbalimbali za Kijamii

Utafiti ulilenga kudhihirisha mielekeo waliyonayo Washona wa marika mbalimbali kuhusu Kiswahili na Kikuyu katika shughuli zao mbalimbali katika jamii. Matokeo yalikuwa kama ifuatavyo:

#### 4.4.2.1 Lugha Inayopendelewa kwenye Shughuli Rasmi

Kimemia (2002) anafafanua kwamba Kiswahili ni lugha rasmi nchini Kenya na ina majukumu mengi na mapana kuliko lugha nyingine za kiasili. Kiswahili ni lugha ambayo inatumika kwenye shughuli zote rasmi na pia ni mojawapo ya somo linalofunzwa kuanzia shule za chekechea hadi vyuo vikuu. Utafiti huu ulitaka kubainisha mielekeo ya Washona kuhusu lugha wanayotumia kwenye shughuli rasmi. Jedwali 4.7 lifuatalo linaonyesha majibu yao.

**Jedwali 4.7: Lugha Inayopendelewa kwenye Shughuli Rasmi**

| Lugha | Mirudio | Asilimia |
|---|---|---|
| Kishona | 8 | 17.8 |
| Kiswahili | 37 | 82.2 |
| Kikuyu | 0 | 0.00 |
| **Jumla** | **45** | **100.0** |

Chanzo: Data ya Nyanjani

Matokeo katika jedwali 4.7 yanadhihirisha kwamba Washona wanapendelea kutumia Kiswahili kwenye shughuli rasmi. Asilimia 82 walikiri kutumia Kiswahili huku asilimia 18 wakikiri kutumia Kishona kwenye shughuli zao rasmi. Lugha ya Kikuyu haikutumiwa kwenye shughuli rasmi miongoni mwa Washona. Watafitiwa walionyesha mielekeo chanya kwa Kiswahili kwa sababu ni lugha ya taifa la Kenya, ni lugha ya masomo, ni lugha ya mawasiliano na ni lugha ya biashara na hivyo basi haina budi kutumiwa katika mazingira na shughuli rasmi. Kwa mujibu wa lengo la tatu la utafiti huu, inabainika kwamba Washona wana mielekeo chanya kwa Kiswahili kwa sababu ya faida nyingi zinazohusishwa na matumizi yake. Sababu hizi zilidhihirika kwenye jedwali 4.8 kama ifuatavyo:

**Jedwali 4.8: Sababu za Kupendelea Kutumia Kiswahili kwenye Shughuli Rasmi**

| Sababu za kutumia Kiswahili | **Mirudio** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Lugha ya taifa | 9 | 23.1 |
| Lugha ya masomo | 6 | 15.4 |
| Lugha rasmi | 3 | 7.7 |
| Lugha ya mawasiliano | 17 | 43.6 |
| Lugha ya biashara | 1 | 2.6 |
| Waliokosa kutoa jibu | 3 | 7.7 |
| **Jumla** | **39** | **100.0** |

Chanzo: Data ya Nyanjani

Madai ya Kimemia (2002) kwamba lugha ya Kiswahili ina matumizi mapana sana kuliko lugha za kiasili za Kenya na ina idadi kubwa ya wazungumzaji ikilinganishwa na lugha nyingine za kiasilia ni kweli kwa kuwa kutokana na matokeo kwenye jedwali 4.8, Washona walibainisha sababu mbalimbali za kupendelea kutumia Kiswahili. Asilimia 23.1 wanatumia Kiswahili kwa kuwa ni lugha ya taifa, asilimia 15.4 wanaitumia Kiswahili kwa miktadha rasmi kwa sababu ni mojawapo ya somo shuleni, asilimia 7.7 wanaitumia kwa kuwa ni lugha rasmi, asilimia 43.6 wanaitumia kwa sababu ni lugha ya mawasiliano na asilimia 2.6 wanaitumia Kiswahili kwa sababu ya biashara. Hivyo basi, kwa kuwa Washona wana matumizi mapana ya Kiswahili, walikiri kuwa na mielekeo chanya kwayo.

UNESCO (2003) na Landweer (2000) wanasema kuwa asilimia kubwa ya wanajamiilugha wanaozungumza lugha husika sanifu hufanya lugha hiyo kuendelea kuimarika kiismujamii. Lugha ya Kiswahili inaendelea kupata idadi kubwa ya wazungumzaji wengi miongoni mwa Washona na kuendelea kuwa imara kila uchao ikilinganishwa na Kishona. Kwa hivyo, inadhihirika kwamba mielekeo ya Washona kuhusu Kiswahili ni chanya na ambayo inafanya uthabiti wa kiisimujamii wa Kiswahili kuwa imara ikilinganishwa na Kishona katika maeneo wanamoishi. Kwenye mahojiano yaliyofanyika katika kanisa la *Gospel of God* lililoko *Valley Road*, jijini Nairobi, wahojiwa walithibitisha haya kupitia kwa dondoo 22 lifuatalo baada ya kuulizwa sababu zinazowafanya kutumia lugha ya Kiswahili:

**Dondoo 22**


> *"Kwanza, shuleni tunatumia Kiswahili, pili, Kiswahili ni lugha rasmi hapa kenya. Tatu, tumezungukwa na makabila mengi na lugha inafaa ni Kiswahili kwa sababu ni lugha rasmi na lugha ya taifa ama Kiingereza..."*

Kutokana na maneno kwenye dondoo 22, mielekeo chanya ya Washona kuhusu Kiswahili ni bayana kwa kuwa wanapendelea kutumia Kiswahili kwa shughuli rasmi bila kulazimishwa nchini Kenya. Garrett (2010) anasema kwamba mielekeo ya lugha yaweza kuwa chanya au hasi kwa kutegemea matumizi yake katika jamii. Lugha iliyo na matumizi mengi katika jamii huwafanya wanajamii kuwa na mielekeo chanya kuihusu na hivyo basi huipatia hadhi ya juu kuliko lugha nyingine katika jamii. Hivyo mtazamo wa wanajamiilugha kuhusu lugha yao huchangia kuimarika na pia kutumika kwa lugha yao.

#### 4.4.2.2 Lugha ya Mazungumzo kwa Utawala wa Mitaa

Utafiti wa Wagalla (2019) ulibainisha kwamba haikuwa rahisi kwa Washona kuwa na mzee wa kijiji kwa sababu ya hali yao ya kutokuwa na vibali vya uraia. Hivyo, uongozi wa mitaa walimoishi ulitwaliwa na viongozi ambao hawakuwa Washona. Hii ilikuwa sababu mojawapo ya Washona kujifunza Kiswahili ili waweze kufanikisha mawasiliano kati yao na uongozi wa kijiji. Utafiti ulisaili kuhusu lugha ambayo Washona walipendelea kutumia katika mazungumzo yao na mzee wa kijiji. Baa-grafu 4.1 lifuatalo linaonyesha majibu yao.

**Baa-grafu 4.1: Lugha Inayopendelewa katika Kuzungumza na Mzee wa Kijiji**




Chanzo: Data ya Nyanjani


Kwenye baa-grafu 4.1, asilimia 61.76 walikiri kupendelea kutumia Kiswahili katika mazungumzo na mzee wa kijiji. Asilimia 12.75 walitumia Kishona, asilimia 11.76 wanatumia Kikuyu wanapoongea na mzee wa kijiji huku asilimia 5.88 wakitumia Kiswahili na Kishona wanapoongea na mzee wa kijiji. Asilimia 7.84 walikiri kutumia lugha za Kiswahili na Kikuyu katika mazungumzo na mzee wa kijiji. Matokeo kwenye baa-grafu 4.1 yanadhihirisha kwamba lugha ya Kiswahili inapendelewa kutumiwa kuliko lugha nyingine kwenye maeneo ya Kiambaa, Kikuyu, Kinoo, Gitaru na Githurai. Kulingana na maoni ya Landweer (2000), Fishman (1972b) na Chambers na Natalie (2013), lugha ikitumika sana katika maeneo mbalimbali ya jamii ya watu fulani, inaimarika na kuwa thabiti. Hii inamaanisha kwamba lugha iliyopewa kipaumbele ni

Kiswahili kwa sababu watafitiwa walikuwa na mielekeo chanya kwayo. Hali hii inadhihirisha kwamba uthabiti wa kiisimujamii wa Kishona umeanza kupungua kwa kuwa haitumiki sana kwenye maeneo wanamoishi Washona huku lugha ya Kiswahili ikiendelea kuwa thabiti kwa sababu ya matumizi mengi na ya kila siku katika jamii. Hali hii ya uthabiti wa kiisimujamii wa Kiswahili dhidi ya Kishona unawezeshwa na mielekeo chanya Washona walionayo kwa Kiswahili kwa mujibu wa lengo la tatu la utafiti huu.

#### 4.4.2.3 Lugha ya Mazungumzo baina ya Marafiki

Mugaddam (2006) anasema kwamba wanajamiilugha waliowachache kwenye mazingira mapya ya wingilugha huogopa kutumia lugha yao kwa kuhofia unyanyapaa. Wao hupendelea kuongea lugha maarufu ili wajenge urafiki kwenye mazingira mapya na wasitengwe na wenzao katika mazingira hayo. Utafiti ulitaka kubainisha lugha ambayo watafitiwa walikuwa wanapendelea kuongea na marafiki zao mitaani wanamoishi. Pai-chati 4.1 lifuatalo linaonyesha majibu yao.

**Pai-chati 4.1: Lugha Inayochukuliwa kuwa Muhimu katika Mazungumzo na Marafiki**




Chanzo: Data ya Nyanjani.

Kwenye pai-chati 4.1, asilimia 59.80 walipendelea kutumia Kiswahili katika mazungumzo yao na marafiki wao. Asilimia 29.41 walipendelea kutumia Kishona huku asilimia 10.78 wakipendelea kutumia Kikuyu katika mazungumzo na marafiki wao. Matokeo katika pai-chati hii ni dhahiri kwamba Washona wana mielekeo chanya kwa Kiswahili kuliko lugha yao ya Kishona na Kikuyu. Mielekeo hii chanya kwa Kiswahili inahatarisha uthabiti wa kiisimujamii wa Kishona kwa kuwa haitumiki kwenye maeneo mengi ya jamii ila maeneo ya nyumbani tu.

Garrett (2010) anasema kwamba mielekeo ya lugha yaweza kuwa chanya au hasi kwa kutegemea matumizi yake katika jamii. Landweer (2000) anasema kuwa lugha iliyo na matumizi mengi katika jamii huwafanya wanajamii kuwa na mielekeo chanya kuihusu

na hivyo basi huipatia hadhi ya juu kuliko lugha nyingine katika jamii. Hivyo mtazamo wa wanajamiilugha kuhusu Kiswahili kupitia kwa matumizi mbalimbali katika jamii yao huchangia kuimarika kwa lugha hiyo kuliko Kishona na Kikuyu.

#### 4.4.2.4 Lugha Inayopendelewa Kutumika kwenye Biashara

Muaka (2011) anasema kwamba lugha ya Kiswahili ilikuwa imepata umaarufu kwa biashara kuanzia mwanzoni mwa karne ya 19 kulipokuwepo biashara za watumwa. Naye Githiora (2002) anasema kwamba lugha ya Kiswahili inatumika kwa shughuli mbalimbali kama vile biashara baina ya makabila mbalimbali nchini Kenya hasa mijini ambapo kuna hali ya wingilugha. Kwenye shughuli za biashara, utafiti huu ulinuia kubainisha mielekeo ya lugha inayopendelewa. Jedwali 4.9 lifuatalo linaonyesha matokeo.

**Jedwali 4.9: Lugha Inayopendelewa Kutumika katika Biashara**

| Lugha ya matumizi | Mirudio | Asilimia |
|---|---|---|
| Kishona | 5 | 4.9 |
| Kiswahili | 92 | 90.2 |
| Kishona na Kiswahili | 4 | 3.9 |
| Kiswahili na Kikuyu | 1 | 1.0 |
| **Jumla** | **102** | **100.0** |

Chanzo: Data ya nyanjani


Inabainika katika jedwali 4.9 kwamba lugha ya Kiswahili inapendelewa na Washona katika shughuli za biashara kuliko lugha nyingine zinazowazunguka. Asilimia 90.2 walikiri kutumia Kiswahili, asilimia 4.9 walisema wanatumia Kishona kwenye shughuli zao za biashara, asilimia 3.9 walichanganya Kishona na Kiswahili kwenye shughuli za biashara huku asilimia moja tu wakitumia lugha za Kiswahili na Kikuyu katika

biashara. Mielekeo chanya inayobainika kwenye jedwali la 4.9 unaendana na maoni ya Appel na Muysken (2005) na Heine (1992) wanaposema kwamba lugha iliyo na hadhi ya juu ni ile ambayo inamnufaisha mzungumzaji katika biashara na maingiliano ya kijamii na manufaa ya kiuchumi kwa wanajamiilugha husika. Landweer (2000) anasema katika nadharia ya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha, mhimili wa nane kwamba lugha yoyote kuwa thabiti hutegemea misingi imara na halali ya kiuchumi wa hiyo lugha. Lugha ambayo haiwanufaishi wazungumzaji wake kiuchumi hubadilika kwa urahisi na hivyo kukosa uthabiti wake.

#### 4.4.2.5 Lugha ya Masomoni

Githiora (2002) na Ontieri (2017) wanasema kwamba Kiswahili hutumika kama mojawapo ya somo nchini Kenya kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu. Vijana pamoja na watoto wa Kishona husoma kwenye shule za kuanzia chekechea hadi vyuo vikuu. Utafiti ulitaka kubainisha mielekeo kuhusu lugha inayopendelewa katika masomo, majibu yao yanadhihirika katika baa-grafu 4.2 ifuatayo.

**Baa-grafu 4.2: Lugha Inayochukuliwa kuwa Muhimu Masomoni**




Chanzo: Data ya Nyanjani

Utafiti ulibainisha kwamba watafitiwa wana mielekeo chanya kwa Kiswahili katika shughuli za masomo shuleni. (86%). Lugha nyingine zilipewa asilimia iliyo chini ya 10 kama vile Kishona na Kiswahili (1%), Kiswahili na Kikuyu (7%) huku Kiswahili na lugha nyingine zikichukua asilimia sita. Kwenye mijadala ya kimakundi, mtafiti aliwasaili vijana na watoto kuhusu mielekeo yao ya Kiswahili na Kikuyu kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Dondoo 23 lifuatalo linadhihirisha mielekeo waliyonayo vijana na watoto wa Kishona kuhusu Kiswahili katika masomo:

**Dondoo 23**

> ***Mtafiti:*** *Je mnaongea lugha ipi kwa wingi?*
>
> ***Kijana II****: Tunazungumza Kiswahili sana na pia Kiingereza. Kishona tunaongea tu nyumbani.*


> ***Mtafiti**: Kwa nini?*
>
> ***Kijana III**: Kwanza, shuleni tunatumia Kiswahili, pili, Kiswahili ni lugha rasmi hapa Kenya. Tatu, tumezungukwa na makabila mengi na lugha mwafaka ni Kiswahili kwa kuwa ni lugha rasmi na lugha ya taifa ama kiingereza. Lakini tukikutana na marafiki Wakikuyu, huwa tunajaribu kuongea lugha yao.*
>
> ***Mtafiti:** Mnachukuliaje lugha ya Kiswahili na Kikuyu?*
>
> ***Kijana IV:** Lugha ya Kiswahili ina manufaa mengi kama vile masomoni, biashara na mambo mengi. Kwa hivyo ni lugha ambayo tunaitumia kwa hiari tu bila kulazimishwa.*
>
> *Chanzo: Data ya Nyanjani*

Kutokana na majibu ya watafitiwa kupitia kwa mijadala ya kimakundi, inabainika kwamba mielekeo ya vijana kuhusu Kiswahili ni chanya. **Kijana III** na **Kijana IV** walikiri kwamba wanatumia Kiswahili kwa sababu ni lugha rasmi nchini Kenya, ni lugha inayotumiwa shuleni kama mojawapo ya somo. Zaidi ya hayo, **Kijana IV** alikiri kwamba wanatumia Kiswahili kwa hiari tu bila kulazimishwa. Kutokana na dondoo hilo, ni dhahiri kwamba lugha ya Kiswahili inapendelewa na Washona katika masomo hapa nchini Kenya kuliko lugha nyingine za kiasili.

#### 4.4.2.6 Mielekeo ya Washona kuhusu Kiswahili kwenye Burudani

Burudani ni sehemu kuu ya utamaduni wa jamii yoyote. Baada ya kazi, burudani ni jambo la busara ili mwili uweze kupumzika. Kuna aina nyingi za burudani ambazo watu hujihusisha nazo kama vile michezo mbalimbali, nyimbo, usafiri na hata kutembeleana. Utafiti ulinuia kudhihirisha lugha ambayo watafitiwa wanapendelea kutumia katika maeneo ya burudani. Majibu ya watafitiwa yanadhihirika kwenye baa-grafu 4.3 ifuatayo:

**Baa-grafu 4.3: Lugha Inayopendelewa Kutumika kwenye Burudani**





Chanzo: Data ya Nyanjani

Watafitiwa walionyesha mielekeo chanya kwa Kiswahili kwenye maeneo ya burudani kwa sababu asilimia 77.45 walikiri kutumia Kiswahili, asilimia 18.63 walikiri kutumia Kishona huku asilimia 3.92 wakionyesha mielekeo chanya kwa Kikuyu katika maeneo ya burudani. Watafitiwa walitoa sababu ya kupendelea kutumia Kiswahili kwenye maeneo ya burudani na kusema kwamba hata nyimbo nyingi zinazochezwa kwenye maeneo hayo ni za Kiswahili na pia maeneo ya burudani huwa na watu wa kabila zote zinazowazunguka.

#### 4.4.2.7 Mielekeo kuhusu Lugha ya Matumizi ya Jumla katika Maisha

Utafiti ulilenga kujua lugha ambayo wanajamiilugha hupendelea katika matumizi muhimu ya maisha kwenye baa-grafu 4.4 ifuatayo:

**Baa-grafu 4.4: Lugha Inayopendelewa Kutumika kwenye Shughuli Muhimu katika Maisha**




Chanzo: Data ya Nyanjani.

Watafitiwa walionyesha mielekeo chanya kwa Kiswahili katika matumizi muhimu ya maisha (asilimia 69.61). Asilimia 21.57 walionyesha mielekeo chanya kwa Kishona huku asilimia 3.92 wakikiri kutumia lugha za Kiswahili na Kishona na Kikuyu. Asilimia moja tu walitumia Kishona na lugha nyingine kwa matumizi muhimu ya maisha. Kwenye mahojiano yaliyofanyika kuhusu sababu za kutumia Kiswahili, watafitiwa waliulizwa swali lililolenga kutambua mielekeo yao kwa matumizi ya Kiswahili kwa jumla kama inavyodhihirika kwenye dondoo 24;

**Dondoo 24:**

> *"Tulikuwa tunatumia Kiswahili ili kutambulikana kama Wakenya. Kwanza siku hizi ndiyo imekuwa vizuri vile tulitambuliwa kama Wakenya mwaka wa 2020. Tunaongea Kiswahili sasa tukiwa Wakenya.*

*Watoto wetu pia wanatumia lugha ya Kiswahili masomoni kwa hivyo lazima wajifunze Kiswahili shuleni.”*

***“****Pia tunazungumza Kiswahili kwa sababu ya kurahisisha mawasiliano baina yetu na makabila mengine hapa nchini Kenya. Lugha ya Kiswahili ni lugha ya mawasiliano.”*

*Data ya Nyanjani*

Kutokana na dondoo 24, ni wazi kwamba Washona wana mielekeo chanya kwa Kiswahili kwa kuwa wameipa matumizi mapana katika jamii yao. Kimemia (2002) anasema kwamba kwa kuwa Kiswahili ni lugha ya taifa nchini Kenya, imepewa matumizi mapana sana kuliko lugha za kiasili za Kenya na pia, ina idadi kubwa ya wazungumzaji ikilinganishwa na lugha nyingine za kiasilia. Landweer (2000) anadai kuwa wanajamiilugha wanaozungumza lugha husika sanifu wakiwa wengi, lugha hiyo inaendelea kuimarika. Utafiti wa UNESCO (2003) unasema kwamba kigezo kimojawapo cha kupima uthabiti wa lugha ni asilimia ya wanajamiilugha ambao huzungumza lugha husika. Asilimia ya wanaozungumza lugha husika kwenye maeneo yao ya kijamii ikiwa kubwa, basi lugha hiyo ni thabiti katika jamii. Mielekeo chanya wa Washona kuhusu lugha ya Kiswahili inaifanya kuendelea kuwa thabiti kiisimujamii ikilinganishwa na Kishona na Kikuyu nchini Kenya. Hali hii imeanza kuathiri uthabiti wa kiisimujamii wa Kishona nchini Kenya na juhudi zisipowekwa za kudumisha Kishona, basi lugha hiyo itatoweka. Hii ina maana pia kwamba Washona wanafaa kuwa na mielekeo chanya kwa lugha yao ya Kishona ili kuikinga dhidi ya kuangamia.

#### 4.4.2.8 Matumizi ya Kiswahili kwa Hiari

Utafiti ulinuia kubainisha ikiwa wanajamiilugha wa Kishona wanazungumza Kiswahili kwa hiari au wanalazimishwa. Jedwali 4.10 linadhihirisha majibu ya swali waliloulizwa la iwapo wanatumia Kiswahili kwa hiari:

**Jedwali 4.10: Mazungumzo ya Kiswahili kwa Hiari**

| | |
|---|---|
| Mtafiti | Je mnazungumza lugha ya Kiswahili kwa hiari tu ama kuna sababu maalum zinawafanya kuzungumza? |
| Mtafitiwa IV | Tunazungumza Kiswahili kwa hiari tu na pia kama tulivyosema hapo awali, kuna sababu nyingi ambazo zinatufanya kuzungumza lugha ya Kiswahili. |
| Kijana IV | Lugha ya kiswahili ina manufaa mengi kama vile masomoni, mawasiliano na makabila mengine, biashara na mambo mengi. Kwa hivyo ni lugha ambayo tunaitumia kwa hiari tu bila kulazimishwa na tunaipenda. |

*Chanzo: Data ya nyanjani*

Kutokana na jedwali 4.10, Washona wana mielekeo chanya kwa Kiswahili kwa kuwa wanaitumia kwa hiari huku wakisema kwamba lugha ya Kiswahili ina manufaa mengi katika maisha yao kama vile masomoni, kwenye biashara na pia maelewano na wanajamiilugha wengine. Hatimaye matumizi ya Kiswahili kwa hiari yanaifanya kuendelea kuwa na uthabiti wa kiisimujamii kama wanavyosema Fishman (1972b) na Chambers na Natalie (2013) kwamba lugha ikitumika sana katika maeneo mbalimbali ya kijamii inaimarika na kuwa thabiti.

### 4.4.3 Mielekeo ya Washona kuhusu Kikuyu nchini Kenya

Baker (1992) na Walker (1982) wanasema kwamba upimaji usio wa moja kwa moja wa mielekeo hutumia mbinu ambazo hazitabainika hadharani na watafitiwa kama vile uchunzaji na mijadala isiyo rasmi ili watafitiwa watoe data ya kuaminika kuhusu

mielekeo ya lugha kuliko wakati ule wanajua kwamba wanatafitiwa kuhusu mielekeo mbalimbali ya lugha.

Utafiti huu ulitumia mawazo haya ya Baker (1992), Triandis (1971) na Fasold (1984) ili kupima mielekeo ya Washona kuhusu matumizi ya Kikuyu kwa njia isiyokuwa ya moja kwa moja. Utafiti huu ulitumia mbinu za uchunzji wa kushiriki na mahojiano yaliyochunguza matumizi mbalimbali ya Kikuyu kwenye maeneo mbalimbali katika jamii ili kubainisha mielekeo inayowachochea Washona kutumia lugha wanayopendelea katika shughuli mbalimbali. Jedwali 4.11 lifuatalo linabainisha maoni ya Washona kuhusu Kikuyu baada ya kuulizwa sababu zinazowafanya kutumia Kikuyu katika maeneo yao ya kijamii.

**Jedwali 4.11: Sababu za Washona za Kupendelea Kutumia Kikuyu**

| Watafitiwa | Swali: Sababu gani zinazowafanya kutumia lugha ya Kikuyu? |
|---|---|
| 1. | Baba zetu walipofika nchini Kenya, walikaribishwa na Wakikuyu katika sehemu za Ngong na Juja kabla ya kuhamia kwenye mitaa ya Kinoo na Kiambaa. Kando na kuzungumza lugha ya Kiswahili, baba zetu pia walijifunza lugha ya Kikuyu. |
| 2. | ...Wale Washona wanasungumsa Kikuyu, husungumsa kwa sababu kuwasiliana. Wakikuyu ni majirani zetu na mawasiliano ni lazima kati yetu. Tunaposungumsa lugha hii ya Kikuyu, watu wengine hufikiria kwamba sisi pia ni Wakikuyu. |
| 3. | ... Sherehe kama vile za harusi au mazishi tunahudhuria. Wakikuyu hutumia lugha yao wakati wa sherehe kama hizi. Inabidi tujue lugha yao ili ikuwe rahisi kwetu kushiriki. Lakini si Washona wote wanajua lugha ya Kikuyu. |
| 4. | Katika maeneo haya tunaishi, biashara nyingi ni za Wakikuyu ambao hutuzungumzia kwa lugha yao ya Kikuyu tunapoenda kununua. Hivyo hata sisi imebidi tujifunze lugha ya kikuyu ili kufanikisha shughuli za biashara. |
| 5. | Ilikuwa ni poa kwetu Washona kuzungumza Kiswahili na Kikuyu kwa sababu askari hawangegundua haraka kama sisi si Wakenya. Lugha hizi za Kenya zilituficha sana. Lakini kuna wakati mwingine |

| | |
|---|---|
| | wanajamii walitusema na tukajipata tumefungwa... |

Chanzo: Data ya Nyanjani

Kutokana na maoni ya watafitiwa kwenye jedwali 4.11, inabainika kwamba baadhi ya Washona wana mielekeo chanya kwa Kikuyu kwa sababu mbalimbali kama vile mawasiliano, ufadhili, biashara, kuhudhuria sherehe zao na pia kwa usalama wao. Kupitia kwa majukumu haya mbalimbali ya Kikuyu, Washona wamejenga mielekeo chanya kwa Kikuyu ndio maana baadhi yao wamejifunza na wanaizungumza lugha hii kwa ufasaha. Nash (1987) na Landweer (2000) wanasema kwamba utambuzi wa lugha ya matumizi katika jamii huletwa na mielekeo mbalimbali kuhusu lugha husika ambayo inachangiwa na matumizi yake na faida za matumizi yake katika jamii. Lugha iliyo na matumizi mengi katika jamii huwafanya wanajamii kuwa na mielekeo chanya kuihusu na hivyo basi huipatia hadhi ya juu kuliko lugha nyingine katika jamii. Hii inamaanisha kwamba, kwa mujibu wa lengo la tatu la utafiti huu, baadhi ya Washona wana mielekeo chanya kwa Kikuyu kwa kuwa wanaitumia kwa shughuli mbalimbali katika jamii yao.

**4.5 Hitimisho**

Sura hii imeshughulikia sababu mbalimbali za Washona za kutumia Kiswahili, Kikuyu na lugha yao ya Kishona kwenye maeneo mbalimbali ya kijamii pamoja na mielekeo yao kuhusu matumizi ya Kiswahili na Kikuyu katika jamii wanamoishi. Ilibainika kwamba Washona wana sababu nyingi za kutumia Kiswahili kama vile: Sababu za kielimu, utaifa wa lugha, sababu za mawasiliano, sababu za kiutangamano, sababu za kushirikiana, kujenga mahusiano baina yao na wanajamiilugha wengine, sababu za kibiashara, sababu za utambulisho, sababu za kidini na sababu za kiusalama.

Ilibainika pia kwamba Washona walikuwa na sababu mbalimbali za kutumia Kikuyu kwa kuwa wanaishi katika mitaa mitano ya kaunti ya Kiambu ambapo wanajamiilugha Wakikuyu ndio wengi wanaoishi humo. Sababu hizi ni kama vile sababu ya ufadhili, umaarufu wa lugha ya Kikuyu katika mitaa wanamoishi, mawasiliano, kushiriki kwenye sherehe mbalimbali za jamii ya Wakikuyu na pia sababu za kibiashara.

Kutokana na data iliyokusanywa, ilibainika kwamba baadhi ya Washona bado wanazungumza lugha yao ya Kishona hata baada ya miongo sita kwa sababu lugha yao imefungamanishwa na utamaduni wao, wanatumia lugha yao katika ibada yao na ni chombo cha kuwaunganisha, lugha yao ni ukumbusho wa asili yao na wanaizungumza ili kuidumisha. Ilidhihirika kwamba licha ya juhudi za wazee kuidumisha, lugha ya Kishona imeanza kupoteza uthabiti wake wa kiisimujamii kwa kizazi cha nne (watoto, miaka 1-17) kwa sababu kulingana na UNESCO (2003), kuna vigezo mbalimbali ambavyo hutumika kukadiria uthabiti wa kiisimujamii wa lugha. Katika kigezo cha kwanza cha kupokezanwa kwa lugha baina ya vizazi, lugha ya Kishona hakika imo katika hatari ya kuangamia kwa sababu ilibainika kwamba watoto hawazungumzi lugha hiyo kama lugha yao ya kwanza kwenye maeneo ya nyumbani. Kishona huzungumzwa na wazazi peke yao kwenda juu. Kigezo kingine ni kuangalia ruwaza katika maeneo mbalimbali ya matumizi ya lugha ambapo lugha ya Kishona imesalia kutumika katika maeneo na shughuli za nyumbani tu na kwenye ibada yao. Washona wana sababu tano tu za kutumia Kishona na Kikuyu katika jamii ikilinganishwa na sababu tisa za kutumia Kiswahili katika maeneo ya Kinoo, Kikuyu, Kiambaa, Gitaru na Githurai.

Utafiti uligundua kwamba lugha ya Kiswahili ina matumizi mengi katika jamii na imeanza kuathiri matumizi ya Kishona kwenye maeneo mbalimbali ya Kijamii. Hali hii inawezeshwa na mielekeo chanya waliyonayo wanajamiilugha wa Kishona kuhusu Kiswahili.

Mielekeo ya Washona katika matumizi ya Kiswahili na Kikuyu ilijadiliwa katika sura hii. Utafiti ulibainisha mielekeo ya Washona kupitia kwa upimaji usio wa moja kwa moja kama vile kushiriki katika shughuli zao, mahojiano na hojaji zilizochunguza matumizi mbalimbali ya Kiswahili na Kikuyu kwenye maeneo mbalimbali katika jamii ili kubainisha mielekeo inayowachochea Washona kutumia lugha wanayopendelea katika shughuli mbalimbali.

Ilibainika kwamba Washona wana mielekeo chanya kwa Kiswahili kwa kuwa wanatumia Kiswahili kwa hiari na kwenye maeneo mengi ya kijamii. Majedwali, pi-chati, baa-grafu na madondoo mbalimbali yalitumiwa kuonyesha asilimia ya umuhimu uliopewa lugha za Kiswahili, Kikuyu na Kishona kisha maelezo yakatolewa chini ya kila jedwali, pai-chati, baa-grafu na kila dondoo.

Ilibainika pia kwamba mielekeo ya Kiswahili imefanya viwango vya uthabiti wa kiisimujamii wa Kishona kushuka kwa kuwa Washona hawaitumii katika maeneo mengi ya kijamii ili kuifanya iwe thabiti bali wanatumia Kiswahili kwa sababu ni lugha maarufu kwenye mitaa wanamoishi na ni lugha iliyo na matumizi mapana. Landweer (2000) na Mirvahedi (2014) wanasema kwamba lugha isipotumika katika mitandao ya kijamii, elimu na serikalini, lugha hiyo inakosa kudumishwa na kuanza kupotea polepole.

Kwa jumla, kupitia kwa data iliyotokana na hojaji, mahojiano, uchunzaji wa kushiriki na mijadala ya kimakundi, malengo yote mawili yaliyoshughulikiwa kwenye sura hii yalitimia kwa kuwa, katika lengo la pili, ilibainika kwamba Washona wana sababu nyingi za kutumia Kiswahili na Kikuyu zikiwemo sababu za kielimu, utaifa wa lugha, mawasiliano, utangamano na ushirikiano, ufadhili na usalama wao. Lengo la tatu pia lilitimika ilipobainika kutoka kwa utafiti kwamba Washona wana mielekeo chanya kwa Kiswahili na baadhi yao wana mielekeo chanya kwa Kikuyu kwa sababu ya majukumu mbalimbali yaliyopewa lugha hizi mbili.

Sura inayofuata ya tano inashughulikia mikakati mbalimbali ambayo Washona wanatumia ili kudumisha lugha yao ya Kishona licha ya shinikizo kutoka kwa lugha maarufu za Kiswahili na Kikuyu zinazowazunguka kwenye mitaa wanamoishi.

# SURA YA TANO: UDUMISHAJI WA KISHONA NCHINI KENYA

## 5.0 Utangulizi

Sura ya nne ilijikita katika kudhihirisha sababu mbalimbali za kutumia Kiswahili, Kikuyu na Kishona nchini Kenya. Utafiti ulibainisha kuwa kuna sababu kadha wa kadha za kutumia Kiswahili kama vile sababu za kielimu, utaifa wa lugha, sababu za mawasiliano, utangamano, ushirikiano, mahusiano, kujitafutia riziki, sababu za utambulisho na sababu za kiusalama. Ilibainika pia kwamba baadhi ya Washona wanatumia Kikuyu kwa sababu ya ufadhili waliopata kutoka kwa wanajamiilugha ya Wakikuyu, umaarufu wake katika maeneo wanamoishi kwenye kaunti ya Kiambu na pia sababu za Kibiashara. Washona, hasa wazee, bado wanatumia Kishona kwa sababu ni lugha ya mama, inawaunganisha, ni ukumbusho wa asili yao na pia wanazungumza ili kuidumisha lugha yao.

Mielekeo ya Washona ya kutumia Kiswahili na Kikuyu katika maeneo mbalimbali ya Kijamii pia ilishughulikiwa katika sura ya nne. Ilibainika kwamba mielekeo ya lugha ni jambo la kijamii ambapo mielekeo chanya ya lugha fulani huipa nafasi ya kuwa na matumizi mengi katika jamii. Ilidhihirika kwamba Washona wana mielekeo chanya kwa lugha ya Kiswahili kwa sababu ina matumizi mapana katika mazingira wanamoishi. Baadhi ya Washona wana mielekeo chanya kwa Kikuyu kwa kuwa pia ina matumizi mbalimbali katika jamii wanamoishi, na pia ni lugha muhimu kwao kwa sababu wanajamiilugha Wakikuyu ndio walikuwa wafadhili wao walipofika Kenya kwa mara ya kwanza kuanzia mwaka wa 1959. Utafiti uligundua kwamba Washona

wanatumia Kiswahili na Kikuyu kwa sababu ya mielekeo ambayo wako nayo kwa lugha hizi mbili katika jamii wanamoishi.

Sura hii ya tano inajikita katika kubainisha iwapo Washona wameidumisha lugha yao ya Kishona nchini Kenya au la licha ya shinikizo kutoka lugha maarufu kama vile Kiswahili na Kikuyu. Utafiti huu uligundua kuwa Washona nchini Kenya bado wanazungumza Kishona licha ya shinikizo kutoka lugha maarufu za Kiswahili na Kikuyu na changamoto mbalimbali walizozipitia kabla ya kupata uraia nchini Kenya.

Udumishaji wa lugha ni hali ya lugha husika kuwa thabiti kupitia kwa matumizi yake mbalimbali katika jamii na vizazi vyake licha ya mtagusano na shinikizo kutoka lugha nyingine maarufu anavyosema Benrabah (2004). Krauss (1992) anasema kwamba lugha ambayo haina wazungumzaji wa umri mchanga imo kwenye hatari ya kutoweka kwa sababu vijana na watoto ndio nyenzo ya kuendeleza na kudumisha lugha. UNESCO (2003) na Batibo (2005) wanasema kwamba wanajamiilugha huanza kuacha kutumia lugha yao iwapo kuna mambo kama vile ubaguzi na ukabila katika nchi wanamoishi. Hivyo basi wao huamua kutumia lugha ya wenyeji wao ili waweze kuepuka dhuluma wanazozipitia kama vile ubaguzi, kunyimwa uhuru na kukubalika katika jamii.

Landweer (2000) anasema kwamba lugha inaweza kuwa na wazungumzaji wachache na bado kiisimujamii iwe thabiti kwa kutegemea msaada inayopokea kutoka kwa asasi mbalimbali za kijamii pamoja na juhudi za wanajamiilugha wenyewe. Washona wameishi nchini Kenya kwa zaidi ya miongo sita na walipitia changamoto za kukosa uraia kwa miaka mingi hadi mwishoni mwa mwaka wa 2020 ambapo aliyekuwa Rais wa nne wa Kenya, Uhuru Kenyatta alipowapatia vibali vya kuwa Wakenya. Kwa hivyo,

sura hii itajadili mikakati wanayotumia katika kudumisha lugha yao licha ya shinikizo na changamoto mbalimbali walizozipitia kabla ya kupewa uraia nchini Kenya.

### 5.1 Mikakati ya Udumishaji wa Kishona

Mikakati ya udumishaji wa lugha ni mbinu zilizowekwa na wanajamiilugha husika kwa madhumuni ya kuendeleza uhai wa lugha yao kwa vizazi vinavyofuata. O'Riagain (1994) anasema kwamba kila kizazi hubuni na kuweka mikakati ya kurithisha kizazi kinachofuata utamaduni wao ikiwemo lugha yao. Mikakati inapowekwa inaweza kufaulu au kutofaulu katika kufanikisha lengo la jamiilugha husika kwa kutegemea juhudi zao pamoja na mbinu wanazozitumia. Washona wamejitahidi kudumisha lugha yao ya Kishona licha ya changamoto na shinikizo kutoka lugha maarufu nchini Kenya kama vile Kiswahili na Kikuyu. Kupitia kwa mahojiano na hojaji kwa vizazi vinne (mwaka 1-17, 18-35, 36-45 na 46+) vya jamiilugha ya Washona, Ilibainika kwamba Washona wamebuni mikakati mbalimbali ya kudumisha lugha yao ya Kishona kama vile uzungumzaji wa lugha yao katika maeneo ya nyumbani, kutumia Kishona kwenye ibada zao, kutembeleana miongoni mwao na kuzungumza lugha yao, kutumia lugha yao katika sherehe mbalimbali za kitamaduni na wazee kufundisha kizazi kichanga lugha ya Kishona. Utafiti ulianza na mjadala kuhusu mkakati wa uzungumzaji wa Kishona katika maeneo ya nyumbani.

#### 5.1.1 Uzungumzaji Kishona katika Maeneo ya Nyumbani

Udumishaji wa lugha asilia unategemea juhudi za familia katika matumizi ya lugha hiyo kwenye maeneo ya nyumbani. Letsholo (2009), Pauwels (2005) na Velázquez (2012) wanasema kwamba nyumbani ndio maeneo ya kipekee ambapo familia inaweza

kudhibiti watoto katika matumizi na maendelezo ya lugha yao asilia. Hii ni kwa sababu watoto hukumbana na shinikizo kutoka kwa lugha zilizo na nguvu za kidemografia wakiwa nje ya maeneo ya nyumbani hasa wanapocheza pamoja, wanapokuwa shuleni na hata kanisani. Clyne (2003, 2005) anasema kwamba lugha haitapitishwa kwa vizazi vijavyo iwapo familia haitajukumika kuwafunza wanao lugha yao asilia. Clyne (kt.) anaendelea kusema kwamba mazingira ya nyumbani huwa kichocheo bora kwa ufanisi wa udumishaji wa lugha kwa vizazi tofauti vya jamiilugha husika.

Kupitia kwa mahojiano yaliyofanyika tarehe 11/03/2023 kwenye maeneo ya kanisa la *Gospel of God* lililoko *Valley Road* jijini Nairobi, wazee wa Kishona walikiri kwamba wanawafunza wanawe Kishona nyumbani kupitia kwa mjadala katika maeneo ya nyumbani. Madondoo mawili yafuatayo yanathibitisha majibu kutokana na swali la njia ambazo Washona hasa wazee wanatumia kuendeleza lugha ya Kishona:

**Dondoo 1**

> *“Mimi nawaongelesha wanangu pamoja na wachukuu wangu Kishona tukiwa katika maeneo ya nyumbani”*

**Dondoo 2**


> *“Mimi najaribu kuwafunza wanangu lugha yetu. Huko nyumbani , hatuzungumzi lugha yoyote isipokuwa Kishona. Hata kama watoto wanazungumza lugha hii ya Kiswahili, mimi husisitiza matumizi ya Kishona nyumbani.”*

*Chanzo: Data ya Nyanjani*

Kupitia kwa dondoo la 1 na 2, wazee huwazungumzia wanawe na wajukuu wao Kishona katika maeneo ya nyumbani. Watoto wanapozungumziwa lugha yao ya kwanza na wazazi wao, hujitahidi na kujifunza lugha ile ile wanayozungumziwa kwayo.

Ilibainika kwamba katika maeneo ya nyumbani, ndipo panapokuwa na matumizi mengi ya Kishona kwa kuwa wahusika katika familia huwa na mengi ya kuzungumzia bila kuwa na mada maalum au mada iliyopangwa mbeleni. Wahusika huzungumza kuhusu vyakula, kazi za nyumbani, mavazi mbalimbali na mafunzo kuhusu maadili mema. Hali hii huwapa watoto nafasi ya kujifunza lugha kwa kuwa wanazungumziwa na kujibu vivyo hivyo wakitumia lugha yao asilia. Baa-grafu 5.1 ifuatayo inabainisha maeneo ya watoto na vijana ya kujifunzia Kishona:

**Baa-grafu 5.1: Maeneo ya Vijana na Watoto kujifunza Kishona**




Chanzo: Data ya Nyanjani.

Matokeo katika baa-grafu 5.1 yanabainisha maeneo ambayo vijana na watoto hujifunzia lugha yao ya Kishona. Asilimia 76.24 walikiri kwamba wao hujifunza lugha yao katika maeneo ya nyumbani. Asilimia 16.83 walikiri kujifunza Kishona wakiwa kanisani huku asilimia 6.93 wakikiri kujifunza Kishona wakiwa nyumbani na kanisani. Kutokana na

usaili huu, ni dhahiri kwamba maeneo bora ya kujifunza Kishona ni nyumbani (76.24%) na kanisani (16.83%). Kulingana na O'Riagain (1994), mikakati ya kurithisha kizazi kingine lugha asilia hufanyika katika maeneo ya nyumbani. Utafiti wa UNESCO (2003) unasema kwamba lugha imo hatarini iwapo matumizi yake yamebakia kutumika katika maeneo ya nyumbani pekee. Hali hii ni sawa na matumizi ya Kishona kwa kuwa matumizi yake mengi ni nyumbani huku asilimia ndogo wakijifunzia lugha hii kanisani. Kukosekana kwa matumizi ya Kishona katika maeneo mbalimbali ya kijamii ni ishara kwamba lugha maarufu za Kiswahili na Kikuyu zimeanza kuathiri uthabiti wa kiisimujamii wa Kishona. Hata hivyo, Washona wanaonyesha jitihada za kudumisha lugha yao ya Kishona licha ya shinikizo kutoka lugha maarufu za Kiswahili na Kikuyu kwa sababu hata baada ya miongo sita, bado wanazungumza lugha yao japo kuna mabadiliko ambayo yanaanza kuonekana kwa kizazi cha nne.

#### 5.1.1.1 Namna ya Kujifunza Kishona katika Maeneo ya Nyumbani na Kanisani

Clyne na Kipp (1999) wanasema kwamba wazazi wana jukumu kuu katika kuweka msingi bora kwa watoto wao kuhusu udumishaji wa lugha. Iwapo matumizi ya lugha ya kwanza yatadididimia katika maeneo ya nyumbani na iwapo lugha ya kwanza haitadumishwa nyumbani, basi hali hiyo itaathiri matumizi ya lugha katika maeneo mengine na huo utakuwa ndio mwanzo wa kubadilika na kuhama kwa lugha yoyote. Familia ndiyo chanzo cha udumishaji wa lugha yoyote.

Utafiti huu ulisaili jinsi ambavyo watoto na vijana hujifunza Kishona wakiwa katika maeneo ya nyumbani na kanisani. Jedwali 5.1 linabainisha majibu yao:

**Jedwali 5.1: Jinsi Watoto na Vijana Hujifunza Kishona**

| Jinsi ya Kujifunza | Mirudio | Asilimia |
|---|---|---|
| Kufunzwa na wazazi | 19 | 67.9 |
| Kuiga wengine wakiongea | 9 | 32.1 |
| **Jumla** | **28** | **100.0** |

Chanzo: Data ya Nyanjani

Katika jedwali 5.1, utafiti uligundua kwamba asilimia 68 ya watoto na vijana hufunzwa Kishona nyumbani na wazazi wao huku asilimia 32 wakijifunza Kishona kupitia kuiga wanajamiilugha wengine wakizungumza hasa katika maeneo ya nyumbani. Utafiti wa UNESCO (2003) unaonyesha kwamba idadi ya watu wanaoishi katika familia moja pia huchangia udumishaji wa lugha. Hali hii inamaanisha kwamba watoto wanaoishi pamoja na wazazi wao huwa na nafasi nzuri ya kujifunza na kudumisha lugha yao kuliko wale wanaoishi pekee yao au mbali na wazazi wao.

Kwenye dondoo la 3, wazee wanaeleza jinsi familia za Kishona huishi pamoja na kuendeleza udumishaji wa Kishona kupitia kwa kuwafunza wanao.

**Dondoo 3**

> *"Familia zetu huishi pamoja na watoto wao hadi wanapofikia umri wa kuanza familia yao. Wakati huu wote, tunawazungumzia Kishona nyumbani. Kwa hivyo watoto wanaendelea kukua wakijua lugha yetu. Lakini wajukuu wetu ni kama wameanza kujifunza lugha ya Kiswahili kwa sababu ukiwaongelesha kwa Kishona, wanakujibu kwa Kiswahili ama wanakuangalia tu."*
>
> *Chanzo: Data ya Nyanjani*

Kutokana na dondoo la 3, ni bayana kwamba watoto wanapoishi pamoja na wazazi wao na kuzungumza lugha yao ya Kishona kila siku, huweza kujifunza lugha yao vyema na hivyo wanadumisha lugha yao. O'Riagain (1994) anasema kwamba lugha ya mama

huwa ni kipengele cha kwanza muhimu ambacho wazazi hurithisha wana wao. Hili linawezekana iwapo wazazi hawa hawajaathiriwa sana na lugha jirani kwa sababu ikiwa wameathiriwa basi huenda wakawahamisha wana wao zaidi kutoka lugha yao asilia. Naye Wolck (2004) anasema kwamba kudumisha lugha ni kuitumia kwa uaminifu wote, kurithisha vizazi vyote na kuonyesha mielekeo chanya kuhusu lugha hiyo. Haya yalibainika kupitia mahojiano na watoto kuhusu jinsi wanavyojifunza lugha yao ya Kishona inavyobainika kwenye dondoo la 4 na la 5.

**Dondoo 4**

> *"Mimi nimejifunza Kishona kupitia kuiskia nyumbani. Ninazungumziwa na wazazi wangu na babu na nyanyangu kwa Kishona na inabidi pia nijaribu kuwajibu kwa Kishona."*


**Dondoo 5**

> *"Ninaendelea kufunzwa hata sasa na wazazi wangu hasa mamangu kwa sababu wakati mwingi tuko na yeye nyumbani. Ndugu yangu pia wananiongelesha tukiwa nyumbani."*

***Chanzo: Data ya Nyanjani***.

Ni bayana kupitia kwa dondoo 4 na 5 kwamba kizazi cha tatu na cha nne katika jamiilugha ya Washona hujifunza lugha yao wakiwa katika maeneo ya nyumbani tu wakizungumziwa na wazazi wao ila hawazungumzi Kishona sanifu kwa sababu ya shinikizo kutoka lugha nyingine maarufu zinazowazunguka hasa Kiswahili. Baa-grafu 5.2 ifuatayo inaonyesha majibu ya vijana kuhusu swali waliloulizwa iwapo wanaongea Kishona kwa undani.

**Baa-grafu 5.2: Kiwango cha Umilisi wa Kishona baina ya Vijana**




Chanzo: Data ya Nyanjani

Utafiti ulilenga kubaini iwapo vijana wanazungumza lugha yao ya Kishona kwa usanifu nao wakakiri kwamba japo wanazungumziwa Kishona katika maeneo ya nyumbani, hawazungumzi lugha hiyo kwa usanifu. Asilimia 70 walikiri kwamba hawaizungumzi lugha yao kwa undani huku asilimia 30 wakikiri kwamba wanazungumza Kishona kwa undani. Hii inaonyesha kwamba japo wazee wametia bidii katika kuwarithisha wanawe lugha yao asilia, ni bayana kwamba kuna dalili za uhamaji ambazo zinaonekana kuanzia kizazi cha tatu.

Ufundishaji wa lugha asilia kutoka kizazi kimoja hadi kingine katika maeneo ya nyumbani ndio mkakati bora zaidi kuliko sheria zozote za kudumisha lugha zinazowekwa na serikali. Mkakati wa uzungumzaji wa Kishona nyumbani ambao Washona wanatumia katika kudumisha lugha yao unaendana moja kwa moja na

nadharia ya Uzalishaji Kijamii ya O'Riagain (1994) ambapo udumishaji wa lugha unategemea urithishaji wa vizazi vinavyofuata. Lugha ya mama huwa ni kipengele cha kwanza muhimu ambacho wazazi hurithisha wana wao kupitia kwa uzungumzaji. Kwa mujibu wa lengo la nne la utafiti huu, Washona wamejaribu kudumisha lugha yao ya Kishona kupitia uzungumzaji wa lugha hiyo nyumbani.

McCarty na Watahomigie (2004) wanasema kuwa udumishaji wa lugha hutegemea juhudi za kifamilia kama vile maamuzi ya lugha watakayotumia katika shughuli zote za nyumbani pamoja na juhudi za kurithisha lugha kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine. Familia, kupitia kwa wazazi, wakiamua kutumia lugha asilia katika mazungumzo yao na kwenye shughuli zao wakiwa na wanao watafaulu katika kudumisha lugha yao. Mahojiano baina ya mtafiti na wazee wa Kishona yalithibitisha kauli ya jinsi wanavyowafunza wanao Kishona kupitia kwa dondoo la 6:

**Dondoo 6**

> ***"...****Tunapofanya kazi zetu na shughuli mbalimbali nyumbani, tunatumia lugha ya Kishona kuwasungumsia watoto wetu. Shughuli kama vile mapishi, kazi zetu za mikono au tunapofanya usafi nyumbani huwa tunawasungumsia lugha ya mama. Kupitia hapo wanajifunza maneno ya lugha yetu ya Kishona."*
>
> *Chanzo: Data ya Nyanjani*

Wolck (2004) anafafanua kwamba udumishaji wa lugha unamaanisha kwamba wanajamiilugha wanafaa kutumia lugha yao vyema na katika maeneo mengi. Wolck anatambua vigezo tisa vinavyofaa katika udumishaji wa lugha na kulingana naye, kigezo kikuu katika udumishaji wa lugha ni mwendelezo wa lugha kutoka kizazi kimoja hadi kingine hasa kutoka kwa wazazi hadi kwa wanao. Utafiti wa UNESCO (2003)

unabainisha kwamba iwapo kuna pengo katika mwendelezo wa lugha, ambapo babu na nyanya wanatumia lugha yao ya kwanza kuwazungumzia wajukuu wao na pia wazazi wanatumia lugha hiyo kuwazungumzia wazazi wao ila wazazi hawa hawaitumii kwa wanawe basi hali hii inatishia uthabiti wa kiisimujamii kwa lugha na hatimaye inaweza kufa. Iwapo lugha itadumishwa, basi sharti kuwe na urithisho kutoka kwa wazazi hadi kwa wanawe kwa kila kizazi. Dondoo  la 7 linathibitisha maoni ya vijana wa Kishona kuhusu matumizi ya Kishona:

**Dondoo 7**

> *“ Kishona inazungumzwa nyumbani na kanisani. Kitambo kidogo ilikuwa inazungumzwa nyumbani tu sababu hatukuwa tumepewa uraia. Lakini siku hizi tunaizungumza hata mahali tunapofanya kazi zetu za mikono na biashara zetu na kanisani bado.”*
>
> *Chanzo: Data ya Nyanjani*

Kutokana na dondoo la 7, maeneo ya matumizi ya Kishona yameanza kupanuka hasa baada ya mwaka wa 2020, wakati ambapo Washona walipewa uraia wa Kenya na aliyekuwa Rais wa nne wa Jamhuri ya Kenya, Uhuru Kenyatta. Vijana wanataja maeneo matatu: nyumbani, Kanisani na kwenye biashara zao ambapo wanatumia lugha yao ya Kishona bila kuogopa. Hii inamaanisha kwamba lugha ya Kishona imeanza kupata nguvu mpya ya kuendelezwa.

### 5.1.2 Udumishaji wa Lugha kupitia kwa Dini


Utafiti kuhusu udumishaji wa lugha unaashiria kwamba dini ni chombo muhimu cha kudumisha lugha. (Baker 2011,  Clyne na Kipp 1999,  Clyne 2005 na  Fishman 1991, 2000). Baker (2011) anasema kwamba dini ni chombo imara cha kudumisha lugha ya waliowachache na pia waliowengi. Baker (kt.) anatoa mfano wa matumizi ya lugha ya

Kiarabu katika dini ya Kiislamu na kusema kwamba dini ya Kiislamu imechangia pakubwa udumishaji wa Kiarabu duniani kote huku dini ya Kiyuda ikichangia udumishaji wa lugha ya Kiiberania nchini Israeli. Fishman (1991), Baker (kt.), Clyne (kt.) na Benrabah (kt.) wana maoni sawa kwa kusema kwamba maandiko ya kidini kama vile Korani ya Kiisilamu yalisaidia sana kuendeleza na kudumisha lugha ya Kiarabu.

Thomason (2001) anasema kwamba, dini ilipatikana kuwa njia mojawapo ya kudumisha na kuendeleza lugha za wahamiaji katika taifa la Australia. Utafiti wake ulijikita katika makundi mawili ya wanauwililugha (Kiitaliano-Kiingereza na Kigiriki-Kiingereza) na kugundua kuwa kundi moja lilihama lugha yao ilhali lingine lilidumisha lugha yao. Kundi la wasemaji wa Kiitaliano-Kiingereza lilihama kutoka Kiitaliano hadi Kiingereza kufikia kizazi cha tatu ilhali kundi la Wagiriki-Wamarekani lilidumisha lugha yao ya Kigiriki kufikia kizazi cha nne. Sababu kuu iliyochangia kudumisha lugha ya Kigiriki ilikuwa ni ibada kwa kanisa moja la Kiothodoksi huku lugha ya Kiitaliano ikihama kwa sababu ya matumizi ya Kiingereza peke yake kupitia kwa ibada za makanisa mbalimbali.

Watafitiwa wengi wa Kishona katika vizazi vyote walikiri kwamba kanisa lao la *Gospel of God*, limekuwa kwenye mstari wa mbele katika kudumisha lugha yao. Katika Pai-chati 5.1 ifuatayo, wasailiwa wanathibitisha kwamba lugha ya Kishona inatumiwa katika ibada yao kanisani.

**Pai-chati 5.1: Matumizi ya Kishona Kanisani**




*Chanzo: Data ya nyanjani*

Wasailiwa wote, asilimia 100 walikiri kwamba lugha ya Kishona bado inatumika katika ibada. Hii inaonyesha kwamba kanisani ni eneo bora ambalo linatumika katika juhudi za kudumisha Kishona hasa katika mazingira ya wingilugha.

Clyne na Kipp (1999) walifanya utafiti kuhusu matumizi ya lugha ya Kiarabu miongoni mwa Waislamu wa Misri na wakagundua kwamba lugha ya Kiarabu ina uhusiano mkubwa na waumini wa dini ya Kiislamu kwa kuwa Korani imeandikwa kwa lugha ya Kiarabu. Matokeo ya utafiti wa Clyne na Kipp (kt.) yalibainisha kwamba waumini wa Kiislamu walifaulu katika kudumisha Kiarabu na kurithisha lugha hii kwa vizazi vyao kupitia kwa mafunzo ya kidini. Naye Gomaa (2011) alifanya utafiti kuhusu familia tatu za Kiislamu katika eneo la Durham nchini Uingereza na kutambua kwamba lugha ya Kiarabu cha Misri ilidumishwa vyema sana kupitia mafunzo ya wikendi yaliyofanywa kwenye msikiti wa chuo kikuu cha Durham kupitia kwenye mafungu ya kukariri kwa watoto wa Kiislamu.

Utafiti huu ulibainisha kwamba shughuli za ibada katika kanisa la *Gospel of God* zilikuwa zinaendeshwa kwa Kishona kutumia Biblia iliyoandikwa kwa Kishona. Baadaye ibada ilianza kutumia pia Kiswahili kwa kuwa waumini wa jamiilugha nyingine za Kenya walijiunga nao. Kupitia kwa mahojiano, watafitiwa wazee na wamama walithibitisha hili kupitia kwa dondoo la 8 na dondoo la 9 kwa kusema kwamba:

**Dondoo 8**

> *"Watoto na vijana wanaendelea kujifunza lugha ya Kishona kupitia kwa kanisani sababu ibada yetu huendeshwa kwa Kishona na kisha wakatafsiri."*

**Dondoo 9**

> *"Sisi tunajua lugha yetu pia katika sherehe mbalimbali za kanisani mwetu kwa mfano Sherehe ya Kuzaliwa kwake mwanzilishi wa kanisa letu ambayo tunasherehekea tarehe moja Oktoba kila mwaka huku tukitumia lugha ya Kishona na kutafsiri kwa lugha ya Kiswahili kwa sababu kuna wale si Washona."*

*Chanzo: Data ya Nyanjani*

Kutokana na maneno ya watafitiwa kwenye dondoo 8 na 9, ni bayana kwamba wanajamiilugha wa Kishona hujifunza lugha yao ya Kishona kupitia kwa ibada katika kanisa lao la *Gospel of God*. Lugha ya Kishona inaendelea kudumishwa kanisani kupitia mafunzo ya kidini na Biblia iliyoandikwa kwa Kishona, mahubiri, nyimbo, mikutano na mahimizano ya washiriki yanayofanywa kwa Kishona yanaendelea kufanikisha udumishaji wa Kishona. Hii inamaanisha kwamba kupitia kwa dini, lugha ya Kishona inaendelea kudumishwa.

### 5.1.3 Maandishi ya Kishona katika Dini

Uchunzaji na mahojiano na vijana yalibainisha kwamba waumini wa kanisa la *Gospel of God*, wanatumia Biblia ambayo imeandikwa kwa Kishona. Wazee wa kanisa

huhimiza waumini kusoma Biblia yao ili waweze kuelewa mambo ya dini vyema. Kupitia Biblia iliyoandikwa kwa Kishona, vijana wanapata kujifunza na kudumisha lugha yao ya Kishona. Dondoo la 10 linathibitisha haya:

**Dondoo 10**

> ***"****Ingawa sanasana tunaongea lugha za Kiswahili na Kiingereza, tumejifunza lugha yetu ya Kishona kwa sababu kanisani ndiyo lugha inayotumika sana na pia Biblia tunayosoma kanisani imeandikwa kwa Kishona."*
>
> *"Kwanza Biblia yetu tunayotumia imeandikwa kwa Kishona. Pili, asilimia 99 ya nyimbo tunazoimba kanisani ni za Kishona lakini sijaona kwenye zimeandikwa. Kuna mafunzo na sheria za kanisa pia zimeandikwa lakini ni chache sana."*

***Chanzo: Data ya Nyanjani****.*

Utafiti huu ulibainisha kwamba maandishi yaliyoandikwa kwa Kishona ni Biblia na mafunzo na sheria za kanisa lao la *Gospel of God*. Nyimbo wanazoimba wakati wa ibada hazijaandikwa kwa vitabu maalum. Hivyo utafiti uligundua kwamba uhaba wa maandishi ya Kishona unahatarisha udumishaji na uthabiti wa kiisimujamii wa Kishona.

Demos (1988) alitafitia kuhusu nafasi ya kanisa katika udumishaji wa lugha ya Kigiriki nchini Amerika. Aligundua kwamba japo kulikuwa na msukumo wa matumizi ya lugha nyingine kama vile Kiingereza katika ibada ya Waothodoksi, bado waumini walitumia lugha ya Kigiriki kwa kuwa walihusisha dini na lugha yao ya kwanza. Demos anaendelea kusema kwamba kanisa ilichukua nafasi kubwa sana katika kudumisha lugha ya Kigiriki kupitia madarasa yaliyokuwa yakifunza lugha na pia kupitia shule za Kigiriki. Vivyo hivyo, uchunzaji uliofanyika katika kanisa la watafitiwa ulibainisha kuwa lugha ya Kishona inaendelea kutumiwa licha ya shinikizo kutoka kwa lugha maarufu kama vile Kiswahili. Hii ina maana kwamba Washona wanajaribu kudumisha

lugha yao kupitia kwa maandishi yanayopatikana kanisani mwao japo ni machache. Utafiti ulibainisha uchache wa maandishi katika Kishona ambapo ni Biblia na nyimbo chache. Mkakati huu wa maandishi unafaa kupigwa jeki kupitia kwa maandishi zaidi ili vizazi vichanga vipate kujua kuandika na kusoma Kishona.

### 5.1.4 Juhudi za Wazee katika Udumishaji wa Lugha

Wazee ndio hazina ya utamaduni wa jamii ikiwemo lugha. Sangili (2019) anadai kwamba mbinu ya kudumisha lugha kupitia kwa wazee imekuwa ikitumika katika jamiilugha zinazolenga kudumisha lugha zao ulimwenguni kote. Obiero na Matu (2013) walitafitia udumishaji na ufufuaji wa lugha ya Kisuba ambayo ilikuwa imeanza kudidimia. Obiero na mwenzake waligundua kwamba wazee walijisatiti sana katika harakati za kufufua na kudumisha lugha yao kwa kuwa walipewa nafasi katika redio ya Kisuba iliyoanzishwa kwa minajili ya kuwafundisha Wasuba lugha yao. Wazee pia walikuwa kwenye mstari wa mbele ili kuhakikisha serikali imefanikisha juhudi za udumishaji wa lugha yao kando na kuwafunza wanawe kwenye maeneo ya nyumbani. Utafiti huu ulibainisha kwamba wazee wametia juhudi kubwa katika kudumisha lugha yao. Maoni ya wazee yanathibitisha haya kupitia dondoo 11.

**Dondoo 11**

> ***“****Tumejaribu kudumisha lugha yetu kwa miaka isitini sasa hata kama kulikuwako na changamoto tulipata kama vile za utambulisho ambazo zingetufanya kusahau lugha yetu. Lakini lugha ya Kishona ndio kitu tu tulibaki nayo ya muhimu tulipoishi bila stakabadhi za uraia nchini Kenya.”*
>
> *Chanzo: Data ya Nyanjani.*

Kupitia kwa kushiriki katika shughuli mbalimbali za Washona na mahojiano na wazee wa Kishona, ilibainika kwamba Wazee wa Kishona wamekuwa katika mstari wa mbele

katika udumishaji wa lugha yao. Wanatumia mbinu nyingi kama vile kuzungumzia wanao pamoja na wajukuu wao lugha yao asilia, kufunza vizazi vipya lugha yao asilia na kuweka mikakati ya kudumisha lugha hasa matumizi yake katika maeneo yao ya ibada. Wazee wa Kishona wanasema kwamba, lugha yao ni utamaduni wao na kwamba ndicho kitu pekee cha thamana walichokuwa nacho kwa muda wote ambao walikuwa bila uraia. Kuzungumza lugha yao kuliwaletea faraja moyoni na matumaini ya kuishi nchini Kenya ambako hawakuwa na jamaa wala uraia. Katika kanisa la *Gospel of God*, lugha iliyokuwa inatumika mwanzoni ilikuwa ni Kishona mara nyingi, kadri miaka iliposonga, waumini wasiokuwa wa Kishona walianza kujiunga na kanisa hili na hivyo ikabidi Kiswahili itumike pia. Hadi sasa, mahubiri hufanyika kwa Kishona huku yakitafsiriwa kwa Kiswahili.

### 5.1.5 Udumishaji wa Lugha kupitia Ndoa za Ndani na Ndoa za Nje ya Jamii

Maoni ya (Baker, 2011; Clyne & Kipp 1999; Clyne, 2005; Holmes, 2013; Namei, 2012) kuhusu lugha za wanajamii waliohamia nchi au mahali fulani yanathibitisha kwamba mpangilio wa ndoa za wanajamii hao unaweza kuendeleza udumishaji wa lugha ama ukafanya lugha asili kuhama au kufa. Athari za ndoa kwa lugha asilia zaweza kuwa chanya kupitia ndoa za ndani au hasi kupitia ndoa za nje ya jamii. Holmes(kt.) na Namei(kt.) wanadai kwamba ndoa za nje ya jamii ni njia mojawapo ya lugha kupoteza uthabiti wake na hatimaye kufa. Hali hii hutokea hasa lugha moja inapopewa hadhi ya juu na majukumu mengi kuliko lugha nyingine katika jamii. Mahojiano na wazee yalidhihirisha jinsi ndoa za nje na ndoa za ndani ya jamii zinaendeleza Kishona kupitia kwa dondoo la 12.

**Dondoo 12**

> ***Mtafiti:*** *Je,kuna watu ambao si Washona lakini wanajua lugha ya Kishona?*
>
> ***"****Wako lakini si wengi sana. Kwanza kuna wale walishaolewa na Washona wetu, hao wamejifunza lugha ya mume na wanaizungumza vizuri. Pili, kuna marafiki wetu ambao wamejifunza kwa kupenda tu. Tatu, Lugha yetu inaendelezwa pia kwa kuwa Washona wanapooa Washona wenziwe, lugha inazidi kudumishwa baina ya Washona na Washona."*
>
> *Chanzo: Data ya Nyanjani.*

Ni bayana kwamba ndoa za ndani na ndoa za nje ya jamii hufanya wanajamiilugha kuongezeka na hivyo lugha yaweza kuwa thabiti kwa kuwa wazungumzaji wameongezeka. Kwa upande mwingine, ndoa za nje ya jamii zinaweza kupunguza uthabiti wa lugha kupitia kupunguka kwa idadi ya wazungumzaji. Utafiti huu uligundua kwamba si Washona wengi ambao wameoa kutoka jamiilugha nyingine na pia wasichana wengi kutoka jamiilugha ya Washona hawajaolewa na wanajamiilugha wengine. Hii inamaanisha kwamba lugha ya Kishona inadumishwa baina ya Washona pekee yao. Baker (2011) anasema kwamba katika jamii ya wingilugha, ndoa baina ya wanawingilugha kutoka jamiilugha ya wachache na mwanalugha mmoja tu kutoka kwa jamiilugha ya waliowengi inaweza kupelekea watoto wao kuzungumza lugha ya wanajamiilugha waliowengi huku wakiacha lugha ya mzazi wao anayetoka katika jamiilugha ya waliowachache. Baadhi ya Washona pia wameoa au kuolewa na watu wasiokuwa wazungumzaji wa Kishona. Jambo hili linachangia kupunguka kwa uthabiti wa kiisimujamii wa Kishona. Mahojiano na wazee wa Kishona yanathibitisha haya kupitia kwa Dondoo la 13.

**Dondoo 13**

> ***Mtafiti:*** *... je, ndoa imeathiri lugha ya Kishona vipi tena?*
>
> ***Mzee I:*** *kuna wasichana wetu wameolewa watu ambao si Washona. Wameenda na kujifunza lugha ya nje. Kwa njia hii, wazungumzaji wa lugha ya Kishona hupungua na kufanya lugha yetu kuwa hatarini. Lakini kuna wale ambao sisi tumewaoa na si Washona. Hao ni wachache ambao wamejifunza lugha yetu.*
>
> *Chanzo: Data ya Nyanjani*

Dondoo hili la 13 linathibitisha kwamba lugha ya Kishona ipo kwenye hatari ya kupotea iwapo ndoa baina ya wanajamiilugha Washona na wanajamiilugha wengine itaendelea. Sensa ya mwaka wa 2016 nchini Australia ilionyesha kwamba uhamiaji kwenda kwa lugha ya Kiingereza ulikuwa wa hali ya juu kwenye kizazi cha pili katika ndoanje, (Australian Bureau of Statistics, ABS, 2016) na Namei (2012). Namei alitoa mfano wa watoto wa familia za Malta, Ujerumani na Uholanzi na kusema kwamba watoto hawa walikuwa hawatumii lugha ya wazazi wao kwa kuwa walikuwa wameshahamia lugha ya Kiingereza ilhali watoto Wagiriki na Waitaliano walidumisha lugha yao kwa muda. Naye Holmes (2013) akagundua kwamba wahamiaji Wagiriki na Wachina hawakujihusisha na ndoanje hali ambayo ilirahisisha udumishaji wa lugha zao.

Utafiti ulibainisha kwamba Washona wameweka sheria kali za kulinda jinsi vijana huchagua wachumba wao, lakini bado kuna baadhi ya vijana ambao wamekiuka na kuoa ama kuolewa nje ya jamiilugha ya Kishona. Kundi hili la ndoanje, kulingana na wazee wa Kishona, huhatarisha lugha yao ya Kishona kwa kuwa wanaenda na kujifunza lugha ya jamiilugha nyingine huku wakiacha lugha yao ya Kishona.

### 5.1.6 Kutembeleana miongoni mwa Washona

Stoessel (2002) anadai kwamba mitandao ya kijamii huwa na ushawishi mkubwa katika udumishaji wa lugha asilia. Stoessel anasema kwamba wahamiaji hujaribu kudumisha lugha yao na wanapozungumza na wenzao mitandaoni, muda unavyosonga, wao huanza kuwa na mitandao yao wenyewe kwa ajili ya kudumisha lugha yao. Wahamiaji hawa huanza kutembeleana ama kuwa na mikutano mbalimbali kwa ajili ya kuzungumza lugha yao asilia. Hali hii hufanya lugha yao kudumu kwa kuwa kila wanapokutana wao hutumia lugha yao ya kwanza ili kuonyesha undugu.

Washona walipofika Kenya walikuwa wachache na kitu kimoja kilichowaleta pamoja wakati wote ni kutembeleana, kuongea na kudumisha lugha yao asilia. Baada ya kupewa uraia nchini Kenya mwishoni mwa Disemba mwaka wa 2020, Washona walipata uhuru wa kuishi kila sehemu ya Kenya hasa mitaa mbalimbali jijini Nairobi. Hata hivyo, Washona wanaendelea kutembeleana ili kudumisha umoja na ushirikiano wao. Kila wanapokutana, lugha wanayotumia katika mazungumzo yao ni Kishona ili kuonyesha umoja na ushirikiano wao inavyodhihirika katika dondoo la 14.

**Dondoo 14**

> *“Mimi humtembelea mamangu siku mbili kwa wiki ili kumsalimia. Hata kama mimi na mke wangu na watoto wangu wawili tunaishi mbali kiasi, huwa namtembelea mama kwa kuwa huko tutaongea lugha yetu. Pia mimi humtembelea Zeph pale alikohamia Kitengela mara kwa mara ili kumsalimia na pia kujua zaidi lugha yetu.”*

*Chanzo: Data ya nyanjani.*

Utafiti ulibainisha kwamba Washona hutembeleana wao kwa wao ili kuendelea kuzungumza lugha yao ya Kishona na kuidumisha. Maneno ya vijana yanathibitisha hii

mbinu ya udumishaji kupitia kwa kutembeleana. Utafiti wa Michieka (2012) uliolenga wanafunzi wa vyuo vikuu kuhusu umuhimu wa kutembeleana, ulithibitisha kwamba kutembeleana ni mkakati mzuri wa kudumisha lugha zao za kiasili kwa kuwa wanapotembeleana wakiwa likizoni, wao huzungumza kwa lugha zao za kiasili badala ya Kiswahili, Kiingereza na Sheng' wanavyofanya wakiwa chuoni.

Landweer (2000), Milroy (1987) na Chambers na Natalie (2013) wanasema kwamba mtandao wa kijamii huwa imara wakati ambapo wanajamiilugha huwa na uhusiano wa karibu kupitia kwa kutembeleana. Katika mazingira ya mashambani, mtandao wa kijamii huwa imara sana kwa sababu ya mipangilio ya makazi yao, kutohamahama na pia mahusiano ya kifamilia na kiukoo. Hali hii huzuia shinikizo la kubadilika kwa lugha kwa sababu ya athari ya lugha nyingine.

Wanajamiilugha wanavyozidi kukaa pamoja katika mitandao yao ya kijamii, lugha yao huzidi kuimarika kwa kuwa wanaiendeleza kupitia mazungumzo ya kila siku. Mtandao wa kijamii pia huimarishwa kupitia kutembeleana na hivyo basi lugha huzidi kudumishwa kupitia kwa matumizi ya kila siku ya lugha asilia, Hildebrandt (2004), Nonaka (2009), Ehala (2010) na Sallabank (2010). Washona walipofika Kenya kuanzia mwishoni mwa miaka ya 1950, waliishi karibu karibu ili kuwa na ulinzi wa wao kwa wao. Wazee wanathibitisha haya kupitia kwa dondoo la 15:

**Dondoo 15**

> *"Tulipofika Kenya kwa mara ya kwanza, nilikuwa mdogo wa miaka kama kumi na tatu hivi, tulianza kwa kukaa kule ngong' mtaa unaoitwa Zambia. Watu walikuwa wanatuita Wazambia kwa kuwa hawakuelewa kuwa sisi ni Wazimbabwe. Baada ya uhuru kupatikana hapa Kenya, mambo yalianza kubadilika tukawa hatuna uhuru tena bila vibali rasmi vya Kenya. Ndio maana tulikuwa tunakaa karibukaribu ili mmoja wetu akipata shida, tuweze kusaidiana. Pia kukaa karibu karibu ilitusaidia kwa kuwa hatungejulikana kwa urahisi kwamba sisi si Wakenya kwa wakati huo. Si kama sasa ambapo sisi ni raia halisi wa Kenya."*
>
> *Chanzo: Data ya Nyanjani*

Kutokana na maneno ya wazee, ni bayana kwamba Washona walianza kwa kukaa pamoja ili kutembeleana iwe rahisi. Kule kukaa karibu karibu kuliwasaidia kudumisha lugha yao kwa kuwa wangekutana kwa haraka sana. Landweer (2000) na Nonaka (2009) wanasema kwamba mtandao wa kijamii wa jamiilugha ukiwa mzuri, huwa wanakutana kila siku na kuongea lugha yao. Hali hii huchangia kudumisha lugha ya jamiilugha husika. Kwa mujibu wa lengo la nne la utafiti huu, mkakati wa kutembeleana umesaidia katika kudumisha Kishona kwa kuwa kila wakati Washona wanapotembeleana, wao huzungumza lugha yao ya Kishona.

### 5.1.7 Mikutano ya Kijamii

Van Aswegen (2008) alitafitia udumishaji na uhamaji wa lugha miongoni mwa Wamaale nchini Ethiopia na kutambua kuwa mikutano ya kijamii ilikuwa mojawapo ya mbinu za kudumisha lugha ya Kimaale cha Ethiopia. Kutokana na utafiti wake, ilibainika kwamba Wamaale walikuwa wakifanya kazi za pamoja (kikoa), waliunda mashirika yao ya wakulima na kisha wakawa na mashindano ya michezo ya kijamii kwa ajili ya kukutana pamoja kila wakati. Shughuli hizi zote za kuwaleta pamoja zilisaidia katika kudumisha na kuendeleza lugha yao. Dondoo la 16 lifuatalo

linathibitisha kwamba Washona pia huwa na mikutano yao mbalimbali na kupitia kwayo, wanadumisha Kishona.

**Dondoo 16**

> ***Mtafiti:*** *Je huwa mnafanya mikutano ya kijamii? Mnatumia lugha gani?*
>
> ***Mama I****: Naam. Huwa tuna mikutano mbalimbali ya kijamii kwa shughuli mbalimbali. Kwanza mikutano mingi tuliyokuwa nayo kabla ya mwaka wa 2020 ilikuwa ya kuweka mikakati ya kupewa uraia. Hapo, tulikuwa tunatumia lugha ya Kishona kwa kuwa sisi ndiyo tulikuwa na shida hapa nchini. Lakini wakati tulikuwa na wasio Washona, tulikuwa tunatumia Kiswahili kwa sababu hawajui Kishona.*
>
> ***Mtafiti:****Mikutano mingine ni ipi?*
>
> ***Mzee II:*** *Siku ya kanisa, huwa tunakutana mapema kabla ya ibada kuanza sisi kama wazee ili kuunda mikakati ya kupata hela za maendeleo Kanisani. Tunapokutana hivyo, tunazungumza lugha ya Kishona pekee. Hali hii imechangia kuendeleza lugha yetu ya Kishona.*
>
> *Chanzo: Data ya Nyanjani*

Kutokana na dondoo la 16, mikutano ya shughuli mbalimbali kama vile kanisani na harakati za kutafuta uraia nchini Kenya kabla ya mwaka wa 2020, ilisaidia wanajamiilugha wa Kishona kudumisha lugha yao kwa kuwa kila walipokutana, walitumia Kishona kuwasiliana ama kwa ajili ya ibada kanisani.

McDuling na Barnes (2012) walitafitia udumishaji wa lugha ya Kigiriki nchini Afrika Kusini baina ya wanafunzi wa vyuo vikuu nchini humo na kugundua kwamba Wagiriki walikuwa na mikutano ya sherehe tofauti za kijamii  kama vile harusi na densi za vilabuni kwa minajili ya  kukutana na kuzungumza lugha yao. McDuling na Barnes (kt.) waligundua kwamba wanafunzi wengi walijihusisha na hafla tofauti za chuoni kupitia michezo ya kuigiza ya Kigiriki, mavazi na vyakula, ibada na mikutano ya jinsia

ya wanafunzi wa Kigiriki nchini Afrika Kusini. Mikutano hii yote ililenga kuendeleza na kudumisha lugha ya Kigiriki.

Mbinu ya uchunzaji ilibainisha kwamba Washona wanapokutana hasa mikutano ya kanisani, wazee kuanzia umri wa 46 kuendelea, huongea wakitumia Kishona licha yao kujua na kuelewa Kiswahili, watu wa kati ya umri wa miaka 36-45, huongea wakitumia lugha ya Kiswahili kwa mara nyingi. Wanatumia Kishona wanapoongea na wazee au wazazi wao. Vijana wa kati ya umri wa 18-35 huongea wakitumia Kiswahili na mara moja moja hutumia Kishona katika mazungumzo yao. Watoto wa kati ya umri wa miaka 1-17, huongea wakitumia Kiswahili pekee yake. Hata wakizungumziwa kwa Kishona, wao hujibu kwa Kiswahili. Hii inamaanisha kwamba japo Washona wamejaribu kudumisha lugha yao kwa miongo sita, kizazi cha nne (miaka 1-17) wameanza kuhama kutoka kwa Kishona. Hali hii inahatarisha Kishona kwa kuwa hapo ndio mwanzo wa kuhama kwa Kishona kwa sababu kizazi hiki (miaka 1-17) hawatajua lugha yao asilia. Hii inamaanisha pia kwamba vizazi vitakavyofuata havitakuwa na ujuzi wa Kishona.

### 5.1.8 Sherehe Mbalimbali za Washona

Sherehe mbalimbali za kitamaduni na za kidini katika jamiilugha fulani huchangia pakubwa udumishaji wa lugha hiyo kwa kuwa lugha na utamaduni haviwezi kutenganishwa. Utafiti wa Kedrebéogo (1998) nchini Bukinafaso ulibainisha kwamba katika maeneo ya Mashariki mwa Bukinafaso, jamiilugha za wachache wanachukulia lugha zao kama utamaduni wao na hivyo wanazithamini sana. Watafitiwa walikuwa na kauli kwamba '*mwanajamiilugha kamili haachi lugha aliyonyonya.'* Hii inamaanisha

kwamba uaminifu katika matumizi ya lugha ya kwanza ni jukumu la kila mmoja katika shughuli za udumishaji wa lugha. Mahojiano kupitia kwa dondoo la 17 yanabainisha udumishaji wa Kishona kupitia kwa sherehe mbalimbali.

**Dondoo 17**

> **Mtafiti:** *Mama, maoni yako kuhusu kuendeleza lugha ya Kishona ni yepi?*
> ***Mama 1****: "Sisi tunajua lugha yetu pia katika sherehe mbalimbali za kanisani mwetu kwa mfano Sherehe ya Kuzaliwa kwake mwanzilishi wa kanisa letu ambayo tunasherehekea tarehe moja Oktoba kila mwaka huku tukitumia lugha ya Kishona na kutafsiri kwa lugha ya Kiswahili kwa sababu kuna wale si Washona"*
> ***Mtafiti:*** *Nani atatuelezea kuhusu Sherehe za Kishona na lugha zinazotumika*
> ***Mzee wa I****: Sisi huwa na sherehe tatu muhimu. Sherehe zetu zimeshikamanishwa na dini yetu kupitia kwa kanisa letu la Gospel of God. Sherehe ya kwanza ni sherehe ya kuzaliwa(kubarwa) kwa mtoto ambapo mtoto akizaliwa, huwa mama na mwanawe hawaonani na mtu yeyote nje ya familia yake isipokuwa mfanyakazi wake. Baada ya siku nane, sherehe kubwa ya kumpa mtoto jina ambalo ni lazima kutoka kwa ukoo wa babake tu, hufanyika. Katika sherehe hizi, Ni lugha ya Kishona tu ambayo hutumika kwa kuwa lugha ya Kishona ni sehemu ya utamaduni wetu..*
> ***Mzee wa II:*** *Sherehe ingine, sherehe ya harusi kati ya Washona pekee yao(muchato), lugha ya Kishona tu hutumika katika shughuli zote na hatua zote. Lakini siku hizi tunatumia pia hata lugha ya Kiswahili sababu tumekuwa na marafiki wengi ambao si Washona kwa hivyo inabidi tutumie lugha ambayo wanaelewa.*
>
> ***Mzee wa III:*** *Sherehe ya mazishi(namu), sisi hutumia lugha mbili kwa kuwa kutakuwa na wageni ambao si Washona wanaohudhuria mazishi...*
> *Chanzo: Data ya Nyanjani*

Mahojiano na wazee wa Kishona yalibainisha kwamba, Washona huwa na sherehe tatu muhimu kwa maisha ya binadamu. Walisema kwamba Sherehe zao zimeshikamanishwa na dini yao kupitia kwa kanisa lao la *Gospel of God*. Sherehe ya kwanza ni sherehe ya kuzaliwa kwa mtoto (*kubarwa*) ambapo mtoto akizaliwa, huwa mama na mwanawe hawaonani na mtu yeyote nje ya familia yake isipokuwa mfanyakazi wake. Baada ya

siku nane, sherehe kubwa ya kumpa mtoto jina ambalo ni sharti liwe kutoka kwa ukoo wa babake tu, hufanyika. Katika sherehe hizi, Ni Kishona tu hutumika kwa kuwa lugha ya Kishona ni sehemu ya utamaduni wa Kishona. Sherehe ya pili, sherehe ya harusi kati ya Washona pekee yao (*muchato*) ama ndoa za ndani ya jamii ambapo ni lugha ya Kishona tu hutumika katika shughuli zote na hatua zote zinazoandamana na ndoa hiyo. Sherehe ya mwisho ambayo ni ya mazishi (*namu*), lugha mbili hutumika kwa kuwa kunaweza kuwa na wageni ambao si Washona wanaohudhuria mazishi. Ilibainika kwamba Kiswahili ni lugha maarufu katika sherehe zote za Washona. Aidha kuna sherehe ya Kumkumbuka mwanzilishi wa kanisa la *Gospel of God* nabii Johanne Masowe. Sherehe hii hufanyika tarehe 1 Oktoba ya kila mwaka. Sherehe hii ilihudhuriwa na mtafiti na wasaidizi wake na wakagundua kwamba lugha mbili hutumika: Kishona na Kiswahili. Kishona hutumika kwa sababu ni utamaduni wao na Kiswahili hutumika kwa kuwa ni lugha maarufu na rasmi nchini Kenya na pia kwa sababu kuna waumini ambao si wa Kishona katika kanisa hilo.

## 5.2 Hitimisho

Katika sura hii, utafiti umeshughulikia mikakati mbalimbali iliyowekwa na Washona ili kudumisha lugha yao ya Kishona. Ilibainika kwamba Washona wa umri mkubwa kuanzia miaka 46 kuendelea (wazee) huwazungumzia wanawe na wajukuu wao Kishona ili waweze kujifunza lugha hii ambayo ni sehemu ya utamaduni wao. Ilibainika kwamba dini yao, kupitia kwa kanisa la *Gospel of God*, ni mahali bora pia pa kujifunza na kuendeleza Kishona kwa kuwa ibada yao huendeshwa kwa Kishona huku ikitafsiriwa kwa Kiswahili. Wazee pia wameweka juhudi kubwa katika kudumisha

Kishona kupitia kwa kuwarithisha watoto wao Kishona. Ilibainika pia kwamba lugha ya Kishona imedumishwa kupitia kwa ndoa za ndani na za nje ya jamii kwa kuwa Mshona anapooa mtu ambaye si Mshona, idadi ya wazungumzaji wa Kishona inaongezeka. Lakini pia ilidhihirika kwamba ndoa za nje ya jamii zinaweza kuhatarisha Kishona kwa kuwa mwanajamiilugha wa Kishona anapoolewa na mtu ambaye si Mshona, anajifunza lugha ya wanajamiilugha nyingine huku akiacha lugha yake.

Mikakati mingine iliyowekwa na Washona katika kudumisha Kishona ni kutembeleana kwa Washona ili wadumishe lugha yao kupitia kwa mazungumzo, mikutano ya Kijamii pamoja na sherehe mbalimbali za kitamaduni. Kwa hivyo lengo la nne la utafiti huu lilitimia kwa kuwa Washona wameonyesha mikakati mbalimbali ya kudumisha lugha yao japo kizazi cha nne (mwaka 1-17) kimeanza kuhama kutoka lugha ya Kishona hadi lugha maarufu ya Kiswahili. Sura inayofuata inashughulikia muhtasari wa kila sura, matokeo ya utafiti, hitimisho la utafiti na mapendekezo pamoja na mchango wa utafiti huu.

# SURA YA SITA: MUHTASARI, MATOKEO, MAPENDEKEZO, MCHANGO NA HITIMISHO

## 6.0 Utangulizi

Utafiti huu ulishughulikia athari za Kiswahili na Kikuyu kwa uthabiti wa kiisimujamii wa Kishona nchini Kenya. Athari mbalimbali zinazotokea kwa lugha fulani kama vile wingilugha, ukopaji maneno, ubadilishaji msimbo, mabadiliko ya lugha na mielekeo mbalimbali ya lugha huja kwa sababu ya mtagusano na lugha hizo mbalimbali katika jamii ya wingilugha. Wanajamiilugha wakiwa na mielekeo chanya kwa lugha fulani, wanakuwa na sababu mbalimbali za kuitumia lugha hiyo katika maeneo mbalimbali ya kijamii.

Muhtasari wa utafiti umetolewa kuanzia sura ya kwanza hadi sura ya mwisho ili kuonyesha athari mbalimbali za Kiswahili na Kikuyu kwa Kishona, sababu mbalimbali za kutumia Kiswahili, Kikuyu na Kishona katika jamii, mielekeo ya Washona kuhusu Kiswahili na Kikuyu na pia mikakati mbalimbali ya kudumisha Kishona nchini Kenya. Sura hii pia imetoa matokeo ya utafiti yaliyopatikana baada ya kuchunguza malengo yote ya utafiti na kuzingatia nadharia mbili zilizotumika kwenye utafiti huu. Mapendekezo mbalimbali yametolewa ili kusaidia katika kuinua viwango vya uthabiti wa kiisimujamii wa Kishona nchini Kenya na kuiepusha na hatari ya kuangamia. Muhtasari wa kila sura unashughulikiwa kwanza.

## 6.1 Muhtasari

Sura ya kwanza ilishughulikia usuli wa mada na swala la utafiti. Malengo manne ya utafiti huu yalitajwa ili kubainisha mwelekeo kamili wa utafiti huu moja kwa moja.

Malengo haya ni pamoja na kubainisha athari za mtagusano wa Kiswahili na Kikuyu kwa Kishona, kuchunguza sababu zinazopelekea Washona kutumia Kiswahili na Kikuyu katika maeneo yao ya kijamii, kudhihirisha mielekeo ya Washona kuhusu Kiswahili na Kikuyu na kubainisha iwapo Washona wamefaulu kudumisha lugha yao asilia ya Kishona nchini Kenya au la.

Nadharia mbili zilizoongoza utafiti huu katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data ili kutimiza malengo manne ya utafiti ziliangaziwa. Nadharia ya Uthabiti wa Kiisimujamii wa Lugha iliyoanzishwa na Giles, Bourhis na Taylor mwaka wa 1977 na kuendelezwa na Landweer (2000), ilishughulikia mambo mbalimbali yanayofanya jamiilugha husika kukaa pamoja na kuendeleza lugha yao katika mazingira ya wingilugha. Wataalamu wa nadharia hii walisema kwamba uthabiti wa lugha yoyote hutegemea mambo matatu ambayo ni hadhi ya lugha husika katika jamii, demografia ya wanajamiilugha husika na usaidizi wa taasisi za kiserikali kuhusu lugha husika. Nadharia ya Uthabiti wa Kiisimujamii wa lugha imejikita kwenye mihimili minane inayofafanua matumizi ya lugha katika jamii na ambayo ilisaidia utafiti huu katika kutimiza malengo matatu ya kwanza. Kwa kuwa utafiti huu ulikuwa na malengo manne, nadharia ya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ilishirikiana na nadharia ya uzalishaji wa kijamii ili kutimiza malengo yote manne ya utafiti huu.

Nadharia ya pili ya Uzalishaji wa Kijamii iliyoanzishwa na Bourdieu (1977) na kuendelezwa na O’Riagain (1994) ilitumika katika kushughulikia lengo la nne la utafiti lililoshughulikia mbinu mbalimbali za kudumisha Kishona kwenye mazingira ya wingilugha nchini Kenya. Nadharia hii ilikuwa na mihimili miwili. Mhimili wa kwanza

ulishughulikia jinsi ambavyo kila kizazi huweka mikakati ya kurithisha kizazi kinachofuata utamaduni wake ikiwemo lugha. Mhimili wa pili wa nadharia hii ulishughulikia athari mbalimbali za mtagusano lugha moja na nyingine kwa kushirikiana na nadharia ya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha.

Mbinu zilizotumika katika ukusanyaji data za utafiti nyanjani zilikuwa hojaji, mahojiano, mijadala ya kimakundi, uchunzaji na kushiriki katika shughuli mbalimbali za Washona ili kuchunguza na kutimiza mahitaji ya malengo manne ya utafiti huu. Utafiti huu uliteua mitaa mitano ya Kaunti ya Kiambu ambayo ni makazi ya jamii ya Washona. Mitaa hii ni Kinoo, Kikuyu, Kiambaa, Gitaru na Githurai ambayo pia inapakana na jiji la Nairobi linalojulikana kwa wingilugha. Data ilikusanywa kutoka kwa wahusika wa umri wote kwa kuwa mtafiti alilenga kubainisha ikiwa lugha ya Kishona imeathiriwa na Kiswahili na Kikuyu kwenye vizazi tofauti vya jamiilugha ya Washona.

Sura ya pili ilishughulikia mapitio ya maandishi kuhusu mtagusano wa Kiswahili na Kikuyu kwa Kishona na athari zake. Athari kama vile ubadilishaji msimbo, ukopaji wa maneno, wingilugha na mabadiliko ya lugha ziliangaziwa kwa undani ili kuweka wazi mada ya utafiti. Maandishi mbalimbali kuhusu udumishaji wa lugha yalipekuliwa ili kujenga utafiti huu. Maandishi kuhusu hali ya lugha duniani na barani Afrika yalipitiwa huku hali ya Washona, utamaduni wao, uchumi wao, makazi yao, dini yao na tafiti mbalimbali kuwahusu zikipekuliwa ili kupata picha halisi ya kuwepo kwao nchini Kenya. Kwenye sura hii, maandishi yalipekuliwa kuhusu Kiswahili na Kikuyu na mielekeo ya Kiswahili nchini Kenya. Uthabiti wa kiisimujamii wa lugha pamoja na

vigezo mbalimbali vya kupima uthabiti wa kiisimujamii wa lugha vilijadiliwa kutokana na utafiti wa UNESCO (2003). Ilibainika kwamba kuna vigezo sita vinavyopima uthabiti wa kiisimujamii wa lugha katika jamii.

Sura ya tatu ilihusu uchanganuzi wa data iliyohusiana na athari mbalimbali za Kiswahili na Kikuyu kwa Kishona. Data ilikusanywa kupitia kwa mahojiano na hojaji ambapo watafitiwa wa umri wote walipewa na kuelekezwa jinsi ya kujaza. Data iliwasilishwa kupitia kwa majedwali, baa-grafu na pai-chati ambazo zilionyesha majibu ya watafitiwa kuhusu matumizi mbalimbali ya lugha na hali mbalimbali za matumizi ya Kiswahili, Kishona na Kikuyu. Uchanganuzi ulilenga kubainisha athari zinazoonekana kwa Kishona kufuatia mtagusano na Kiswahili na Kikuyu. Ilibainika kutoka kwa baa-grafu 3.2, jedwali 3.3 na 3.4 kwamba Washona wameathirika na Kiswahili kupitia kwa ukopaji wa maneno na ubadilishaji wa msimbo na kuipea lugha ya Kiswahili hadhi ya juu katika matumizi mbalimbali ya kijamii kuliko lugha za Kishona na Kikuyu.

Utafiti uligundua kwamba lugha ya Kiswahili ina matumizi mengi katika jamii kwa sababu ni lugha maarufu, ni lugha rasmi, ni lugha ya taifa na ni lugha ya masomoni. Ilibainika kwamba Washona ni wanawingilugha (Taz.baa-grafu 3.12) kwa sababu ya kutagusana na jamiilugha mbalimbali katika makazi yao. Ilidhihirika kwamba lugha ya Kishona imeanza kubadilika hasa kwa watafitiwa watoto kwa kuwa wanatumia Kiswahili katika maeneo ya nyumbani (baa-grafu 3.9). Ilidhihirika pia kwamba lugha ya Kishona inatumika tu katika maeneo ya nyumbani na kwenye ibada katika kanisa la *Gospel of God* ambalo watafitiwa huabudia. Lugha ya Kikuyu haitumiwi sana na

Washona kwa kuwa kulingana nao, lugha hii haina manufaa mengi isipokuwa ujirani na kwenye biashara.

Sura ya nne ilijumlisha lengo la pili na lengo la tatu la utafiti huu. Lengo la pili lilifafanua sababu mbalimbali za kutumia Kiswahili, Kikuyu na Kishona katika maeneo mbalimbali ya jamii ya Washona kupitia kwa uchunzaji, mahojiano na mijadala ya kimakundi. Data ya nyanjani ilibainisha kwamba Washona wana sababu tisa za kutumia Kiswahili katika maeneo wanamoishi, Sababu tano za kutumia Kikuyu kwa baadhi ya Washona na sababu tano za kutumia Kishona katika mitaa wanamoishi.

Lengo la tatu lilishughulikiwa pia kwenye sura hii ya nne na lilidhihirisha mielekeo ya Washona katika matumizi ya Kiswahili na Kikuyu. Utafiti huu ulipima mielekeo ya Washona kuhusu Kiswahili na Kikuyu kwa kutumia upimaji usio wa moja kwa moja ili kupata data ya kuaminika anavyosema Baker (1992). Ilidhihirika kwamba Washona wana mielekeo chanya kuhusu Kiswahili kuliko Kikuyu kupitia kwa matumizi ya lugha kwenye maeneo mbalimbali ya kijamii na pia kwenye shughuli tofauti za kijamii. Lugha ya Kiswahili ilipendelewa katika shughuli rasmi, mazungumzo na viongozi wa kijiji, kwenye mazungumzo baina ya marafiki, kwenye biashara na pia kwenye masomo. Utafiti ulibainisha kwamba Washona wanatumia Kiswahili kwa hiari tu bila kulazimishwa kwa kuwa walikuwa na mielekeo chanya kuhusu lugha hii.

Katika sura ya tano, mikakati mbalimbali ya udumishaji wa Kishona ilishughulikiwa. Mbinu ya mahojiano na uchunzaji pamoja na mijadala ya vikundi vidogo vidogo zilitumika ili kukusanya data iliyochanganuliwa katika sura ya tano. Ilibainika kwamba Washona wameweka mikakati mbalimbali ya kudumisha Kishona kama vile kutumia

lugha yao katika maeneo ya nyumbani, kwenye ibada, kutembeleana, katika sherehe mbalimbali za kitamaduni na wazee kufunza kizazi kichanga lugha ya Kishona. Ilibainika pia kwamba watoto wa umri wa miaka kumi na saba kuja chini hawatumii Kishona kama inavyotarajiwa, jambo ambalo linaonyesha mwanzo wa mabadiliko ya Kishona. Ilibainika kwamba wazee ndio walio na juhudi kubwa katika kudumisha Kishona.

## 6.2 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga kuchunguza athari za Kiswahili na Kikuyu kwa uthabiti wa kiisimujamii wa Kishona nchini Kenya na kubainisha sababu zinazowafanya Washona kutumia Kiswahili na Kikuyu kwenye maeneo yao katika jamii. Vilevile, utafiti huu ulilenga kuweka wazi mielekeo waliyonayo Washona kuhusu Kiswahili na Kikuyu na pia mikakati waliyonayo katika kudumisha lugha yao ya Kishona licha ya shinikizo kutoka lugha maarufu nchini Kenya. Utafiti huu ulikuwa na matokeo mbalimbali.

### 6.2.1 Athari za Kiswahili na Kikuyu kwa Kishona

Lengo la kwanza lilikuwa kubainisha athari za mtagusano wa Kiswahili na Kikuyu kwa Kishona. Katika kuchunguza haya, mbinu za uchunzaji, kushiriki, mahojiano, mijadala ya vikundi vidogo vidogo na hojaji zilitumika. Matokeo yalibainisha kuwa Washona hukopa maneno ya Kiswahili na kuyatumia wanapozungumza lugha yao ya Kishona hasa vijana ambao ndio hupenda kutalii lugha mbalimbali wanavyosema Kerswill na Williams (2000). Ilibainika pia kwamba Washona hasa vijana hubadilisha msimbo wanapoongea, kwa sababu ya mtagusano na lugha za Kiswahili na Kikuyu. Ilibainika pia kwamba lugha ya Kiswahili imepewa majukumu mengi katika jamii wanamoishi

wanajamiilugha wa Kishona. Lugha ya Kishona ina matumizi machache ambapo inatumika tu katika maeneo ya nyumbani na kanisani ambapo bado lugha ya Kiswahili inatumika. Kwenye shughuli za biashara, elimu na kujitafutia na kupata riziki, wanajamiilugha wa Kishona walipendelea kutumia Kiswahili kuliko Kishona na Kikuyu. Hii inamaanisha kwamba lugha ya Kiswahili imepewa hadhi ya juu kuliko lugha za Kishona na Kikuyu katika jamii wanamoishi wanajamiilugha wa Kishona. Hali hii inadhihirisha kwamba Washona ni wanawingilugha. Utafiti uligundua pia kwamba lugha ya Kishona imeanza kuhama hasa kwa watoto wa Kishona kwa kuwa wazazi wao hawawazungumzii kwa Kishona na pia kwa sababu ya mtagusano na lugha ya Kiswahili. Hivyo basi kwa ujumla, ilibainika kwamba lugha ya Kishona imeathirika na mtagusano lugha ya Kiswahili.

### 6.2.2 Sababu za Washona Kutumia Kiswahili na Kikuyu

Lengo la pili lilikuwa linachunguza sababu za washona za kutumia Kiswahili na Kikuyu kwenye maeneo yao ya kijamii. Mbinu za uchunzaji, mijadala ya kimakundi na mahojiano zilitumika ili kukusanya data inayohusiana na lengo hilo.

Ilidhihirika kwamba sababu kuu ya kutumia Kiswahili ni kwamba ni lugha rasmi ya taifa la Kenya ambayo ina wazungumzaji wengi nchini Kenya, Afrika Mashariki na siku hizi ni lugha ya Kimataifa. Sababu nyingine ni kwamba Kiswahili ni mojawapo ya somo ambalo hufunzwa kuanzia chekechea hadi vyuo vikuu nchini. Washona pia wanatumia Kiswahili na Kikuyu kwa mawasiliano na wanajamiilugha wengine wanaowazunguka na pia kwa sababu ni lugha inayowaunganisha na kurahisisha utangamano. Pia, Washona walijifunza Kiswahili na Kikuyu ili kuimarisha nafasi ya

kujipatia riziki na pia kujitambulisha na wenyeji wa jamiilugha za Kenya. Kabla ya kupewa uraia wa Kenya mwaka wa 2020, Washona walitumia Kiswahili kwa usalama wao na pia kueneza injili kwa kuwa ndilo lengo kuu lililowaleta nchini Kenya. Kwa hivyo, ilidhihirika kwamba Washona wana sababu kadha wa kadha zinazowapelekea kutumia Kiswahili na Kikuyu katika maeneo yao ya kijamii.

### 6.2.3 Mielekeo ya Washona kuhusu Matumizi ya Kiswahili na Kikuyu Nchini Kenya

Uchunguzi wa lengo la tatu la utafiti huu ulidhihirisha kwamba mielekeo ya Washona katika matumizi ya Kiswahili ni chanya. Utafiti huu ulitumia mbinu zisizo za moja kwa moja ili kujua mielekeo ya Washona kuhusu matumizi ya Kiswahili na Kikuyu. Hojaji za kuchunguza matumizi ya lugha kwenye maeneo mbalimbali zilitumika pamoja na mijadala ya kimakundi ili kubainisha mielekeo ya Washona kuhusu Kiswahili na Kikuyu.

Kwenye shughuli rasmi kama vile masomoni, Wanajamiilugha walipendelea kutumia Kiswahili kuliko Kishona na Kikuyu. Walitoa sababu kwamba Kiswahili ni lugha ya taifa la Kenya na ni lugha rasmi ambayo imekubalika kufunzwa kama mojawapo ya somo kuanzia shule za chekechea hadi vyuo vikuu nchini Kenya na pia kutumika kwenye mikutano rasmi.

Shughuli nyingine kama vile kwenye biashara, kuzungumza na viongozi wa kijijini, kuzungumza na marafiki na katika burudani, ilidhihirika kwamba Kiswahili inapendelewa sana kuliko lugha nyingine kwa kuwa Washona wanaitumia lugha hii kwa hiari bila dalili ya kulazimishwa. Kutotumiwa kwa Kishona kwenye shughuli

mbalimbali za jamii ni ishara tosha kwamba lugha ya Kishona imeanza kuhama. Hali hii ilidhihirika kwa watafitiwa watoto ambao hawapendelei kuzungumza Kishona katika mazingira ya nyumbani.

### 6.2.4 Udumishaji wa Kishona Nchini Kenya

Mwisho, lengo la nne lilikuwa la kubainisha iwapo Washona wamefaulu kudumisha lugha yao asilia nchini Kenya au la. Data ilikusanywa kupitia kwa hojaji, mijadala ya kimakundi, uchunzaji, kushiriki na mahojiano kwa wanajamiilugha wa Kishona kwenye mitaa wanamoishi na sehemu ya ibada ambayo ni kanisa la *Gospel of God*. Matokeo yalibainisha kwamba Washona huzungumza lugha yao wakiwa katika mazingira ya nyumbani na kwenye kanisa lao la *Gospel of God* ambapo wanatumia Kishona huku ikitafsiriwa kwa Kiswahili kwa waumini ambao si Washona. Ilidhihirika kwamba Washona hutembeleana ili kuzungumza lugha yao, huitumia lugha yao kwenye sherehe mbalimbali za kitamaduni na wazee kuwafundisha watoto lugha ya Kishona. Ilibainika pia kwamba, licha ya juhudi hizi za kudumisha lugha yao, Washona wa Kenya hawajaandika vitabu vya hadithi kwa lugha yao ya Kishona. Kwenye maandishi, Biblia tu na nyimbo chache ndizo zimeandikwa kwa Kishona. Kutokana na haya, Ilibainika kuwa hata kama kuna shinikizo kutoka kwa lugha maarufu zinazowazunguka, Washona wamejitahidi kupitia kwa mikakati mbalimbali ya kudumisha lugha yao hasa baada ya kupewa utambulisho wa kuwa Wakenya mwaka wa 2020 ila wanafaa kuhifadhi lugha hii kwa njia ya maandishi na pia kuwarithisha kizazi cha nne ambacho ni kuanzia miaka 1-17.

### 6.3 Mapendekezo

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, ni bayana kwamba lugha ya Kishona imeanza kuathiriwa na Kiswahili na Kikuyu nchini Kenya. Hivyo basi utafiti huu unatoa mapendekezo ya kuinua viwango vya uthabiti wa kiisimujamii wa Kishona nchini Kenya kwa kuwa ni mojawapo ya lugha za Kenya zilizo kwenye hatari ya kuangamia.

#### 6.3.1 Kuinua Viwango vya Uthabiti wa Kiisimujamii wa Kishona

Kuimarisha uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ni shughuli nzima ya kijamii ambapo wanajamii wanatakikana kulivalia swala hilo njuga kwa pamoja. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kwamba Kiswahili ndiyo lugha inayotumiwa sana katika shughuli nyingi za kijamii. Hivyo basi pendekezo la kwanza ni kuwa Washona wanastahili kushughulikia lugha yao kwa kuitumia katika shughuli nyingi za kijamii kama vile kwenye burudani, kuongea na viongozi wao, watoto wahimizwe kuizungumza wakiwa katika michezo yao na wakiwa nje ya shule ili kuinua viwango vya uthabiti wa lugha yao. Wazazi pia wanahimizwa kubuni nyimbo za watoto kwa Kishona ili kuwavutia watoto kwa minajili ya kujifunza Kishona. Hii ni kwa sababu ilibainika kwamba kizazi cha nne(mwaka 1-17), hawatumii Kishona kwenye maeneo yao ya nyumbani. Hivyo basi Washona watumie mkakati wa uzungumzaji wa Kishona katika maeneo mengine na maeneo ya nyumbani ili watoto wajifunze lugha hii.

Lugha inayodumu ni lugha ya maandishi. Utafiti ulibainisha kwamba lugha ya Kishona haina maandishi isipokuwa kwa Biblia, nyimbo za injili ambazo si zote zimeandikwa na kanuni za kanisa la *Gospel of God* ambazo pia hazijaandikwa kikamilifu. Hivyo basi ili lugha ya Kishona idumu na ikumbukwe kwa vizazi vijavyo, juhudi za kuandikwa kwa

vitabu hasa vya hadithi lazima ziwekwe ili vizazi vichanga vipate kusoma kwa lugha yao ya Kishona. Vijana Washona wanahimizwa waweze kuanza kuandika vitabu kama vile vitabu vya hadithi za watoto ili kujikumbusha na kudumisha lugha yao na pia kuwafunza watoto wao. Hili linawezekana iwapo mashirika ya kuchapisha vitabu yanaweza kuwasaidia vijana katika kuchapisha na pia wanajamiilugha wa Kishona waandae mashindano ya uandishi wa Kishona ili kuwapa vijana moyo wa kujua kuandika lugha yao.

Uthabiti wa kiisimujamii wa lugha pia huimarika kupitia mtandao thabiti wa jamiilugha husika. Milroy (1987) anasema kwamba mtandao imara hasa kwenye mazingira ya mijini, husaidia katika kudumisha lugha asilia. Washona wanahimizwa kutilia maanani mtandao wao wa kijamii hasa baada ya kupewa uraia wa Kenya. Kupewa uraia kuliwapa ruhusa ya kuishi mahali popote wanapendelea nchini Kenya, hali ambayo imewafanya Washona kuanza kutawanyika kutoka makazi yao ya muda mrefu (Kikuyu, Kinoo, Kiambaa, Gitaru na Githurai). Hali hii itafanya mtandao wao kuwa hafifu na hivyo basi, itahatarisha juhudi zao za kudumisha lugha yao. Mtandao hafifu, hupelekea kupunguka kwa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha inayohusika, Milroy(kt.). Hivyo basi utafiti huu unapendekeza kuwa Washona waongeze juhudi za kutembeleana au waongeze juhudi kwenye matumizi ya mikutano ya mitandaoni kama vile matumizi ya simu na pia wadumishe mtandao wao wa kijamii ili kuendeleza lugha yao ya Kishona.

### 6.3.2 Juhudi za Serikali katika Kuinua Uthabiti wa Kiisimujamii wa Kishona

Jambo lingine la kuinua viwango vya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ni usaidizi wa asasi za kiserikali wanavyosema Fishman (1991), Yamamoto (1998) na Crystal (2002).

Utafiti huu uligundua kwamba asasi ya pekee ambayo imekuwa ikiwasaidia wanajamiilugha wa Kishona kuendeleza lugha yao ni kupitia kanisa lao la *Gospel of God* na katika maeneo ya nyumbani tu. Hivyo basi pendekezo la utafiti huu ni kwamba serikali kupitia kwa asasi zake kama vile huduma mbalimbali, elimu, afya na usalama katika jamii wanamoishi Washona zihusishe Kishona ili Washona wapate motisha ya kuendeleza lugha yao.

Ushirikiano na nchi ya Zimbabwe unafaa kuimarishwa. Hii ni kwa sababu, Kishona cha Zimbabwe hutumiwa hata shuleni na huzungumzwa na watu takribani millioni tisa. Hii inamaanisha kwamba uthabiti wa kiisimujamii wa Kishona ni imara nchini humo. Hivyo basi, Pendekezo la utafiti huu ni kwamba serikali ya Kenya itafute msaada kutoka nchi ya Zimbabwe katika juhudi za kuimarisha Kishona cha Kenya. Serikali pia ianzishe kuwatuma wanafunzi wa Kishona nchini Zimbabwe ili waweze kujifunza na kufanya utafiti zaidi kuhusu Kishona na mwisho Washona waweke juhudi za kushirikiana na Washona wa Zimbabwe mitandaoni ili waendeleze Kishona cha Kenya.

Pendekezo lingine ni kwamba kwa kuwa serikali ya Kenya imetambua Kishona kuwa ni lugha mojawapo ya lugha asilia, utafiti unapendekeza serikali itumie taasisi mbalimbali za kudumisha lugha hizi za wachache ili ziweze kudumu inavyopendekezwa na shirika la UNESCO (2003) na Landweer (2000).

### 6.3.3 Tafiti za Baadaye kuhusu Kishona

Utafiti huu unapendekeza watafiti wa baadaye kuzamia athari za Kiswahili na Kikuyu kwa viwango vingine vya lugha kama vile kifonetiki, kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia na kisemantiki. Hali kadhalika, watafiti wengine wanaweza kuchunguza

vipengele vya fasihi na umuhimu wake katika kudumisha Kishona na pia wanaweza kuchunguza sosholojia ya Kishona nchini Kenya.

**6.4 Mchango wa Utafiti**

Baada ya kukusanya data, kuichanganua na hatimaye kuonyesha matokeo, tasnifu hii imetoa mchango kwa taaluma ya Isimujamii katika eneo la mtagusano lugha hasa katika eneo la udumishaji na uhuishaji wa lugha zilizo na idadi ndogo ya wazungumzaji.

Kwa jumla, utafiti huu umetoa mchango wa kiisimujamii kwa kuweka bayana hali ya kiisimujamii ya Kishona nchini Kenya. Utafiti huu umebainisha kwamba Washona wanaoishi nchini Kenya wana asili yao nchini Zimbabwe na walihamia Kenya miaka ya 1950 kwa lengo kuu la kueneza injili kupitia kwa dini yao ya *Gospel of God* (Taz 2.6.2.1). Idadi ya Washona wanaoishi Kenya ni ndogo (kuanzia 2500) na kwa miaka hii yote, wametangamana na lugha asilia na maarufu za Kenya kama vile Kiswahili na Kikuyu zinazowapa shinikizo la kuihama lugha yao asilia ya Kishona.

Licha ya shinikizo hili la muda mrefu kutoka kwa lugha maarufu nchini Kenya kama vile Kiswahili na Kikuyu, utafiti huu umeweza kuthibitisha wazi kuwa, Washona nchini Kenya bado wanaizungumza lugha yao ya Kishona katika maeneo machache ya kijamii kama vile nyumbani, kanisani (dini), sherehe za kitamaduni na mikutano ya kijamii. Matokeo haya basi, yanaashiria wazi kuwa Washona nchini Kenya wameweza kuidumisha na kuihuisha lugha yao na basi kuweza kuiepusha na hatari ya kuangamia.

Utafiti huu basi unatoa mchango kwa kuonyesha mikakati mbalimbali inayotumiwa na Washona nchini Kenya ili kuidumisha na kuihuisha lugha yao. Mikakati hii inaweza kutumiwa na wanaisimujamii wengine katika harakati za kudumisha na kuhuisha lugha

nyingine zilizo na idadi ndogo ya wazungumzaji nchini Kenya na zilizo katika hatari ya kuangamia pindi zinavyozidi kutagusana na lugha nyingine maarufu kama vile Kiswahili, Kikuyu, Kiingereza n.k. Lugha hizi zilizo katika hatari ya kuangamia hapa nchini Kenya ni kama vile Suba, Terik, El molo, Rendile Ogiek, Boni, Burji, Bong'om na Njemps.

Lugha hizi zinaweza kuwa zile asilia nchini Kenya au zilizo na asili ya kigeni zinazokumbwa na shinikizo kutoka kwa lugha maarufu nchini Kenya. Hali hii basi inaziweka katika msururu wa lugha zilizokabiliwa na tishio la kuangamia pindi miaka inavyosonga. Basi utafiti huu ni kichocheo mwafaka kwa wanaisimujamii nchini Kenya kuanzisha harakati za kuzidumisha na kuzihuisha lugha kama hizi.

**6.5 Hitimisho**

Utafiti huu uliangazia athari za Kiswahili na Kikuyu kwa uthabiti wa Kiisimujamii wa Kishona nchini Kenya. Uthabiti wa kiisimujamii wa lugha hutegemea viashiria vitatu: hadhi ya lugha husika, demografia ya wanajamiilugha na usaidizi au juhudi za taasisi za kiserikali kama vile kwenye elimu, huduma mbalimbali za serikali, dini na vyombo vya habari. Uthabiti wa jamiilugha pia hutegemea juhudi za jamii husika za kurithisha vizazi vyake utamaduni wake ikiwemo lugha yao. Lugha ya Kishona imepambana na shinikizo kutoka lugha maarufu za Kiswahili na Kikuyu na ilibainika kwamba, japo Kishona kimeathiriwa na lugha hizi maarufu, Washona wamejaribu kudumisha lugha yao japo kuna mabadiliko mbalimbali hasa kuanzia kizazi cha nne.

Utafiti ulibainisha kwamba mtagusano wa Kishona, Kiswahili na Kikuyu ndiyo sababu kuu ya kuathirika kwa Kishona na hatimaye kupunguka kwa uthabiti wake wa

kiisimujamii hasa kwenye kizazi cha nne. Kwenye maeneo mengi wanamoishi Washona, lugha maarufu zinazozungumzwa ni Kiswahili na Kikuyu. Hivyo basi, lugha hizi zina matumizi mengi kuliko Kishona. Jambo hili limehatarisha Kishona kwa kuwa athari zilizoshuhudiwa ni ukopaji wa maneno, ubadilishaji msimbo, wingilugha, kushuka kwa uthabiti wa kiisimujamii wa Kishona na mabadiliko yake.

Vilevile, utafiti huu ulibainisha kwamba Washona wana sababu nyingi za kutumia Kiswahili na baadhi yao wana sababu za kutumia Kikuyu. Ilibainika kwamba Washona wanatumia Kiswahili katika masomo kwa viwango mbalimbali vya elimu. Ilibainika kwamba Washona wanatumia Kiswahili kwa sababu ni lugha rasmi na lugha ya taifa la Kenya, Afrika Mashariki na pia lugha ya kimataifa. Lugha ya Kiswahili hutumika kwa sababu ya mazungumzo na mawasiliano, kuimarisha mahusiano na kuunganisha Washona na wanajamiilugha wengine nchini Kenya. Ilibainika kwamba Washona pia wanatumia Kiswahili kwa sababu ya kujitafutia na kurahisisha utafutaji wa riziki na pia walitumia Kiswahili ili kueneza injili kupitia kwa kanisa lao la *Gospel of God* lililoko *Valley road* jijini Nairobi. Washona Walitumia Kiswahili kwa usalama wao kabla ya kupata uraia wao mwaka wa 2020. Utafiti uligundua kwamba baadhi ya Washona wanatumia Kikuyu kwa sababu za kibiashara, kwa sababu ni lugha maarufu kwenye kaunti ya Kiambu, kushiriki kwenye sherehe za kitamaduni za Wakikuyu na pia kwa sababu ya mawasiliano.

Hali kadhalika, utafiti huu ulidhihirisha mielekeo ya Washona kuhusu Kiswahili na Kikuyu. Ilibainika kwamba Washona wana mielekeo chanya kwa Kiswahili kwa sababu ya umaarufu wake na pia matumizi mengi katika maeneo wanamoishi. Ilibainika pia

kwamba baadhi ya Washona wana mielekeo chanya kwa lugha ya Kikuyu kwa sababu Wakikuyu ndiyo waliowakaribisha na kuwapa makao walipofika Kenya kwa mara ya kwanza. Ilibainika pia kwamba baadhi ya Washona wana mielekeo chanya kwa Kikuyu kwa sababu ni lugha ya biashara na matumizi mengine katika jamii.

Hatimaye, utafiti ulibainisha kwamba Washona wamedumisha lugha yao ya Kishona licha ya shinikizo kutoka Kiswahili na Kikuyu. Ilibainika kwamba Washona hasa wale walio na umri mkubwa wameweka mikakati mingi ya kudumisha lugha yao. Kwanza, mkakati wa uzungumzaji wa lugha nyumbani ambapo wazee wanawazungumzia wanawe ili waweze kufahamu Kishona. Washona pia hutumia Kishona katika ibada yao kanisani na pia wazee wametia juhudi kubwa katika kudumisha lugha yao. Washona pia wamejitahidi kudumisha lugha yao kupitia ndoa za ndani na za nje ya jamiilugha ya Kishona. Hali kadhalika, wao hutembeleana ili kuzungumza lugha asilia na pia wanadumisha lugha yao kupitia sherehe mbalimbali kama vile kuzaliwa na kupewa jina kwa watoto, harusi au sherehe za mazishi.

**MAREJELEO**

Abelson, R., Frey, K. na Gregg, A. (2004). *Experiments with people: Revelations from Social Psychology*. Mahwah, N.J: Lawrence Erlbaum.

Agoya, C. (2012). The Role of Indigenous Languages in Kenya: A Case for Using Them as Languages of Instruction Throughout Primary School. *The University of Nairobi Journal of Language and Linguistics*, Vol. 2 (2012), 89-105

Akello, O. (2021, july 28). Shona Community Finally Becomes Kenyans six decades later. *The Star*. https://www.the-star.co.ke/news/2021-07-28

Al-Khatib, M. & Alzoubi, A. (2009). The impact of sect-affiliation on dialect and cultural maintenance among the Druze of Jordan: An exploratory study. *Glossa*, *4*(2), 186–219

Allport, G. W. (1954). *The Nature of Prejudice*. Cambridge, MA: Perseus Books.

Al-Nahar, R. (2009). Language maintenance among the Armenians of Jordan. *Unpublished MA thesis), MEU, Amman: Jordan*.

Amatubi, M.N. (2002). “Globalization and the mainstreaming of Kiswahili research in the 21st Century” Utafiti wa Kiswahili pp. 43 – 48.

Ang’iela, D. O. (2002). Literacy, attitudes and language revitalization. In Owino, F.R (ed) *Speaking African: African Languages for Education and Development.* Cape Town: CASAS Book Series pp 200-216.

Appel, R., na Muysken, P. (2005). *Language contact and bilingualism*. Amsterdam University Press.

Aswegen, J. (2008). *Language Maintenance and Shift in Ethiopia: The Case of Maale.* University of South Africa: Tasnifu ya Uzamili.

Auer, P. na Wei L. (2009). Code-switching/mixing. *The SAGE handbook of sociolinguistics*, 460-478.

Austin, J.L. (1962). *How to do things with Words*. Oxford. Oxford University Press

Babusa, H. (2019). Ukopaji wa Lugha: Etimolojia na Mabadiliko ya Maana na Utamkaji wa Msamiati wa Kiarabu katika Kiswahili. *International Journal of Advanced Research*.

Batibo, H. M. (2005). *Language Decline and Death in Africa. Causes, Consequences and challenges*, Toronto: Multilingual Matters Ltd.

Baker, C. (1992). Attitudes and language. Clevedon, UK: Multilingual Matters.

Baker, C. (2011). Foundations of Bilingual Education and Bilingualism. Bilingual Education & Bilingualism. *Multilingual Matters*.

Barasa, S. (2016). Spoken code-switching in written form? Manifestation of code-switching in computer mediated communication. *Journal of Language Contact*, *9*(1), 49-70.

Bartram, B. (2010). Attitudes to modern foreign language learning. *Attitudes to Modern Foreign Language Learning*, 1-208.

Benrabah, M. (2004). Language and politics in Algeria. *Nationalism and ethnic politics*, *10*(1), 59-78.

Best, W. na Kahn, J. (2010). *Research in Education*, New Jersey U.S.A: Person Prentice.

Bhatia, T. K., na Ritchie, W. C. (2004). The bilingual mind and linguistic creativity. *Journal of Creative Communications*, *3*(1), 5-21.

Bichang'a, W. N (2019) "Language Shift or Maintainance? A Sociolinguistic Analysis of the Ilwana Language of Tana River County," *Les Cahiers d'Afrique de l'Est*/The East African Review[online],53|2019 URL:http://journals.openedition.org/eastafrica/839;DOI:https://doi.org/10.4000eastafrica.839

Blythe, R. na Croft, W. (2012). S-Curves and the Mechanisms of Propagation. Language Change. *Language*, Volume 88, Number 2, June 2012, Pp. 269-304 imesomwa Disemba, 2021.

Bourdieu, P. (1977). Cultural reproduction and social reproduction. In *Knowledge, education, and cultural change* (pp. 71-112). Routledge.

Bourdillon, M. F. (1976). *The Shona peoples: An ethnography of the contemporary Shona, with special reference to their religion* (Vol. 1). Mambo press.

Bourhis, Y., Giles, H., na Rosenthal, D. (1981). Notes on the construction of a 'subjective vitality questionnaire' for ethnolinguistic groups. *Journal of Multilingual and Multicultural Development*, *2*(2), 145–155.

Buliba, A. Njogu, K. na Mwihaki, A. (2006). *Isimu Jamii kwa Wanafunzi wa Kiswahili*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Campbell, R. N., & Schnell, S. (1987). Language conservation. *The annals of the American academy of political and social science*, *490*(1), 177-185.

Chakrani, B. (2011). Covert language attitudes: A new outlook on the sociolinguistic space of Morocco. In *Selected proceedings of the 40th annual conference on African linguistics* (Vol. 11, pp. 168-177). Somerville: Cascadilla Proceedings Project.

Chambers, J. na Natalie, S. (2013) *The Handbook of Language Variation and Change* (ed) Malaysia: Ho printing (M) Sdn Bhd.

Chambers, J. na Jack, K. **(**1995**)**. *Sociolinguistic theory: Linguistic variation and its social significance*. Oxford: Blackwell.

Charo, F. K., & Ong'onda, A. N. (2022). Language Maintenance Mechanisms of Kigiriama Language in Ganze Sub-County, Kilifi County, Kenya.

Clément, R., na Norton, B. (2021). Ethnolinguistic vitality, identity and power: Investment in SLA. *Journal of Language and Social Psychology*, *40*(1), 154-171.

Clyne, M. (2003). Towards a more language-centred approach to plurilingualism. *Multilingual Matters*, 43-55.

Clyne, M., & Kipp, S. (1999). Pluricentric Languages in an Immigrant Context: Spanish, Arabic and Chinese.

Clyne, M. (2005). *Australia's language potential*. University of New South Wales Press.

Clyne, M., & Kipp, S. (2011). *Pluricentric languages in an immigrant context: Spanish, Arabic and Chinese* (Vol. 82). Walter de Gruyter.

Cook, V. J. (2010). The relationship between first and second language acquisition revisited. *The Continuum companion to second language acquisition*, 137-157.

Crystal, D. (1997). *English as a global language*. Cambridge university press.

Crystal, D. (2002). *Language death*. Cambridge University Press.

Danver, S. L. (2015). *Native peoples of the world: An encyclopedia of groups, cultures and contemporary issues*. Routledge.

Demos, V. (1988). Ethnic mother-tongue maintenance among Greek Orthodox Americans. *International journal of the sociology of language*, (69), 59-71.

Denzin, K. na Lincoln, Y. (2011). *The SAGE Handbook of Qualitative Research*. U.S.A: SAGE Publication, Inc.

Department of Culture and Language for elders and Youth (2014). Translation policy. government of Nunavut. http://www.gov.nu.ca imesomwa 2023.

Duran, L. (2005). Toward a better understanding of code switching and interlanguage in bilinguality: Implications for bilingual instruction. *The journal of educational issues of language minority students*, *14*(2), 69-88.

Dweik, B. S., Nofal, M. Y., na Qawasmeh, R. S. (2014). Language use and language attitudes among the Muslim Arabs of Vancouver/Canada: A sociolinguistic study. *International Journal of Linguistics and Communication*, *2*(2), 75-99.

Dweik, B. and Al-Obaidi, T.(2014). Language contact, use and attitudes among the Chaldo-Assyrians of Baghdad, Iraq: A sociolinguistic study. *Journal of Advances in Linguistics*. 3 (3), 219-232.

Ehala, M. (2010). Ethnolinguistic vitality and intergroup processes1. *Multilingual*, *29*, 203221.

Extra, G., & Yağmur, K. (Eds.). (2004). *Urban multilingualism in Europe: Immigrant minority languages at home and school* (Vol. 130). Multilingual Matters.

Faltis, C. J. (1989). Code- switching and bilingual schooling: An examination of Jacobson's new concurrent approach. *Journal of multilingual & multicultural development*, *10*(2), 117-127.

Fang, F. G. (2017). English as a lingua franca: Implications for pedagogy and assessment. *TEFLIN*, *28*(1).

Fasold, R. W. (1984). *The sociolinguistics of society*. Oxford, UK and Cambridge

Fasold, R. W., & Connor-Linton, J. (Eds.). (2014). *An introduction to language and linguistics*. Cambridge university press.

Fishman, J. A., & Haugen, E. (1966). Language loyalty in the United States: the

maintenance and perpetuation of non-English mother tongues by American ethnic and religious groups. *Ianua linguarum/Series maior*, *21*.

Fishman, J. (1991). *Reversing Language Shift: Theoretical and Empirical Foundations of Assistance to Threatened Languages.* Clevedon: Multilingual Matters Ltd.

Fishman J.(1989). "*Language and Ethnicity in minority sociolinguistic perspective" Multilingual Matters*. Philadelphia: Clevedon.

Fishman, J. (1972b). Domains and the relationship between micro- and macro-sociolinguistics. In John J Gumperz & Dell Hymes (eds.), *Directions in sociolinguistics: The ethnography of communication,* 435-453. New York: Holt, Rinehart and Winston.

Fishman, J. A. (2000). Language planning for the "other Jewish languages" in Israel: An agenda for the beginning of the 21st century. *Language Problems and Language Planning*, *24*(3), 215-231.

Florian, L. (1998) ' Inclusive practice: what, why and how?' in C. Tilstone, L. Florian and R. Rose (eds) *Promoting Inclusive Practice*. London: Routledge.

Fraenkel, J. and Wallen, N. (2006). How to design and evaluate research in education. (6th ed). Boston: McGraw-Hill.

Garrett, P. (2010). *Attitudes to Language*. Cambridge, UK: Cambridge University Press.

Garrett, P., Coupland, N. na Williams, A. (2003) *Investigating Language Attitudes: Social Meanings of Dialect, Ethnicity and Performance*. Cardiff: University of Wales Press.

Giles, H., Taylor, D. M., na Bourhis, R. Y. (1977). Dimensions of Welsh identity. *European Journal of Social Psychology*, *7*(2), 165-174.

Ginting, S. A. (2018). Language Attitude of Sellers in Traditional Market toward Karonese Language. *English Language Teaching*, *11*(7), 125-130.

Githaiga, H. (2022, June 7). Uganda finally adopts Kiswahili as Official language. *The East African Standard*

Githiora, C. (2002), Sheng: Peer Language, Swahili Dialect or Emerging Creole? In: *Journal of African Cultural Studies*, 15, 2, 159-181.

Gomaa, Y. A. (2011). Language maintenance and transmission: The case of Egyptian Arabic in Durham, UK. *International Journal of English Linguistics*, *1*(1), 46.

Gordon J, R. G. (2005). Ethnologue, languages of the world. http://www.ethnologue.com/

Government of Kenya (GoK) (2010). The Constitution of Kenya 2010. Nairobi: Government Printer.

Greenberg, J. H. (1963). African linguistic classification. *General history of Africa*, *1*, 113-121.

Grimes, E. (2009) Indigenous languages in education: What the research Actually Shows. Darwin: Australia.

Grosjean, F. (1982). *Life with two languages: An introduction to bilingualism*. Harvard University Press.

Gumperz, J. J. (1964). Linguistic and social interaction in two communities. *American anthropologist*, *66*(6), 137-153.

Gumperz, J. J. (1976). Language, communication, and public negotiation. In *Anthropology and the public interest* (pp. 273-292). Academic Press.

Habwe, J. H., na Karanja, P. (2004). Misingi ya sarufi ya Kiswahili.

Hachipola, S. J. (1998). A survey of the minority languages of Zimbabwe. University of Zimbabwe Publications, Mount Pleasant, Harare, Zimbabwe.

Hamde, K.(2005). Blin Language Maintenance, Shift and Revitalization: A Study on Language, Culture and Identity. First Conference on Blin Language and Culture in London, 14-16:5

Haugen, E. (1953). The ecology of language. *The ecolinguistics reader: Language, ecology and environment*, 57-66.

Heine, B. (1992). Language Policies in Africa. In: R. Herbert (ed.*), Language and Society in Africa. The Theory and Practice of Sociolinguistics*, pp. 23–35. Cape Town: Witwatersrand University Press.

Hidalgo, M. (1986). Language contact, language loyalty, and language prejudice on the Mexican border. *Language in society*, *15*(2), 193-220.

Hildebrandt, K. A. (2004). A grammar and glossary of the Manange language. In *Tibeto-Burman languages of Nepal: Manange and Sherpa*. Pacific Linguistics.

Holmes, J. (2001). *An introduction to sociolinguistics.* New York; Harlow, Eng: Longman.

Holmes, J., & Wilson, N. (2013). *An introduction to sociolinguistics*. Routledge.

Hymes, D. (1975). Speech and language. *World Englishes: Critical Concepts in Linguistics*, *5*, 154.

Iseke, J. M. (2013). Negotiating Métis culture in Michif: disrupting Indigenous language shift. *Decolonization: Indigeneity, Education & Society*, *2*(2).

Janghorban, R.,Latinejad, R., na Taghipour, A. (2013). Pilot study in Qualitative Research: The roles and Values. *Hayat journal of School of Nursing and Midwifery*. Tehran University of medical sciences. 2013;19(4):1-5

Kalantizis, M. (1985). Community languages: Politics or pedagogy? *Australian Review of Applied Linguistics. Series S*, *2*(1), 168-179.

Kalmanlehto, I. (2014). *Mixed domains and multilingual practices-an ethnographic study of Tanzanian university students language use* (Master's thesis).

Kamau, S. (2015) *Taathira za kiswahili na lugha nyingine kwa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha za mama mijini Nairobi, Kiambu na Thika*. Chuo kikuu cha Kenyatta.Tasnifu ya Uzamifu

Kame, G. (2012). Multilingualism in African Nation States: Stepping Stones or Stumbling Blocks for Development. *Americas*, *1*, 14-5.

Kedrebeogo, G. (1998). Language maintenance and language shift in Burkina Faso: The case of the Koromba.

Kenya Human Rights Commission (KHRC). 2019. African Missionaries in Identity Limbo: The Shona People of Kenya. *KHRC* https://www.khrc.or.ke/publications/221-african-missionaries-in-identity-limbo-the-shona-of-kenya/file.html

Kerswill, P. and Williams, A. (2000). Creating a new town koine: Children and

language change in Milton Keynes. *Language in society*, *29*(1), 65-115.

Khadidja, B. (2013). Language of Blood: Language of Love. Sage Publication.

Kibui, A. W. (2014). Language policy in Kenya and the New Constitution for Vision 2030. *International Journal of Educational Science and Research*, *4*(5), 89-98.

Kimemia, J. N. (2002). *Language, Curriculum Processes, and Emerging Issues in Education*. New Era International.

King, K. A. (2022). 21 Researching Multilingualism and Language Education across Borders and over Decades. *Multilingualism and Education: Researchers' Pathways and Perspectives*, 176.

King'ei, K. G. (2010). *Misingi ya isimujamii*. Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kloss, H. (1966). Types of multilingual communities: A discussion of ten variables. *Sociological Inquiry*, *36*(2), 135-145.

Kombo, D. na Tromp, D**.** (2006). *Proposal and Thesis Writing: An Intoduction*. Nairobi. Paulines Publications Afrika.

Kothari, C. R. (2004). Research methodology: Methods and Techniques (2nd ed.). New Delhi: New Age International Limited Publishers. Krauss, M. (1992). ‘The World’s Languages in Crisis. *Language* 68:4-10

Kwak, S., & You, S. H. (2019). Analysis of Koreans' Overt and Covert Language Attitudes towards Jeju Dialect. *Speech and Language Therapist*, *29*, 26-54.

Landweer, L.(2000). Indicators of Ethno Linguistic Vitality’. Notes on Sociolinguistics pg 5 – 22 [ Online:http//www.s.l. org /socialx/ndg-lg-indicators.html]

Lee, J. S. (2002). The Korean language in America: The role of cultural identity in heritage language learning. *Language culture and curriculum*, *15*(2), 117-133.

Letsholo, R. (2009). Language maintenance or shift? Attitudes of Bakalanga youth towards their mother tongue. *International Journal of Bilingual Education and Bilingualism*, *12*(5), 581-595.

Lune, H., Pumar, E. S., na Koppel, R. (Eds.). (2010). *Perspectives in Social Research Methods and Analysis: a reader for sociology*. Sage.

Machakanja, I. (2006). *Conceptual metaphors in English and Shona: A cross-linguistic and cross-cultural study* (Doctoral dissertation, University of South Africa).

Maho, J. F. (2009). The linear ordering of TAM/NEG markers in the Bantu languages. *Kula and Marten (eds.)*, 213-225.

Malechova, M. (2016) Multilingualism as a Sociolinguistic Contact Phenomenon With Regard to Current Forms of Multilingual Communication: Codeswitching as One of The Contemporary Communication Trends. *Informatologia*,*49*(1-2), 86-93. Retrieved from http://hreak.srce.hr/161904

Malik, T. G. (1994). Lexical Borrowing: A Study of Punjabi and Urdu Kinship Terms. *Language in India*, *10*(8).

Mathiot, M., na Garvin, P. L. (1968). The functions of language: a sociocultural view. *Anthropological Quarterly*, 148-156.

Mathooko, P. (2007). *Isimu Jamii: Misingi na Nadharia*. Nairobi: Njigua Books.

Maya, R. (2009). *Language Shift and the Speech Community: Sociolinguistic Change in a Garifuna Community in Belize*: PhD Dissertation University of Pennsylvania.

Mberia, K. (2014). The place of indigenous languages in African development. *Language*, *2*, L2.

McCarty, T. L., na Watahomigie, L. J. (2004). Language and literacy in American Indian and Alaska Native communities. In *Sociocultural contexts of language and literacy* (pp. 89-120). Routledge.

McDuling, A., na Barnes, L. (2012). What is the future of Greek in South Africa? Language shift and maintenance in the Greek community of Johannesburg. *Language Matters*, *43*(2), 166-183.

Mekacha, R. (2011). Isimujamii: Nadharia na Muktadha wa Kiswahili. Dar Es Salaam: TUKI

Mhlanga, T (2018, Oktoba 15). The Shona people of Zimbabwe: 5 Fascinating Facts. *Rhinoafrica.com*

https://blog.rhinoafrica.com/2018/10/15/5-fascinating-facts-about-shona-people-of-zimbabwe/

Michieka, M. (2012). Language maintenance and shift among Kenyan university students. In *Selected Proceeding of the 41st Annual Conference on African Linguistics, ed. Bruce Cornell and Nicholas Rolle* (pp. 164-170).

Milroy, L. (1987). *Language and social networks*. Oxford: Basil Blackwell.

Milroy, L., na Muysken, P. (Eds.). (1995). *One speaker, two languages: Cross-disciplinary perspectives on code-switching* (Vol. 10). Cambridge University Press.

Mirvahedi, S. (2014). *Language policy, language practices and language shift in tabriz.*, Victoria University of Wellington, Australia. Unpublished doctoral dissertation

Mohochi, E. S. (2005). Language and regional integration: foreign or African languages for the African union?.

Muaka, L. (2011). "Language Perceptions and Identity Among Kenyan Speakers." In: Eyamba, G.B et al. *Selected Proceedings of the 40th Annual Conference on African Linguistics*, (ed) Somerville, MA Cascadilla Proceedings Project pp 217-230.

Muchena, T., na Jakaza, E. (2022). Language Preservation, Evolution, and Loss: The Case of the Shona Language Spoken in Kenya. *Language Matters, 53*(2), 23-36. https://doi.org/10.1080/10228195.2022.2089718

Muchemi, L., & Popowich, F. (2011). An Ontology-based Architecture for Natural Language Access to Relational Databases.

Mufwene, S. S. (2003). Language endangerment: What have pride and prestige got to do with it. *When languages collide: Perspectives on language conflict, language competition, and language coexistence*, 324-346.

Mufwene, S. S. (2014). Language ecology, language evolution, and the actuation question. *The sociolinguistics of grammar*, 13-36.

Mugaddam, A. R. (2006). Language maintenance and shift in Sudan: the case of migrant ethnic groups in Khartoum. *International journal of the sociology of language*, (181), 123-136.

Mugenda, O. na Mugenda, A (2003). *Research Methods: Quantitative and Qualitative. Approaches*: Nairobi. African Centre for Technology Studies (ACTS) Press.

Mulinya, D. (2020, Desemba 30). Shona Celebrate Kenyan Citizenship as Decades of Closed Legal Doors Open. *Citizenship Rights in Africa Initiative*.

Muriuki, G. (1976) The Kikuyu in the Pre- Colonial Period in Kenya before 1900. Nairobi: East African Publishing House.

Myers, S. (1995). *Social Motivations for Code switching: Evidence for Africa. Newyork: Oxford University Press.*

Nabea, W. (2009). Language Policy in Kenya: Negotiation with Hegemony. *Journal of pan African studies, 3*(1).

Nagy, N. (1996). *Language Contact and Language Change in the Faetar Speech community* (Doctoral dissertation, University of Pennsylvania).

Nagy, G. (2010). Language and Meter. *A companion to the ancient Greek language*, 370-387.

Namei, S. (2012). *Iranians in Sweden: A study of language maintenance and shift*. Edita Västra Aros.

Nash, J. (1987). Policy and practice in the American sign language community. *International Journal of the Sociology of Language* 68. 7-23.

Ndubi, M. (2017, Novemba 9). The Shona: A Stateless Community in Kenya

Yearning to Gain Citizenship. *UNHCR.*

https://www.unhcr.org/ke/12739-shona-stateless-community-kenya-yearning-gain-citizenship.html

Nettle, D., na Romaine, S. (2000). *Vanishing voices: The extinction of the world's languages*. Oxford: Oxford University Press.

Ngechu, M. (2004). *Understanding the Research Process and Methods: An Introduction to Research Methods*. Acts Press, Nairobi.

Ngugi, B. (2014). *Umilisi wa Stadi za Maamkizi katika Ujifunzaji wa Kiswahili. Chuo Kikuu cha Kenyatta.* Tasnifu ya Uzamifu.

Ngure, K (2012). *From Rendille to Samburu: A Language Shift Involving Two Mutually Unitelligible Languages of Northern Kenya*. University of Nairobi: Tasnifu ya Uzamifu.

Nonaka, A. M. (2009). Estimating size, scope, and membership of the speech/sign communities of undocumented indigenous/village sign languages: The Ban Khor case study. *Language & Communication*, *29*(3), 210-229.

Nove, C. R. (2021). Outcomes of language contact in New York Hasidic Yiddish. *German (ic) in language contact*, 43.

Obiero, O. J. & Matu, P.M. (2013) Appliction of the Vitality Test on Small Languages: The Case of Suba in Kenya. *The African Review: A Journal of African Politics, Development and International Affairs*, 40(1), 179-202.

http://www.jstor.org/stable/45342091

Obiols, M. (2002). "The Matched Guise Technique: A Critical Approcimation to a Classic Test for Formal Measurement of Language Attitudes.

Odenyo, A. na Ntinyari, C. (2021, Agosti 23). We lived like ghosts before we got IDs — Shona community members. *The Star*.

Ontieri, J. (2017). Nafasi ya Kiswahili kama Lugha Rasmi nchini Kenya: Majukumu na Changamoto. *Mulika Journal*, *32*(1-2).

Orcutt-Gachiri, H. A. (2009). *Kenyan language ideologies, language endangerment, and Gikuyu (Kikuyu): How discourses of nationalism, education, and development have placed a large, indigenous language at risk*. The University of Arizona.

O'Riagain, P. (1994). Language maintenance and language shift as strategies of social reproduction. *Journal of Multilingual and Multicultural Development* 15(2&3): pp. 179-197

Orodho, J. (2004). *Elements of Educational Research and Social Science Research Methods*. Nairobi: Masola Publishers.

Patton, M. (1990). *Qualitative evaluation and research methods* (2nd ed) Newbury: London.

Paulston, C.(1994f). Social factors in language maintenance and shift. In *Linguistic minorities in multilingual settings,* ed. C. B. Paulston, 9-24. Amsterdam: John Benjamins.

Pauwels, A. (2005). Maintaining the community language in Australia: Challenges and roles for families. *International journal of bilingual education and bilingualism, 8*(2-3), 124-131.

Pfaff, C. W. (1979). Constraints on language mixing: Intrasentential code-switching and borrowing in Spanish/English. *Language*, 291-318.

Poplack, S. (1980). Sometimes I'll start a sentence in spanish y termino en espanol: toward a typology of code-switching1.

Poplack, S., & Sankoff, D. (1984). Borrowing: the synchrony of integration.

Poplack, S., na Meechan, M. (1998). Introduction: How languages fit together in codemixing. *International journal of bilingualism*, *2*(2), 127-138.

Ralli, A. (2001). Morphology in language contact: verbal loanblend formation in Asia Minor Greek (Aivaliot). *Morphologies in contact (Studia Typologica). Berlin: Academie Verlag*, 185-201.

Richards, C. J., & Schmidt, R. (2002). Longman Dictionary of Language Teaching and Applied Linguistics 3rd edition.

Roche, G. (2017). Introduction: The transformation of Tibet's language ecology in the twenty-first century. *International Journal of the Sociology of Language*, *2017*(245), 1-35.

Romaine, S. (1994). Hawaii Creole English as a literary language. *Language in Society*, *23*(4), 527-554.

Rottland, F. na Okombo,O. (1992). "Language Shift Among Suba of Kenya." In Brenzinger, M. (ed) (1992). *Language Death.* Berlin: Mounton De Gruyter.

Ryan, E. na Giles, H. (1982). *Attitudes towards language Variation*. London: Edward Arnold.

Sallabank, J. (2010). Language documentation and language policy. *Language Documentation and Description*, *7*, 144-171.

Sangili, N. N. K. (2019). *Udumishaji wa lugha ya kimaragoli katika eneobunge la uriri, Kenya* (Doctoral dissertation).

Sarnoff, I. (1970). Social attitudes and the resolution of motivational conflict. *Attitudes*, 279-284.

Simandan, U. R. (2016). Determining the influence of attitude toward teacher's accents on language learning. *Educația Plus*, *14*(3), 112-140.

Statistics, A. D. (2010). Australian Bureau of Statistics. *Retrieved (18 May 2021) from http://www. abs. gov. au*.

Stoessel, S. (2002). Investigating the role of social networks in language maintenance and shift. *International Journal of the Sociology of Language*, *2002*(153).

Thomason, S. G., na Kaufman, T. (1988). *Language Contact* (Vol. 22). Edinburgh: Edinburgh University Press.

Thomason, S. G. (2000). Linguistic areas and language history. In *Languages in contact* (pp. 311-327). Brill.

Thomason, S.G. (2001). *Language Contact*. Edinburgh: Edinburgh University Press.

Tsangwa, J. K. (2017). *Ukopaji wa Maneno ya Kiswahili Sanifu katika Lugha ya Kigiriama: Michakato na Sheria za Kifonolojia* (Doctoral dissertation, Pwani Unversity).

Tsounis, M. P. (1974). Greek education in Australia. Canberra: The Australian National University.

T'sou, B. K. (2001). Language contact and lexical innovation. In *New Terms for New Ideas* (pp. 35-56). Brill.

Triandis, H. C. (1971). Attitude and attitude change. Wiley Publishers.

UNESCO (2003). *Language vitality and endangerment: UNESCO ad hoc expert group on endangered languages*. Paris: UNESCO.

UNESCO (2011). Atlas of the world's languages in danger. Paris: UNESCO.

Van Aswegen, K. (2008). The maintenance of Maale in Ethiopia. *Language Matters*, *39*(1), 29-48.

Van Hout, R., na Muysken, P. (1994). Modeling lexical borrowability. *Language variation and change*, *6*(1), 39-62.

Veettil,R., Binu, P. na Karthikeyan, J. (2020) Language Maintainance and Language Shift among Keralites in Oman. *Arab World English Journal,11(4) 319-327* DOI: https://dx.doi.org/10.24093/awej/vol11no4.21

Velázquez, I. (2012). Mother's social network and family language maintenance. *Journal of Multilingual and Multicultural Development*, *34*(2), 189-202.

Wagalla, S. (2019). *Citizens or Refugees? The Case of the Shona in Kenya (1962-2017)* (Doctoral dissertation, University of Nairobi).

Wasike, A. (2021, July 28). Stateless Shona Community gets Kenyan Citizenship. https://www.aa.com.tr/en/africa/stateless-shona-community-gets-kenyan-citizenship/2317077

Wei, L. (1998). Banana split? Variations in language choice and code-switching patterns of two groups of British-born Chinese in Tyneside. *Codeswitching worldwide*, *1*, 153.

Weinreich, U (1953). *Languages in Contact*. NewYork: Linguistic Circle of New York

Were-Mwaro, A. G. (2002). The Future of Local African Languages in Kenya's Education System. *Egerton Journal*, *4*(1), 89.

Wolck, W. (2004). *Universals of language maintenance, shift and change*. Collegium antropologicum, 28(1), 5-12.

Yamamoto, M. (1998). Language use in families with parents of different native languages: An investigation of Japanese-non-English and Japanese-English families. *Journal of multilingual and multicultural development*, *23*(6), 531-554.

## KIAMBATISHO A

## MWONGOZO WA HOJAJI

**KITANGULIZI**

Mimi ni Mercy Moraa Motanya, Mtafiti kutoka Chuo kikuu cha Kenyatta, idara ya Kiswahili. Ninafanya utafiti kuhusu Kishona nchini Kenya kwa minajili ya kutosheleza mahitaji ya Shahada ya Uzamifu chuoni. Mchango wako utatumika tu kama data ya kuandikia tasnifu.

**Athari za Mtagusano Kiswahili na Kikuyu kwa Kishona**

1. Kati ya lugha zifuatazo tatu, ni lugha ipi unafahamu vyema sana
    a) Kishona.........................
    b) Kiswahili.......................
    c) Kikuyu..........................
2. Ukiongea katika shughuli rasmi, unatumia lugha ipi? Kwa nini?

    ..............................................................................................................................
    ..............................................................................................................................
3. Unapoongea Kishona, kuna maneno ya Kiswahili unaingiza kwa Kishona? Yataje
    a) ........................
    b) .......................
    c) ........................
4. Unapoongea Kishona, kuna maneno ya Kikuyu unaingiza kwenye Kishona? Yataje.
    a) ..........................
    b) ..........................
    c) ..........................
5. Je, lugha za Kiswahili na Kikuyu zimeathiri lugha yako ya Kishona? Vipi?

Tafadhali weka alama ( ✓ ) kwenye kisanduku kulingana na matumizi ya lugha katika sehemu na hali mbalimbali zifuatazo

| | Hali | lugha | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Kishona | Kiswahili | Kikuyu | Lugha nyingine |
| 1. | Unapoongea na babu na nyanya, unatumia lugha ipi? | | | | |
| 2. | Babu na nyanya hukuzungumzia lugha ipi? | | | | |
| 3. | Unapoongea na mama mzazi, unatumia lugha ipi? | | | | |
| 4. | Unapoongea na baba mzazi, unatumia lugha ipi? | | | | |
| 5. | Baba mzazi hukuzungumzia na lugha ipi? | | | | |
| 6. | Mama mzazi hukuzungumzia na lugha ipi? | | | | |
| 7. | Mnapoongea na ndugu zako, mnatumia lugha ipi? | | | | |
| 8. | Unapoongea na mzee wa kijiji, unatumia lugha ipi? | | | | |
| 9. | Unapoongea na marafiki, unatumia lugha ipi? | | | | |
| 10. | Unapoenda dukani/sokoni, unatumia lugha ipi? | | | | |
| 11. | Kanisani mnatumia lugha ipi? | | | | |

Tafadhali weka alama ya kukubali ( ✓ ) kwenye kisanduku ukionyesha umuhimu wa lugha zifuatazo kwa:

| | Mahali | Lugha | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Kishona | Kiswahili | Kikuyu | Lugha nyingine |
| 1. | Shuleni. | | | | |
| 2. | Biashara. | | | | |
| 3. | Burudani na marafiki. | | | | |
| 4. | Shughuli za Kijamii/kitamaduni. | | | | |
| 5. | Matumizi muhimu katika maisha. | | | | |

# KIAMBATISHO B

## MWONGOZO WA HOJAJI

### KITANGULIZI

Mimi Mercy Moraa Motanya, Mtafiti kutoka Chuo kikuu cha Kenyatta, Idara ya Kiswahili. Ninafanya utafiti kuhusu mielekeo ya Kishona nchini Kenya kwa minajili ya kutosheleza mahitaji ya Shahada ya Uzamifu chuoni. Mchango wako utatumika tu kama data ya kuandikia tasnifu.

**Mielekeo ya Lugha ya Kiswahili (Wazee /Wakongwe Zaidi wa Kishona)**

1. Unaweza kukumbuka mwaka ambao Washona walifika hapa Kenya?
2. Mlipofika hapa kenya, mlikuwa mnaogea na Wakenya mkitumia lugha gani, je, mlielewanaje na Wakenya kilugha?
3. Je, ni lugha zipi ambazo mnajua kusoma na kuandika?
   a) Kiswahili
   b) Kishona
   c) Kikuyu
4. Mlijifunzaje lugha ya Kiswahili?
5. Je, ni sababu gani zinawafanya kuzungumza?
   a) Kiswahili
   b) Kishona
   c) Kikuyu
6. Je, unazungumza Kiswahili kwa hiari tu ama kuna sababu maalum zinakufanya kuzungumza Kiswahili?

## KIAMBATISHO C

## MWONGOZO WA HOJAJI

### KITANGULIZI

Mimi Mercy Moraa Motanya, Mtafiti kutoka Chuo Kikuu cha Kenyatta, Idara ya Kiswahili. Ninafanya utafiti kuhusu mielekeo ya Kishona nchini Kenya kwa minajili ya kutosheleza mahitaji ya Shahada ya Uzamifu chuoni. Mchango wako utatumika tu kama data ya kuandikia tasnifu.

**Mielekeo ya Kishona (Hojaji kwa Vijana wa Kishona)**

1. Lugha yako ya kwanza ni ipi?
2. Je mnaongea lugha ipi sana?
3. Mnachukuliaje lugha za Kiswahili na Kikuyu?
4. Ni sababu zipi zinazowafanya mtumie Kiswahili?
5. Mkiwa nyumbani huwa mnaongea lugha gani na:
    a) Wazazi?
    b) Mkicheza?
    c) Kanisani?
6. Umejifunzaje Kiswahili?
7. Ulijifunzaje Kikuyu?
8. Utakapokuwa na familia yako utawafunza lugha gani kwanza?

    Kwa nini?

# KIAMBATISHO D

## MWONGOZO WA MAHOJIANO

### KITANGULIZI

Mimi ni Mercy Moraa Motanya, Mtafiti kutoka Chuo Kikuu cha Kenyatta, Idara ya Kiswahili. Ninafanya utafiti kuhusu udumishaji wa Kishona nchini Kenya kwa minajili ya kutosheleza mahitaji ya Shahada ya Uzamifu chuoni. Mchango wako utatumika tu katika data ya kuandikia tasnifu.

**Udumishaji wa Kishona (Mahojiano ya Wazee Washona)**

1. Je mnazungumza Kishona kwa undani?
2. Ni rika gani haitumii Kishona wanapozungumza?
   a) Watoto
   b) Vijana
   c) Wazee
3. Ni lugha zipi zingine ambazo Washona wengi huzungumza?
   a) ..............................
   b) ..............................
   c) ..............................
4. Washona walipofika Kenya mwaka wa 1959, wakajenga kanisa lao, je ni lugha zipi walikuwa wanatumia wakati huo?
   a) ...............................
   b) ...............................
5. Je? Kanisani bado kunatumika Kishona? Na ni lugha ipi nyingine inayotumika kanisani tena?
6. Watoto na vijana wanajifunza aje Kishona?
7. Ni changamoto gani inawapata watoto na vijana wanapoongea Kishona?
8. Unapokutana na Vijana, watoto na wazee, unawapata wakiongea lugha gani?

9. Washona wanapokutana na Washona wengine, wao huongea lugha ipi?
10. Washona wanapokutana na watu wengine, wao huongea lugha ipi?
11. Ni sababu zipi zinazowafanya kuzungumza Kishona hadi sasa?
12. Ni shughuli zipi za kitamaduni mnazofanya ambazo huendeleza lugha yenu ya Kishona?

## KIAMBATISHO E

## SABABU ZA KUTUMIA KISWAHILI NA KISHONA

## MJADALA WA KIMAKUNDI (WAZEE) TAREHE 11/03/2023

## (*Valley Road*-Kanisa la *Gospel of God*)

**Mtafiti**: Habari za leo?

**Watafitiwa**: Nzuri.

**Mtafiti**: Yangu ni njema sana. Karibuni kwa kikao hiki cha leo. Je kuna mwingine ambaye tunamtarajia?

**Mtafitiwa I**: Hapana. Tunaweza kuendelea.

**Mtafiti**: Nawashukuru kwa kufika na kunipatia muda wenu ili tuweze kujadiliana. Nawaomba muwe huru katika mjadala huu na mweze kuchangia kadiri ya uwezo wenu.

**Watafitiwa**: Sawa

**Mtafiti**: Mimi naitwa Mercy Moraa Motanya, mwanafunzi katika Chuo Kikuu cha Kenyatta, Idara ya Kiswahili. Ninafanya utafiti kuhusu athari za Kiswahili na Kikuyu kwa uthabiti wa Kiisimujamii wa Kishona nchini Kenya. Hivyo basi, mjadala wetu asubuhi ya leo unahusu mada hii na ni ombi langu kwamba mtanipa habari itakayonisaidia katika utafiti huu.

**Watafitiwa**: Sawa.

**Mtafiti**: Tuanze na swali hili, mnaweza kukumbuka mwaka ambao Washona wa kwanza walifika Kenya?

**Mtafitiwa I**: Walifika Kenya mwaka wa 1957. Wengine wakakuja miaka iliyofuata ya 1959,1960,1962,na 1963

**Mtafiti**: washona wa Kwanza kufika Kenya walikuwa wangapi?

**Mtafitiwa II**: Kumi na sita.

**Mtafiti**: Niambie safari yao kutoka Zimbabwe hadi Kenya ilikuwaje?

**Mtafitiwa III**: Walitoka Zimbabwe wakapitia Zambia, Kongo, Tanzania na mwishowe kufika Kenya. Wakenya walikuwa wanatuita Wazambia.

**Mtafiti:** Kwa nini Mliitwa Wazambia?

**Mtafitiwa III**: Sababu ya kuitwa Wazambia ni kwamba safari ilipitia nchini Zambia.

**Mtafiti**: Mlihusianaje na Wakenya?

**Mtafitiwa IV**: Ilibidi tuongee na Wakenya sababu lengo letu lilikuwa ni kueneza injili. Hivyo basi lugha ya Kiswahili ilikuwa nzuri kwa mahusiano yetu na Wakenya sababu ndiyo ilikuwa lugha ya taifa la Kenya. Tulijifunza kwa haraka sana ili tuweze kuhubiria Wakenya kwa maana katika dini, ushirikiano ni lazima

**Mtafiti**: Mlipofika Kenya, mlielewanaje na Wakenya kilugha?

**Mtafitiwa** IV: Tulipofika Kenya wakati huo hatukuwa tunajua lugha ya Kiswahili vizuri lakini tulijifunza haraka kushirikiana raisi. Kiswahili kilikuwa rahisi kujifunza kwa sababu safari yetu kutoka Zimbabwe tulipitia Tanzania kwenye tulijifunzia Kiswahili kidogo. Tulipata Wakenya wanazungumza Kiswahili pia na sisi tukaendelea. Lugha hii ilirahisisha ushirikiano hapa Kenya. Lugha ya Kiswahili ilituunganisha na Wakenya.

**Mtafiti**: Oooh, basi ilikuwa afueni kwenu kupata Wakenya wakizungumza lugha ambayo mnaielewa hata kama ni kidogo tu.

**Watafitiwa**: Eeeh.

**Mtafitiwa IV**: Katika safari yetu tulikuwa tumepitia Kongo na Tanzania ambapo lugha ya Kiswahili inazungumzwa. Tulikuwa tumejifunza kidogo lugha hii na sasa tulipofika Kenya, ilikuwa rahisi kidogo kuzungumza na kuwasiliana na Wakenya.

**Mtafiti**: Lengo lenu la kuja Kenya lilikuwa lipi?

**Mtafitiwa V**: Ni kueneza injili ambayo nabii Baba Johanne Masowe alikuwa ameonyeshwa na Mungu kupitia kwa kanisa letu la *Gospel of God*.

**Mtafiti:** Kuna lugha nyingine ambazo mlikuwa mnafahamu wakati huo?

**Mtafitiwa IV**: Ehe, tulikuwa tunafahamu Kiingereza, na wengine wetu Kindebele.

**Mtafiti:**Lugha mnazojua kusoma na kuandika ni zipi

**Watafitiwa**: Kiswahili, Kishona na Kiingereza. Baadhi yetu wanajua Kikuyu.

**Mtafiti**: Mlijifunzaje lugha ya Kikuyu?

**Mtafitiwa V**: Baba zetu walipofika nchini Kenya, walikaribishwa na Wakikuyu katika sehemu za Ngong na Juja kabla ya kwenda mitaa ya Kinoo na Kiambaa. Kando na kuzungumza lugha ya Kiswahili, baba zetu pia walijifunza lugha ya Kikuyu.

**Mtafitiwa III**: Mimi na wenzangu tumeishi sehemu hii ya Kinoo kwa zaidi ya miaka ishirini. Lugha inayozungumzwa hapa sana ni lugha ya Kikuyu kwa sababu hapa kuna Wakikuyu wengi sana na hivyo ni rahisi kwetu kujifunza lugha ili kufanya shughuli zetu kwa urahisi. Pia, ndugu zetu Wakikuyu ndio waliwakaribisha Washona wa kwanza waliofika hapa nchini kwa shughuli za kueneza injili. Wale Washona wanasungumsa Kukuyu, husungumsa kwa sababu kuwasiliana. Wakikuyu ni majirani zetu na

mawasiliano ni lazima kati yetu. Tunaposungumsa lugha hii ya Kikuyu, watu wengine hufikiria kwamba sisi pia ni Wakukuyu.

**Mtafitiwa I**: Hata saii ukitoka hapa kwa barabara na umpate mtu yeyote, jaribu kumsungumsia Kikuyu, atakujibu tu kwa Kikuyu kwa sababu watu wengi hapa ni Wakikuyu na wale ambao si Wakikuyu kama sisi Washona, wamejifunza lugha hii.

**Mtafiti:** Kuna sherehe za kikuyu ambazo mnahudhuria?

**Mtafitiwa IV**: Naam. Sherehe kama vile za harusi au mazishi tunahudhuria. Wakikuyu hutumia lugha yao wakati wa sherehe kama hizi. Inabidi tujue lugha yao ili ikuwe rahisi kwetu kushiriki. Lakini si Washona wote wanajua lugha ya Kikuyu.

**Mtafiti**: Je, nyinyi mnafanya biashara katika maeneo mnayoishi? Lugha mnayotumia sana ni ipi?

**Mtafitiwa I:** Kwa kuwa tulikosa stakabadhi muhimu za kuturuhusu kuendelea na masomo na hatimaye kupata kazi za ofisini, tulijishughulisha na biashara ndogondogo kama vile vioski na biashara za kuuza mboga na matunda. Wateja wetu wengi ni Wakikuyu sababu sehemu hii wako wengi. Kupitia shughuli za biashara, tumejifunza Kikuyu ili kuzirahisisha.

**Mtafitiwa**: Tunafanya kazi ya kusuka vikapu ambavyo tunauza kwa ajili ya hela. Huwa tunatumia Kiswahili tukiongea na wateja wetu.

**Mtafitiwa:** Tumekuwa tukitumia Kiswahili katika kazi yetu ya useremala tunapotafuta wanunuzi kwa kuwa wateja wetu wengi ni Wakenya

**Mtafiti**: Mlijifunzaje lugha ya Kiswahili?

**Mtafitiwa VI**: Kupitia kuzungumza na Wakenya, kuiga vile wanaongea na pia watoto wetu wamejifunza kupitia shuleni.

**Mtafiti**: Kwa nini mlijifunza Kiswahili?

**Mtafitiwa III**: Tulijifunza lugha ya Kiswahili ili kurahisisha maingiliano na makabila mengine ya Kenya. Kwa vile katika maisha ya kila siku lazima tuongee na watu, na lugha ya Kiswahili ilikuwa lugha mwafaka kwetu.

**Mtafiti**: Je kuna sababu zinawafanya kuzungumza lugha ya Kiswahili?

**Watafitiwa**: Ndio, zipo

**Mtafiti**: Kama zipi?

**Mtafitiwa VII**: Tunatumia lugha ya Kiswahili kutafuta na kufanya kazi za mikono ili tupate wateja na pia tunatumia Kiswahili katika ibada yetu.

**Mtafitiwa VIII**: Tunatumia Kiswahili kwa sababu ni lugha ya taifa, na pia kwa sababu ni lugha ya mawasiliano. Kiswahili pia kinatumiwa kutuunganisha na Wakenya wengine.

**Mtafitiwa IX**: Tunatumia lugha ya Kiswahili kwa sababu ya kuhusiana na Wakenya wengine. Tunapokuja pamoja pia, huwa tunafanya hivyo kwa kutumia Kiswahili.

**Mtafitiwa X**: Zamani tulikuwa tunatumia Kiswahili kwa sababu ya usalama wetu. Hii ilikuwa inafanyika kwa sababu hatukuwa tumepewa vitambulisho, tulikuwa tunaongea Kiswahili ili polisi wasijue ati sisi si wakenya. Lakini siku hizi tunafurahia sababu tulitambuliwa kama Wakenya.

**Mtafitiwa VII:** Ilikuwa ni poa kwetu Washona kuzungumza Kiswahili na Kikuyu kwa sababu askari hawangegundua haraka kama sisi si Wakenya. Lugha hizi za Kenya zilitufícha sana. Lakini kuna wakati mwingine wanajamii walitusema na tukajipata tumefungwa...”

**Mtafiti**: Kuna sababu nyingine za kutumia Kiswahili?

**Mtafitiwa**: Ili kuepuka changamoto hasa zile zinazohusiana na utambulisho hapa Kenya, ilibidi tujifunze Kiswahili ili turahisishe utambulisho na Wakenya...

**Mtafitiwa X**: Ndiyo, mawasiliano.

**Mtafitiwa I**: Tulikuwa tunatumia Kiswahili ili kutambulikana kama Wakenya. Kwanza siku hizi ndiyo imekuwa vizuri vile tulitambuliwa kama Wakenya mwaka wa 2020. Tunaongea Kiswahili sasa tukiwa Wakenya. Watoto wetu pia wanatumia lugha ya Kiswahili masomoni kwa hivyo lazima wajifunze Kiswahili shuleni.

**Mtafitiwa II**: Pia, tunazungumza Kiswahili ili kurahisisha maongezi kati yetu na makabila mengine hapa nchini Kenya. Lugha ya Kiswahili inafanya tuwasiliane.

**Mtafiti.** Asante sana. Je, bado mnazungumza Kishona

**Watafitiwa**: Ndiyo. Hatujasahau lugha ya mama.

**Mtafiti**: Ni kwa nini bado mnazungumza Kishona?

**Mtafitiwa I:** Tunazungumza Kishona kwa sababu ni lugha ya mama na inaweka utamaduni wetu. Kwa hivyo tunaidumisha kupitia kuongea. Tunazungumza Kishona pia kwa sababu siku hizi lugha yetu imetambuliwa kuwa lugha mojawapo ya Kenya.

**Mtafitiwa II**: Tunatumia Kishona pia kanisani katika ibada ya kanisa yetu.

**Mtafiti:** Je, mnatumia lugha ya Kiswahili Kanisani?

**Mtafitiwa II**: Mwanzoni tulikuwa tunatumia lugha ya Kishona pekee kanisani, tulikuja tukagundua kwamba kuna waumini walijiunga na kanisa letu ambao hawajui Kishona, ndio tukaanza kutumia lugha ya Kiswahili pia katika ibada kupitia kwa ukalimani.

**Mtafiti:** Majukumu ya lugha ya Kishona ni yapi?

**Mtafitiwa III**: Lugha ya kishona inatuunganisha pamoja kwa sababu siku hizi Washona wengi wameenda mitaa mbalimbali hapa Nairobi. Lugha ya Kishona pia inatukumbusha kwenye tulitoka Zimbabwe kwenye Washona original wengi wanaishi.

**Mtafiti**: Je mnazungumza lugha ya Kiswahili kwa hiari tu ama kuna sababu maalum zinawafanya kuzungumza?

**Mtafitiwa IV**: Tunazungumza Kiswahili kwa hiari tu na pia kama tulivyosema hapo awali, kuna sababu nyingi ambazo zinatufanya kuzungumza lugha ya Kiswahili.

**Mtafiti**: Asante kwa ushirikiano na mchango wenu kuhusu lugha. Mbarikiwe sana. Asanteni.

## KIAMBATISHO F

## UDUMISHAJI WA KISHONA

## MAHOJIANO YA TAREHE 11/03/2023

## (WAZEE, AKINA MAMA,WATOTO NA VIJANA. KINOO)

**Mtafiti:** Hamjambo wanakikundi?

**Watafitiwa:** Hatujambo.

**Mtafiti:** Mimi naitwa Mercy Moraa Motanya, mwanafunzi katika Chuo Kikuu cha Kenyatta, Idara ya Kiswahili. Ninafanya utafiti kuhusu athari za Kiswahili na Kikuyu kwa uthabiti wa Kiisimujamii wa Kishona nchini Kenya. Hivyo basi mjadala wetu asubuhi ya leo unahusu mada hii na ni ombi langu kwamba mtanipa habari itakayonisaidia katika utafiti huu. Karibuni.

**Watafitiwa**: Asante

**Mtafiti**: Bado mnazungumza lugha ya Kishona? Na ni kwa nini?

**Mzee wa 1**: Ndiyo. Sisi wazee tunasungumsa sababu ni lugha yetu. Na ni utamaduni wetu. Utamaduni wetu unaenda pamoja na lugha yetu kwa hivyo tunajaribu kila njia ili kuendeleza utamaduni huu. Watoto wetu wanaweza kujua utamaduni wetu kupitia kwa lugha yetu. Kwa mfano jinsi tunavyowapatia watoto wetu majina ya ukoo.

**Mzee wa II**: Kitu ambacho kimetuweka pamoja kwa muda huu wote ni lugha yetu na utamaduni wetu kama Washona. Huwa tunatembeleana hata kupigiana simu ili tuweze kuongea lugha yetu ndio tusisahau.

**Mzee wa III**: Tunazungumza Kishona ili tuwasiliane vyema na Washona wengine na pia mawasiliano haya kwa lugha yetu hutuweka pamoja.

**Mtafiti**: Ni njia zipi ambazo mnatumia kuendeleza Kishona.

**Mzee wa II:** “Mimi nawaongelesha wanangu pamoja na wachukuu wangu Kishona tukiwa katika maeneo ya nyumbani”
**Mzee wa I**: “Mimi najaribu kuwafunza wanangu lugha yetu. Huko nyumbani , hatuzungumzi lugha yoyote isipokuwa Kishona. Hata kama watoto wanazungumza lugha hii ya Kiswahili, mimi husisitiza matumizi ya Kishona nyumbani.”

**Mtafiti:** Mzee , Njia nyingine za kudumisha lugha katika maeneo ya nyumbani ni ipi?
**Mzee wa III**: Familia zetu huishi pamoja na watoto wao hadi wanapofikia umri wa kuanza familia yao. Wakati huu wote, tunawazungumzia Kishona nyumbani. Kwa hivyo watoto wanaendelea kukua wakijua lugha yetu. Lakini wajukuu wetu ni kama wameanza kujifunza lugha ya Kiswahili kwa sababu ukiwaongelesha kwa Kishona, wanakujibu kwa Kiswahili ama wanakuangalia tu.

Pili, Tunapofanya kazi zetu na shughuli mbalimbali nyumbani, tunatumia lugha ya Kishona kuwasungumsia watoto wetu. Shughuli kama vile mapishi, kazi zetu za mikono au tunapofanya usafi nyumbani huwa tunawasungumsia lugha ya mama. Kupitia hapo wanajifunza maneno ya lugha yetu ya Kishona.

**Mtafiti**: Msichana, Je ulijifunzaje Kishona?
**MT1:** Mimi nimejifunza Kishona kupitia kuiskia nyumbani. Ninazungumziwa na wazazi wangu na babu na nyanyangu kwa Kishona na inabidi pia nijaribu kuwajibu kwa Kishona.
**Mtafiti:** Na wewe ulijuaje lugha ya Kishona?
**MT2:** Ninaendelea kufunzwa hata sasa na wazazi wangu hasa mamangu kwa sababu wakati mwingi tuko na yeye nyumbani. Ndugu yangu pia wananiongelesha tukiwa nyumbani.
**Mtafiti:** Kwa maoni yenu, Vijana hujifunzaje lugha?
**Mzee wa I:** Vijana pia hujifunza lugha yetu ya Kishona sanasana wakiskia tukizungumza nyumbani.
**Mzee wa II:** Vijana wanawasikiliza wazazi wao na ndugu zao wakizungumza.
**Mama wa I:** Wanajifunza wakisikia tukiongea Kishona nyumbani.
**Mtafiti:** Ni kwa nini mmeendelea kuongea lugha ya Kishona licha ya shinikizo kutoka kwa lugha maarufu na pia miaka mingi nchini Kenya?
**Mama wa II:** Tunasema Kishona sababu ni lugha yetu ya mama na pia sisi sasa ni Wakenya kwa sababu tulipewa uraia wa kuwa Wakenya tarehe 12/12/2020 na rais Kenyatta. Kwa hivyo lugha yetu imetambuliwa hapa Kenya.
**Mzee wa II:** Tumejaribu kudumisha lugha yetu kwa miaka isitini sasa hata kama kulikuwako na changamoto tulipata kama vile za utambulisho ambazo zingetufanya kusahau lugha yetu. Lakini lugha ya Kishona ndio kitu tu tulibaki nayo ya muhimu tulipoishi bila stakabadhi za uraia nchini Kenya.
**Mtafiti:** Kijana, wewe umejifunzaje Kishona?
**Kijana I:** Kishona inazungumzwa nyumbani na kanisani. Kitambo kidogo ilikuwa inazungumzwa nyumbani tu sababu hatukuwa tumepewa uraia. Lakini siku hizi tunaizungumza hata mahali tunapofanya kazi zetu za mikono na biashara zetu na kanisani bado.
**Kijana II:** "Ingawa sanasana tunaongea lugha za Kiswahili na Kiingereza, tumejifunza lugha yetu ya Kishona kwa sababu kanisani ndiyo lugha inayotumika sana na pia Biblia tunayosoma kanisani imeandikwa kwa Kishona."

**Mtafiti:** Nyimbo za ibada ni za Kiswahili ama Kishona?

**Kijana I:** Kwanza Biblia yetu tunayotumia imeandikwa kwa Kishona. Pili, asilimia 99 ya nyimbo tunazoimba kanisani ni za Kishona lakini sijaona kwenye zimeandikwa. Kuna mafunzo na sheria za kanisa pia zimeandikwa lakini ni chache sana

**Kijana III:** Siku hizi ninaelewa kwamba tukizungumza Kishona, tunaendeleza lugha yetu.
**Mtafiti**: Wazee mnasemaje kuhusu watoto na vijana kujifunza lugha ya Kishona?

**Mzee wa I na mzee wa II:** "Watoto na vijana wanaendelea kujifunza lugha ya Kishona kupitia kwa kanisani sababu ibada yetu huendeshwa kwa Kishona na kisha wakatafsiri."
**Mtafiti:** Mama maoni yako kuhusu kuendeleza lugha ya Kishona ni yepi?
**Mama 1**: Sisi tunajua lugha yetu pia katika sherehe mbalimbali za kanisani mwetu kwa mfano sherehe ya kuzaliwa kwake mwanzilishi wa kanisa letu ambayo tunasherehekea tarehe moja Oktoba kila mwaka huku tukitumia lugha ya Kishona na kutafsiri kwa lugha ya Kiswahili kwa sababu kuna wale si Washona"
**Mtafiti**: Kijana, naona unataka kuongeza jambo tena kuhusu udumishaji wa lugha yenu ya Kishona.
**Kijana I**: Naam. Mimi humtembelea mamangu siku mbili kwa wiki ili kumsalimia. Hata kama mimi na mke wangu na watoto wangu wawili tunaishi mbali kiasi, huwa namtembelea mama kwa kuwa huko tutaongea lugha yetu. Pia mimi humtembelea Zeph pale alikohamia Kitengela mara kwa mara ili kumsalimia na pia kujua zaidi lugha yetu.

**Mtafiti:** Je, huwa mnafanya mikutano ya kijamii? Mnatumia lugha gani?

**Mama I:** Naam. Huwa tuna mikutano mbalimbali ya kijamii kwa shughuli mbalimbali. Kwanza mikutano mingi tuliyokuwa nayo kabla ya mwaka wa 2020 ilikuwa ya kuweka mikakati ya kupewa uraia. Hapo, tulikuwa tunatumia lugha ya Kishona kwa kuwa sisi ndiyo tulikuwa na shida hapa nchini. Lakini wakati tulikuwa na wasio Washona, tulikuwa tunatumia Kiswahili kwa sababu hawajui Kishona.

**Mtafiti**:Mikutano mingine ni ipi?

**Mzee II:** Siku ya kanisa, huwa tunakutana mapema kabla ya ibada kuanza sisi kama wazee ili kuunda mikakati ya kupata hela za maendeleo Kanisani. Tunapokutana hivyo, tunazungumza lugha ya Kishona pekee. Hali hii imechangia kuendeleza lugha yetu ya Kishona.

**Mtafiti**: Mzee, twambie mlivyodumisha lugha yenu hapo awali.

**Mzee wa III:** Tulipofika Kenya kwa mara ya kwanza, mimi nilikuwa mdogo wa miaka kama kumi na tatu hivi, tulianza kwa kukaa kule ngong' mtaa unaoitwa Zambia. Watu walikuwa wanatuita Wazambia kwa kuwa hawakuelewa kuwa sisi ni Wazimbabwe. Baada ya uhuru kupatikana hapa Kenya, mambo yalianza kubadilika tukawa hatuna uhuru tena bila vibali rasmi vya Kenya. Ndio maana tulikuwa tunakaa karibukaribu ili mmoja wetu akipata shida, tuweze kusaidiana. Pia kukaa karibu karibu ilitusaidia kwa kuwa hatungejulikana kwa urahisi kwamba sisi si Wakenya kwa wakati huo. Si kama sasa ambapo sisi ni raia halisi wa Kenya.

**Mtafiti:** Nani atatuelezea kuhusu Sherehe za Kishona na lugha zinazotumika
**Mzee wa I**: Sisi huwa na sherehe tatu muhimu. Sherehe zetu zimeshikamanishwa na dini yetu kupitia kwa kanisa letu la *Gospel of God*. Sherehe ya kwanza ni sherehe ya kuzaliwa kwa mtoto(*kubarwa*) ambapo mtoto akizaliwa, huwa mama na mwanawe hawaonani na mtu yeyote nje ya familia yake isipokuwa mfanyakazi wake. Baada ya siku nane, sherehe kubwa ya kumpa mtoto jina ambalo ni lazima kutoka kwa ukoo wa

babake tu, hufanyika. Katika sherehe hizi, ni lugha ya Kishona tu ambayo hutumika kwa kuwa lugha ya Kishona ni sehemu ya utamaduni wetu..
**Mzee wa II:** Sherehe ingine, sherehe ya harusi kati ya Washona pekee yao(*muchato*), lugha ya Kishona tu hutumika katika shughuli zote na hatua zote. Lakini siku hizi tunatumia pia hata lugha ya Kiswahili sababu tumekuwa na marafiki wengi ambao si Washona kwa hivyo inabidi tutumie lugha ambayo wanaelewa.

**Mzee wa III:** Sherehe ya mazishi (*namu*), sisi hutumia lugha mbili kwa kuwa kutakuwa na wageni ambao si Washona wanaohudhuria mazishi. Aidha kuna sherehe ya Kumkumbuka mwanzilishi wa kanisa la *Gospel of God* church baba Johanne Masowe. Sherehe hii hufanyika kila tarehe 1 Oktoba ya kila mwaka ambapo lugha mbili hutumika: lugha ya Kishona na lugha ya Kiswahili. Lugha ya Kishona hutumika kwa sababu ni utamaduni wetu na lugha ya Kiswahili hutumika kwa kuwa ni lugha ya taifa la Kenya na pia kwa sababu huwa kuna wageni na waumini ambao si wa Kishona katika kanisa letu..

**Mtafiti**: Je,kuna watu ambao si Washona lakini wanajua lugha ya Kishona?

**Mzee wa II**: Wako lakini si wengi sana. Kwanza kuna wale walishaolewa na Washona wetu, hao wamejifunza lugha ya mume na wanaizungumza vizuri. Pili, kuna marafiki wetu ambao wamejifunza kwa kupenda tu. Tatu, Lugha yetu inaendelezwa pia kwa kuwa Washona wanapooa Washona wenziwe, lugha inazidi kudumishwa baina ya Washona na Washona.

**Mtafiti:** Vyema sana, je ndoa imeathiri lugha ya Kishona vipi tena?

**Mzee wa I:** Kuna wasichana wetu wameolewa watu ambao si Washona. Wameenda na kujifunza lugha ya nje. Kwa njia hii, wazungumzaji wa lugha ya Kishona hupungua na kufanya lugha yetu kuwa hatarini. Lakini kuna wale ambao sisi tumewaoa na si Washona. Hao ni wachache ambao wamejifunza lugha yetu.

**Mtafiti**: Asante sana kwa ushirikiano wenu.

## KIAMBATISHO G

## MIELEKEO NA MATUMIZI YA LUGHA YA KISWAHILI

## MAHOJIANO KWA VIJANA NA WATOTO WA KISHONA

## TAREHE 19/03/2023, GITARU/KIAMBAA/KIKUYU

**Mtafiti**: Hamjambo vijana na watoto?

**Watafitiwa**: Hatujambo.

**Mtafiti:** Kwa majina mimi ni Mercy Moraa Motanya, mtafiti kutoka Chuo Kikuu cha Kenyatta, Idara ya Kiswahili. Ninafanya utafiti kuhusu mielekeo na matumizi ya lugha ya Kiswahili nchini Kenya kwa minajili ya kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamifu chuoni. Mchango wenu utatumika tu kama data ya kuandikia tasnifu.

**Watafitiwa:** Sawa.

**Mtafiti**: Naomba ushirikiano wenu ili kufaulisha mahojiano haya

**Watafitiwa:** Sawa.

**Mtafiti kwa kijana I**: Lugha yako ya kwanza ni ipi?

**Kijana I**: Mamangu alikuwa ananizungumzia Kishona. Hivyo lugha yangu ya kwanza ni Kishona

**Mtafiti:** Je, mnaongea lugha ipi kwa wingi?

**Kijana II:** Tunazungumza Kiswahili sana na pia Kiingereza. Kishona tunaongea tu nyumbani.

**Mtafiti:** Kwa nini?

**Kijana III:** Kwanza, shuleni tunatumia kiswahili, pili, Kiswahili ni lugha rasmi hapa kenya. Tatu, tumezungukwa na makabila mengi na lugha inafaa ni Kiswahili kwa sababu ni lugha rasmi na lugha ya taifa ama Kiingereza. Lakini tukikutana na marafiki Wakikuyu, huwa tunajaribu kuongea lugha yao.

**Mtafiti:** Watoto, mnaongea lugha ipi kwa sasa?

**Mtoto I**: Tulipoingia shuleni, mwalimu anatuzungumzia kwa lugha ya Kiswahili. Kisha tunasoma mambo mbalimbali yaliyoandikwa kwa Kiswahili.

**Mtafiti:** Na wewe uko darasa la ngapi na kwa nini unatumia lugha ya Kiswahili?

**Mtoto II**: Mimi niko darasa la saba, moja ya masomo tunayosoma ni Kiswahili. Ninapenda sana tunaposoma sehemu ya ufahamu kwa sababu ya hadithi hizo zilizoandikwa kwa Kiswahili.

**Mtafiti:** Nawe msichana?

**Mtoto III:** Niko kidato cha pili. Huwa tunasoma somo la Kiswahili mara moja kwa kila siku. Ninapenda upande wa fasihi simulizi.

**Mtafiti:** Vizuri sana, kijana maoni yako kuhusu Kiswahili?

**Mtoto IV:** Niko katika kidato cha nne. Kiswahili ni somo rahisi sana. Kuna hata fasihi ambapo tunasoma riwaya na tamthilia ili kuelewa mambo katika jamii.

**Mtafiti:** Asante sana. Je, mnazungumza lugha ya Kiswahili nje ya darasa?

**Mtoto I:** Ndiyo. Tukitoka darasani wakati wa mapumziko mafupi bado tunazungumza lugha ya Kiswahili.

**Mtoto II**: Tunazungumza Kiswahili njiani tunapoenda shuleni na marafiki na hata tunapocheza.

**Mtoto III:** Hata tukiwa na marafiki zetu Washona na wale si Washona kule nyumbani tunazungumza Kiswahili.

**Mtafiti:** Bado mkitumwa mahali kama dukani huwa mnatumia Kiswahili?

**Mtoto IV:** Ndiyo. Tukitumwa dukani tunaongea Kiswahili na mwenye duka tukienda kununua kitu.

**Mtafiti:** Vijana, mkiwa Sekondari, mnatumia lugha ya Kiswahili nje ya darasani?

**Kijana III:** Naam, tunapenda kutumia kiswahili tukiwa kwenye mapumziko mafupi shuleni. Lakini bado pia siku hizi, lugha ya Sheng' imeanza kubobea japo hairuhusiwi kutumika kwenye mazingira ya shule yetu

**Mtafiti:** Mnachukuliaje lugha ya Kiswahili na Kikuyu?

**Kijana IV**: Lugha ya Kiswahili ina manufaa mengi kama vile masomoni, mawasiliano na makabila mengine, biashara na mambo mengi. Kwa hivyo ni lugha ambayo tunaitumia kwa hiari tu bila kulazimishwa na tunaipenda.

**Mtafiti:** Na Kikuyu?

**Kijana V:** Tunatumia lugha ya Kikuyu lakini kidogo tu kwa sababu ya marafiki wetu Wakikuyu. Kuna baadhi yetu wanaongea Kikuyu kwa ufasaha lakini si wengi.

**Kijana IV**: Katika maeneo haya tunaishi, biashara nyingi ni za Wakikuyu ambao hutuzungumzia kwa lugha yao ya Kikuyu tunapoenda kununua. Hivyo hata sisi imebidi tujifunze lugha ya Kikuyu ili kufanikisha shughuli za biashara.

**Mtafiti**: Ni sababu zipi zinazowafanya mtumie lugha ya Kiswahili?

**Kijana VI:** Sababu ni nyingi kama vile mwenzangu alivyosema hapo awali, tunatumia Kiswahili masomoni, kwenye biashara, kwa mawasiliano na hata mahusiano baina ya makabila mbalimbali yanayotuzunguka.

**Mtafiti:** Mkiwa nyumbani huwa mnaongea lugha gani na wazazi.

**Kijana I**: Huwa tunaongea Kishona na Kiswahili kwa sababu muda mwingi tunatumia Kiswahili hapa nje. Tukiingia nyumbani sasa kuna kusahau na kutumia Kiswahili.

**Mtafiti:** Mlijifunzaje Kiswahili?

**Kijana VII:** Sana sana tumejifunzia shuleni kuanzia shule ya msingi hadi shule ya upili. Pia tunajifunza lugha ya Kiswahili hapa mtaani tunapozungumza na wanajamii.

**Mtafiti:** Utakapokuwa na familia yako utawafunza lugha gani kwanza?

**Kijana VIII:** Watoto wangu nitawafunza Kiswahili kwanza kwa sababu tunaishi Kenya na lugha rasmi hata ya kutafuta kazi ni Kiswahili, pili, mimi mwenyewe hata sijui kuandika kwa Kishona, hivyo basi itakuwa vigumu niwafunze watoto wangu lugha ambayo siijui vizuri.

**Mtafiti:** Je, kuna mahali ambapo mnasoma lugha ya Kishona?

**Vijana kwa Jumla**: La

**Mtafiti**: Kwa nini?

**Kijana I:** Tuko na Biblia iliyoandikwa kwa Kishona. Hatuna vitabu vingine vya kishona kama vile vitabu vya hadithi ambavyo tunaweza kusoma. Lakini tungependa kuwa navyo ili lugha yetu isipotee.

**Mtafiti:** Ni muhimu kuweka mikakati kama hiyo ya kuwa na vitabu vilivyoandikwa ili watoto waweze kusoma. Nawashukuru kwa ushirikiano wenu.

## KIAMBATISHO H

## MWONGOZO WA UCHUNZAJI

**Viwango vya Uzungumzaji wa Kishona**

| **ENEO** | **SANA** | **KIDOGO** | **KUCHANGANYA NDIMI** |
|---|---|---|---|
| Kanisani | ✓ | | |
| Michezoni | | | ✓ |
| Nyumbani | ✓ | | |
| Sokoni/Kazini | | ✓ | |
| Sherehe | ✓ | ✓ | |

**Viwango vya Uzungumzaji wa Kiswahili**

| **ENEO** | **SANA** | **KIDOGO** | **KUCHANGANYA NDIMI** |
|---|---|---|---|
| Kanisani | ✓ | | |
| Michezoni | ✓ | | ✓ |
| Nyumbani | | ✓ | ✓ |
| Sokoni/Kazini | ✓ | | ✓ |
| Sherehe | | | ✓ |

**Viwango vya Uzungumzaji wa Kikuyu**

| **ENEO** | **SANA** | **KIDOGO** | **KUCHANGANYA NDIMI** |
|---|---|---|---|
| Kanisani | | ✓ | |
| Michezoni | | ✓ | |
| Nyumbani | | | |
| Sokoni/Kazini | | ✓ | |
| Sherehe | | | |

**KIAMBATISHO I**



Aliyekuwa Rais wa nne wa Kenya, Uhuru Kenyatta akiwapa Washona vyeti vya uraia tarehe 12/12/2020



Ibada ya Milimani



Mahojiano na wazee wa kanisa la *Gospel of God, Valley Road*, Nairobi




Baadhi ya watoto



Ibada milimani

## KIAMBATISHO J

KENYATTA UNIVERSITY
GRADUATE SCHOOL

E-mail: kubps@yahoo.com
dean-graduate@ku.ac.ke
Website: www.ku.ac.ke

P.O. Box 43844, 00100
NAIROBI, KENYA
Tel. 8710901 Ext. 57530

**Our Ref:** C82/21369/21

**Date:** 21st October, 2022

The Director General,
National Commission for Science, Technology & Innovation,
P.O. Box 30623-00100,
**NAIROBI**

Dear Sir/Madam,

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION FOR MS.MERCY M. MORAA - REG. NO. C82/21369/21**

I write to introduce Ms. Moraa who is a Postgraduate Student of this University. She is registered for a Ph.D. degree programme in the **Department of Kiswahili & African Languages in the School of Humanities & Social Sciences.**

Ms. Moraa intends to conduct research for Ph.D. thesis entitled, **"Athari za Kiswahili na Lugha Nyingine kwa Uthabiti wa Kiisimujamii kwa Lugha ya Kishona Nchini Kenya".**

Any assistance given will be highly appreciated.

Yours faithfully,

for

PROF. ELISHIBA KIMANI
DEAN, GRADUATE SCHOOL

EO/cao

# KIAMBATISHO K

REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: **104299**

Date of Issue: **28/October/2022**

## RESEARCH LICENSE



**This is to Certify that Ms.. MERCY moraa MOTANYA of Kenyatta University, has been licensed to conduct research as per the provision of the Science, Technology and Innovation Act, 2013 (Rev.2014) in Kiambu, Nairobi on the topic: ATHARI ZA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE KWA UTHABITI WA KIISIMUJAMII KWA LUGHA YA KISHONA NCHINI KENYA for the period ending : 28/October/2023.**

License No: **NACOSTI/P/22/21415**

**104299**

Applicant Identification Number

Director General

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

**See overleaf for conditions**

National Commision for Science, Technology and Innovation -

**THE SCIENCE, TECHNOLOGY AND INNOVATION ACT, 2013 (Rev. 2014)**
Legal Notice No. 108: The Science, Technology and Innovation (Research Licensing) Regulations, 2014

**The National Commission for Science, Technology and Innovation**, hereafter referred to as the Commission, was the established under the Science, Technology and Innovation Act 2013 (Revised 2014) herein after referred to as the Act. The objective of the Commission shall be to regulate and assure quality in the science, technology and innovation sector and advise the Government in matters related thereto.

## CONDITIONS OF THE RESEARCH LICENSE

1. The License is granted subject to provisions of the Constitution of Kenya, the Science, Technology and Innovation Act, and other relevant laws, policies and regulations. Accordingly, the licensee shall adhere to such procedures, standards, code of ethics and guidelines as may be prescribed by regulations made under the Act, or prescribed by provisions of International treaties of which Kenya is a signatory to
2. The research and its related activities as well as outcomes shall be beneficial to the country and shall not in any way;
    i. Endanger national security
    ii. Adversely affect the lives of Kenyans
    iii. Be in contravention of Kenya's international obligations including Biological Weapons Convention (BWC), Comprehensive Nuclear-Test-Ban Treaty Organization (CTBTO), Chemical, Biological, Radiological and Nuclear (CBRN).
    iv. Result in exploitation of intellectual property rights of communities in Kenya
    v. Adversely affect the environment
    vi. Adversely affect the rights of communities
    vii. Endanger public safety and national cohesion
    viii. Plagiarize someone else's work
3. The License is valid for the proposed research, location and specified period.
4. The license any rights thereunder are non-transferable
5. The Commission reserves the right to cancel the research at any time during the research period if in the opinion of the Commission the research is not implemented in conformity with the provisions of the Act or any other written law.
6. The Licensee shall inform the relevant County Director of Education, County Commissioner and County Governor before commencement of the research.
7. Excavation, filming, movement, and collection of specimens are subject to further necessary clearance from relevant Government Agencies.
8. The License does not give authority to transfer research materials.
9. The Commission may monitor and evaluate the licensed research project for the purpose of assessing and evaluating compliance with the conditions of the License.
10. The Licensee shall submit one hard copy, and upload a soft copy of their final report (thesis) onto a platform designated by the Commission within one year of completion of the research.
11. The Commission reserves the right to modify the conditions of the License including cancellation without prior notice.
12. Research, findings and information regarding research systems shall be stored or disseminated, utilized or applied in such a manner as may be prescribed by the Commission from time to time.
13. The Licensee shall disclose to the Commission, the relevant Institutional Scientific and Ethical Review Committee, and the relevant national agencies any inventions and discoveries that are of National strategic importance.
14. The Commission shall have powers to acquire from any person the right in, or to, any scientific innovation, invention or patent of strategic importance to the country.
15. Relevant Institutional Scientific and Ethical Review Committee shall monitor and evaluate the research periodically, and make a report of its findings to the Commission for necessary action.

National Commission for Science, Technology and
Innovation(NACOSTI),
Off Waiyaki Way, Upper Kabete,
P. O. Box 30623 - 00100 Nairobi, KENYA
Telephone: 020 4007000, 0713788787, 0735404245
E-mail: dg@nacosti.go.ke
Website: www.nacosti.go.ke